JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI

RIPOTI YA MWAKA YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/22





SERIKALI KUU





MACHI 2023

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Audit House, 4 Barabara ya Ukaguzi, S.L.P. 950, 41104 Tambukareli, Dodoma.
Simu ya upepo "Ukaguzi" Simu: +255 (026) 2161200
Nukushi: +255 (026) 2117527; Barua pepe: ocag@nao.go.tz Tovuti: www.nao.go.tz

Unapojibu tafadhali rejea:
Kumb. Na. CGA.319/421/01B **29 Machi 2023**


Mh. Dkt. Samia Suluhu Hassan,
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,
Ikulu,
S.L.P. 1102,
1 Barabara ya Julius Nyerere,
11400 Chamwino,
40400 DODOMA.

YAH: RIPOTI YA MWAKA YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KUHUSU UKAGUZI WA SERIKALI KUU KWA MWAKA WA FEDHA ULIOISHIA TAREHE 30 JUNI 2022.

Ninayo furaha kuwasilisha kwako Ripoti Kuu ya ukaguzi wa Serikali Kuu kwa mwaka wa fedha 2021/22 kwa mujibu wa Ibara ya 143(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ya waka 1977 na Kifungu cha 34 (1) (c) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura ya 418.

Naomba kuwasilisha,

Charles E. Kichere
Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali



Kufanya kazi kwa uhuru na bila upendeleo

Sisi ni taasisi ya umma isiyo na upendeleo, inayotoa huduma za ukaguzi wa hali ya juu kwa wateja wetu kwa njia isiyo na upendeleo.

Kufanya kazi kwa ushirikiano

Tunathamini na kufanya kazi kwa kushirikiana na wadau wa ndani na nje.

Kufanya kazi kwa kuzingatia matokeo

Tunazingatia katika kufikia malengo muhimu yenye kuaminika kwa wakati, usahihi na utumizi stahiki.



Kufanya kazi kwa utaalam

Tunatoa huduma za ukaguzi za hali ya juu kwa kuzingatia maarifa ya kitaaluma, ujuzi na mbinu bora.

Kufanya kazi kwa uadilifu

Tunazingatia na kudumisha viwango vya juu vya maadili na sheria katika utoaji wa huduma za ukaguzi.

Kufanya kazi kwa ubunifu na uvumbuzi

Tunahimiza, kuvumbua, na kubuni mawazo ya kuongeza thamani kwa ajili ya kuboresha huduma za ukaguzi

YALIYOMO

ORODHA YA MAJEDWALI iv
ORODHA YA VIELELEZO viii
ORODHA YA VIAMBATISHO ix
VIFUPISHO xi
SALAMU KUTOKA KWA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI xiii
MUHTASARI xiv
MAELEZO YA AWALI 1
SURA YA KWANZA 5
HATI ZA UKAGUZI 5
SURA YA PILI 9
UFUATILIAJI WA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA MIAKA ILIYOPITA 9
SURA YA TATU 14
TATHMINI YA UFANISI WA KIUTENDAJI, UDHIBITI WA NDANI, USIMAMIZI WA VIHATARISHI NA UTAWALA 14
SURA YA NNE 50
MAANDALIZI NA UTEKELEZAJI WA BAJETI 50
SURA YA TANO 63
USIMAMIZI WA UKUSANYAJI WA MAPATO YA KODI, DENI LA TAIFA, HUDUMA ZA SERIKALI, UKAGUZI WA AWALI WA MAFAO YA WATUMISHI WALIOMALIZA MUDA KAZINI NA HESABU JUMUIFU ZA SERIKALI 63
SURA YA SITA 98
USIMAMIZI WA MATUMIZI 98
SURA YA SABA 112
MENEJIMENTI YA RASILIMALI WATU, USIMAMIZI WA MISHAHARA NA MAFAO YA WASTAAFU 112
SURA YA NANE 125
USIMAMIZI WA MALI NA MADENI 125
SURA YA TISA 135
UNUNUZI NA USIMAMIZI WA MIKATABA 135
SURA YA KUMI 177

USIMAMIZI WA RASILIMALI MAJI NA USAMBAZAJI MAJI 177
SURA YA KUMI NA MOJA 207
UKAGUZI WA WAKALA ZA SERIKALI, MIFUKO MAALUMU YA FEDHA, NA TAASISI NYINGINE 207
SURA YA KUMI NA MBILI.....241
UTENDAJI KATIKA UENDESHAJI WA HOSPITALI ZA RUFAA ZA MIKOA NA HOSPITALI MAALUMU 241
SURA YA KUMI NA TATU.....256
UKAGUZI WA OFISI ZA BALOZI ZA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA 256
SURA YA KUMI NA NNE 283
VYAMA VYA SIASA 283
SURA YA KUMI NA TANO 297
KAGUZI MAALUMU NA ZA KIUCHUNGUZI 297
VIAMBATISHO.....314

NATIONAL AUDIT OFFICE
NAOT

ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali Na. 1: Taasisi Zilizojumuishwa Katika Ripoti hii Lakini Hazikuripotiwa katika Ripoti ya Mwaka wa Fedha 2020/2021 2
Jedwali Na. 2: Taasisi ambazo Zilijumuishwa Katika Ripoti ya Serikali Kuu kwa mwaka 2020/21 Lakini Zimeripotiwa Katika Ripoti ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa mwaka 2021/2022 3
Jedwali Na. 3: Mwenendo wa Hati za Ukaguzi..... 7
Jedwali Na. 4: Uwasilishaji wa Hali ya Utekelezaji wa Mapendekezo kwenye Ripoti za Mwaka..... 11
Jedwali Na. 5: Orodha ya Maeneo ya Akiolojia yenye Migogoro 24
Jedwali Na. 6: Orodha ya Magereza yenye Matumizi Madogo ya Ardhi ya kilimo .. 26
Jedwali Na. 7: Idadi ya Wahalifu Walioingizwa Upya Magerezani 27
Jedwali Na. 8: Orodha ya Magari Manne Yaliyotengenezwa na TATC lakini Hayakufaa 29
Jedwali Na. 9: Matukio ya Zimamoto na Uokoaji..... 33
Jedwali Na. 10: Sampuli ya Mikoa Inayoonesha Mwenendo wa Ukaguzi wa Mikoa ya Zimamoto 35
Jedwali Na. 11: Kanzidata isiyo Halisi 35
Jedwali Na. 12: Utendaji wa Uchunguzi wa Moto 36
Jedwali Na. 13: Mapungufu yaliyobainishwa katika Maandalizi na Utekelezaji wa Mpango Mkakati 40
Jedwali Na. 14: Orodha ya Taasisi ambazo Hazina Sera ya ICT na Kamati ya Uendeshaji..... 46
Jedwali Na. 15: Taasisi ambazo hazikuandaa Mpango wa Kurejesha huduma na ambazo hazikuwa vituo vya nje vya Kuhifadhi Nakala 47
Jedwali Na. 16: Mwenendo wa asilimia za Makusanyo kutoka kila chanzo kilichoainishwa..... 53
Jedwali Na. 17: Kusuluhisha Ukusanyaji Halisi wa Mapato na Amana katika Mfuko Mkuu wa Hazina (Kiasi katika Sh. Trilioni) 56
Jedwali Na. 18: Makusnyo dhidi ya Matumizi yaliyofanywa katika Akaunti ya Mfuko Mkuu 57
Jedwali Na. 19: Fedha zilizotolewa zaidi ya Bajeti 60
Jedwali Na. 20: Taasisi zenye Matumizi nje ya Bajeti Iliyoidhinishwa 61
Jedwali Na. 21: Mchanganuo wa Makusanyo ya Mapato (Tanzania Bara) 64
Jedwali Na. 22: Mchanganuo wa Makusanyo ya Mapato (Zanzibar)..... 64
Jedwali Na. 23: Mwenendo wa Ukusanyaji wa Mapato wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzia 2017/18 hadi 2021/22 (Tanzania Bara & Zanzibar) 66
Jedwali Na. 24: Uwiano wa kodi kwa Pato la Taifa kwa Tanzania na nchi nyingine za Afrika Mashariki kwa Miaka Mitano 67

Jedwali Na. 25: Mashauri ya Kikodi yaliyopo kwenye Mahakama ya Rufani ya Tanzania (CAT) (Tanzania Bara) 70
Jedwali Na. 26: Mashauri ya Kikodi yalipo Mahakama ya Rufaa ya Mapato ya Kodi 71
Jedwali Na. 27: Kesi za Kikodi zilizopo Katika Bodi ya Rufani ya Mapato ya kodi . 71
Jedwali Na. 28: Mashauri ya Kikodi yalipo Mahakama ya Rufaa ya Mapato ya 71
Jedwali Na. 29: Kesi za Kikodi Zilizopo Katika Bodi ya Rufani ya Mapato ya kodi . 72
Jedwali Na. 30: Ada za Kukodisha Majengo Ambazo Hazijakusanywa 76
Jedwali Na. 31: Makusanyo Yaliyokusanywa Nje ya Mfumo wa GepG 82
Jedwali Na. 32: Madai ya Makusanyo yasiyotokana na Kodi 83
Jedwali Na. 33: Mwenendo wa Deni la Ndani (Deni Halisi) 86
Jedwali Na. 34: Mwenendo wa Ukopaji wa Ndani (Thamani Halisi) 87
Jedwali Na. 35: Mwenendo na Mseto wa Deni la Nje 87
Jedwali Na. 36: Taasisi za Serikali Zilizojumuisha kiasi cha Mtaji Kisichostahili .. 93
Jedwali Na. 37: Taasisi zenye Masurufu yasiyorejeshwa 102
Jedwali Na. 38: Taasisi ambazo Hazikuweka Taarifa za Masurufu kweye Rejista 103
Jedwali Na. 39: Taasisi Zilizotoza Masurufu kama Matumizi 103
Jedwali Na. 40: Mfuko usiotumika katika Akaunti ya Matumizi 104
Jedwali Na. 41: Taasisi zenye Malipo Yenye Mapungufu 106
Jedwali Na. 42: Malipo yaliyofanywa kwa kutumia vifungu visivyo sahihi 107
Jedwali Na. 43: Taasisi za Serikali zilizofanya malipo bila kuomba risiti za kielektroniki 108
Jedwali Na. 44: Taasisi ambazo Hazikuwasilisha Kodi ya Zuio 110
Jedwali Na. 45: Upungufu wa Watumishi kwenye Taasisi Serikali Kuu 113
Jedwali Na. 46: Taasisi zenye Changamoto kwenye Matumizi ya Mfumo wa HCMIS 116
Jedwali Na. 47: Taasisi zenye Watumishi Wanaokaimu zaidi ya Miezi Sita 117
Jedwali Na. 48: Taasisi Ambazo Hazikuwasilisha Makato Ya Mishahara..... 118
Jedwali Na. 49: Majalada ya Wastaafu Yaliyokaguliwa 2021/22 121
Jedwali Na. 50: Majalada ya Mafao Yaliyokokotolewa Kimakosa 121
Jedwali Na. 51: Majalada Yaliyocheleweshwa..... 123
Jedwali Na. 52: Taasisi Zisizotumia Mfumo wa GAMIS..... 128
Jedwali Na. 53: Maelezo ya Majengo Yasiyokarabatiwa..... 129
Jedwali Na. 54: Magari Yaliyolipiwa ila Hayajapokelewa 130
Jedwali Na. 55: Viwanja vya Serikali ambavyo Havijaendelezwa..... 131
Jedwali Na. 56: Madai ya Matibabu Kutoka Hospitali za Rufaa India 133
Jedwali Na. 57: Kasoro Zilizobainika kwenye Ununuzi wa Vishikwambi 137
Jedwali Na. 58: Orodha ya Wizara, Vitengo na Wakala zilizokiuka Mpango wa Ununuzi wa Mwaka 141
Jedwali Na. 59: Uchambuzi wa utekelezaji wa Mpango wa Ununuzi wa Mwaka . 144
Jedwali Na. 60: Orodha ya Taasisi vilizonunua bidhaa na huduma bila idhini ya Bodi ya Zabuni..... 145

Jedwali Na. 61: Orodha ya Taasisi ambazo zilifanya manunuzi ya bidhaa na huduma pasipo ushindani 149
Jedwali Na. 62: Orodha ya Taasisi ambazo zilifanya manunuzi kwa kutumia njia ya chanzo kimoja 152
Jedwali Na. 63: Mikataba Iliyotolewa Zaidi ya Bajeti 154
Jedwali Na. 64: Orodha ya Taasisi ambazo miradi ilitekelezwa kwa Dhamana ya Benki ya Utendaji iliyoisha muda wake 155
Jedwali Na. 65: Orodha ya Taasisi zilizotekeleza Mikataba pasipokuwa na Bima 157
Jedwali Na. 66: Orodha ya Kazi ambazo hazikukamilika (Taa za barabarani) ... 159
Jedwali Na. 67: Uchambuzi wa Maelezo ya Mkataba na Malipo kwa Mkandarasi Ambaye ana Upungufu wa Watumishi Muhimu na mitambo 164
Jedwali Na. 68: Orodha ya miradi iliyotelekezwa na TBA na maendeleo yake .. 170
Jedwali Na. 69: Orodha ya taasisi ambazo miradi yake ilichelewa kukabidhiwa 171
Jedwali Na. 70: Hali ya Utoaji wa Fedha kwa SMKWSIP 180
Jedwali Na. 71: Muhtasari wa Mikataba Inayotekelezwa SMKWSIP 181
Jedwali Na. 72: Malipo yaliyofanywa kwa Mradi wa Mugango–Kiabakari–Butiama 185
Jedwali Na. 73: Vibali vya matumizi ya maji vilivyokwisha muda wake 188
Jedwali Na. 74: Shughuli za Binadamu zenye Athari Mbaya kwa Uhifadhi wa Vyanzo vya Maji ndani ya Mita Sitini 189
Jedwali Na. 75: Uchambuzi wa Madai ya Muda Mrefu kwa Kitengo cha Uchimbaji ambayo Hayajakusanywa 194
Jedwali Na. 76: Hali ya Utendaji Kazi wa Vituo vya Kuchotea Maji kwenye Miradi ya Maji 195
Jedwali Na. 77: Hali ya Visima Vilivyopangwa Na Vilivyochimbwa 196
Jedwali Na. 78: Makusanyo ya mapato ya CBWSO 198
Jedwali Na. 79: Udhaifu Uliobainishwa katika Usimamizi wa CBWSO 199
Jedwali Na. 80: Orodha ya Mamlaka za Maji zenye Wateja Wasiofungiwa Mita za Maji 201
Jedwali Na. 81: Gharama kubwa za umeme kwa Mamlaka za Maji katika Kusambaza Huduma ya Maji 202
Jedwali Na. 82: Mamlaka za Maji Zenye Uwezo Mdogo wa Kusambaza Maji 205
Jedwali Na. 83: Halmashauri ambazo Hazijarejesha Mkopo 239
Jedwali Na. 84: Fedha zilizokopwa na Wizara 240
Jedwali Na. 85: Orodha ya Hospitali zenye Kiasi kikubwa cha Fedha Kinachoshikiliwa na Bohari Kuu ya Dawa 243
Jedwali Na. 86: Hospitali za Rufaa zenye Wataalamu wa Afya Wasio na Leseni za Kufanya Taaluma zao 244
Jedwali Na. 87: Msamaha kutolewa kwa Wagonjwa Wasiostahili 245
Jedwali Na. 88: Hasara Iliyopatikana Kutokana na Dawa zilizoisha Muda wake . 247
Jedwali Na. 89: Orodha ya Hospitali Zenye Ununuzi wa Dawa bila Uthibitisho Kutoka Bohari Kuu ya Dawa 250

Jedwali Na. 90: Vifaa na Mashine za Hospitali Kutofanyiwa Matengenezo na Kutotumika Kabisa. 253
Jedwali Na. 91: Orodha ya Hospitali za Rufaa Zenye Makusanyo Yasiyolingana na Taarifa za Mfumo 254
Jedwali Na. 92: Fedha ambazo Hazikurejeshwa kwenye Mfuko Mkuu 263
Jedwali Na. 93: Bajeti pamoja na Balozi zenye Shughuli ambazo hazijatekelezwa 266
Jedwali Na. 94: Mali zinazotumika Chini ya Kiwango katika Balozi za Tanzania 268
Jedwali Na. 95: Matumizi ya Kodi kwa Kila Balozi kwa Mwaka wa Fedha 2021/22 269
Jedwali Na. 96: Mali zilizotelekezwa na zisizoendelezwa katika Ofisi za Balozi 270
Jedwali Na. 97: Majengo yaliyochakaa 271
Jedwali Na. 98: Mali zilizochakaa na hazijauzwa 272
Jedwali Na. 99: Manunuzi Madogo madogo ambayo hayajaripotiwa kwenye Bodi ya Zabuni 277
Jedwali Na. 100: Bidhaa na Huduma Zilizopokelewa na Kukubalika kabla ya Kukaguliwa..... 277
Jedwali Na. 101: Upungufu wa Watumishi Muhimu katika Balozi za Tanzania ... 279
Jedwali Na. 102: Miamala ya Muda Mrefu ambayo Haijasuluhishwa..... 281
Jedwali Na. 103: Orodha ya Vyama vya Siasa vilivyoshindwa Kukusanya Mapato yaliyobajetiwa 284
Jedwali Na. 104: Orodha ya Vyama vya Siasa vilivyotumia mapato yaliyokusanywa kabla ya kuwekwa benki 285
Jedwali Na. 105: Orodha ya Vyama vya Siasa ambavyo havikuwasilisha taarifa za fedha kwa ajili ya ukaguzi ifikapo tarehe 30 Septemba, 2022 295

ORODHA YA VIELELEZO

Kielelezo Na. 1: Mgao wa Matumizi ya Serikali 51
Kielelezo Na. 2: Mwenendo wa Makusanyo.....54
Kielelezo Na. 3: Mwenendo wa Ufandili wa Bajeti 55
Kielelezo Na. 4: Makadirio, Fedha zilizotolewa na Matumizi halisi ya Fedha za Matumizi ya Kawaida kwa kipindi cha Miaka Mitatu 59
Kielelezo Na. 5: Makadirio, Fedha zilizotolewa na Matumizi Halisi ya Fedha za Maedeleo katika kipindi cha Miaka Mitatu 62
Kielelezo Na. 6: Ulinganifu wa Uchangiaji wa Makusanyo Halisi kwa Idara 2021/22 na 2020/21 (Tanzania bara) 65
Kielelezo Na. 7: Ulinganifu wa Uchangiaji wa Makusanyo halisi kwa Idara 2021/22 na 2020/21 (Zanzibari).....65
Kielelezo Na. 8: Mwenendo wa Ukuaji wa Deni la Serikali.....86
Kielelezo Na. 9: Uchambuzi wa Mwenendo wa Ajira Zilizoidhinishwa, Ajira Zilizoombwa na Vibali Halisi Vilivyotolewa na Serikali 113
Kielelezo Na. 10: Uwiano wa Utekelezaji wa Mipango ya Manunuzi ya Mwaka ya Taasisi za Serikali 143
Kielelezo Na. 11: Ulinganisho wa Hasara Kutokana na Dawa zilizoisha Muda Wake 249

NATIONAL AUDIT OFFICE
NAOT

ORODHA YA VIAMBATISHO

Kiambatisho Na. I: Mtiririko wa Hati Zilizokaguliwa kwa Miaka Mitatu 314
Kiambatisho Na. II: Taasisi Zilizopata Hati Isiyoridhisha 330
Kiambatisho Na. III: Taasisi Zilizopata Hati Mbaya..... 337
Kiambatisho Na. IV: Taasisi Ambazo Hazikupata Maoni 339
Kiambatisho Na. V: Taasisi Ambazo Zina Mapungufu katika Uzingatiaji wa Sheria na Kanuni za Ununuzi wa Umma 340
Kiambatisho Na. VI: Orodha ya Vituo vya Kuchukulia Maji ya Kuzima Moto..... 344
Kiambatisho Na. VII: Orodha ya Taasisi zilizoshindwa Kuanzisha na Kudumisha Bodi ya Uongozi 345
Kiambatisho Na. VIII: Orodha ya Taasisi zenye Utendaji Usiofaa wa Kamati ya Ukaguzi..... 348
Kiambatisho Na. IX: Orodha ya Taasisi Vinazofanya Kazi bila Kuanzisha Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani..... 351
Kiambatisho Na. X: Orodha ya Taasisi Zenye Upungufu katika Usimamizi wa Vihatarishi 351
Kiambatisho Na. XI: Upungufu wa Watumishi..... 352
Kiambatisho Na. XII: Maelezo kwa Wafanyakazi Wanakaimu kwa Muda Mrefu... 355
Kiambatisho Na. XIII: Taasisi Zisizokuwa na Mpango wa Matengenezo ya Mali... 356
Kiambatisho Na. XIV: Magari, Mitambo na Vifaa vya Serikali Vilivyotelekezwa kwa Muda Mrefu 357
Kiambatisho Na. XV: Taasisi zenye Madeni..... 359
Kiambatisho Na. XVI: Taasisi zenye Madeni Tarajiwa 364
Kiambatisho Na. XVII: Orodha ya Taasisi ambazo Manunuzi Yake Madogo madogo hayakuripotiwa Kila Mwezi kwa Bodi ya Zabuni 365
Kiambatisho Na. XVIII: Orodha ya Taasisi ambazo Zimechelewa Kupokea Vifaa na Huduma Zilizonunuliwa 366
Kiambatisho Na. XIX: Orodha ya Taasisi Zilizochelewa Kukamilisha Miradi 367
Kiambatisho Na. XX: Orodha ya Taasisi Ambazo Zilifanya Manunuzi nje ya TANEPs 370
Kiambatisho Na. XXI: Orodha ya Taasisi ambazo Zilipokea Bidhaa na Huduma bila Kukaguliwa..... 371
Kiambatisho Na. XXII: Orodha ya Miradi iliyoanza kutekelezwa bila Cheti cha Mazingira..... 371
Kiambatisho Na. XXIII: Vyanzo vya Kuchukulia Maji Visivyo na Mfumo wa Mita.. 374
Kiambatisho Na. XXIV: Uhaba wa Jumuia za Watumia Maji Katika Bodi za Mabonde ya Maji..... 375
Kiambatisho Na. XXV: Kuchelewa kukamilika kwa miradi ya maji inayotekelezwa na RUWASA 376
Kiambatisho Na. XXVI: Mamlaka za Maji Zenye Kiwango cha Juu cha Maji Yasiyo ya Mapato 381
Kiambatisho Na. XXVII: Mapato Yasiyokusanywa Kutokana na Mauzo ya Maji.... 383
Kiambatisho Na. XXVIII: Utoaji wa Huduma Usioridhisha katika Hospitali za Rufaa za Mikoa..... 385

Kiambatisho Na. XXIX: Upotevu wa Mapato Kutokana na Kukataliwa kwa Madai ya Bima ya Afya..... 386
Kiambatisho Na. XXX: Kucheleweshwa kwa Uwasilishwaji wa Dawa na Vifaa Tiba Vilivyolipiwa 387
Kiambatisho Na. XXXI: Vifaa vya Matibabu na Majengo ya Hospitali Yaliyokamilika lakini Hayatumiki 388
Kiambatisho Na. XXXII: Kuchelewa kukamilika kwa Ujenzi wa Majengo ya Hospitali za Rufaa za mikoa na Hospitali Maalumu..... 389
Kiambatisho Na. XXXIII: Fursa Kutoka Balozini zenye Muitikio Hafifu 392
Kiambatisho Na. XXXIV: Changamoto zinazokabili Balozi za Tanzania katika kutekeleza Shughuli za Diplomasia ya Uchumi 394
Kiambatisho Na. XXXV: Shughuli ambazo Hazijatekelezwa Ipasavyo 396

VIFUPISHO

AGITF	Mfuko wa Pembejeo wa Taifa
ASA	Wakala wa Mbegu za Kilimo
ATCL	Shirika la Ndege Tanzania
BADEA	Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Kiuchumi Barani Afrika
BRELA	Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni
BUWSSA	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira, Biharamulo
BWB	Bodi ya Maji ya Bonde
CBWSO	Chombo cha Watoa Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii
DAWASA	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira, Dar es Salaam
EFD	Mashine ya Kutoa Risiti za Kielektroniki
eHMIS	Mfumo wa Taarifa za Usimamizi wa Afya za wagonjwa
EWURA	Mamlaka ya Udhibiti wa Matumizi ya Nishati na Maji
FETA	Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi
GAMIS	Mfumo wa Taarifa za Usimamizi wa Mali za Serikali
GePG	Mfumo wa Serikali wa Kukusanya Mapato
GOT	Serikali ya Tanzania
GPSA	Wakala wa Ununuzi wa Umma
GST	Utafiti wa Jiolojia wa Tanzania
HCMIS	Mfumo wa Taarifa Shirikishi za Kiutumishi na Mishahara
ICU	Kitengo cha Uangalizi Maalumu wa Wagonjwa
IPSAS	Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Hesabu Katika Sekta ya Umma
ISCF	Mfuko wa Ushirika wa Ukaguzi na Usimamizi
JKT	Jeshi la Kujenga Taifa
JNIA	Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere
KFD	Mfuko wa Kuwait kwa Maendeleo ya Uchumi wa Kiarabu
LITA	Wakala wa Mafunzo ya Mifugo
LTBWB	Bodi ya Maji ya Bonde la Ziwa Tanganyika
MDAs	Wizara, Idara na Wakala
MoFP	Wizara ya Fedha na Mipango
MOHA	Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi
MoU	Mkataba wa Maelewano
MPWSSA	Mamlaka ya Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Makonde Plateau
MSD	Bohari ya Dawa
Na.	Namba
NEMC	Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira
NFRA	Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula
NHIF	Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya

NIDA	Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa
NRW	Maji Yasiyo na Mapato
NSSF	Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Taifa
OFID	Mfuko wa OPEC kwa Maendeleo ya Kimataifa
OI	Taasisi Nyingine
OSHA	Mamlaka ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi
PFR	Kanuni za Fedha za Umma
PPA	Sheria ya Ununuzi ya Umma
PPRA	Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma
PSSSF	Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma
RBWB	Bodi ya Maji ya Bonde la Rufiji
REA	Wakala wa Nishati Vijijini
RRH	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa
RSCBWB	Bodi ya Maji ya Bonde la Ruvuma Kusini mwa Pwani
RSDMS	Mfumo wa Utoaji na Usimamizi wa Huduma za RUWASA
RUWASA	Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini
SFD	Mfuko wa Maendeleo wa Saudi Arabia
SH	Hospitali Maalumu
Sh.	Shilingi
SMKWSIP	Mradi wa Uboreshaji wa Usambazaji Maji wa Same-Mwanga-Korogwe
TAA	Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania
TANePS	Mfumo wa Ununuzi kwa Njia ya Mtandao
TANESCO	Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania
TANROADS	Wakala wa Barabara Tanzania
TATC	Shirika la Nyumbu
TBA	Wakala wa Ujenzi Tanzania
TEMESA	Wakala wa Ufundi na Umeme
TIA	Taasisi ya Uhasibu Tanzania
TPSC	Ofisi ya Rais Tanzania Chuo cha Utumishi wa Umma
TRA	Mamlaka ya Mapato Tanzania
UNESCO	Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni
UNICEF	Shirika la Watoto la Umoja wa Mataifa
USD	Dola ya Marekani
VAT	Kodi ya Ongezeko la Thamani
WMA	Wakala wa Vipimo
WSSAs	Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira
ZRH	Hospitali ya Rufaa ya Kanda



SALAMU KUTOKA KWA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

Ninayo furaha kuwasilisha Ripoti yangu ya mwaka ya ukaguzi wa Serikali Kuu kwa mwaka wa fedha 2021/22, kama ilivyoagizwa na Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ya mwaka 1997, na Kifungu cha 34 (1) (c) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura ya 418.

Ripoti hii inaangazia, ushauri na mapendekezo katika maeneo tofauti ya usimamizi wa fedha za umma, ikijumuisha uzingatiaji wa sheria na kanuni, taarifa za kifedha, uzalishaji wa mapato, ununuzi na usimamizi wa mali. Taarifa hii pia inabainisha maeneo ya kuboresha na kuimarisha ufanisi katika mipango na huduma za serikali, ikiwa ni pamoja na usimamizi wa rasilimali za maji, utendaji kazi wa Hospitali za Mikoa za Rufaa na Hospitali Maalumu, na utendaji wa ofisi za Balozi za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia, taarifa hii inalenga ukaguzi wa vyama vya siasa na ukaguzi maalum.

Wadau mbalimbali, ikiwemo serikali, mashirika, asasi za kiraia, washirika wa maendeleo, na umma, kupata mwongozo wa kufanya maamuzi sahihi, kuunda sera, na kutekeleza programu na miradi bora kwa ajili ya wananchi.

Kwa kuhitimisha, chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ripoti hii itatumika kama nyenzo muhimu ya kuimarisha uwazi, uwajibikaji na utawala bora ndani ya sekta ya umma. Kwa kuangazia maeneo ya uboreshaji na kutoa mapendekezo muhimu, inachangia katika uimarishaji endelevu wa usimamizi wa rasilimali za umma na kufikiwa kwa malengo ya maendeleo kwa manufaa ya taifa na wananchi.

Charles E. Kichere,
Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

MUHTASARI

Ripoti hii inatoa uchambuzi wa kina wa hoja za ukaguzi, mapendekezo, na hitimisho kutokana na ukaguzi wa taarifa za fedha na uzingatiwaji wa sheria kwa Wizara,Idara na Wakala wa Serikali,na Taasisi nyingine za Serikali. Ukaguzi umehusisha jumla ya Wizara na Idara za Serikali 65, Ofisi za Balozi 43, Wakala za Serikali 30 na Mifuko Maalum 16, Vyama vya Siasa 19, Hospitali za Rufaa na Maalum 34, Taasisi Nyingine 129 na kaguzi maalum tatu. Zaidi ya hayo, ukaguzi ulijumuisha Mamlaka ya Mapato Tanzania, Hesabu jumuifu na ukaguzi wa awali wa mafao ya wastaafu kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2022.

(i) Aina na Mwenendo wa Hati za Ukaguzi

Kwa mwaka wa fedha 2021/22, nilitoa jumla ya Hati 336 kwa taasisi ambazo ziliwasilisha taarifa za fedha kwa ajili ya ukaguzi. Kati ya hizo, Hati 323 zilikuwa zinaridhisha, Hati 10 zilikua hati zenye shaka, Hati mbili zilikuwa mbaya, na nilishindwa kutoa maoni kwa taasisi moja. Maelezo zaidi yanapatikana katika sura ya kwanza ya ripoti hii.

(ii) Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Mapendekezo ya Miaka Iliyopita

Hadi tarehe 30 Juni 2021, jumla ya mapendekezo 7,365 na maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali yalitolewa kwa Maafisa Masuuli na Mlipaji Mkuu wa Serikali. Kati ya mapendekezo 6,947 yalitolewa kwa Maafisa Masuuli kupitia taarifa za kila Taasisi za mwaka 2020/21, mapendekezo 246 yalitolewa kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali kupitia Ripoti ya Mwaka ya Ukaguzi wa Serikali Kuu iliyotolewa Machi, 2022; na mapendekezo 172 yaliyobaki ni Maagizo yaliyotolewa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali kwa Maafisa Masuuli.

Kati ya mapendekezo 246 yaliyojibiwa, 10 (4%) yametekelezwa, 192 (78%) utekelezaji unaendelea, 8 (3%) hayajatekelezwa, 34 (14%) yalirudiwa na mapendekezo 2 (1%) yalifutwa kutokana na kupitwa na wakati.

Kwenye taarifa kila Taasisi, Kati ya hayo mapendekezo 6947, 2380 (34%) yalitekelezwa kikamilifu, 2506 (36%) utekelezaji unaendelea, 1104 (16%) hayajatekelezwa, 320 (5%) yalifutwa kutokana na kupitwa na wakati na mapendekezo 637 (9%) yalirudiwa. Wakati hali ya jumla ya utekelezaji inaonyesha kuboreka kidogo ikilinganishwa na miaka ya nyuma.

Aidha, tathmini yangu kuhusu hali ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali hadi mwaka wa fedha 2021/22 ilibainisha kuwa; kati ya maagizo 172 ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali yaliyotolewa kutoka katika ripoti yangu ya miaka ya nyuma, 35 (20%) yalitekelezwa kikamilifu, 113 (65%) utekelezaji unaendelea, 22 (13%) hayakutekelezwa huku pendekezo 1 (1%) lilirudiwa na 1 (1%) lilifutwa kutokana na kupitwa na wakati.

(iii) Tathmini ya Mifumo ya Udhibiti wa Ndani na Utawala Bora

Nilibaini mapungufu katika usimamizi wa POS kwa mapato yanayokusanywa na TEMESA sh. bilioni 4.105; ikiwa ni pamoja na ukosefu wa rejista ya POS, mashine za POS kutokuunganishwa na seva kuu, kukosekana kwa mashine 52 za POS katika makao makuu ya TEMESA na Kanda ya Ziwa na pia kutokufanyiwa usuluhisho makusanyo ya sh. Bilioni 1.194 yaliyokusanywa kupitia Mashine za POS katika kivuko cha MV Kilindoni.

Nilibaini kuwepo kwa mapungufu katika matengenezo ya Uwanja wa Benjamin Mkapa na Uwanja wa Uhuru, ambapo miundombinu mibovu imebainika. Nimebaini pia kuwa hakuna mpango wa matengenezo, na kuna mapungufu katika usalama wa uwanja, hasa katika maeneo muhimu kama vile viashiria vya moto na mifumo ya kengele.

Nilibaini pia kuwa licha ya fidia ya Sh. bilioni 3.026 ili kujenga soko la kimataifa Njombe, hakuna soko la kimataifa lililojengwa kufikia Desemba 2022 nilipohitimisha ukaguzi.

Ukaguzi wangu pia ulibaini kuwa, hakukuwa na utaratibu wa kutosha dhidi ya waharibifu wa Mnada wa kielekroniki kwa vitalu vya uwindaji, na kusababisha upotevu wa Dola za Marekani 343,000 sawa na Sh. milioni 792,7.

Nilibaini kuwa Idara ya Jeshi la Magereza ilikuwa na wahamiaji 3,110 haramu ambao vifungo vyao vilimalizika magerezani, hivyo kuigharimu serikali Sh. bilioni 5.675 kila mwaka. Ukaguzi wangu pia ulibainisha kuwa Tanzania inaendesha magereza 129 yenye uwezo wa kuchukua wafungwa 29,902, hata hivyo, wastani wa wafungwa 32,058 wamelazwa katika magereza hayo katika kipindi cha mwaka mmoja na kusababisha wafungwa zaidi 2,156 hali iliyosababisha kujazana na msongamano katika vituo

vilivyopo. Nilibaini kuwa wilaya 49 hazina magereza, hali inayozidisha suala la msongamano katika vituo vilivyopo sasa.

Kuhusu Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, nilibaini upungufu wa vituo 283,370 vya vya kuchukulia maji ya kuzima moto sawa na asilimia 99.4 ya mahitaji. Pia nilibaini upungufu wa vifaa vya zimamoto na uokoaji 6,352 sawa na asilimia 91. Pia nilibaini kuwa jeshi hilo linarekodi matukio ya mlipuko wa moto na uokoaji kwa njia ya kizamani na kusababisha takwimu zisizo sahihi kwa kufanya maamuzi. Nilibaini pia kwamba, jeshi lilishindwa kukagua majengo 62,581 sawa na 62%. Si hivyo tu, uchambuzi wangu ulibaini kuwa jumla ya milipuko 1,718 ya moto iliyotokea katika mikoa 28 ya zimamoto katika kipindi cha mwaka mmoja haikuchunguzwa.

Jeshi la Polisi, kupitia Baraza la Taifa la Usalama Barabarani, lilitoa stika za usalama barabarani bila kufanya ukaguzi wa magari na pikipiki kama inavyotakiwa na Kanuni ya 15 (2) ya Kanuni za Ukaguzi wa Magari Barabarani ya mwaka 2015. Zaidi ya hayo, stika hizo za usalama hazijasajiliwa kwenye mfumo wa kielektroniki na mapato hayo yalikusanywa kwa njia ya fedha taslimu badala ya kutumia Mfumo wa Ukusanyaji Mapato wa Serikali (GePG). Aidha, Baraza halijatayarisha taarifa za fedha kwa kipindi kilichoishia tarehe 30 Juni 2022.

Kwa upande wa mifumo ya utawala, niligundua kuwa taasisi tatu hazikuanzisha bodi zao za ushauri au uongozi, huku taasisi tano zilishindwa kufanya vikao vya bodi vya kisheria. Niliona kuwa taasisi nne zilikuwa zinafanya kazi bila mipango ya kimkakati.

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa Kitengo cha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu hakikuwa huru na kukinzana na jukumu la Mkurugenzi wa Uvuvi juu ya menejimenti ya Kitengo. Nilibaini kuwa kitengo hicho kinapokea maelekezo kutoka mamlaka mbalimbali, ikiwa ni pamoja na Mkurugenzi wa Uvuvi, Bodi na Katibu Mkuu wa Wizara husika, kama ilivyoainishwa katika Sheria. Kitengo kiko chini ya Mkurugenzi wa Uvuvi ambaye humteua Meneja wa Kitengo kwa mashauriano kutoka Bodi wakati Mkurugenzi ni mjumbe wa Bodi.

Zaidi ya hayo, niliona kuwa kamati za ukaguzi hazikusimamia ipasavyo utendaji wa kitengo cha ukaguzi wa ndani na usimamizi wa vihatarishi, na taasisi 22 hazijaanzisha kitengo cha ndani.

(iv) Uandaaji na Utekelezwaji wa Bajeti

Katika mwaka wa fedha 2021/22, Serikali ilikusanya jumla ya Sh. trilioni 38.298 zaidi ya bajeti iliyoidhinishwa ya Sh. trilioni 37.992 hivyo kiasi cha Sh. bilioni 306 kilikusanywa zaidi. Aidha, nilibaini kuongezeka kwa makusanyo ya Sh. trilioni 6.972 (22%) ikilinganishwa na Sh. trilioni 31.326 zilizokusanywa katika mwaka wa fedha uliopita 2020/21.

Makusanyo ya ndani kutoka katika vyanzo vya Kodi, Makusanyo yasiyotokana ya Kodi na Makusanyo ya Serikali za Mitaa yalichangia bajeti kwa Sh. trilioni 24.546 (64%), wakati Sh. trilioni 13.752 (36%) zilitokana na Misaanda na Mikopo; (Sh. trilioni 1.305 zilitokana na Misaada na Sh. trilioni 12.447 zilitokana na Mikopo).

Aidha, nilibaini kuwa Serikali ilikuwa na nakisi ya Sh. bilioni 577 katika Mfuko Mkuu iliyotokana na fedha zilizotolewa zaidi ya makusanyo yaliyopokelewa na Mfuko hadi kufikia tarehe 30 Juni 2022. Vilevile, Wizara ya Fedha na Mipango ilitoa fedha kiasi Sh. bilioni 258.36 kwa taasisi saba zaidi ya bajeti iliyoidhinishwa, zaidi nilibaini Taasisi saba zilitumia jumla ya Sh. trilioni 1.46 nje ya bajeti iliyoidhinishwa.

(v) Usimamizi wa Mapato

Nilibaini jumla ya lita 3,293,306 za mafuta yenye kodi iliyotathminiwa ya Sh. bilioni 2.60 yaliyoagizwa kutoka nje ya nchi kwa utaratibu wa ghala la dhamana (Bonded warehouse) yakiwa yamebaki kwenye matanki ya Kampuni za uuzaji wa Mafuta kwa muda wa zaidi ya miezi sita bila kutolewa kwenda sehemu husika au kufanyiwa utaratibu wa kuuzwa ndani ya nchi.

Aidha, nilibaini kutokuwepo kwa mfumo wa kufuatilia matukio/malalamiko kutoka kwa watumiaji wa nje wa mifumo ya Mamlaka (yani walipakodi) kwenye mfumo wa kodi za forodha (TANCIS), Mfumo wa risiti za kielektroniki (EFDMS), Mfumo wa kielektroniki wa kuwasilisha ritani za kodi (e-filing) na Mfumo wa usajili wa walipakodi (TIN).Vilevile,kulikuwa na uchelewaji wa utatuzi wa matukio/malalamiko yaliyoripotiwa kwa watumiaji wa ndani wa mifumo ya Mamlaka.

Zaidi ya hayo, nilibaini kutofuatwa kwa sheria za kodi kwa walipakodi waliosajiliwa kama Wajumuishi (Consolidator) ambapo wanaunganisha mizigo ya wasafirishaji wadogo wanaoingiza bidhaa kwa kiasi kidogo kwenye kontena moja, kisha mjumuishi (consolidator) kutoa bidhaa hizo bandarini baada ya kulipa kodi, ushuru na tozo kwa kutumia utambulisho wa mlipa kodi (TIN) za mjumuishi mwenyewe, baada ya hapo hutoa risiti za kielekroniki (EFD) kwa wateja wao ambayo inajumuisha kodi, ada nyinginezo na kamisheni ya huduma. Hata hivyo ni kamisheni ya huduma pekee ndio inajumuishwa kwenye ritani ya kodi ya ongezeko la thamani (VAT) na taarifa za fedha ambapo ni tofauti na kiasi kinachooneka kwenye ankara/risiti iliyotolewa kwenye mashine ya kielektroniki ya kutolea risiti.

(vi) Usimamizi wa Makusanyo Yasiyotokana na Kodi

Ukaguzi ulibaini Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi haikukusanya ada ya ziada kiasi cha Sh. bilioni 41.4 iliyotozwa wakati wa kusafirisha Mizigo yenye uzito mzito iliyopewa kibali maalumu. Nilibaini kuwa Taasisi nne zilikusanya mapato ya kiasi cha Sh. bilioni 69.47 nje ya Mfumo wa Kielektroniki wa Serikali (GePG). Aidha nilibaini upotevu wa mapato ya Sh. milioni 919.6 uliofanywa na TEMESA kwa kukodisha mitambo na vifaa bila kuwa na makubaliano ya kimkataba na kutokusanywa kwa malipo yatokanayo na ukodishaji wa mitambo. Nilibaini kuwa Idara ya Zimamoto, Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) pamoja na Mahakama hazikutoza makusanyo ya Sh. bilioni 8.43 baada ya kutoa huduma, vilevile Wakala wa Majengo Tanzania ilishidwa kukusanya Sh. milioni 874.3 na kuchukua hatua dhidi ya wanunuzi wa nyumba za Serikali walioshindwa kulipa madai yao kwa wakati.

Tume ya TEHAMA ilikusanya Sh. milioni 786.44 kutoka katika vyanzo mbalimbali ikiwa ni pamoja na makusanyo ya ada za usajili na kitaaluma bila kuwa na kanuni zinazosimamia na kuhalalisha viwango vinavyotumika katika makusanyo.

(vii) Usimamizi wa Deni la Serikali

Deni la Serikali kufikia tarehe 30 Juni 2022 lilikuwa Sh. bilioni 71,312.42 (linajumuisha deni la ndani na nje Sh. bilioni 24,040.11 na Sh. bilioni 47,272.31 mtawalia) ikilinganishwa na Sh. bilioni 64,519.63 lililoripotiwa mwaka 2020/21. Ongezeko hilo limesababishwa na kushuka kwa thamani ya sarafu za wakopeshaji dhidi ya Shilingi na mikopo halisi (mapokezi ya mikopo mipya dhidi ya ulipaji wa mikopo).

Pia nilibaini kuwa, deni la Serikali ni himilivu. Uwiano wa thamani ya sasa ya deni la Serikali (deni la nje na deni la ndani) kwa Pato la Taifa (GDP) umebaki kuwa chini ya kiwango ukomo/elekezi. Hata hivyo, nilibaini kuwa vihatarishi vya deni la nje bado vipo kiwango cha wastani kama ilivyokuwa mwaka uliopita. Hii ilichangiwa na athari za janga la UVIKO-19, na uhafifu wa mauzo ya nje na kushuka kwa uchumi wa dunia kwa ujumla. Pia, nilibaini uwapo wa mikopo 8 yenye thamani ya shilingo bilioni 1,597 iliyosainiwa kati ya mwaka 1990 na 2017, lakini fedha zake hazikupokelewa hadi tarehe 30 Juni 2022.

Kadhalika nilibaini changamoto zinazofanana zinazoathiri utekelezaji mzuri wa miradi inayofadhiliwa na fedha za madeni. Mambo hayo ni pamoja na Ucheleweshaji wa uidhinishaji wa fedha kupitia mfumo wa fedha zinazopelekwa moja kwa moja kwenye miradi (D-Fund) katika ngazi zote, Kutotimizwa kwa wakati kwa masharti yanayotakiwa ili kuufanya mkopo uwe tayari kusainiwa na mkopeshaji kuanza kuleta fedha, Ucheleweshaji katika taratibu za manunuzi (Hii ni pamoja na kutoa notisi ya Serikali (GN) kwa miradi yenye msamaha wa kodi) na changamoto katika ulipaji fidia kwa watu walioathiriwa na mradi.

(viii) Usimamizi wa Matumizi

Wakati wa ukaguzi wangu, nilibaini mapungufu mbalimbali katika usimamizi wa matumizi uliofanywa na Taasisi za umma.

Nilibaini usimamizi usioridhisha wa fedha zilizotolewa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa ajili ya kupima, kupanga na kumilikisha ardhi – Sh. bilioni 26.03 kwa Halmashauri. Manispaa ya Shinyanga na Halmashauri za Wilaya ya Shinyanga zilitumia Sh. bilioni 2.35 katika shughuli zisizohusiana na kupima, kupanga na kumilikisha ardhi. Aidha, Halmashauri ya wilaya ya Musoma, Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga, Halmashauri ya Manispaa ya Tabora na Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara, ziliingiza mapato ya jumla ya Sh.bilioni 2.02. Hata hivyo, Halmashauri hizo hazikulipa mkopo wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na kutumia sehemu ya mapato hayo jumla ya Sh. bilioni 1.37 kwa ajili ya shughuli nyingine.

Vilevile, nilibaini ucheleweshaji wa kulipa mashauri ya kisheria yalisababisha kuzuiliwa kwa ndege ya Serikali na hatimaye Serikali kulipa dola za Marekani milioni 29.69 (Sawa na Sh. Bilioni 68.60.

Nilibaini, kuwa, taasisi 21 zilifanya malipo jumla ya kiasi cha Sh. bilioni 15.31 bila kudai risiti za Kielektroniki.

(ix) Usimamizi wa Rasilimali Watu, Mishahara na Mafao kwa Wastaafu

Katika ukaguzi wa Menejimenti ya Usimamizi wa Rasilimali Watu,Usimamizi wa Mishahara na Mafao ya Wastaafu, upungufu wa watumishi bado ni tatizo linaloendelea kama nilivyobainishwa katika ukaguzi wangu wa sasa ambapo nimebaini upungufu wa watumishi 16,525 katika Taasisi za Umma. Kama ilivyoelezwa kwenye Taarifa yangu mwaka uliopita, pia nimebaini taasisi 40 zilikuwa na watumishi 258 waliokaimu nafasi za juu kwa kipindi cha kati ya miezi 6 hadi 108 wakati muda unaohitajika ni mpaka miezi 6, nilibaini kutowasilishwa kwa makato ya kisheria ya Sh. bilioni 1.60 kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii na Taasisi nyingine za Serikali.

Aidha, nilibaini ucheleweshwaji kwenye uandaaji na uwasilishwaji wa majalada ya mafao 727 kwa ajili ya ukaguzi wa awali kwa kipindi cha kuanzia mwaka 1 hadi miaka 30. Ucheleweshwaji huo unaathiri hali ya maisha ya wastaafu au wategemezi kwani wengi wao hutegemea mafao ya kustaafu kama pato la kuendesha maisha yao baada ya kumaliza utumishi wa umma.

(x) Usimamizi wa Mali na Madeni

Nimekagua udhibiti na taratibu za mali na madeni na kubaini mupungufu yafuatayo; taasisi tano zina majengo yaliyoharibika ambayo hayatumiki; taasisi 37 hazina Mpango wa Matengenezo ya Mali. Taasisi nane zilinunua magari yenye thamani ya Sh. bilioni 3.39, ambayo bado hayajawasilishwa kwa muda mrefu; taasisi 58 zina mali zilizoharibika ambazo hazijauzwa au kufanyiwa matengenezo. Nimebaini kwamba taasisi 21 hazina hati miliki za ardhi zao ikilinganishwa na taasisi 32 zilizoripotiwa mwaka wa 2020/21 na Taasisi 16 hazikuanzisha mfumo wa serikali wa kurekodi na kudhibiti mali (unaojulikana kama GAMIS).

Nimebaini madeni ya wazabuni jumla ya Sh. trilioni 4.08 hadi tarehe 30 Juni 2022. Kuhusu madeni tarajiwa, nimeonyesha katika ripoti yangu uwepo wa

kesi za kisheria zenye madai ya jumla ya Sh. trilioni 3.833 katika taasisi 23, zikisubiria maamuzi ya Mahakama. Kiasi hicho kikubwa cha madai tarajiwa kinatisha iwapo maamuzi hayatapendelea taasisi husika.

(xi) Usimamizi wa Ununuzi na Mikataba

Nilifanya ukaguzi katika maeneo wa mchakato wa ununuzi wa kazi, bidhaa, na huduma katika Wizara, Wakala na Vitengo. Mapungufu yalioyobainishwa ni kama ifuatavyo;

Wizara ya Mambo ya Ndani ilinunua magari matatu ya injini za zimamoto yenye thamani ya Sh. bilioni 2.98 kutoka kwa mtengenezaji asiyeruhusiwa. Hata hivyo, malori hayo ya injini hizo za zimamoto yalikuwa bado hayajawasilishwa hadi kufikia wakati wa ukaguzi wangu Desemba 2022 (kupelekea ucheleweshwaji wa kipindi cha miezi 24) licha ya ukweli kwamba muuzaji alikuwa amelipwa kiasi cha Sh. bilioni 2.23 mnamo mwezi Februari 2021 kuwa asilimia 75 ya gharama zote na hakuna gharama za ucheleweshwaji zilizokatwa kulingana na matakwa ya Kanuni ya 243(5) (b) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma, 2013.

Tathmini yangu ilibaini kasoro mbalimbali katika ununuzi wa vishikwambi vipatavyo 300,000 vilivyofanywa na Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia kwa ajili ya zoezi la sensa ya watu na makazi. Kasoro hizo ni pamoja na kubadilisha vipimo vya kiufundi bila kuhusisha idara ya mtumiaji, chanzo kisichojulikana cha wazabuni, kushindwa kuanzisha makadirio ya bei ya soko, kutoa wazabuni siku mbili badala ya siku 14 kujibu hati ya zabuni, bodi ya zabuni kuidhinisha zabuni bila kukidhi akidi inayotakiwa na sheria, kutoa zabuni kwa muuzaji kabla ya kuidhinishwa na bodi ya zabuni na utoaji kwa mikataba ya Sh. bilioni 46.86 kwa muuzaji bila mkataba kuhakikiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Sambamba na hilo nilibaini kuwa, Msambazaji ambaye mkataba wake haukuhakikiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali alichelewa kusambaza vishikwambi ndani ya muda uliokubaliwa, pia muda wa nyongeza wa mkataba haukutafutwa na muuzaji na gharama za ucheweshwaji hazikutozwa na Wizara kinyume na masharti ya mkataba.

Taasisi nane zililipa jumla ya Sh. bilioni 6.10 (pamoja na VAT jumuishi) kwa ajili ya ununuzi wa bidhaa na huduma kwa kutumia njia moja ya ununuzi wa chanzo bila uhalali sahihi. Taasisi 22 zilinunua bidhaa na huduma kiasi cha

Sh. bilioni 13.27 bila kupata kibali cha awali kutoka Bodi ya Zabuni, jambo ambalo linakiuka kifungu cha 33 cha Sheria ya Ununuzi wa Umma, 2011.

Pia kulikuwa na ucheleweshaji wa utoaji wa bidhaa na huduma zenye thamani ya Sh. bilioni 18.75 kwa Taasisi 16 za Serikali kwa kipindi cha kuanzia wiki 5 hadi miezi 27 kinyume na muda uliokubaliwa.

Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA) ilifanya manunuzi madogo kuliko ukomo wa ununuzi ulioidhinishwa kwa kiasi cha Sh. 7.35 bilioni kinyume na kanuni ya 66(2) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma ya mwaka 2013.

Taasisi tano zilitekeleza miradi yenye thamani ya Sh. bilioni 151.03 kwa kutumia dhamana za benki za utendaji zilizoisha muda wake ambayo inaweza kusababisha upotevu wa fedha za umma endapo makandarasi watashindwa kufanya kazi.

Taasisi nane zilianza miradi yenye thamani ya Sh. bilioni 547.02 kabla ya kupata Hati ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii kutoka Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC) yenye thamani ya Sh. bilioni 547.02 kinyume na Sehemu ya 81 (3) ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004.

Kuhusu utekelezaji wa mradi wa ujenzi, nilibaini kuwa mkandarasi aliutelekeza mradi wenye thamani ya Sh. milioni 903.60 (Ujenzi wa Daraja la Mkombo). Pia, Wakala wa barabara (TANROADS) haijafidia Waathirika wa mradi wapatao 236 kwa kiasi cha Sh. bilioni 3.76 kinyume na Kanuni ya 13 (1-3) ya Ardhi (Tathmini ya Thamani ya Ardhi kwa Fidia) ya Kanuni za Ardhi za mwaka 2001, katika mradi wa ujenzi wa kituo kimoja cha ukaguzi katika eneo la Idofi katika Halmashauri ya Mji wa Makambato.

Nilibaini kuwa, Wizara ya Afya ililipa Sh. bilioni 10.75 kwa Shirika la UNICEF kwa ajili ya ununuzi wa magari ya wagonjwa (Ambulances) na pikipiki, huku muda wa utoaji huduma ukipangwa kuanzia mwishoni mwa Juni 2022 hadi mwishoni mwa Mwezi Agosti 2022. Pamoja na hayo, hadi ukaguzi uliofanyika Desemba 2022, magari hayo yalikuwa bado hayajawasilishwa.

Nilibaini kuchelewa kukamilika kwa miradi 26 ya ujenzi yenye thamani ya Sh. bilioni 197.36 katika Taasisi za Serikali kuanzia miezi 1 hadi miezi 96

kinyume na Kanuni ya 242 (2) ya Kanuni ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2013. Miradi iliyocheleweshwa zaidi ni Wakala wa Ujenzi Tanzania (miezi 96), Wakala wa Hifadhi ya Taifa ya Chakula (miezi 84) na Taasisi ya Maendeleo ya Jamii ya Tengeru (miezi 18).

Nilibaini kuwa, Taasisi 36 zilifanya manunuzi kiasi cha Sh. bilioni 46.15 nje ya Mfumo wa Ununuzi (TANePs). Pia, taasisi 9 zilifanya manunuzi madogo madogo kiasi cha Sh. bilioni 1.31 lakini hazikuripoti kila mwezi kwenye Bodi zao za Zabuni kulingana na matakwa ya Kanuni ya 166 (7) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma, 2013. Taasisi saba vilinunua bidhaa na huduma kiasi cha Sh. bilioni 2.72 ambazo hazikuwamo katika mipango ya manunuzi ya mwaka ya chombo husika.

(xii) Usimamizi wa Rasilimali Maji na Usambazaji Maji

Katika sura ya kumi, nimefafanua matokeo muhimu ya ukaguzi ya Taasisi mbalimbali zinazohusika na usimamizi wa maji nchini Tanzania kama ifuatavyo: Wizara ya Maji imebainika kuchepuka kutoka kwenye lengo la msingi la kupanga na kusimamia utekelezaji wa sera na mikakati; ukosefu wa miongozo ya uendeshaji katika utoaji leseni za uchunguzi na uchimbaji wa maji ardhini. Pia nilibaini kumalizika kwa mikataba ya ufadhili wa fedha yenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 112.68 ambayo ilisababisha kusitishwa kwa ujenzi wa mradi wa uboreshaji wa maji Same-Mwanga-Korogwe awamu ya kwanza wenye thamani ya Sh. bilioni 95.37, na kuchelewa kukamilika kwa mradi wa Mugango–Kiabakari-Butiama wenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 24.43 ukiwa nyuma kwa asilimia 24 dhidi ya lengo la kukamilika la asilimia 93 kufikia 28 Desemba 2022.

RUWASA ilibainika kuwa na miradi ya maji isiyo uendelevu yenye vituo 16,806 vya usambazaji maji visivyo na tija, uwepo wa visima 57 visivyo na tija, malimbikizo ya madai ya muda mrefu ya Sh. bilioni 1.9 na kuathiri uendeshaji wa sehemu ya uchimbaji visima, udhibiti na ufuatiliaji usioridhisha wa Vyombo vya Watoa Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii vilivyokusanya Sh. bilioni 68.2, ucheleweshaji wa huduma ya maji katika miradi 74 yenye thamani ya Sh. bilioni 76.1. Tathmini ya Mamlaka za Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira ilibaini kiwango cha juu cha upotevu wa maji na wateja wasiofungiwa mita hivyo kusababisha upotevu mkubwa wa mapato kiasi cha Sh. bilioni 9.32.

Bodi za Maji za Mabonde zilibainika kuwa na vibali vya matumizi ya maji vilivyokwisha muda wake ambavyo viliendelea kuchota maji yenye thamani ya Sh. bilioni 3.5, kutofungwa mita za jumla za mtiririko wa maji, shughuli za kibinadamu zenye athari mbaya katika uhifadhi wa vyanzo vya maji ndani ya mita sitini, na ukosefu wa programu za ukaguzi na udhibiti wa uchafuzi wa mazingira katika maeneo mbalimbali.

(xiii) Ukaguzi wa Wakala wa Serikali, Mifuko Maalumu na Taasisi Nyingine

Katika ukaguzi wa Wakala wa Majengo Tanzania (TBA), nilibaini kuwa TBA ililipa ROIL Dola za Marekani milioni 12.15 mnamo tarehe 12 Mei 2022, kugharamia madai yanayohusiana na uwekezaji wa jengo la Chimara. Malipo haya yalijumuisha deni halisi la Dola za Marekani milioni 6.60, riba ya Dola za Marekani milioni 5.21kwa kucheleweshwa kwa malipo, na kodi ya ongezeko la thamani ya Dola za Marekani 332,559. Hata hivyo, ni maoni yangu riba iliyotozwa kwa kuchelewa kwa malipo ya Dola za Marekani milioni 5.21 (Sh. Bilioni 11.99), imeweka mzigo mkubwa wa kifedha kwa walipa kodi.

Nilibaini pia kuwa Wakala wa Ndege wa Serikali (TGFA) iliipatia ATCL bili ya kukodi ndege na akiba ya matengenezo, yenye jumla ya Sh. bilioni 191.19 kwa kipindi cha kati ya mwaka 2016 hadi 2022. Hata hivyo, ATCL ililipa kiasi cha Sh. bilioni 3 na kiasi kilichobakia cha Sh. bilioni 188.19 hakikuwa kimelipwa mpaka tarehe 30 Juni 2022. Kutolipwa kwa malipo haya kunapelekea TGFA kushindwa kugharamia shughuli zake za kila siku na kushindwa kuhakikisha ATCL inafanya matengenezo makubwa kwenye Ndege 11 za Serikali.

TANROADS, nilibaini mapungufu kadhaa, ikiwemo hasara ya Sh. Sh. bilioni 7.24 iliyotokana na kurekebisha hitilafu za mapema za barabara katika barabara ya Ndundu – Somanga (Km 60), kutorejeshwa kwa malipo ya ziada kwa mkandarasi ya Sh. bilioni 1.39, Riba ya Sh. bilioni 36.86 Iliyotokana na kuchelewa kwa malipo ya wakandarasi na washauri katika miradi ya ujenzi ya barabara, kushindwa kutoa zabuni za miradi ya ujenzi ya barabara yenye jumla ya Sh. bilioni 2,914.11, matengenezo na uboreshaji wa barabara ambayo yako nje ya mamlaka ya TANROADS yenye jumla ya Sh. bilioni 10.74, na Magari 119,899 yalipita kwenye mizani bila kupimwa kutokana na usimamishaji wa shughuli za mizani mara kwa mara.

Vile vile, ukaguzi wangu wa PBPA umebaini mzabuni alitoza waingizaji mafuta jumla ya Dola za Marekani milioni 13.91 (Sh. Bilioni 32.07) kama ada ya uchelewaji wa ushushaji wa mafuta. Ada hizi kwa kawaida hujumuishwa katika ukomo wa bei za mafuta na hivyo kugharamikiwa na watumiaji wa mwisho. Pia, ada hii husababisha ongezeko lisilo la lazima la bei ya mafuta ambalo lingeweza kuepukwa.

Katika ukaguzi nilioufanya kwenye Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), nilibaini mambo mawili muhimu. Kwanza, NIDA ilishindwa kuzalisha Vitambulisho 7,188,098, na kushindwa kufikia malengo ya mpango ya kuzalisha vitambulisho 10,043,868 katika mwaka wa fedha 2021/22. Pili, NIDA ilitoa Nambari za Vitambulisho vya Taifa (NINs) kwa watu 15 ambao ama walikuwa na umri chini ya miaka 18, jambo ambalo ni kinyume na Kanuni ya 4(2) ya Kanuni ya Usajili na Utambulisho wa Watu, 2014.

Ukaguzi wangu wa Bodi ya Mfuko wa Barabara (RFB) ulibaini kuwa Wizara ya Fedha na Mipango ilihamisha tozo ya mafuta ya Sh. bilioni 330.33 moja kwa moja kwenda TARURA. Hata hivyo, Wizara ya Fedha na Mipango haina mamlaka ya kupeleka fedha hizo moja kwa moja kwa TARURA, na kitendo hicho kilikiuka Kifungu cha 5 (4) (g) cha Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta, ambacho kinaitaka RFB kuhamisha tozo ya mafuta kutoka kwenye akaunti ya Mfuko.

Kulingana na ukaguzi wangu wa shughuli za AGITF, niligundua kuwa AGITF ilifuta mikopo yenye thamani ya Sh. bilioni 19.49 kati ya mikopo chechefu. Hatua hii ilichukuliwa kwa sababu AGITF ilibaini kuwa haitawezekana kukomboa mikopo hii kutoka kwa wakopaji.

(xiv) Utendaji katika Uendeshaji wa Hospitali za Rufaa na Hospitali Maalumu

Katika sura ya kumi na mbili ya ripoti ya ukaguzi, mapungufu mbalimbali yalibainika kama ifuatavyo: Kutotolewa kwa huduma duni za rufaa katika Hospitali za Rufaa za Mikoa kutokana na upungufu wa wataalamu wa afya na vifaa maalumu. Fedha za hospitali zenye thamani ya Sh. bilioni 20.66 zinashikiliwa na Bohari Kuu ya Dawa licha ya kukosekana kwa dawa na vifaa tiba. Pia nimebaini upotevu kadhaa wa mapato, ikiwa ni pamoja na kukataliwa kwa madai ya bima yenye thamani ya Sh. Bilioni 7.8, hasara iliyopatikana kutokana na dawa zilizoisha muda wake zenye thamani ya Sh.

Bilioni 2.24 bilioni, na Sh. Milioni 703 katika misamaha inayotolewa kwa wagonjwa wasiostahili.

Aidha, nilibaini kuwapo kwa wataalamu wa afya 289 wanatoa huduma bila kuwa na leseni halali, ununuzi wa dawa na vifaa tiba vyenye thamani ya Sh.bilioni 1.75 bila ya uhakiki wa kutosha wa upatikanaji kutoka bohari Kuu ya Dawa, na malipo ya dawa na vifaa tiba ambavyo havikuwasilishwa, vyenye thamani ya Sh. bilioni 16.85 bilioni. Ukaguzi pia ulibaini kuwa vifaa tiba vyenye thamani ya Sh. bilioni 4.56 vilinunuliwa lakini havikutumika, na kulikuwa na ucheleweshaji wa ujenzi wa majengo ya Hospitali yenye thamani ya Sh. bilioni 74.15. Mwishowe nilibaini kuwapo kwa mtiririko wa taarifa zisizolingana kati ya GoT-HoMIS, Afyacare, na GePG ndani ya mamlaka ya hospitali hiyo.

(xv) Ukaguzi wa Ofisi za Balozi za Tanzania

Ukaguzi wa ofisi za balozi za Tanzania, ulibaini uwepo wa masuala yafuatayo: ushirikiano usioridhisha kutoka serikalini katika kuhamasisha fursa za uwekezaji na biashara zinazopatikana kutoka ofisi za balozi za Tanzania ikiwa ni pamoja na nchini China, Brazil, na Korea. Pia, kuna changamoto zinazokabili jumuiya ya watanzania waishio nje ya nchi katika kutekeleza majukumu yao. Kuhusu matumizi ya fedha, kulikuwa na ulipaji wa kodi ya majengo ya Sh. milioni 283.39 kwenye jengo lililotelekezwa katika ubalozi wa Tanzania mjini Washington. Aidha, kulikuwa na kodi ya ongezeko la thamani ya Sh. milioni 153.25 ambayo haikurudishwa baada ya kulipwa kwa ajili ya ukarabati wa majengo ya ubalozi wa Tanzania Stockholm. Pia, kodi ya ongezeko la thamani ya Sh. milioni 252.82 pia ililipwa kwenye kodi ya pango la ubalozi wa Tanzania mjini Moscow. Fedha za amana ambazo hazikurejeshwa mfuko mkuu zenye thamani ya Sh. milioni 880.8 zilitumika kwa matumizi yasiyohusika na vile vile malipo ya nje ya bajeti yaliyofanyika kwa kiwango cha Sh. milioni 161.94.

Aidha, kulikuwa na upungufu katika usimamizi wa mali, manunuzi na mikataba ikiwa ni pamoja na kuchelewesha utekelezaji wa mpango wa ukarabati na ujenzi wa majengo ya ofisi za balozi za Tanzania, mali zilizotelekezwa na chakavu, na kasoro katika utekelezaji wa mikataba ya ukarabati wa majengo ya ubalozi wa Tanzania nchini Msumbiji, na Ubelgiji. Kuhusu Msumbiji, ilibainika kuwa ukarabati wa jengo la Ubalozi ulichelewa kukamilika tangu tarehe 19 Februari 2013, huku mkandarasi akilipwa zaidi

ya kazi iliyofanyika kwa kiasi cha Dola za Kimarekani 482,090.87 sawa na Sh. bilioni 1.16. Nchini Ubelgiji, nilibaini kutokuwepo kwa mapitio ya mawanda ya kazi, ambayo yalisababisha nyongeza ya Euro 328,758.93 sawa na Sh. milioni 800, ambayo ni asilimia 48 ya mkataba wa awali. Aidha, hakukuwa na mkataba wa nyongeza hiyo ya mawanda ya kazi na kibali cha nyongeza hiyo kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali au Mamlaka ya Kuidhinisha Bajeti, kinyume na kanuni za manunuzi ya umma.

(xvi) Ukaguzi wa Vyama vya Siasa

Wakati wa ukaguzi wa vyama vya siasa, ilibainika kuwa makubaliano ya ubia baina ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Mbia katika ujenzi na uendeshaji wa mradi wa Darajani Corridor Commercial Bazaar uliopo visiwani Zanzibar hayakusimamiwa ipasavyo kutokana na kukosekana kwa msimamizi wa Mradi na taarifa za fedha za kuthibitisha usahihi wa mgao wa faida .

Aidha, vyama vya siasa tisa vilishindwa kukusanya mapato yaliyobajetiwa ya jumla ya Sh. bilioni 28.85 na vyama vya siasa saba vilitumia jumla ya kiasi cha Sh. milioni 40.42 kabla ya kuwekwa benki. Pia, CCM ilinunua vitu mbalimbali vyenye thamani ya Sh. milioni 58.60, ambavyo vimepitwa na wakati na havitumiki. Aidha,Chama cha Wananchi (CUF) kilikuwa na magari kumi na kangavuke (jenereta) mbili zenye thamani ya Sh. milioni 302.93 ambazo zimekaa kwa muda mrefu bila ya kutumika, kutengenezwa wala kuuzwa. Aidha, Bodi za Wadhamini za vyama vya CHADEMA, CUF na DP zilibainika kutokuwa na ufanisi katika kusimamia shughuli zao za vyama. Maelezo ya kina yanapatikana katika Sura ya 14 ya ripoti hii.

(xvii) Kaguzi Maalumu na Kaguzi za Kiuchunguzi

Katika mwaka huu wa fedha, Ofisi yangu imefanya kaguzi maalumu tatu. Mojawapo ya ukaguzi ulilenga kuchunguza usimamizi wa Mfuko wa Tuzo na Tozo na Mfuko wa Kufa na Kuzikana, ambayo yote inasimamiwa na Jeshi la Polisi Tanzania. Kaguzi zingine mbili zilifanyika katika Ofisi ya Taifa ya Mashtaka (NPS). Kaguzi hizi zililenga kuangalia taratibu za makubaliano ya Kukiri Kosa na taratibu na usimamizi wa mali zilizotaifishwa. Masuala yaliyogbainika wakati wa kaguzi hizi maalumu yamefafanuliwa hapa chini:

Ukaguzi Maalumu wa Mfuko wa Tuzo na Tozo na Mfuko wa Kufa na Kuzikana katika Jeshi la Polisi Tanzania

Uchunguzi wangu ulibaini matukio kadhaa ya usimamizi usioridhisha wa matumizi ya fedha za Mfuko wa Tuzo na Tozo na hivyo kusababisha ubadhirifu wa fedha za mfuko kiasi cha jumla ya Sh.bilioni 1.04. Aidha, uchunguzi ulibaini mapungufu makubwa katika utawala na usimamizi wa fedha za Mfuko wa Kufa na Kuzikana, uliosababisha ubadhirifu wa fedha za mfuko, kiasi cha jumla ya Sh. bilioni 4.84, ambapo kati ya kiasi hicho, Sh.bilioni 2.44 zilitumiwa vibaya na Jeshi la Polisi Tanzania Bara na kiasi cha Sh.bilioni 2.4 kilitumika vibaya Zanzibar. Maelezo zaidi kuhusu uchunguzi yanapatikana katika Sura ya 15 ya ripoti hii.

Ukaguzi Maalumu Kuhusu Usimamizi na Uendeshaji wa Mikataba ya Makubaliano ya Kukiri Kosa iliyosimamiwa na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka

Wakati wa ukaguzi maalumu, ilibainika kuwa washitakiwa wa makubaliano ya kukiri kosa hawajafanya malipo ya fidia yenye thamani ya Shilingi bilioni 170.61 kama ilivyokubalika katika makubaliano ya kukiri kosa na hukumu za Mahakama. Aidha, Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) alishindwa kukusanya ahadi hizo na hakuchukua hatua za kuwasilisha maombi ya kukamata mali kwa wale walioshindwa kutekeleza makubaliano ya ahadi. Aidha, iligundulika kuwa DPP alikusanya Silingi bilioni 10.16, ambazo hazikuwa na uhusiano na mchakato wa kesi za kukiri kosa.

Pia, ukaguzi ulibaini kuwa aliyekuwa Mkurugenzi wa Mashtaka na maafisa wake walikiuka taratibu za makubaliano ya kukiri kosa katika kukamata, kuendesha mashtaka, na kushughulikia kesi. Aidha, ukiukwaji huu unaonesha ukosefu wa uwazi katika zoezi la uandikishaji mikataba ya kukiri kosa, ambao unahitaji uchunguzi zaidi wa uwezekano wa uwepo wa ukiukwaji wa maadili na matumizi mabaya ya mamlaka. Maelezo zaidi yapo katika Sura ya 15 ya ripoti hii.

Ukaguzi Maalumu Kuhusu Taratibu za Utaifishaji Mali pamoja na Taratibu za Makabidhiano, Ugawaji na Usimamizi wa Mali zilizotaifishwa na Ofisi ya Taifa ya Mashitaka

Ukaguzi ulibaini kasoro katika taratibu za kufuatilia mali na fedha zilizotaifishwa, ikiwa ni pamoja na ukosefu wa daftari sahihi la kurekodi fedha na mali zilizotaifishwa. Kasoro hizi zilisababisha athari mbaya, kama

vile kupungua kwa thamani ya mali zilizotaifishwa na hasara ya kifedha kutokana na mali zilizosahaulika. Ukosefu wa taarifa za msingi za mali zilizotaifishwa baada ya uamuzi wa Mahakama, kunaonesha mapungufu katika usimamizi na ufuatiliaji wa mali zilizotaifishwa.

Aidha, ukaguzi ulibaini mapungufu katika usajili na umiliki wa magari yaliyotaifishwa na kutofanyika kwa tathmini ya mali zilizotaifishwa. Pia, kulikuwa na mashaka juu ya usimamizi sahihi wa fedha zilizotaifishwa kutokana na kushindwa kurejeshwa kwa kiasi kikubwa cha fedha zilizotaifishwa kutoka kwenye mabenki ya biashara yaliyopo ndani na nje ya nchi. Kwa ujumla, ukaguzi umebaini haja ya uwepo wa taratibu bora za ufuatiliaji na usimamizi wa mali na fedha zilizotaifishwa. Maelezo zaidi yapo katika Sura ya 15 ya ripoti hii.

NATIONAL AUDIT OFFICE
NAOT

MAELEZO YA AWALI

Ripoti hii inatoa matokeo na mapendekezo yaliyobainika wakati wa ukaguzi wa taasisi za Serikali Kuu kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2022.

Ripoti hii inajumuisha maeneo mbalimbali, ikiwa ni pamoja na hati za ukaguzi, utekelezaji wa mapendekezo ya miaka iliyopita, usimamizi wa vihatarishi, udhibiti wa mifumo ya ndani na utawala, maandalizi na utekelezaji wa bajeti, usimamizi wa mapato na matumizi, usimamizi wa rasilimali watu na utendaji kazi.

Malengo ya ukaguzi

Ukaguzi ulilenga kutoa hati iwapo taarifa za fedha zilitayarishwa kwa kuzingatia viwango vya uandaaji wa taarifa za fedha. Aidha, ukaguzi ulilenga kupitia na kutathmini ufuataji wa sheria za manunuzi pamoja na sheria ya bajeti, kanuni, na miongozo husika.

Mbinu ya ukaguzi

Ukaguzi ulifanywa kwa kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya Taasisi za Juu za Ukaguzi wa Serikali (ISSAI) vilivyotolewa na Shirika la Kimataifa la Taasisi za Juu za Ukaguzi wa Serikali (INTOSAI), pamoja na Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi (ISA).

Mbinu za ukaguzi zilijumuisha hatua mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kukagua nyaraka, kufanya mahojiano, kuchambua taarifa na kutembelea maeneo husika. Ukaguzi pia ulihusisha tathmini ya mifumo ya udhibiti wa ndani na kuangalia kama inazingatia sheria, kanuni, na sera husika.

Mawanda ya Ukaguzi

Ukaguzi ulijumuisha ukaguzi wa taarifa za fedha na utekelezaji wa sheria katika maeneo ya usimamizi wa mapato, usimamizi wa matumizi, usimamizi wa manunuzi na mikataba, mishahara na usimamizi wa rasilimali watu, na utendaji kazi. Aidha, ukaguzi ulijumuisha tathmini ya usimamizi wa vihatarishi, udhibiti wa mifumo ya ndani na utawala katika Wizara, Idara na Wakala za Serikali. Vilevile, ukaguzi ulihusisha ukaguzi wa awali wa mafao ya watumishi wa Serikali walioastaafu ambao mafao yao yanalipwa moja kwa moja kutoka kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali.

Nimetekeleza ukaguzi wa taasisi 338 zilizoko chini ya Serikali Kuu na nimeainisha matokeo yake kwenye ripoti hii. Idadi ya taasisi zilizokaguliwa

imeongezeka kutoka 331 katika mwaka wa fedha wa 2020/21 hadi 338 katika mwaka wa fedha wa 2021/22. Ongezeko hilo limechangiwa na taasisi 45 ambazo hazikuripotiwa mwaka wa fedha wa 2020/21, kama ilivyooneshwa katika **Jedwali Na. 1**. Aidha, kwa mwaka wa fedha uliomalizika taasisi tano[1] ziliunganishwa na taasisi nyingine. Vilevile, kuna taasisi 34 ambazo ziliripotiwa katika taarifa ya ukaguzi wa Serikali Kuu katika mwaka wa fedha wa 2020/21, lakini katika mwaka wa fedha wa 2021/22 zimeripotiwa katika taarifa ya Ukaguzi wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kama ilivyoelezwa katika **Jedwali Na. 2**.

Jedwali Na. 1: Taasisi Zilizojumuishwa Katika Ripoti hii Lakini Hazikuripotiwa katika Ripoti ya Mwaka wa Fedha 2020/2021

Na.	Taasisi	Aina
1.	Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara	Fungu
2.	Mfuko wa Ukimwi	Mfuko
3.	Mfuko wa Taifa katika Sekta ya Maji, Wizara ya Maji	Mfuko
4.	Mfuko wa Barabara - Wizarani	Mfuko
5.	Hospitali ya Kanda Mtwara	Hospitali
6.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Biharamulo	TN
7.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Handeni Busega	TN
8.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Handeni Chato	TN
9.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Chunya	TN
10.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Gairo	TN
11.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Itumba	TN
12.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kasulu	TN
13.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kibaya	TN
14.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kibondo Daraja C	TN
15.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kilindoni Daraja C	TN
16.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kilwa Masoko Daraja C	TN
17.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kiomboi Daraja C	TN
18.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kishapu Daraja C	TN
19.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kondoa Daraja C	TN
20.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Liwale Daraja C	TN


[1] Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira-Katesh iliyounganishwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira-Babati Mji, RUWASA-DS imeunganishwa na RUWASA-Makao Makuu, na Mamlaka ya Majisafi na usafi wa Mazingira-Handeni imeunganishwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira HTM Handeni. SAGCOT ilibadilishwa jina kuwa TACT, na Fungu namba 9 iliunganiswa na Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora

Na.	Taasisi	Aina
21.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Loliondo Daraja C	TN
22.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Ludewa Daraja C	TN
23.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Lushoto Daraja C	TN
24.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Maganzo Daraja C	TN
25.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mahenge Daraja C	TN
26.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Manyoni-Itigi Daraja C	TN
27.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbinga Daraja C	TN
28.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbulu Town Daraja C	TN
29.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mombo Daraja C	TN
30.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanhuzi Daraja C	TN
31.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Namanyere Daraja C	TN
32.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Namtumbo Daraja C	TN
33.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Rombo Daraja C	TN
34.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Rujewa Daraja C	TN
35.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Songe-Kilindi Daraja C	TN
36.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Turiani Daraja C	TN
37.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Ushirombo Daraja C	TN
38.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Utete DAraja C	TN
39.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Vwawa Daraja C	TN
40.	Mkataba wa Kugawana Uzalishaji wa Nishati (MEM-PSA) wa Wizara ya Nishati	TN
41.	SUMAJKT Kampuni ya Umeme	TN
42.	SUMAJKT Ushauri Elekezi	TN
43.	Kamati ya Kitaifa ya Kusimamia Fedha kutoka kwa Mfuko wa Dunia	TN
44.	Mradi wa kibiashara wa Afrika Mashariki	TN
45.	Mfuko wa Kuchochea Kilimo Tanzania	TN

Jedwali Na. 2: Taasisi ambazo Zilijumuishwa Katika Ripoti ya Serikali Kuu kwa mwaka 2020/21 Lakini Zimeripotiwa Katika Ripoti ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa mwaka 2021/2022

Na.	Taasisi	Aina
1.	Tume ya Utumishi wa Walimu	Fungu
2.	Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa	Fungu
3.	Sekretarieti ya Mkoa wa Katavi	Fungu
4.	Sekretarieti ya Mkoa wa Simiyu	Fungu
5.	Sekretarieti ya Mkoa wa Njombe	Fungu
6.	Sekretarieti ya Mkoa wa Geita	Fungu

Na.	Taasisi	Aina
7.	Sekretarieti ya Mkoa wa Arusha	Fungu
8.	Sekretarieti ya Mkoa wa Pwani	Fungu
9.	Sekretarieti ya Mkoa wa Dodoma	Fungu
10.	Sekretarieti ya Mkoa wa Iringa	Fungu
11.	Sekretarieti ya Mkoa wa Kigoma	Fungu
12.	Sekretarieti ya Mkoa wa Kilimanjaro	Fungu
13.	Sekretarieti ya Mkoa wa Lindi	Fungu
14.	Sekretarieti ya Mkoa wa Mara	Fungu
15.	Sekretarieti ya Mkoa wa Mbeya	Fungu
16.	Sekretarieti ya Mkoa wa Morogoro	Fungu
17.	Sekretarieti ya Mkoa wa Mtwara	Fungu
18.	Sekretarieti ya Mkoa wa Mwanza	Fungu
19.	Sekretarieti ya Mkoa wa Ruvuma	Fungu
20.	Sekretarieti ya Mkoa wa Shinyanga	Fungu
21.	Sekretarieti ya Mkoa wa Singida	Fungu
22.	Sekretarieti ya Mkoa wa Tabora	Fungu
23.	Sekretarieti ya Mkoa wa Tanga	Fungu
24.	Sekretarieti ya Mkoa wa Kagera	Fungu
25.	Sekretarieti ya Mkoa wa Dar es Salaam	Fungu
26.	Sekretarieti ya Mkoa wa Rukwa	Fungu
27.	Sekretarieti ya Mkoa wa Songwe	Fungu
28.	Sekretarieti ya Mkoa wa Manyara	Fungu
29.	Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka Dar es Salaam (DART)	Wakala
30.	Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA)	Wakala
31.	Mfuko wa Barabara (TAMISEMI)	Mfuko
32.	Jumuiya ya Tawala za Mitaa Tanzania (ALAT)	TN
33.	Bodi ya Mikopo Serikali za Mitaa (LGLB)	TN
34.	Kitengo cha Uchimbaji Visima-RUWASA	TN



SURA YA KWANZA

HATI ZA UKAGUZI

1.1 Utangulizi

Hati (Maoni) ya ukaguzi hupatikana kwa kuzingatia tathmini ya hitimisho inayotokana na ushahidi wa ukaguzi uliopatikana, kama taarifa za fedha kwa ujumla wake zimetayarishwa kwa kuzingatia viwango vya kimataifa vya uhasibu (kama vile IFRS au IPSAS). Hati ya ukaguzi hutolewa kwa mujibu wa kiwango cha Kimataifa cha Taasisi za Juu za Ukaguzi (ISSAI) 1700.

Hili linafanikiwa na kufikiwa kwa kuandaa na kufanya ukaguzi kwa namna ambayo itamuwezesha Mkaguzi kupata uhakika kuhusu tathmini ya matokeo dhidi ya kiwango cha juu kisichohimilika (Materiality) kilichowekwa.

1.2 Aina ya Hati za Ukaguzi

Kuna aina nne tofauti ya Hati za Ukaguzi:

Hati Inayoridhisha – Hati hii hutolewa pale Mkaguzi anaporidhika kuwa taarifa za fedha alizokagua zimetayarishwa kwa usahihi na kwa kuzingatia viwango kubalifu vya kimataifa vinavyohusu uandaaji wa taarifa za fedha.

Hati Yenye Shaka – Hati hii hutolewa pale taarifa za fedha zinapokuwa zimetayarishwa kwa usahihi isipokuwa:

- Pale ambapo Mkaguzi amepata ushahidi wa kutosha wakati wa ukaguzi, akahitimisha kuwa kulikuwa na dosari ama moja moja au kwa ujumla wake, ambazo ni kubwa lakini hazijaathiri sehemu kubwa ya taarifa za fedha; au

- Pale ambapo Mkaguzi ameshindwa kupata ushahidi wa kutosha kumwezesha kutoa maoni ya ukaguzi, lakini akahitimisha kwamba

dosari zilizotokana na kukosa ushahidi ni kubwa lakini hazijaathiri sehemu kubwa ya taarifa za fedha.

Hati Mbaya –Hati hii hutolewa pale ambapo Mkaguzi amepata ushahidi wa kutosha kuwa dosari ama moja moja au kwa ujumla zilizobainika wakati wa ukaguzi ni kubwa na zimeathiri sehemu kubwa ya taarifa za fedha hivyo kupelekea taarifa hizo kutokuwa sahihi.

Kushindwa kutoa Maoni –Hali hii hutokea pale mkaguzi anaposhindwa kupata ushahidi wa kutosha utakaomuwezesha kutoa maoni ya ukaguzi; Mkaguzi atahitimisha kwamba athari zinazoweza kutokea za dosari zisizogundulika za taarifa za fedha, zinaweza kuwa kubwa na zinaweza kuathiri sehemu kubwa ya taarifa za fedha. Mkaguzi atashindwa kutoa maoni, katika mazingira nadra sana yaliyohusisha mashaka kwa kiasi kikubwa, atahitimisha kwamba, ingawa amepata ushahidi wa kutosha wa ukaguzi kuhusu kila shaka, haitowezekana kutoa maoni juu ya taarifa za fedha kwa sababu ya mwingiliano wa hayo mashaka na athari zake kwenye taarifa za fedha.

1.3 Aya ya Masuala Yenye Msisitizo

Aya hii hutolewa pale ambapo nimeona kuwa, kuna umuhimu wa kuwaarifu watumiaji wa taarifa za fedha husika kuhusu suala ambalo limeoneshwa kwenye taarifa za fedha, na ambalo limeonekana kuwa muhimu na la msingi kwa ajili ya kuleta uelewa wa taarifa hizo, nitaijumuisha Aya ya Masuala yenye Msisitizo katika ripoti yangu, endapo nitakua nimepata vielelezo vya kutosha kuwa suala hilo halina dosari kubwa katika taarifa za fedha. Aya hiyo inarejelea tu kwa suala lililooneshwa kwenye taarifa za fedha.

1.4 Aya ya Masuala Muhimu ya Ukaguzi

Aya hii inatoa maelezo ya ziada kwa watumiaji wa taarifa za fedha ili kuwasaidia kuelewa masuala hayo ambayo, kwa maoni ya kiweledi ya mkaguzi, yalikuwa na umuhimu mkubwa katika ukaguzi wa taarifa za fedha za taasisi husika.Kuwasilisha masuala muhimu ya ukaguzi huongeza ubora wa taarifa za fedha kutokana na uwazi uliotokana na ukaguzi uliofanyika.

1.5 Hati za Ukaguzi Zilizotolewa kwa Mwaka wa Fedha 2021/22

Katika mwaka wa fedha 2021/22, Nilikamilisha ukaguzi wa taasisi 338 za Serikali Kuu. Kati ya taasisi 338, 323 zilitolewa hati zinazoridhisha, 10 zilitolewa hati zenye Shaka, mbili zilitolewa hati Mbaya, nilishindwa kutoa maoni kwa taasisi moja, huku taasisi mbili[2] hazikuandaa taarifa za fedha hivyo sikutoa hati kwa taasisi hizo. Orodha ya Taasisi zilizokaguliwa pamoja na hati za ukaguzi zilizotolewa zimeoneshwa katika **Kiambatisho Na. I**.

Sababu zilizopelekea kutolewa kwa hati zenye shaka, hati mbaya na kushindwa kutoa maoni zimeoneshwa kwenye **Kiambatisho Na. II**, **Kiambatisho Na. III**, na **Kiambatisho Na. IV** mtawalia.

1.6 Mwenendo wa Hati za Ukaguzi

Mwenendo wa Hati za Ukaguzi zilizotolewa kwa Taasisi za Serikali Kuu kwa kipindi cha miaka mitano toka mwaka 2017/18 mpaka 2021/22 unaoneshwa katika **Jedwali Na. 3**.

Jedwali Na. 3: Mwenendo wa Hati za Ukaguzi

Aina ya Hati	2017/18	2018/19	2019/20	2020/21	2021/22
Inayoridhisha	197	253	278	315	323
Yenye Shaka	9	24	12	5	10
Mbaya	2	5	2	5	2
Kushindwa Kutoa Maoni	6	12	9	2	1
Jumla	**214**	**294**	**301**	**327**	**336**

Chanzo: *Uchambuzi wa Taarifa za Fedha Zilizokaguliwa*

1.7 Ripoti Inayohusu Uzingatiwaji wa Sheria na Kanuni za Ununuzi wa Umma

Pamoja na ukaguzi wa hesabu, nilifanya pia tathmini ya uzingatiaji wa sheria na kanuni za ununuzi wa umma pamoja na ufanisi wa mifumo ya udhibiti wa ndani kama Kiwango cha Kimataifa cha Taasisi za Juu za Ukaguzi (ISSAI) Na. 4200 kinavyoelekeza. Pia, Kifungu Na. 48(3) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma Na.7 ya mwaka 2011 kinanitaka kueleza katika ripoti

[2] Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo na Mfuko Mkuu wa Serikali

yangu ya ukaguzi ya kila mwaka kama taasisi niliyoikagua imezingatia matakwa ya sheria ya ununuzi wa umma na kanuni zake.

Hivyo, kulingana na ukaguzi nilioufanya kwa mwaka wa fedha 2021/22, nilibaini mapungufu katika kuzingatia sheria na kanuni za ununuzi wa umma kwa taasisi 167 za Serikali kuu zilikua na mapungufu katika uzingatiaji wa sheria na kanuni za ununuzi wa umma. Idadi ya taasisi zenye mapungufu zimeoneshwa katika **Kiambatisho Na. V**. Aidha,Sura ya Tisa ya ripoti hii inatoa maelezo ya mapungufu yaliyotokana na kutofuatwa kwa Sheria na Kanuni za Ununuzi wa Umma.



SURA YA PILI

UFUATILIAJI WA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA MIAKA ILIYOPITA

2.1 Utangulizi

Kupitia sura hii, nimetoa muhtasari wa hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi niliyoyatoa kwa menejimenti na wale wanaohusika na usimamiaji Utawala Bora Katika eneo la Serikali Kuu , pamoja na hatua zilizochukuliwa na Maafisa Masuuli husika katika kujibu na kutekeleza mapendekezo hayo.

Katika kutekeleza majukumu yangu, nilifanya mapitio ya ufuatiliaji wa mapendekezo ya ukaguzi yanayohusu miaka ya fedha iliyopita ili kutoa tathmini inayoonesha jinsi Maafisa Masuuli walivyochukua hatua za kurekebisha mapungufu yaliyoibuliwa kupitia utekelezaji wa mapendekezo hayo ya miaka ya nyuma.

Madhumuni ya mapitio haya na ufuatiliaji wake ni kuhakikisha kuwa hatua za urekebishaji zilizochukuliwa na Maafisa Masuuli zinakuwa na ufanisi katika kushughulikia masuala yaliyoibuliwa katika ukaguzi wa miaka ya nyuma, na kuwapa wananchi na wadau wengine uhakika kuhusu mapendekezo yaliyotolewa yametekelezwa kikamilifu. Aidha, nathamini na kuendelea kushukuru jitihada zinazofanywa na Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) na Maafisa Masuuli katika kujibu hoja za ukaguzi katika ripoti zangu na kutoa mipango kazi ya utekelezaji wa mapendekezo hayo.

2.2 Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi wa Miaka iliyopita kwenye Ripoti Kuu za Mwaka za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

Kifungu cha 40 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura ya 418 kinanitaka kujumuisha hali ya utekelezaji wa mpango kazi uliotayarishwa na Maafisa Masuuli na kuunganishwa na Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) katika Ripoti ya Mwaka ya Ukaguzi. Kwa kuzingatia sheria hiyo tajwa, Serikali kupitia Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) iliwasilisha kwangu majibu yanayohusu mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti yangu ya mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2021. Kwa mwaka huo nilitoa mapendekezo 246 yakiwemo mapendekezo 21 ya ukaguzi maalum ambapo Mlipaji Mkuu wa Serikali alijibu mapendekezo yote 246 kupitia majibu ya Julai, 2022. Kati ya mapendekezo 246 yaliyojibiwa, 10 (4%) yametekelezwa, 192 (78%) utekelezaji unaendelea, 8 (3%) hayajatekelezwa, 34 (14%) yalirudiwa na mapendekezo 2 (1%) yalifutwa kutokana na kupitwa na wakati.

2.3 Hali ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi wa Miaka Iliyopita Yaliyotolewa kupitia Ripoti za Ukaguzi wa Taasisi za Serikali Kuu.

Kanuni ya 38 ya Kanuni za Ukaguzi wa Umma za mwaka 2009 inamtaka kuwa waziri mwenye dhamana, kwa kadri itakavyokuwa, atawasilisha majibu kwa maandishi kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ndani ya kipindi cha miezi mitatu tangu tarehe ya kupokea mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kuandaa mpango kazi unaoeleza ni kwa kiasi gani, mapendekezo yaliyotolewa yametekelezwa.

Kama ilivyoainishwa katika Kifungu cha 40 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura ya 418 ya sheria, ni wajibu wangu kujumuisha katika Ripoti ya Mwaka ya Ukaguzi hali ya utekelezaji wa mpango kazi uliotayarishwa na Maafisa Masuuli na kuunganishwa na Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG).

Sharti hili linalenga kuhakikisha kuwa maendeleo yaliyofikiwa katika kushughulikia masuala yaliyoainishwa katika ukaguzi uliopita yanatolewa taarifa kwa usahihi na kuhakikisha kuwa mapendekezo yanatekelezwa ipasavyo. Hivyo, sura hii inatoa muhtasari wa hali ya utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa kupitia ukaguzi wa miaka iliyopita ya fedha na

kuonesha kwa kina hatua zilizochukuliwa na Maafisa Masuuli husika katika kushughulikia mapendekezo haya.

Katika mwaka huu wa ukaguzi, nilifuatilia utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi wa mwaka uliopita katika taasisi zipatazo 338 za Serikali Kuu zilizokuwa na jumla ya mapendekezo 6947.

Aidha, tathmini iliyofanyika inaonesha kuwa; kufikia tarehe 30 Juni 2022, kulikuwa na jumla ya mapendekezo 6947 ya ukaguzi ambayo yalikuwa bado kutekelezwa. Kati ya hayo mapendekezo 6947, 2380 (34%) yalitekelezwa kikamilifu, 2506 (36%) utekelezaji unaendelea, 1104 (16%) hayajatekelezwa, 320 (5%) yalifutwa kutokana na kupitwa na wakati na mapendekezo 637 (9%) yalirudiwa. Wakati hali ya jumla ya utekelezaji inaonyesha kuboreka kidogo ikilinganishwa na miaka ya nyuma. Maelezo ya Hali ya Utekelezaji wa mapendekezo hayo yanaoneshwa kwenye **Jedwali Na. 4.**

Jedwali Na. 4: Uwasilishaji wa Hali ya Utekelezaji wa Mapendekezo kwenye Ripoti za Mwaka

Mwaka wa Fedha	Mapendekezo yaliyotekelezwa	Utekelezaji unaendelea	Mapendekezo hayajatekelezwa	Mapendekezo yamerudiwa	Mapendekezo yamefutwa kutokana na kupitwa na wakati	Jumla
2017/18	1474	1588	1080	286	308	4736
2018/19	1508	2003	1211	259	502	5483
2019/20	2308	2441	1257	621	333	6960
2020/21	5290	6032	3548	1166	1143	17179
2021/22	2380	2506	1104	637	320	6947

Chanzo: *Ripoti za Taasisi za Serikali mwaka 2021/22*

Hivyo, ni muhimu kuendelea kufuatilia na kutathmini maendeleo yaliyofikiwa katika utekelezaji wa mapendekezo ambayo hayajakamilika na kuchukua hatua za kurekebisha inapobidi.

2.4 Kufuatilia Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) ndicho chombo cha juu zaidi cha uangalizi kwa Wizara, Idara na Wakala wa Serikali Kuu (MDAs), kwa mujibu wa Kanuni ya 14 ya jedwali la 8 la Kanuni za Kudumu za Bunge, toleo lililorekebishwa la Juni 2020. Majukumu ya Kamati yameelezwa kwa undani chini ya kanuni ya 14 ya toleo la nane la Kanuni za Kudumu za Bunge. Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ni taarifa muhimu kwa Kamati.


Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali kwa jinsi wanavyotekeleza majukumu yao. Mchango wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali katika kuhakikisha kunakuwepo na uwazi na uwajibikaji katika matumizi ya fedha za serikali ni muhimu sana. Hii hufanyika kwa kuchunguza kwa makini mapendekezo ya ukaguzi, Kamati kwa umahiri mkubwa imekuwa ikitoa maagizo muhimu kwa wahusika kuhusu umuhimu wa ufanisi wa matumizi ya rasilimali za umma. Maagizo yao ya uboreshaji yamekuwa na tija na muhimu katika kuhakikisha kuwa fedha za walipa kodi zinatumika ipasavyo na kwa njia ya kuwajibika na yenye manufaa makubwa kadiri iwezekanavyo.

Aidha, jukumu la Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali katika kukuza uwepo wa utawala bora na uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma ni muhimu sana. Juhudi za Kamati za mara kwa mara zinazotumika katika usimamizi wa rasilimali za umma, pamoja na Maagizo yao kwa serikali yana mchango mkubwa hasa katika kufanya maamuzi ya utungaji wa sera. Aidha,tunayo bahati ya kuwa na timu ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali inayofanya kazi kwa umakini ya kudumisha uadilifu wa matumizi ya fedha za umma na kuhakikisha kuwa uwajibikaji wa serikali unasalia kuwa kipaumbele cha kwanza cha majukumu yao.

Tathmini yangu kuhusu hali ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali hadi mwaka wa fedha 2021/22 imebaini kuwa; kati ya maagizo 172 ya PAC yaliyotolewa kutoka katika ripoti zangu za miaka iliyopita, 35 (20%) yalitekelezwa kikamilifu, 113 (65%) utekelezaji unaendelea, 22 (13%) hayakutekelezwa huku agizo 1 (1%) lilirudiwa na 1 (1%) lilifutwa kutokana na kupitwa na wakati.

Aidha, ufuatiliaji usioridhisha na ucheleweshaji wa utekelezaji wa mapendekezo yangu ya ukaguzi na maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali inatoa taswira kuwa kasoro zilizobainika na kutolewa mapendekezo ya uboreshaji hazijashughulikiwa ipasavyo na hivyo, kuwa na uwezekano wa kuendelea kuziweka taasisi husika kwenye hatari ya udanganyifu na ukosefu wa ufanisi katika uendeshaji wa taasisi husika.

Nilipendekeza na naendelea kusisitiza kuwa Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) kwa kushirikiana na Maafisa Masuuli kuweka juhudi zaidi katika kutekeleza kikamilifu mapendekezo ya ukaguzi na maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali ili kuboresha utendaji wa Taasisi kwa kushughulikia vyanzo vinavyohusiana na hivyo ili kupunguza au kuondoa isitokee siku za baadaye.



SURA YA TATU

TATHMINI YA UFANISI WA KIUTENDAJI, UDHIBITI WA NDANI, USIMAMIZI WA VIHATARISHI NA UTAWALA

3.1 Utangulizi

Katika sura hii, ninawasilisha matokeo ya ukaguzi wangu wa taasisi za Serikali Kuu kuhusu ufanisi wa kiutendaji, udhibiti wa mifumo ya ndani, usimamizi wa vihatarishi, na utawala bora. Vipengele mahususi nilivyokagua ni utendaji wa kazi, utendaji wa kamati za ukaguzi, kazi za ukaguzi wa ndani, michakato ya tathmini ya vihatarishi, kuzuia udanganyifu na udhibiti, na masuala ya utawala bora.

3.2 Ufanisi wa Kiutendaji

Kwa muhtasari, ufanisi wa kiutendaji katika taasisi za serikali ni uwezo wa kutoa huduma kwa ubora na ufasaha huku zikiboresha matumizi ya rasilimali. Ni muhimu kutoa huduma bora, kupunguza gharama, kuboresha uwajibikaji na uwazi, na wananchi kufurahia huduma.Ili kufikia ufanisi wa kiutendaji, kunahitajika mambo yafuatayo: matumizi ya matumizi ya teknolojia, uboreshaji wa mchakato, usimamizi wa nguvu kazi, uamuzi unaotokana na taarifa, uboreshaji endelevu, uvumbuzi, ushirikiano, uongozi thabiti, na mipango ya kimkakati. Lengo kuu ni kuboresha maisha ya wananchi kwa kutoa huduma bora za Umma kwa wakati, gharama nafuu, na uwazi.

Baada ya kukagua utendaji kazi wa Wizara na Idara, zilibainika dosari mbalimbali zinazokwamisha uwezo wa taasisi hizo kutoa huduma kwa ufanisi. Baadhi ya kasoro hizi ni ukosefu wa ufanisi katika michakato, matumizi duni ya rasilimali, na ucheleweshaji wa utoaji huduma. Zifuatazo ni kasoro zilizobainika:

3.2.1 Usimamizi Usioridhisha wa Utoaji wa Stika za Usalama Barabarani kwa Wamiliki wa Magari

Baraza la Taifa la Usalama Barabarani lilipata mapato ya Sh. milioni 440.59 kutokana na mauzo ya stika za usalama barabarani kati ya tarehe 1 Julai 2021 na 30 Juni 2022 kwa mujibu wa taarifa ya hesabu ya makusanyo na matumizi ya tarehe 30 Juni 2022 ambayo haikukaguliwa. Baraza la Taifa la Usalama Barabarani lilikusanya mapato hayo kupitia viwango vyake vilivyowekwa vya kutoa stika, ambavyo vilikuwa Sh. 2,000 kwa pikipiki, Sh. 5,000 kwa magari binafsi na Sh. 7,000 kwa magari ya biashara. Hata hivyo, katika ukaguzi wangu wa utoaji wa stika hizo za usalama kwa wamiliki wa magari, nilibaini dosari kadhaa zinazohitaji utatuzi wa haraka, kama ilivyoainishwa hapa chini:

- Baraza la Taifa la Usalama Barabarani lilitoa stika za usalama barabarani kwa wananchi bila kufanya ukaguzi wa magari na pikipiki husika. Hatua hii ni kinyume na Kanuni ya 15 (2) ya Kanuni za Udhibiti wa Usafiri wa Barabarani za mwaka 2015, ambazo zinawaagiza wakaguzi wa magari baada ya uchunguzi wa kina wa gari hilo kutoa hati ya usalama barabarani.

- Stika za usalama barabarani hazikuhifadhiwa kwenye mfumo wa utambuzi wa kielektroniki, hivyo kusababisha kushindwa kuhakiki uhalisi wake kwa kuhakikiwa na polisi.

- Baraza la Taifa la Usalama Barabarani lilikusanya ada za ukaguzi kutokana na mauzo ya stika za usalama barabarani zenye thamani ya Sh. milioni 440.59 kwa fedha taslimu, kinyume na matakwa ya Kifungu cha 7(2) cha Sheria ya Fedha za Umma (Sura ya 348 Toleo la mwaka 2020). Kifungu hiki kinamtaka Afisa Masuuli kuhakikisha kuwa fedha zote za Umma zinakusanywa kupitia Mfumo wa Serikali wa Malipo kwa njia ya Kielektroniki (GePG).

- Pia, nilibaini kuwa menejimenti ya Baraza haikuandaa taarifa za fedha kwa kipindi kilichoishia tarehe 30 Juni 2022. Hii ni kinyume na Kifungu cha 30 (3) cha Sheria ya Fedha za Umma (Sura ya 348 Toleo la mwaka 2020) inayotaka afisa yeyote wa Umma anayesimamia wakala, amana au mfuko mwingine wowote au akaunti ambayo haijatolewa katika

kifungu hiki, kuandaa, kusaini na kuwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali taarifa za jumla za fedha kwa mujibu wa viwango vya kimataifa vya uhasibu na miongozo iliyotolewa na Mhasibu Mkuu.

Kwa maoni yangu, dosari zilizobainika katika utoaji wa stika za usalama barabarani zinaweza kuchangiwa zaidi na kutokuwapo kwa mifumo na taratibu madhubuti, pamoja na kutokuwapo kwa taratibu za uangalizi wa kuhakikisha usalama barabarani. Makosa haya yanaweza kuhatarisha usalama wa watumiaji wa barabara na kuongeza hatari ya ajali na vifo, kwa kuwa stika za usalama barabarani zilitolewa bila ukaguzi unaostahili. Zaidi ya hayo, kutokuwepo kwa mifumo ya uthibitishaji wa kielektroniki kunawezesha ulaghai, kwani stika zisizo halali zinaweza kutengenezwa na kutumiwa bila kubainika.

Ninapendekeza Baraza la Taifa la Usalama Barabarani kuanzisha mfumo wa uthibitishaji wa kielektroniki, kuimarisha taratibu za ukaguzi wa magari, na kukusanya tozo za ukaguzi kupitia Mfumo wa Serikali wa Malipo kwa njia ya Kielektroniki (GePG). Aidha, napendekeza vyombo vya upelelezi kufanya uchunguzi wa kina juu ya dosari zilizojitokeza katika utoaji wa stika za usalama barabarani na kuchukua hatua stahiki kwa watumishi watakaobainika kukiuka sheria. Pia, Baraza linapaswa kuandaa taarifa za fedha na kuziwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa ukaguzi kama inavyotakiwa na Sheria ya Fedha za Umma.

3.2.2 Utendaji Usioridhisha wa Viwanja vya Benjamin Mkapa na Uhuru

Kifungu cha 14 cha Muongozo wa Usimamizi wa Mali za Umma wa mwaka 2019, Afisa Masuuli atahakikisha kuwa mpango wa matengenezo unaandaliwa na kufuatwa kwa mali zote za Taasisi. Ili kuhakikisha kuwa mali zinabaki na ubora wake, ili ziwezeshe kutoa huduma na kuleta mafanikio ya kiuchumi. Kila Mkuu wa Kitengo anapaswa kuandaa mpango wa matengenezo na kutoa ripoti ya utekelezaji wake kwa Afisa Masuuli kila robo mwaka, na kuhifadhi rejista ya matengenezo ya mali.

Eneo la michezo la Changamani ni eneo linalosimamiwa na Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo. Wizara ina viwanja vitatu vya michezo

ambavyo ni Benjamin Mkapa, Uhuru na eneo lina uwanja wa ndani. Kuna wafanyakazi 24 waliopo Benjamin Mkapa na Uhuru Stadium, ambapo 19 kati yao wana ujuzi mbalimbali ikiwa ni pamoja na kilimo, michezo, umeme, ujenzi, maji, afya, mawasiliano ya habari na wafanyakazi 5 ni kwa ajili ya rasilimali watu na utawala. Uwanja wa Benjamin Mkapa ni uwanja wa michezo wa kisasa wenye uwezo wa viti vya michezo 60,000 na Uwanja wa Uhuru una uwezo wa viti vya michezo 20,000.

Ujenzi wa Uwanja wa Benjamin Mkapa ulikamilika mwaka 2007 na kuanza kufanya kazi tangu mwaka huo, wakati Uwanja wa Uhuru ulijengwa mwaka 1959 na kukamilika mwaka 1960. Matengenezo makubwa yalifanywa mwaka 2016.

Hata hivyo, nimebaini mapungufu kadhaa kuhusiana na utendaji wa viwanja ambayo yanahitaji usimamizi wa menejimenti;

- **Miundombinu na vifaa duni**, viti vimevunjika na havijarekebishwa, hii inaweza kuwakatisha tamaa mashabiki kuhudhuria mechi na inaweza kuathiri mapato. Pia, nimebaini hali isiyoridhisha kuhusu miundombinu ya choo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.
- **Matengenezo Yasiyotosheleza**, uangalizi duni wa uwanja kutokana na kutokuwepo kwa mpango wa matengenezo wa mali ambao umesababisha usalama kuwa mdogo kwasababu viyoyozi havifanyi kazi vizuri. Usambazaji wa maji na mfumo wa usafi haukufanya kazi kwa njia inayoridhisha.
- **Mapungufu katika Usalama Uwanjani**, taratibu za kiusalama hazifanyi kazi kwani mfumo wa utambuaji wa moto na mfumo wa tahadhari (alarm system) haufanyi kazi katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, wakati mfumo wa kuzima moto kwa maji haufanyi kazi kwa uwanja wa Uhuru.

Nilibaini kuwa mapungufu haya ya utendaji katika viwanja vya mpira unatokana na matengenezo yasiyotosheleza, usimamizi duni, na ukosefu wa fedha za kutosha kwa ajili ya matengenezo.

Ninaamini kuwa utendaji usioridhisha wa viwanja vya mpira unaweza kuwa na athari kubwa kwenye mapato, ushiriki wa mashabiki, na utendaji wa timu. Ni muhimu kuchukua hatua za kushughulikia kwa kutekeleza

mapendekezo sahihi ili kuweza kusaidia kuboresha ufanisi wa viwanja na kuhakikisha vinadumu kwa muda mrefu.

Ninapendekeza Menejimenti ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kuweka mpango wa matengenezo na kufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa usalama ili kuboresha usalama wa viwanja, ili kuvifanya vidumu miaka mingi na kuokoa upotevu wa mapato.

3.2.3 Dosari Zilizobainika katika Usimamizi wa Mashine za Kielektroniki za Kukusanyia Mapato (POS) kwa Mapato Sh. Bilioni 4.11

Kifungu cha 6.5 cha Mwongozo wa Usimamizi wa Mali za Umma wa mwaka 2019 kinaainisha majukumu ya Mkuu wa Kitengo cha Usimamizi wa Ununuzi, ambayo ni pamoja na kumshauri Afisa Masuuli kuhusu masuala ya manunuzi, kununua mali kwa mujibu wa Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2011, kuhuisha daftari la mali wakati wa kupokea na kugawanya mali, kuhakikisha mali zinapokelewa katika hali nzuri, na kuweka namba za utambulisho baada ya ununuzi.

Kwa mujibu wa taarifa za fedha za mwaka ulioishia 30 Juni 2022, Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA) walikusanya jumla ya Sh. bilioni 16.32 kutokana na shughuli za vivuko, ambapo Sh. bilioni 4.11 zilikusanywa kwa kutumia mashine za POS. Ukaguzi huo, ulibaini kasoro katika usimamizi wa mashine za POS katika vituo mbalimbali vya TEMESA, na umakini wa haraka unahitajika katika maeneo hayo. Yafuatayo ni maelezo ya kasoro hizo:

i. Kutotunza rejista ya mashine za POS

Nilibaini kuwa Ofisi ya Makao Makuu ya TEMESA ilinunua mashine 71 za POS na kupelekwa katika vituo mbalimbali vya kukusanya mapato, ikiwamo vituo vya feri. Kituo cha kivuko cha Kigongo Busisi kilipelekewa mashine 43 za POS na TEMESA. Hata hivyo, makao makuu ya TEMESA na Kituo cha Kivuko Kigongo – Busisi hazikutunza rejista za POS, kinyume na matakwa ya Kifungu cha 6.5 (ii) cha Mwongozo wa Usimamizi wa Mali za Umma wa mwaka 2019.

ii. Mashine za POS kutokuunganishwa na seva kuu

Nilibaini kuwa mashine za POS katika vituo vyote vya ukusanyaji mapato vya TEMESA hazijaunganishwa na kanzidata kuu. Hii ina maana kuwa takwimu za mapato haziwekwi katika seva moja. Badala yake, kila mashine ya POS hutumiwa kwa namna ya kujitegemea. Kwa hiyo mashine ikipata hitilafu, takwimu za mapato hupotea na haziwezi kufuatiliwa.

iii. Kukosekana kwa mashine 52 za POS

Nilithibitisha kutoka kwa menejimenti kuwa mashine 68 za POS zilizopelekwa na Makao Makuu ya TEMESA kwenda vivuko vinavyofanya kazi Ziwa Viktoria, Kisorya – Rugezi, Bugorola – Ukara, Kayenze – Bezi - Bukimwi, Irunda - Luchelele -Tafico na Pangani – Bweni. Hata hivyo, ni mashine 16 tu za POS zilipatikana katika vituo vya vivuko vilivyotajwa. Kwa hiyo mashine 52 zilizobaki za POS hazikuonekana, si Makao Makuu ya TEMESA wala TEMESA Kanda ya Ziwa na vivuko vingine viliweza kutoa ufafanuzi wa kukosekana kwa mashine hizo.

iv. Kutokufanyiwa usuluhisho wa Makusanyo yaliyokusanywa na mashine za POS katika kivuko cha MV Kilindoni

Pia nilikagua mapato yaliyokusanywa na kivuko cha MV Kilindoni yanayosimamiwa na TEMESA mkoa wa Pwani katika kipindi cha mwaka 2021/22. Katika ukaguzi huo, nilibaini kuwa abiria wa kivuko hicho waliosafiri kutoka Mafia kwenda Nyamisati walilipa nauli za kivuko kwa fedha taslimu kwa Mtunza Fedha kabla ya kupewa risiti ya mashine za POS. Aidha, Kivuko cha MV Kilindoni kilikusanya na kuweka benki Sh. bilioni 1.19 kati ya Julai 2021 na Juni 2022 kupitia namba 273 za malipo zilizotolewa. Hata hivyo, usahihi wa fedha zilizokusanywa kupitia mashine za POS hazikuweza kuwianishwa kwa kuwa ripoti za makusanyo zinazotokana na mashine za POS hazikupatikana. Aidha, uongozi ulishindwa kuwasilisha ripoti hizo kutoka mashine za POS.

Ninahusisha kasoro zilizobainishwa na udhibiti usioridhisha wa ndani uliowekwa na manejimenti katika ukusanyaji wa mapato. Maoni yangu ni kuwa udhaifu uliobainika umeleta mwanya wa upotevu wa mapato.

Menejimenti ilieleza kuwa tayari wameanza kushughulikia madhaifu yaliyobainishwa katika usimamizi wa POS. Wamepata mashine mpya 60 za POS ambazo zinasubiri uwekwaji wa programu na kuziunganisha kwenye

kanzi data. Hii itaruhusu taarifa zote zinazohusiana na shughuli za POS kupatikana mtandaoni. Menejimenti pia inafanya jitihada za kutafuta mashine za POS zilizokosekana katika kila kituo cha Kivuko ambako zilipelekwa.

Napendekeza menejimenti ya TEMESA ichukue hatua za haraka kurekebisha madhaifu yote yaliyobainishwa hapo juu kuhusu usimamizi wa POS. Pia wanapaswa kufanya uchunguzi juu ya suala la upotevu wa POS na kuchukua hatua stahiki.

3.2.4 Kutokuanzishwa kwa Soko la Kimataifa la Makambako Njombe licha ya Kulipwa Fidia ya Ardhi yenye thamani ya Sh. Bilioni 3.03

Aya ya 224 ya hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara ya mwaka 2016/17 ilieleza kuwa Sh. bilioni 3.48 zilitengwa kwa ajili ya kuwalipa fidia wananchi wa Makambako ili kupata ardhi kwa ajili ya kuanzisha Soko la Kimataifa ambalo lililenga kuwahudumia wananchi wa Nyanda za Juu Kusini kama kituo kimoja cha kuuza bidhaa za kilimo na bidhaa nyingine kwa misingi ya Kimataifa.

Hata hivyo, nilibaini kuwa fidia ya Sh. bilioni 3.03 ililipwa kati ya Januari na Februari 2018. Zaidi, nilibaini kuwa ujenzi wa soko hilo bado haujaanza. Kwa mujibu wa menejimenti kutoanziashwa kwa soko hilo kumesababishwa na ukosefu wa fedha na msaada wa kifedha kutoka kwa washirika wa maendeleo.

Hii inadhihirisha utendaji usioridhisha wa menejimenti ya wizara, kwani hawakutoa kipaumbele kwenye mradi huu na kucheleweshaji shughuli nyingine chanya za maendeleo kwa kufidia ardhi isiyotumika.

Wizara ilieleza katika mwaka 2021/22 bado inafanya utaratibu wa upatikanaji wa fedha ili kuharakisha utekelezaji wa mradi wa Makambako. Ni wasiwasi wangu kuwa miaka mitano sasa imepita bila ya kuwapo kwa maendeleo yanayoonekana kuhusiana na soko.

Ili kuepusha ucheleweshaji zaidi, napendekeza Wizara ya Uwekezaji, Viwanda, na Biashara ihakikishe soko kuu la kimataifa linaanzishwa ili kufikia malengo yaliyokusudiwa ya kufidia gharama za ardhi.

3.2.5 Usimamizi Usioridhisha wa Wizara ya Maliasili na Utalii katika Pembe za Ndovu

Wakati wa ukaguzi wa Wizara ya Maliasili na Utalii, nilibaini kuwa tarehe 16 Mei, 2022, Katibu Mkuu wa Wizara aliunda timu ya uhakiki mali ambayo ilijumuisha wajumbe kutoka TAWA, DW, NCAA, na TANAPA. Timu hiyo iliundwa kwa lengo la kuanzisha mchakato wa kuhesabu na kupima akiba ya nyara katika ghala la Dar es Salaam. Nilibaini kasoro zifuatazo:

a) Kutopatikana kwa taarifa sahihi za pembe za ndovu zilizohifadhiwa, kwaajili ya kufanya tathmini, na kuzipima upya pembe hizo za ndovu;
b) Hali isiyoridhisha ya pembe zote zilizohifadhiwa kiasi cha kusababisha kuharibika kwa ubora na hadhi yake;
c) Kushindwa kuhuisha rejista juu ya hali na thamani za pembe za ndovu.
d) Programu iliyotumika kurekodi na kusajili akiba ya pembe za ndovu na nyara zingine kutounganishwa na seva kuu ya programu ya Wizara kwa sababu programu hiyo ilikuwa imepitwa na wakati;
e) Baadhi ya pembe za ndovu zilikosa taarifa zake za maandishi, huku nyingine zikiwa na taarifa zisizosomeka kutokana na ubovu wa paa ya kuhifadhia jambo linalopelekea kuvuja kwa paa hilo.
f) Zana za kuwekea alama zilizotumiwa kurekodi taarifa juu ya pembe za ndovu ziliandikwa kwa wino unaoweza kufutika, na kuzifanya ziweze kufutika kwa urahisi; na
g) Ghala la kuhifadhia lilikuwa katika hali mbaya kutokana na kuwa na nafasi ndogo, paa kuvuja, hewa chafu, mazingira machafu, umeme usio imara, ukosefu wa vifaa vya kamera, pamoja na ukosefu wa vifaa vya kuzima moto.

Mbali na hayo, nilibaini kuwa mwaka 2013 kulikuwa na moto katika ghala la pembe za ndovu ambao ulisababisha kupotea kwa taarifa muhimu zinazohusiana na pembe za ndovu zilizohifadhiwa. Jambo la kushangaza ni kuwa hakuna uchunguzi uliofanyika ili kubaini chanzo cha moto huo na madhara yake hadi wakati wa ukaguzi.

Kwa maoni yangu, ukosefu wa udhibiti sahihi wa Pembe za Ndovu unaweza kusababisha upotevu wa taarifa zinazohusiana na pembe za ndovu. Taarifa

hii ni muhimu katika kesi za kisheria dhidi ya ujangili na juhudi nyingine zinazolenga kudhibiti vitendo vya ujangili.

Menejimenti ya Wizara ya Maliasili na Utalii imethibitisha kuwepo kwa mapungufu hayo na itafanya uhakiki wa nyara kila baada ya miaka mitatu hadi minne, kulingana na upatikanaji wa rasilimali.

Napendekeza Wizara ya Maliasili na Utalii iweke mfumo madhubuti wa kudhibiti na kusimamia Pembe za Ndovu. Pia, iandae mfumo madhubuti wa kuhifadhi kumbukumbu za taarifa zote zinazohusiana na Pembe za Ndovu, ukiwamo mpango mkakati wa taarifa za upotevu kutokana na matukio yasiyotarajiwa kama vile moto.

3.2.6 Mbinu Zisizotosheleza Dhidi ya Wanaokiuka Vigezo vya Mnada wa Kielekitroniki

Nilibaini kuwa Wizara ya Maliasili na Utalii, kupitia Mkurugenzi wa Wanyamapori, iliandaa mnada kwa njia ya mtandao kwa vitalu 111 vya uwindaji, kama ilivyoagizwa na Kanuni ya 8(1) ya Kanuni za Uhifadhi wa Wanyamapori za Uwindaji wa Kitalii za mwaka 2015. Mnada huo ulitangazwa kwenye tovuti ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Nilibaini zaidi kuwa tarehe 26 Septemba 2021 M/s Game Hunters Tanzania Ltd alishinda vitalu vitano vya uwindaji kati ya vitalu 111.

Hata hivyo, niligundua kuwa mzabuni aliyeshinda, hakulipia zabuni kiasi cha dola za Marekani 343,000 sawa na Sh. Milioni 792.65. Vitendo hivyo vinaweza kusababisha Wizara kulazimika kutenga rasilimali za ziada ikiwa ni muda na fedha ili kuitisha tena zoezi la mnada huo katika siku zijazo. Ninaamini kwamba, kimsingi upungufu huu unaweza kuhusishwa na mifumo isiyotosheleza ya udhibiti ambayo haielezi hatua zinazopaswa kuchukuliwa endapo kutakuwa na wanaokiuka vigezo na masharti ya mnada.

Hivyo, hali hii ilisababisha muda na rasilimali muhimu zilizowekezwa katika kuwezesha mchakato wa mnada kupotea, huku makusanyo ya mapato yaliyotarajiwa hayakuweza kukusanywa.

Kwa sasa, menejimenti inaandaa kanuni za mnada wa kielekitroniki. Mara baada ya kukamilika, kanuni hizi zitawasilishwa kwa Kamati ya Ushauri wa

Ugawaji wa Vitalu vya Uwindaji (HBAAC) kwa ajili ya maoni kwa mujibu wa kifungu cha 38 cha Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori Na. 5 ya mwaka 2009. Wakati huo huo, Wizara ya Fedha na Mipango inapitia upya Sheria ya Mnada wa Kielekitroniki ili kujumuisha hatua kali dhidi ya wabadhirifu wa minada ya kielekitroniki.

Napendekeza Wizara ya Maliasili na Utalii ipitie na kurekebisha vigezo na masharti ya mnada yaliyopo ili kujumuisha vifungu vilivyo wazi vinavyoainisha madhara ya kushindwa kulipa zabuni.

3.2.7 Kuwapo kwa Maeneo ya Kale yenye Migogoro

Maeneo ya kale yanahusu mahali ambapo pana mabaki ya kihistoria, kitamaduni, au ya akiolojia au miundo kutoka zama za kale. Maeneo haya mara nyingi huchukuliwa kama sehemu muhimu ya urithi wa utamaduni. Hivyo, huweza kulindwa na sheria au kanuni za kuyahifadhi kwa vizazi vijavyo. Maeneo ya kale yanaweza kujumuisha magofu, makaburi, mahekalu, mabaki, na vitu vingine vya kitamaduni.

Kifungu cha 3(2) cha Sheria ya Mambo ya Kale (Marekebisho ya mwaka 1979), kinasema kuwa Mkurugenzi wa Mambo ya Kale anaweza kuchapisha orodha ya makaburi/minara na maeneo ya hifadhi katika Gazeti. Kuingizwa kwa mahali, tovuti, au muundo katika orodha yoyote iliyochapishwa itachukuliwa kama ushahidi kwamba tovuti au makaburi/minara au eneo la hifadhi kama ilivyofafanuliwa katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu cha 2. Ushahidi huu utakuwa wa msingi katika kesi zote, iwe ya kiraia au ya jinai.

Baada ya kupitia orodha ya maeneo ya Urithi wa Taifa, nimebaini maeneo matano ya akiolojia ambayo yanakabiliwa na migogoro ya kijamii na wenye maeneo hayo. Uchunguzi wa karibu wa suala hilo unaonesha kuwa migogoro mingi husababishwa na mipaka isiyoeleweka, uvamizi, na kusita kwa upande wa wananchi kuachilia maeneo hayo kwa madhumuni ya uhifadhi.

Aidha, wakati wa ukaguzi wangu, nilibaini kuwa moja ya eneo la akiolojia la unyayo wa binadamu wa kale katika kijiji cha Engareselo halikutangazwa katika gazeti la Serikali (GN) ili kuonesha umiliki wake pamoja na utambuzi wa eneo la uhifadhi kama inavyotakiwa na kifungu cha 3(2) cha Sheria ya

Mambo ya Kale (Marekebisho ya mwaka 1979). Orodha ya maeneo ya akiolojia yenye migogoro inaoneshwa katika **Jedwali Na. 5**.

Jedwali Na. 5: Orodha ya Maeneo ya Akiolojia yenye Migogoro

Na.	Jina	Mahali	Tangazo la Serekali Na.	Aina ya Mgogoro
1	Makaburi ya kale kutoka karne ya 8 hadi 18	Kunduchi Dar Es Salaam	411/1968	Uvamizi wa wananchi
2	Nyayo za binadamu wa kale wenye miaka 1300 Engareselo	Kijiji cha Engareselo	-	Kusitasita kwa wanakijiji kutoa eneo la ardhi
3	Makumbusho ya Bagamoyo	Bagamoyo	93/1983	Mipaka kutokana na kutawanyika kwa majengo ya kihistoria
4	Mapango ya Amboni	Kiomoni Tanga	182/1987	Uvamizi kwa Uchimbaji Chokaa
5	Kituo cha Miamba na Michoro ya Kale	Kijiji cha Mumba	186/1987	Uvamizi kwa shughuli za kilimo

Chanzo: *Ripoti ya Mwaka 2021/22*

Ninaamini kuwa migogoro katika maeneo ya akiolojia yaliyotambuliwa na kutokutangazwa kwenye gazeti la Serikali (GN) ni hatari kwa usimamizi wa uhifadhi. Pia, kutokuwapo kwa ulinzi sahihi wa kisheria huongeza uwezekano wa kupoteza maeneo haya ya kihistoria.

Ukosefu wa elimu miongoni mwa wananchi kuhusu mambo ya kale pamoja na kasi ndogo ya utatuzi wa migogoro kutokana na ukosefu wa fedha za kutosha pia huchangia tatizo hilo.

Hii inafanya usimamizi wa uhifadhi kuwa na changamoto; hivyo kuongeza hatari ya kupoteza maeneo haya muhimu ya kihistoria. Kwa mujibu wa menejimenti, idara inapanga kutathmini matangazo yote ya serikali (GN) kwa maeneo hayo ili kuwa na mikakati ya kudumu juu ya uvamizi wa maeneo hayo.

Napendekeza Menejimenti ya Mfuko wa Taifa wa Mambo ya Kale iandae mpango wa utekelezaji wa kutatua migogoro yote na kufuatilia usajili wa maeneo ya kihistoria ambayo hayajasajiliwa.

3.2.8 Kuwa kwa Wahamiaji Haramu 3,110 Magerezani Ijapokuwa Wamekamilisha Adhabu za Kifungo

Kifungu cha 24 cha Sheria ya Uhamiaji (Sura ya 54) ya mwaka 2016 kinafanya kuwa ni kinyume cha sheria kwa wahamiaji haramu kuingia au kubaki Tanzania. Kanuni namba 538 ya Kanuni za Kudumu za Magereza za mwaka 2003 inaeleza kuwa mtu anayesubiri kufukuzwa na kuwekwa kizuizini gerezani kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Wakimbizi ya mwaka 1998, anatakiwa kuchukuliwa kama mfungwa ambaye hajahukumiwa na kwa mujibu wa sheria na kanuni zote zinazotumika kwa tabaka hili la wafungwa. Katika ukaguzi wangu, nilibaini Idara ya Jeshi la Magereza ina wahamiaji 4,419 haramu kutoka nchi mbalimbali, huku 1,264 wakiendelea kutumikia vifungo, 45 wamewekwa mahabusu na 3,110 wanaotakiwa kurejeshwa makwao. Uwepo wa wafungwa ambao wamemaliza vifungo vyao lakini bado wako gerezani katika kipindi cha mwaka mmoja hadi mitano unatokana na kutokutolewa amri ya kuachiliwa huru na Wizara ya Mambo ya Ndani.

Gharama za kuwahudumia wahamiaji hao ni kubwa, huku Chakula cha mfungwa mmoja kilitengewa bajeti ya Sh. 5,000 kwa siku. Kitendo cha kuwa na wahamiaji 3,110 katika magereza hayo huigharimu Sh. bilioni 5.68 kwa mwaka; hivyo kuipa mzigo serikali.

Idara ya Jeshi la Magereza imeitaka Idara ya Uhamiaji kuchukua hatua stahiki za kuwarejesha makwao wahamiaji haramu wanaomaliza vifungo vyao ili kuepuka gharama za ziada. Waziri wa Mambo ya Ndani ametoa maagizo ya kuzuiliwa ili kuwabakisha wafungwa wa kigeni wanaohitaji kurejeshwa makwao. Hata hivyo, kuwafukuza wahamiaji haramu ni suala la kidiplomasia linalohitaji mashauriano na Mabalozi wa nje ya nchi.

Natoa wito kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, ikishirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, kufanya juhudi zaidi kuhakikisha kwamba maagizo yanatolewa kikamilifu ili kuwarejesha raia wa kigeni walioachiliwa huru nchini kwao na kutatua suala hili kwa ukamilifu wake, na hivyo kupunguza gharama zisizo za lazima.

3.2.9 Matumizi Kidogo ya Sehemu ya Ardhi Inayofaa kwa Kilimo kwa Magereza

Kamishna Mkuu Jeshi la Magereza alitangaza magereza tisa ambayo ni Kitete, Kalilankulukulu, Kitai, Kitengule, Mollo, Pawaga, Songwe, Arusha na Usharo kuwa vituo vya kilimo ili kuhakikisha Idara ya Jeshi la Magereza inajitosheleza kwa chakula. Magereza hayo yanatarajiwa kusimamia shughuli zao kibiashara kwa gharama nafuu kwa kutumia mbinu za kisasa za usimamizi.

Tathmini ya ufanisi wa utendaji kazi wa Jeshi la Magereza imebaini kuwa magereza yaliyotajwa yana jumla ya ekari 19,770 za ardhi ya kilimo, lakini ni ekari 3,850 tu (sawa na asilimia 19) zilizotumika katika msimu wa 2021/22. Hii ina maana kuwa ekari 15,950 (81%) za ardhi ya kilimo hazikutumika kutokana na ukosefu wa rasilimali fedha. Maelezo yanaoneshwa katika **Jedwali Na. 6**.

Jedwali Na. 6: Orodha ya Magereza yenye Matumizi Madogo ya Ardhi ya kilimo

Na	Gereza	Mkoa	Sehemu ya Arthi Inyofaa kwa Kilimo (Ekari)	Ardhi iliyotumika mpaka 2021/22 (Ekari)	Ardhi ambayo Haijtumika (Ekari)	Asilimia ya ardhi ambayo haijatumika (Ekari)
1	Gereza la Kitete	Rukwa	500	150	350	70
2	KalilanKulukulu	Rukwa	1,500	100	1,400	93
3	Kitai	Ruvuma	1,500	600	900	60
4	Kitengule	Kagera	6,000	300	5,700	95
5	Mollo	Rukwa	6,336	600	5,736	91
6	Pawaga	Iringa	600	200	400	67
7	Songwe	Mbeya	2,000	1,000	1,000	50
8	Arusha	Arusha	734	650	84	11
9	Usharo	Singida	600	250	350	58
	Jumla		**19,770**	**3,850**	**15,920**	**81**
	Wastani wa % ya matumizi					**66**

Chanzo: *Majalada ya Mawasiliano ya Mashamba ya Magereza*

Kwa mtazamo wangu matumizi madogo ya ardhi yanaweza kuzuia lengo la idara la kujitosheleza katika suala la upatikanaji wa chakula.

Napendekeza menejimenti ya Idara ya Jeshi la Magereza ihakikishe inatumia ardhi ya kilimo iliyopo ili kuwezesha magereza kujitegemea katika uzalishaji wa chakula. Menejimenti pia inapaswa ije na mikakati ya kuboresha ardhi inayofaa kwa kilimo.

3.2.10 Wahalifu 3,252 Warudishwa Kufungwa tena Magerezani

Suala la wafungwa kurudishwa tena magerezani bado ni changamoto, na huenda linachangiwa na sababu mbalimbali, kama vile kukosekana kwa fursa za ajira pamoja na unyanyapaa katika jamii unaowakabili wafungwa walioachiwa huru.

Nilipitia Ripoti ya Magereza ya mwaka 2021/22 na kubainisha kuwa wafungwa 3,252 wamerudishwa gerezani tena katika kipindi cha mwaka mmoja; wafungwa 2,320 wamerudishwa gerezani tena kwa mara ya pili na wafungwa 932 wamerudishwa gerezani tena kwa mara ya tatu kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 7**. Hata hivyo, kiwango kisichoridhisha cha kuwabadilisha tabia wafungwa wakati wa kifungo chao kinaweza kuwa sababu kubwa inayochangia halii hii.

Jedwali Na. 7: Idadi ya Wahalifu Walioingizwa Upya Magerezani

Aina	Kifungo jela kwa mara ya pili (namba)	Hukumu ya kifungo kwa mara ya tatu (namba)	Jumla (Idadi)
Wanaume	2,261	924	3,185
Wanawake	46	4	50
Vijana (Chini ya miaka 14)	13	4	17
Jumla	**2,320**	**932**	**3,252**

Chanzo: *Taarifa ya Mwaka ya Magereza 2021/22*

Hii inamaanisha kuwepo kwa gharama kubwa za kuwatunza wafungwa hawa jambo linaloiweka Serikali katika matumizi makubwa ya rasilimali.

Menejimenti ilieleza kuwa inajitahidi kufanya mageuzi makubwa katika mipango ya urekebishaji, na wameandaa na kuwasilisha rasimu ya marekebisho kwa mamlaka za juu. Kwa sasa wanatoa mwongozo na mafunzo

kuhusu programu za kuwarekebisha tabia, kutumia rasilimali zilizopo ndani ya huduma hiyo, na kufanya shughuli mbalimbali kama vile viwanda vidogo vidogo, kilimo, ufugaji, ujenzi, uvuvi na mafunzo ya ufundi stadi katika Chuo cha Ruanda mkoani Mbeya kwa wafungwa wote waliotiwa hatiani.

Ninapendekeza menejimenti ya Idara ya Jeshi la Magereza kuimarisha utaratibu wa kurekebisha tabia na kuanzisha mipango ya motisha ambayo inaweza kuwa njia bora za kushughulikia tatizo la kurudia vifungo. Programu za kurekebisha tabia zinapaswa kuzingatia ujuzi wa ufundi pamoja na kushughulikia sababu za msingi za tabia ya uhalifu kwa wafungwa, kama vile uraibu wa dawa za kulevya au afya ya akili. Mipango ya kuwapa motisha wafungwa inaweza kuwahamasisha kushiriki katika mipango ya urekebishaji wa tabia na kuwapa msaada wanaohitaji ili waweze kufanikiwa kuingia tena katika jamii.

3.2.11 Matengenezo yasiyoridhisha ya Magari Matano ya Jeshi la Zimamoto yaliyopelekwa TATC

Kifungu cha IV (v) cha hati ya maelewano (MOU) kati ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji na Shirika la Nyumbu (TATC) cha tarehe 28 Mei 2020, inaipa TATC jukumu la kukarabati magari ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji yanapofikishwa katika kituo hicho kwa ajili ya matengenezo, kwa muda usiozidi miezi minne.

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa tarehe 26 Machi 2020 magari matano ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ya Manispaa yalipelekwa Shirika la Nyumbu (TATC) kwa ajili ya matengenezo, na Sh. 444,289,200 zililipwa kwa TATC. Hata hivyo, mapungufu yafuatayo yalibainika;

a) Magari hayo ya kuzima moto yalikabidhiwa kwa TATC kabla ya kusainiwa kwa mkataba wa makubaliano (MOU). MOU ilisainiwa tarehe 28 Mei, 2020 na magari yalikabidhiwa kwa TATC tarehe 26 Machi 2020.
b) Matengenezo hayo yalicheleweshwa kwa miezi saba. Kwa mujibu wa MOU, matengenezo yalipaswa kukamilika ndani ya miezi minne kuanzia tarehe ya makabidhiano, yaani ifikapo tarehe 26 Julai 2020. Hata hivyo, matengenezo yalikamilika tarehe 26 Februari 2021.

c) Matengenezo ya magari matano ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji yaligharimu Sh. 444,289,200, lakini ni gari moja tu kati ya matano lilifanyiwa marekebisho kwa usahihi, huku manne yaliyobaki yakihitaji matengenezo zaidi.

Nilifanya uhakiki mwezi Novemba 2022 wa magari husika na kubainisha kuwa magari manne ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji yaliyotengenezwa hayafanyi kazi, licha ya jumla ya Sh. 380,985,360 kulipwa kwa TATC kwa ajili ya matengenezo. Kwa hiyo, hakuna thamani ya fedha iliyopatikana kwa ajili ya matengenezo husika. Orodha ya magari hayo ya kuzimamoto yamewekwa katika **Jedwali Na. 8**.

Jedwali Na. 8: Orodha ya Magari Manne Yaliyotengenezwa na TATC lakini Hayakufaa

Na.	Maelezo	Mahali	Hali hadi Tarehe ya makabidhiano (Machi 2020)	Hali hadi sasa (Novemba 2022)	Gharama za Matengenezo (Sh.)
1	STG 6388 M/Benz 2630	Ilala	Halitembei	Halitembei	129,798,840
2	SM 5838 Nissan UD	Ilala	Halitembei	Halitembei	67,848,840
3	SM 5238 M/Benz	Temeke	Halitembei	Halitembei	89,768,840
4	SM 6726 Ford	Kibaha	Halitembei	Halitembei	93,568,840
	Jumla				**380,985,360**

Chanzo: *Rejista ya Mali ya FRF 2021/22*

Menejimenti ina mpango wa kuendelea na matengenezo ya kawaida na ukarabati wa magari ya zimamoto, lakini wanakabiliwa na changamoto kutokana na gharama kubwa na ukarabati wa mara kwa mara unaohitajika kwa magari ya zimamoto yaliyonunuliwa kwa muda mrefu. Aidha, uhaba na upatikanaji mdogo wa vipuri sokoni unasababishwa na mahitaji madogo na teknolojia iliyopitwa na wakati ya vifaa vya Magari ya zimamoto nchini Tanzania.

Udhaifu huu unaonyesha ukosefu wa uzingatiaji wa taratibu sahihi za matengenezo na viwango vya vifaa vya kuzima moto, ambavyo vinaweza kusababisha hatari kubwa kwa usalama wa Umma.

Napendekeza menejimenti ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji itekeleze mpango mzuri wa matengenezo wa magari yake na sio kusubiri hadi yanapoharibika, jambo ambalo linaweza kusababisha gharama kubwa za matengenezo.

3.2.12 Upungufu wa Vituo vya Kuchukulia Maji ya Kuzimia Moto 283,370

Kifungu cha 5(1) na 13(1) cha Sheria ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Na.14 ya mwaka 2007, kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2021, kinaeleza majukumu ya Jeshi hilo ikiwa ni pamoja na kuzuia vifo, majeruhi na uharibifu wa mali unaosababishwa na majanga mbalimbali ikiwemo moto. Pia kinalitaka Jeshi hilo kutoa na kutunza maji ya kuzimia moto na mitambo mingine muhimu ya maji kwa madhumuni ya kuzima moto.

Aidha, kifungu cha 21(a) cha Sheria ya Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Na.5 ya mwaka 2019 kinatoa idhini kwa mamlaka ya maji kupata, kujenga na kuendesha kazi za maji na usafi wa mazingira. Aidha, Kifungu cha 4.3 katika Hatua ya 8 ya Mwongozo wa Usimamizi wa Ujenzi wa Ubunifu na Mwongozo wa Matengenezo kinaeleza kuwa mahitaji ya zimamoto ni muhimu katika maeneo yanayokua kwa kasi na vituo vya kibiashara vijijini na kwamba asilimia 2 ya mahitaji ya maji yanapaswa kutengwa kwa madhumuni ya kuzima moto.

Wakati wa ukaguzi wangu wa kanzidata ya vituo vya kuhifadhia maji ya kuzimia moto, nilibaini kuwa kuna vituo vya kuhifadhia maji ya kuzimia moto 2,343 vinavyomilikiwa na taasisi binafsi na za serikali. Hata hivyo, kati ya vituo hivyo vya kuhifadhia maji ya kuzimia moto, ni 1,630 tu (sawa na asilimia 70) ambazo vinafanya kazi vizuri, wakati 712 (30%) havifanyi kazi, hii ina maana kwamba malengo ya Kikosi hayatafikiwa.

Nilibainisha zaidi kuwa, ili Jeshi hili litekeleze majukumu yake kwa ufanisi, linahitaji jumla ya vituo 285,000 vya kuhifadhia maji ya kuzimia moto. Hata hivyo, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji lina vituo 1,630 vya kuhifadhia maji ya

kuzimia moto tu ambavyo vinafanya kazi vizuri na kusababisha upungufu wa vituo 283,370 vya kuhifadhia maji ya kuzimia moto ambavyo ni sawa na asilimia 99.4.

Baada ya kukagua kanzidata, nilibaini kuwa Mikoa ya Zimamoto ya Temeke, Geita, Songwe na Singida inahitaji vituo vya kuhifadhia maji ya kuzimia moto 31,000 ili kuboresha hali yao, lakini kwa sasa ina vituo vya kuhifadhia maji ya kuzimia moto 9 tu vinavyofanya kazi. Aidha, Manyara inahitaji vituo vya kuhifadhi maji ya kuzimia moto 7,000, lakini ina vituo vya kuhifadhia maji ya kuzimia moto viwili tu na visivyofanya kazi, hivyo kuifanya mikoa hii kuwa katika hatari kubwa ya athari ya moto. Rejea **Kiambatisho Na. VI.**

Nahusisha hali hiyo na menejimenti kushindwa kuwasiliana na mamlaka za maji kujumuisha vituo vya kuhifadhia maji ya kuzimia moto wakati wa kubuni miradi ya maji, pia hakuna kipaumbele kilichowekwa na Jeshi juu ya matengenezo ya vituo husika vya kuhifadhia maji ya kuzimia moto.

Utunzaji duni wa mifumo ya kuzima moto kunaweza kusababisha hatari kubwa ya vifo, majeraha, na uharibifu wa mali.

Napendekeza menejimenti ya Jeshi la Zimamoto (FRF) kushirikiana na Wizara ya Maji kuweka miundombinu ya vituo ya kuchukulia maji wakati wa kubuni miradi ya maji hasa katika maeneo ya mijini na wilaya zinazokua kwa kasi, ili kuongeza idadi ya vituo vya kuhifadhia maji ya kuzimia moto. Pia kipaumbele kitolewe katika matengenezo na ukarabati wa vituo vya kuhifadhia maji ya kuzimia moto ambavyo havifanyi kazi vizuri.

3.2.13 Upungufu wa Vifaa 6,352 vya Zimamoto na Uokoaji Sawa na Asilimia 91

Kifungu cha 7(1) na (2) cha Sheria ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji namba 14, ya mwaka 2007 inalitaka Jeshi hilo kwa lengo la kuzima moto katika maeneo yake na kulinda uhai na mali pindi moto unapotokea kupata watumishi na vifaa muhimu ili kukidhi mahitaji yote ya kawaida. Aidha, kifungu cha 9(3) cha Sheria ya Zimamoto na Uokoaji namba 14 ya mwaka 2007 kinaeleza kuwa Jeshi hilo linatakiwa kuwa na uwezo na kuhakikisha upatikanaji wa vifaa hivyo.

Katika ukaguzi wangu wa ripoti ya mwaka ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kwa mwaka 2021/22, nilibaini kuwa jeshi hilo linahitaji vifaa vya zimamoto na uokoaji 7,012. Hata hivyo, jeshi hilo lina vifaa 660 tu na kusababisha upungufu wa vifaa 6,352 ambavyo ni sawa na asilimia 91.

Pia nilifanya ziara katika Mikoa ya Zimamoto ya Mwanza, Kagera, Mara, Mtwara, Dar es Saalam na Tanga na kubaini uhaba wa vifaa vya uokoaji vinavyohitajika kwa ajili ya uokoaji unaotegemea maji. Vifaa hivyo ni pamoja na boti za uokoaji na zimamoto au meli, makoti ya kupiga mbizi, SCUBA, machela zinazoelea, mabegi ya upepo, tochi za kupiga mbizi, makoti ya kuokoa maisha, na compressors zinazobebeka.

Bajeti isiyotosheleza inaweza kuwa sababu ya kukosekana kwa vifaa vya kutosha vya zimamoto kwa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji.

Kushindwa kuwa na idadi inayotakiwa ya vifaa vya kuzima moto kunakwamisha utendaji wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kwa watu pamoja na mali.

Nilifahamishwa na menejimenti kuwa bajeti ya sh. bilioni 9 imetengwa kwa mwaka 2022/23 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya zimamoto, ujenzi wa vituo vipya vya zimamoto na ukarabati wa vituo vilivyopo. Pia wanashirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango kuingia katika Mkataba wa Makubaliano na washirika wa maendeleo kama vile Austria na Ujerumani kupata zabuni za vifaa vya kuzima moto na vifaa vya uokoaji.

Napendekeza menejimenti ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji (FRF) kutenga bajeti ya ununuzi wa vifaa vya zimamoto na uokoaji kila mwaka. Aidha, napendekeza jeshi hilo kuandaa mpango mkakati unaozingatia namna ya kuondokana na changamoto ya upungufu wa vifaa vya zimamoto na uokoaji ikiwemo kuongeza vituo vya maji ya zimamoto na kununua vyombo vya moto kwa gharama nafuu.

3.2.14 Kukosekana kwa Mfumo wa Kurekodi Matukio ya Milipuko ya Moto

Kifungu cha 5(1) cha Sheria ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji namba 14 ya mwaka 2007 kimelipa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji jukumu la kuzuia na kupunguza viwango vya vifo, majeruhi kwa watu na uharibifu wa mali zinazotokana na majanga mbalimbali, kama ilivyoainishwa. Aidha, Kanuni 117 ya Kanuni za Fedha za Umma, 2001 inaruhusu matumizi ya mbinu zilizoidhinishwa za kutunza au kuandaa kumbukumbu zinazohitajika na Sheria au Kanuni za Fedha za Umma, wakati Waraka wa Uhasibu Na. 1 wa 1999/2000 unataka miamala yote ya serikali kuchakatwa kwenye Mfumo Jumuishi wa Usimamizi wa Fedha (IFMS).

Hata hivyo, wakati wa ukaguzi nilipitia matukio ya milipuko ya moto na uokoaji kwa miaka mitatu kuanzia 2019/20 hadi 2021/22, na kubaini kuwa matukio hayo yalirekodiwa kwa mifumo ya kizamani ambayo haiwezi kuaminika na haina uwezo wa kuhifadhi taarifa . Hii inaashiria kuwa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji halizingatii kikamilifu kanuni na matakwa yaliyotajwa hapo juu.

Aidha, nilibaini kuwa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji (FRF) linatumia mfumo wa ukusanyaji mapato unaoitwa Mfumo wa Ukaguzi wa Usalama wa Moto na Usimamizi wa Mapato (FSIRMS) kwa ajili ya kurekodi ukaguzi kwa kufuata kanuni za moto na kutoa vyeti vya moto. Hata hivyo, haina moduli ya kutunza kumbukumbu za matukio ya milipuko ya moto ambayo imetokea. **Jedwali Na. 9** linaonyesha Idadi ya Matukio ya Zimamoto na Uokoaji kuanzia mwaka 2019/20 hadi 2021/22.

Jedwali Na. 9: Matukio ya Zimamoto na Uokoaji

Mwaka	Matukio ya mlipuko wa moto				Matukio ya uokoaji		
	Jumla ya Matukio	Vifo	Majeruhi	Kudhibitiwa	Jumla ya Matukio	Vifo	Majeruhi
2021/22	1,718	66	250	1,402	1,379	458	921
2020/21	1,967	72	202	1,693	1,701	553	1,148
2019/20	2,023	90	155	1,778	1,197	317	880

Chanzo: *Matukio ya Zimamoto na Uokoaji*

Kutoka jedwali hapo juu, idadi ya vifo na majeruhi vinavyotokana na milipuko ya moto na matukio ya uokoaji imepungua kwa asilimia 16 na asilimia 13 kwa mtiririko kutoka mwaka wa fedha 2020/21 hadi 2021/22. Hii inaonyesha uboreshaji wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji (FRF).
Kukiwa na taarifa sahihi zaidi na za kuaminika, itakuwa rahisi kupima mwenendo wa utendaji.

Kulingana na mtazamo wa usimamizi hii inasababishwa na kukosekana kwa moduli ya kurekodi matukio ya mlipuko wa moto katika Mfumo wa Ukaguzi wa Usalama wa Moto na Usimamizi (FSIRMS).

Bila takwimu sahihi za matukio ya moto, ni vigumu kubaini mwenendo na kuchukua hatua madhubuti kuzuia matukio ya baadaye.

Natoa ushauri kwa menejimenti kukidhi na kuhakikisha utunzaji sahihi wa kumbukumbu. Hii itasaidia kuhakikisha usahihi, uaminifu na usalama wa takwimu za matukio ya milipuko ya moto na uokoaji, ambayo ni muhimu kwa kazi ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji katika kutimiza wajibu wake wa kuzuia na kupunguza madhara yanayotokana na majanga.

3.2.15 Jumla ya Majengo 62,581 Hayajakaguliwa na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji (FRF)

Kanuni ya 10(1) ya Kanuni za Jeshi la Zimamoto na Uokoaji (Ukaguzi wa Usalama, Vyeti na Tozo), 2008 inataka pale ambapo katika ukaguzi Mamlaka ya Zimamoto hairidhishwi na maudhui ya mpango wa tahadhari katika kituo cha msingi au cha uwasilishaji itatumia taarifa za mmiliki au mwendeshaji inayoeleza kasoro na hatua zitakazochukuliwa na mmiliki au mwendeshaji ndani ya muda maalumu ili kurekebisha kasoro kabla ya utoaji wa Cheti cha Usalama wa Moto. Aidha, Kanuni ya 4(1) ya Kanuni za Marekebisho ya Sheria ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji (Safety Inspections and Certificates), 2014 inataka ukaguzi ufanyike na Cheti cha Usalama wa Moto kitolewe kwa majengo kulingana na Jedwali la Kwanza.

Nilipitia kanzidata za Mikoa ya ZimaMoto zinazotunzwa na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji (FRF) na kubaini kuwa kuna majengo 101,475 (majengo ya biashara na ofisi) ndani ya nchi. Hata hivyo, ripoti ya utendaji kazi kwa mwaka hadi tarehe 30 Juni 2022 ilionyesha kuwa ni asilimia 38 tu

ya majengo (majengo 38,894) yalikaguliwa na kuacha asilimia 62 (majengo 62,581) bila kukaguliwa.

Aidha, uchambuzi wa mwenendo wa ukaguzi katika Mikoa ya Zimamoto kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2019/20 hadi 2021/22 umebaini kuwa Mikoa sita ya Zimamoto ilipungua kulingana na ukaguzi uliofanyika kwa miaka miwili mfululizo. Maelezo hayo yameoneshwa katika **Jedwali Na. 10**:

Jedwali Na. 10: Sampuli ya Mikoa Inayoonesha Mwenendo wa Ukaguzi wa Mikoa ya Zimamoto

Na.	Mikoa	2019/20	2020/21	2021/22
1	Tanga	1023	955	749
2	Kagera	688	447	387
3	Kilimanjaro	1197	1187	1061
4	Geita	680	555	507
5	Kinondoni	4318	4137	4060
6	Temeke	2772	2546	2519

Chanzo: *Taarifa za ukaguzi 2021/22*

Uchambuzi zaidi umebaini kuwa kanzidata za mikoa mitatu ya Pwani, Arusha na Tanga hazikuwa na uhalisia kwani idadi halisi ya ukaguzi uliofanyika ulikuwa mkubwa kuliko idadi iliyorekodiwa ya majengo katika kanzidata ya mkoa wao. Maelezo yametolewa katika **Jedwali Na. 11**:

Jedwali Na. 11: Kanzidata isiyo Halisi

Na.	Mikoa	Hifadhi data	Ukaguzi uliofanyika	Tofauti	Asilimia Mafanikio
1	Pwani	691	1437	(746)	208
2	Arusha	2911	3362	(451)	115
3	Tanga	716	749	(33)	105

Chanzo: *Usajili wa Kanzidata ya Mkoa*

Kwa mtazamo wangu hii imesababishwa na uhaba wa nguvu kazi na zana za kazi kama magari na ukosefu wa vituo vya zimamoto katika wilaya nyingine.

Kazi ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji (FRF) ni kulinda maisha na mali dhidi ya hali yoyote ya dharura kupitia utayari, kuzuia, na kuelimisha Umma haikufanikiwa, na kuweka majengo na watumiaji katika hatari ya moto na kifo.

Napendekeza Jeshi la Zimamoto na Uokoaji liunde kikosi kazi kitakachofanya ukaguzi katika maeneo kwa kutumia rasilimali zilizopo ili kuongeza idadi ya ukaguzi katika mikoa hiyo. Pia, kufanya usimamizi wa ofisi za Kanda ili kuhakikisha kuwa shughuli zilizopangwa na zinazolengwa zinafanikiwa. Aidha, kuanzisha mpango kazi wa kila mwaka na kuwapa kazi watumishi wote wa mkoa na kuandaa mpango mkakati wa kuhakikisha majengo yote yanakaguliwa na mikoa yao.

3.2.16 Kutofanyika Uchunguzi wa Milipuko na Matukio ya Moto

Kifungu cha 5(2c) cha Sheria ya Zimamoto na Uokoaji Na. 14, 2007 kinaipa mamlaka Jeshi la Zimamoto na Uokoaji (FRF) kufanya ukaguzi wa moto ili kupata taarifa zinazohusiana na chanzo cha moto na hasara iliyosababishwa na moto.

Uchambuzi uliofanywa wakati wa ukaguzi umebaini kuwa jumla ya milipuko 1,718 ya moto ilitokea katika mikoa 28 ya zimamoto katika kipindi cha mwaka 2021/22. Hata hivyo, ilibainika kuwa hakuna tukio lolote kati ya matukio hayo ya moto lililochunguzwa, jambo ambalo ni kinyume na Kifungu cha 5(2c) cha Sheria ya Zimamoto na Uokoaji Na. 14 ya mwaka 2007. Aidha, katika kipindi cha mwaka 2020/21, kati ya milipuko 1,967 ya moto iliyorekodiwa, ni matukio 560 tu yaliyochunguzwa na kusababisha matukio 1,407 ya moto sawa na asilimia 72 kutokuchunguzwa. Kwa matokeo haya ukosefu wa uchunguzi unaweza kuzuia uwajibikaji na kuathiri juhudi zinazolenga kuzuia matukio ya moto kwa baadaye. **Jedwali Na. 12** linaonyesha mwenendo wa uchunguzi wa Moto kwa miaka miwili 2020/21 na 2021/22.

Jedwali Na. 12: Utendaji wa Uchunguzi wa Moto

Mwaka	Matukio ya moto	Yaliyochunguzwa	Yasiyochunguzwa	Asilimia ya Kutokuchunguzwa
2021/22	1718	-	-	100
2020/21	1967	560	1407	72

Chanzo: *Matukio ya mlipuko wa moto na ripoti ya uchunguzi*

Kutofanya uchunguzi wa moto kumesababishwa na uhaba wa watumishi. Hii inamaanisha kuwa, sababu za moto hazifahamiki, jambo ambalo linaweza kusababisha ukosefu wa hatua za kuzuia moto na uwezekano wa matukio ya moto kujirudia.

Kulingana na matokeo ya ukaguzi, ninashauri mamlaka husika zichukue hatua zifuatazo:

i. **Kuhakikisha kufuata Kifungu cha 5(2c) cha Sheria ya Zimamoto na Uokoaji Na. 14 ya mwaka 2007, kwa kufanya uchunguzi wa milipuko na matukio yote ya moto yanayotokea ndani ya mikoa ya Zimamoto.**

ii. **Kuandaa na kutekeleza mfumo wa kuchunguza matukio ya moto ambayo ni pamoja na miongozo na itifaki za kubaini chanzo cha matukio ya moto na kuchukua hatua stahiki za kurekebisha.**

iii. **Kuongeza fedha kwa ajili ya shughuli za uchunguzi wa moto ili kuwezesha mafunzo kwa wachunguzi, ununuzi wa vifaa muhimu, na kuboresha mchakato wa uchunguzi kwa ujumla.**

iv. **Kuimarisha uelewa wa wananchi juu ya umuhimu wa kutoa taarifa za matukio ya moto mara moja na kwa usahihi ili kuboresha ubora wa taarifa zilizopo kwa ajili ya uchunguzi.**

3.3 Ufanisi katika Utawala

Mwongozo wa Wizara ya Fedha na Mipango wa Kuimarisha Mifumo ya Udhibiti wa Ndani katika taasisi za Umma wa Desemba 2014, unafafanua utawala bora kama seti ya kanuni, taratibu na mifumo inayoelekeza na kudhibiti taasisi kufikia malengo yake, kuongeza thamani yake, na kuwanufaisha wadau wote kwa muda mrefu. Kwa kuzingatia miongozo hii, nilifanya ukaguzi ili kutathmini ufanisi wa mifumo ya udhibiti wa ndani na utawala bora, ikiwa ni pamoja na utendaji wa bodi zinazosimamia, zinazohusiana na uendeshaji wa taasisi za serikali. Ukaguzi ulibaini mapungufu yafuatayo:

3.3.1 Kushindwa Kuanzisha Bodi za Uongozi na Bodi za Uongozi Zilizokwisha Muda wake

Mwongozo wa Wizara ya Fedha na Mipango wa Kuimarisha Mifumo ya Udhibiti wa Ndani katika Mashirika ya Sekta ya Umma ya Desemba 2014 unaeleza kuwa bodi ni chombo cha juu cha usimamizi katika taasisi, chenye jukumu la kusimamia na kufanya maamuzi ya kimkakati. Bodi za ushauri za wizara zinatakiwa kuanzishwa kwa kifungu cha 6 (1) cha Sheria ya Wakala wa Serekali, 1997 (GN Na. 83 ya mwaka 2003) huku taasisi nyingine zikianzisha bodi kulingana na majukumu yao.

Nilipitia nyaraka za bodi za ushauri kuhusu uwepo wa bodi za uongozi na utendaji wa bodi ya uongozi iliyopo, na kubainisha kuwa taasisi tatu zilikuwa zinafanya kazi bila kuanzisha bodi za uongozi, taasis kumi na moja zilikuwa zinafanya kazi na bodi za ushauri ambazo muda wake umekwisha na bodi tano za ushauri zilizopo zilishindwa kufanya idadi ya mikutano inayohitajika kama ilivyoelezwa kwa kina katika **Kiambatisho Na. VII**.

Nahusisha mapungufu haya na ucheleweshaji wa uteuzi wa wajumbe wa bodi unaofanywa na mamlaka husika. Aidha, bodi hizo zilishindwa kufanya mikutano kwa sababu akidi ya bodi haikufikiwa, na pia walishindwa kuyapa kipaumbele majukumu yao.

Kukosekana kwa bodi hai kunasababisha ucheleweshaji wa kufanya maamuzi pamoja na kudhoofisha kazi ya usimamizi wa ndani katika kutoa mwelekeo wa kimkakati wa taasisi hatimaye, kuathiri utendaji. Vivyo hivyo, kutekelezwa kwa majukumu ya bodi na bodi iliyomaliza muda wake kunaweza kusababisha kushindwa kuwawajibisha kwa maamuzi yao.

Napendekeza mamlaka zenye dhamana zianzishe bodi zinazosimamia na kuteua wajumbe kabla ya kumalizika muda wa uongozi ili kuhakikisha bodi zinazofanya kazi kwa ajili ya kusimamia shughuli za taasisi. Zaidi napendekeza bodi zinazosimamia taasisi hizi zifanye idadi ya mikutano yote inayohitajika kufanywa kisheria kama sehemu ya wajibu na majukumu yao.

3.3.2 Kutoandaliwa kwa Mikakati ya Utekelezaji wa Sera ya Wanyamapori na Mambo ya Kale

Kwa mujibu wa Mwongozo wa Nyaraka za Baraza la Mawaziri wa mwaka 2010 (toleo la 2014), Kiambatisho Na.4, uandaaji wa mkakati wa utekelezaji wa sera unatakiwa kuainisha mfululizo wa shughuli zinazofanywa na wadau ili kufikia malengo na malengo ya taarifa za sera. Licha ya kuandaa sera kama vile Sera ya Wanyamapori ya mwaka 1998 na Sera ya Mambo ya Kale ya mwaka 2008, Wizara ya Maliasili na Utalii haijaandaa mkakati wa utekelezaji wa sera kama inavyotakiwa na mwongozo huo, ambao unakwamisha utekelezaji mzuri wa sera hizo.

Kuhusu hayo hapo juu, Wizara ilieleza kuwa Idara ya Wanyamapori iliandaa mkutano wa wadau kutathmini utekelezaji wa Sera ya Wanyamapori ya Tanzania ya mwaka 2007, kwa lengo la kubaini nguvu na mapungufu katika uhifadhi na ulinzi wa wanyamapori nchini. Maoni na mapendekezo kutoka kwa wadau mbalimbali yalichambuliwa na kuandikwa. Hata hivyo, ninaamini kuwa kuchelewa kuanzisha mkakati wa utekelezaji wa sera kumeathiri ufanikishaji wa malengo yanayotarajiwa kutoka kwa sera zilizotajwa hapo juu.

Nashauri menejimenti ya Wizara iweke kipaumbele katika uandaaji wa mkakati wa utekelezaji wa sera ili kuhakikisha kuwa sera zinatekelezwa kwa ufanisi . Hii itaiwezesha Wizara kufikia malengo yake yaliyoainishwa katika sera hizo, huku pia ikitoa mwongozo kwa wadau kuhusu majukumu yao katika kufikia malengo hayo.

3.3.3 Upimaji wa Utendaji wa Mipango Mikakati ya Miaka Mitano

Mpango mkakati ni mwongozo ulioandikwa ambao unaelezea mbinu ya shirika ya kutekeleza mkakati uliochaguliwa na kuelezea mwenendo wa taasisi kwa kipindi kilichofafanuliwa. Mpango huo unaelezea malengo ya taasisi, kuweka vipaumbele, kutenga rasilimali, na kuboresha shughuli ili kuhakikisha kuwa wafanyakazi na wadau wanaendana na malengo ya pamoja, na kuchangia kufikia malengo ya kitaifa ya muda mrefu na ajenda za maendeleo. Kwa ujumla, mpango mkakati ni chombo cha kuzingatia nguvu na rasilimali kuelekea kufikia matokeo yanayotakiwa.

Taasisi za Serikali zimekuwa zikitekeleza mipango yao ya kimkakati kwa vipindi tofauti. Katika mwaka wa fedha 2021/22, mipango mikakati iliyoanza kutekelezwa kati ya mwaka 2017/18 na 2021/22 ilifikia hitimisho huku baadhi ya mipango mingine ikiwa katika hatua mbalimbali za utekelezaji kwa taasisi za Serikali.Katika ukaguzi wangu wa mwaka wa fedha 2022/22, nilifanya tathmini ya uwepo na ufanisi wa mipango mikakati ambayo ama ilikuwa imeisha au ilikuwa inakaribia kukamilika. Kutokana na tathmini yangu, nilibaini kuwa taasisi saba zilizohitimisha mpango mkakati wake mwaka 2021/22 hazikufanya mapitio na kuhuhisha mipango mkakati yake. Pia taasisi tatu hazikuandaa taarifa za utekelezaji wa mpango mkakati. Aidha, taasisi zingine 12 zilikuwa zimepiga hatua kubwa kuelekea kufanikisha mpango mkakati wao.

Aidha, niliona kuwa taasis nne zimekuwa zikifanya kazi bila mipango mikakati au kwa mipango ambayo tayari ilikuwa imekwisha muda wake. **Jedwali Na. 13** linaonyesha taasis zenye upungufu uliobainishwa.

Jedwali Na. 13: Mapungufu yaliyobainishwa katika Maandalizi na Utekelezaji wa Mpango Mkakati

Na.	Mapungufu	Taasisi
1.	Kutoandaliwa kwa Mpango Mkakati	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Musoma
		Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari ya Kina Kirefu
		Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi
		Kituo cha Teknolojia ya Magari Tanzania
2.	Uwepo wa Mipango Mikakati iliyopitwa na wakati bila kuhuisha	Ofisi ya Waziri Mkuu-Fungu 37
		Tume ya Ukimwi Tanzania (TACAIDS)-Fungu 92
		Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia-Fungu 46
		Mamlaka ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya-Fungu 91
		Tume ya Taifa ya Elimu, Sayansi na Utamaduni wa Umoja wa Mataifa (UNESCO)
		Hospitali ya Magonjwa ya Kuambukiza ya Kibong'oto
		Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Magereza
3.	Kutokuandaa ripoti ya utekelezaji ya mpango mkakati	Wizara ya Utalii na Maliasili
		Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC)-Fungu 24
		Jeshi la Zimamoto na Uokoaji
4.	Utekelezaji usioridhisha wa mipango mikakati kwa hatua iliyofikiwa	Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula
		Mfuko wa Ulinzi wa Wanyamapori Tanzania
		Kampuni ya Ulinzi ya SUMAJKT
		Taasisi Rasmi ya Kudhibitisha Mbegu Tanzania (TOSCI)
		Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.
		Tume ya UKIMWI Tanzania-Fungu 92
		Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum-Fungu 53
		Taasisi ya Ardhi Morogoro
		Bodi ya Usajili ya Afisa Mipango Miji
		Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC)-Fungu 24
		Tume ya Taifa ya Elimu, Sayansi na Utamaduni la Umoja wa Mataifa (UNESCO)
		Bodi ya Usajili wa Wathamini

Chanzo: *Barua za Mapungufu kwa menejimenti za 2021/22*

Nina maoni kwamba kutoandaliwa kwa mipango mikakati na uwepo wa mipango mikakati iliyopitwa na wakati kulitokana na menejimenti kutotoa kipaumbele kwa umuhimu wa mipango mikakati. Bila mpango mkakati, inakuwa vigumu kuongoza kwa ufanisi shughuli zinazolenga kufikia malengo ya muda mrefu na kutimiza dhamira ya taasisi. Aidha, kushindwa kutoa taarifa za maendeleo kunapunguza uwezo wa kutathmini utendaji wa mpango uliopita.

Ili kushughulikia masuala haya, napendekeza Menejimenti iharakishe mchakato wa kuandaa na kutekeleza mipango mipya ya kimkakati kwa wakati na pia ripoti juu ya tathmini ya utendaji wa mipango iliyotangulia. Zaidi ya hayo, inashauriwa kwa Menejimenti kuweka malengo yanayoweza kufikiwa ndani ya muda uliokubaliwa.

3.3.4 Kutokuwa huru kwa Kitengo cha Hifadhi za bahari na Maeneo Tengefu (MPRU) na majukumu yanayokinzana ya Mkurugenzi wa Uvuvi juu ya Usimamizi wa Kitengo

Kifungu cha 3 (1) cha Sheria ya Hifadhi za Bahari na Hifadhi za Bahari ya mwaka 1994 kimeanzisha Kitengo cha Hifadhi za bahari na Maeneo Tengefu, huku kifungu cha 3 (2) kikieleza kuwa Kitengo hicho kitakuwa ndani ya Idara ya Uvuvi na kitaanzishwa na Mkurugenzi kwa kushauriana na Bodi, ambaye atamteua Meneja wa Kitengo. Kifungu cha 4-(1) kinaunda Bodi ya Wadhamini ya hifadhi za bahari na hifadhi zenye majukumu ikiwa ni pamoja na kutunga sera kwenye hifadhi za bahari, kusimamia matumizi ya hifadhi za bahari na maeneo tengefu, kumshauri Mkurugenzi juu ya usimamizi wa hifadhi za bahari, na kumshauri Waziri juu ya idhini, mapitio, na marekebisho ya mpango mkuu wa usimamizi wa hifadhi zozote za bahari.

Kitengo cha Hifadhi za Bahari, kilichoanzishwa chini ya Sheria ya Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu ya mwaka 1994, kilianza shughuli zake Januari 2000 kikiwa na mamlaka yaliyoainishwa katika kifungu cha 4 cha sheria hiyo. Hata hivyo, mapitio ya uendeshaji na mfumo wake yamebaini kuwa kitengo hicho hakina uhuru kwa kuwa kinapokea maelekezo kutoka mamlaka mbalimbali, akiwamo Mkurugenzi wa Uvuvi, Bodi na Katibu Mkuu wa Wizara husika, kama ilivyoainishwa katika Sheria hiyo. Tathmini hiyo inaonesha kuwa huenda kulikuwa na mapitio yasiyoridhisha ya Sheria ya Hifadhi za Bahari na Mapori ya Mwaka 1994.

Nimebaini kuwa, kuna majukumu yanayokinzana katika kufanya maamuzi, kwani Kitengo kiko chini ya Mkurugenzi wa Uvuvi ambaye humteua Meneja wa Kitengo kwa kushauriana na Bodi. Aidha, Mkurugenzi pia ni Mjumbe wa Bodi ya Kitengo na anashauri kuhusu hifadhi za bahari kwa mujibu wa Sheria. Zaidi ya hayo, Sheria inaweka ukomo wa jukumu la Bodi kwani ni lazima waripoti kwa Mkurugenzi kwa ushauri kuhusu masuala yanayohusiana na hifadhi za bahari, pamoja na majukumu yao ya uangalizi.

Napendekeza menejimenti ianzishe mapitio ya Sheria iliyopo ili kutenganisha majukumu ya Mkurugenzi wa Uvuvi kama mdhibiti na Mjumbe wa Bodi ya Kitengo, na kufikiria kumteua Mkurugenzi wa Kitengo ambaye atawajibika kwa Bodi ya Wadhamini.

3.4 Udhibiti wa Mifumo ya Ndani

Kwa mujibu wa Aya ya 2.2 ya Mwongozo wa Wizara ya Fedha wa Kuimarisha Mifumo ya Udhibiti wa Ndani katika Mashirika ya Sekta ya Umma ya Desemba 2014, udhibiti wa mifumo ya ndani ni mchakato unaotumiwa na menejimenti na wafanyakazi wa shirika. Madhumuni yake ni kusimamia vihatarishi na kutoa uhakikisho unaofaa kwamba shughuli za taasisi zinatekelezwa kwa utaratibu, maadili, kiuchumi, ufanisi, na ufasaha. Udhibiti wa ndani, pamoja na usimamizi wa hatari na utawala bora, husaidia kuhakikisha shughuli za uaminifu zinazopelekea utoaji bora wa huduma, matumizi bora ya rasilimali, usimamizi bora wa miradi, na kuboresha shughuli za serikali.

Kanuni ya 11 (3) (d) ya Kanuni za Fedha za Umma, 2001 [Toleo lililorekebishwa 2004] inaagiza Maafisa Masuuli kuanzisha na kudumisha mfumo mzuri wa udhibiti wa ndani juu ya shughuli za kifedha na zinazohusiana na uwajibikaji. Mapema iwezekanavyo,Lazima pia waunde, kitengo cha ukaguzi wa ndani ambacho mara kwa mara kinatathmini utoshelevu wa kufuata mfumo wa udhibiti wa ndani.

3.4.1 Utendaji usioridhisha wa Kamati za Ukaguzi

Kwa mujibu wa Kanuni ya 30 ya Kanuni za Fedha za Umma 2001, inahitaji kila Wizara na Idara za Serikali kuunda Kamati ya Ukaguzi. Majukumu na muundo wa kamati umeainishwa katika Kanuni ya 31 na 32 ya kanuni za fedha za Umma, kwa mtiririko.

Kamati ya Ukaguzi inasimamia na kuhakikisha ufanisi wa kazi za ukaguzi ndani ya Wizara, Wakala au Idara. Wanakutana kila robo mwaka, kuidhinisha mipango ya ukaguzi, kupitia ripoti za ukaguzi, na kutoa ushauri juu ya hatua muhimu zinazopaswa kuchukuliwa. Wanaratibu programu za ukaguzi na kutoa ushauri kuhusu taarifa za fedha. Wanaandaa taarifa ya mwaka kuhusu majukumu yao itakayowasilishwa kwa Katibu Mkuu, Mhasibu Mkuu na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Nilibaini taasisi 18 zimeunda Kamati za Ukaguzi hata hivyo kamati husika hazijatimiza kikamilifu majukumu yake waliyokabidhiwa kama vile, kutopitia na kuidhinisha mipango ya ukaguzi wa ndani ya mwaka na kimkakati, kutopitia taarifa za fedha, mikutano ya robo mwaka kutofanyika, kutokuandaa mkataba wa kamati na kutokuandaa ripoti ya mwaka ya kamati. Orodha ya kina ya taasisi zenye upungufu inaoneshwa katika **Kiambatisho Na. VIII.**

Mapungufu haya yanatokana na kuchelewa kwa uteuzi wa wajumbe wapya wa kamati ya ukaguzi na rasilimali fedha zisizotosheleza kwa ajili ya kutekeleza shughuli za kamati hizo.

Ni maoni yangu kuwa kazi za usimamizi na ushauri wa kamati ya ukaguzi kwa Afisa Masuuli hazikufanyika kwa ufanisi jambo ambalo linaweza kusababisha hatari ya hesabu kutokuwa sahihi bila Menejiment kutambua .

Napendekeza Menejimenti ya Taasisi husika kuhakikisha utendaji kazi wa kamati unakuwa na ufanisi katika kutoa ushauri kwa Afisa Masuuli kuhusu masuala ya fedha, mchakato wa ukaguzi, mifumo ya udhibiti wa ndani na uzingatiaji wa taratibu.

3.4.2 Kutokuwepo kwa Kamati za Ukaguzi

Kanuni ya 30 ya Kanuni za Fedha za Umma 2001, inahitaji kila Wizara na Idara za Serikali kuunda Kamati ya Ukaguzi. Majukumu na muundo wa kamati umeainishwa katika Kanuni ya 31 na 32 ya kanuni za fedha za Umma, kwa mtiririko. Waraka wa Hazina Na 09 wa mwaka 2003/2004 na Mwongozo wa Kamati ya Ukaguzi wa Desemba 2019.

Nilibaini kuwa taasisi tano ambazo ni Hospitali ya Rufaa ya Kanda Chato, Hospitali ya Mount Meru, Tume ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Bodi ya Maji ya Bonde la Kati (IDBWB), Bodi ya Maji ya Bonde la Ruvuma na Pwani ya Kusini (RSCBWB) bado hazijaunda kamati za ukaguzi kulingana na matakwa ya Kanuni ya 30 ya Kanuni za Fedha za Umma, 2001. Kwa maoni yangu, mapungufu haya yanahusishwa na kusitasita kwa menejimenti katika kuanzisha kamati madhubuti ya ukaguzi na ukosefu wa uzoefu.

Kwa kukosekana kwa kamati madhubuti za ukaguzi, taasisi zinakosa kamati za usimamizi juu ya shughuli za kifedha, udhibiti wa ndani, masuala ya ushirika, utii wa kisheria, maadili, masuala ya ukaguzi, na usimamizi wa vihatarishi.

Napendekeza menejimenti ya taasisi hizo kuhakikisha kamati za ukaguzi zinaundwa na kutekeleza majukumu yake kama inavyotakiwa na kanuni tajwa.

3.4.3 Kutoanzishwa kwa Vitengo vya Ukaguzi wa Ndani

Kwa mujibu wa Mwongozo wa Wizara ya Fedha wa Kuimarisha Mifumo ya Udhibiti wa Ndani katika Mashirika ya Sekta ya Umma ya Desemba 2014, vitengo vya ukaguzi wa ndani vina jukumu la kutoa uhakikisho na ushauri wa malengo juu ya ufanisi na utoshelevu wa mfumo wa udhibiti wa ndani wa taasisi za serikali na vipengele vyake binafsi. Aidha, Kanuni.28 (1) Kanuni za Fedha za Umma za mwaka 2001 zinawataka maafisa masuuli kuanzisha vitengo vya ukaguzi wa ndani vyenye ufanisi ili kutoa uhakika juu ya utoshelevu na ufanisi wa udhibiti wa mifumo ya ndani ya taasisi.

Wakati wa tathmini yangu ya uwepo wa kitengo cha ukaguzi wa ndani kwa wizara, idara na wakala kwa mwaka wa fedha ulioishia 2021/22, nilibaini kuwa taasisi 22, zikiwemo hospitali za rufaa za mkoa 7, mamlaka za maji 10, bodi za maji 3, na taasisi nyingine 2, zinafanya kazi bila kuanzisha vitengo hivyo, kinyume na Kanuni ya 28(1) ya Kanuni za Fedha za Umma za mwaka 2001. Orodha ya taasisi inaoneshwa katika **Kiambatisho Na. IX**.

Ikilinganishwa na tathmini ya mwaka uliotangulia, kuna ongezeko kutoka taasisi 8 hadi 22 ambazo hazikuanzisha kitengo cha ukaguzi wa ndani, hali inayoashiria kuwa tatizo hilo linaendelea. Hii imechangiwa na ukosefu wa

jitihada za menejimenti kuanzisha vitengo vya ukaguzi wa ndani vyenye ufanisi ndani ya taasisi zao. Kwa maoni yangu, kukosekana kwa vitengo vya ukaguzi wa ndani kunainyima taasisi fursa ya mapema zaidi ya kutambua matukio ya kutofuata kanuni, na mapungufu katika mfumo wa udhibiti wa ndani.

Ili kuimarisha utendaji na uhakika wa mifumo na taratibu za udhibiti wa ndani, napendekeza Maafisa Masuuli waanzishe vitengo vya ukaguzi wa ndani na kuhakikisha vinakuwa na rasilimali watu na fedha za kutosha.

3.4.4 Usimamizi wa TEHAMA katika Taasisi za Serikali Kuu

Kama sehemu ya Usimamizi wa taasisi, usimamizi wa teknolojia ya habari na mawasiliano umeundwa ili kuimarisha usimamizi wa TEHAMA na kupata thamani kutokana na matumizi ya fedha za umma zilizowekezwa katika mipango ya teknolojia. Kupitia tathmini yangu ya usimamizi na matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano, kubaini kuwa ikiwa rasilimali za teknolojia ya habari na mawasiliano zitasimamiwa kwa ufanisi na ikiwa zitakua zinatumiwa kwa ufanisi ili kusaidia malengo ya kimkakati ya taasisi. Kulingana na tathmini yangu, matokeo yafuatayo yalibainika:

i. Kukosekana kwa Kamati ya Uendeshaji na Sera ya TEHAMA

Kifungu cha 18(1) cha Sheria ya Serikali Mtandao, 2019 kinaelekeza kuwa Maafisa Masuuli waunde Kamati ya Uendeshaji ya Taasisi kwa ajili ya kutoa mwongozo wa kiufundi juu ya utekelezaji wa mipango ya TEHAMA. Na kifungu cha 3(a) cha Sheria hiyo kinaelekeza zaidi Kamati za Uendeshaji za TEHAMA ndani ya taasisi za Serikali kupitia na kuidhinisha sera na mikakati ya TEHAMA ya taasisi.

Hata hivyo, ukaguzi wangu ulibaini kuwa taasisi 12 hazikuwa na Kamati za Uendeshaji za TEHAMA ambazo zitasimamia maendeleo na utekelezaji wa sera ya TEHAMA wakati taasisi sita hazikuanzisha Sera ya TEHAMA. Rejea **Jedwali Na. 14**,

Jedwali Na. 14: Orodha ya Taasisi ambazo Hazina Sera ya ICT na Kamati ya Uendeshaji

Na.	Taasisi Zisizo na Kamati ya Uendeshaji ya ICT
1.	Hospitali ya Benjamin Mkapa
2.	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mawenzi
3.	Hospitali ya Rufaa ya Kanda, Mbeya
4.	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Katavi
5.	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Morogoro
6.	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Temeke
7.	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Njombe
8.	Bodi ya Filamu Tanzania,
9.	Kituo cha Mafunzo ya Takwimu Afrika Mashariki
10.	Ofisi ya Taifa ya Mashtaka
11.	Shirika la Mzinga
12.	Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania
	Taasisi ambavyo hazikuanzisha Sera ya TEHAMA
1.	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma
2.	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Morogoro
3.	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Temeke
4.	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Njombe
5.	Ofisi ya Taifa ya Mashtaka
6.	Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru

Chanzo: *Barua za Mapungufu kwa menejimenti za 2021/22*

Maoni yangu ni kwamba kukosekana kwa Kamati ya Uendeshaji na Sera ya TEHAMA kunasababishwa na ukosefu wa uelewa wa umuhimu wa udhibiti huu, rasilimali zisizotosheleza, au ukosefu wa kipaumbele kwa usimamizi wa teknolojia ya habari na mawasiliano. Hizi zinaweza kusababisha usimamizi usioendana na usiofaa wa teknolojia ya habari na mawasiliano, udhibiti duni wa usalama na matumizi yasiyofaa ya rasilimali.

Nashauri Maafisa Masuuli husika kuanzisha sera ya TEHAMA inayoainisha malengo ya kimkakati, kanuni na miongozo, na Kamati za Uendeshaji zinazosimamia sera hiyo ili kuhakikisha zinaendana na mkakati wa jumla

wa taasisi. Kamati inapaswa kukagua mara kwa mara masuala yanayohusiana na teknolojia ya habari na mawasiliano, kufuatilia utendaji, na kuhakikisha kuwa sera ya teknolojia ya habari na mawasiliano inabaki kuwa muhimu na ya kisasa.

ii. Kutoandaliwa kwa Mpango wa Kurejesha Huduma Wakati wa Maafa na Ukosefu wa Vituo vya Nje vyakuhifadhi Nakala

Kifungu cha 42(a)-(c) cha Sheria ya Serikali Mtandao, 2019 kinazielekeza Taasisi za Umma kuandaa na kutekeleza mifumo sahihi ya kurejesha huduma na udhibiti wa mifumo ya TEHAMA, kuandaa na kutekeleza na kupima mpango wa kurejesha huduma na kuwasilisha taarifa hiyo kwa Mamlaka.

Kinyume na sheria tajwa hapoo juu, ukaguzi wangu ulibaini kuwa taasisi 10 hazikuandaa mpango wa kurejesha huduma wakati wa maafa, taasisi 2 hazikupima na zingine tatu hazikuwa na vituo vya nje vya kuhifadhi nakala ili kujikwamua kutoka kwenye maafa au matukio yasiyotarajiwa kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 15**.

Jedwali Na. 15: Taasisi ambazo hazikuandaa Mpango wa Kurejesha huduma na ambazo hazikuwa vituo vya nje vya Kuhifadhi Nakala

Na.	Jina la taasisi
Tasisi ambazo hazikuandaa Mpango wa Kurejesha Huduma wakati wa Maafa	
1.	Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mbeya
2.	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Katavi
3.	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Tanga
4.	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Tumbi
5.	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Tabora
6.	Chuo cha Sheria Tanzania
7.	Kituo cha Mafunzo ya Takwimu Afrika Mashariki
8.	Ofisi ya Taifa ya Mashtaka
9.	Shirika la Mzinga
10.	Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania
Taasisi ambazo hazikupima Mpango wa Kurejesha Huduma wakati wa Maafa	
1.	Chuo cha Uongozi
2.	Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni

Na.	Jina la taasisi
Taasisi ambazo hazikuandaa wala kutekeleza mpango vituo vya nje vya kuhifadhi nakala	
1.	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Katavi
2.	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Morogoro
3.	Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni

Chanzo: *Barua za Mapungufu kwa menejimenti za 2021/22*

Upungufu huu unaweza kusababishwa na Menejimenti kutozingatia umuhimu wa mpango wa kurejesha huduma au kituo cha kuhifadhi kumbukumbu, vile vile inaweza kusababishwa na uhaba wa rasilimali za kuwekeza katika uokoaji wa maafa.

Bila mpango wa kurejesha huduma wakati wa Maafa na Ukosefu wa vituo vya nje vyakuhifadhi nakala, taasisi iko katika hatari ya kupoteza taarifa, mfumo kutofanya kazi vizuri, na upotevu wa kifedha. Ikiwa kuna janga au tukio lisilotarajiwa, taasisi haiwezi kurejesha taarifa muhimu, ambayo inaweza kusababisha kupoteza sifa, wateja, na mapato.

Maafisa Masuuli wanashauriwa kuandaa mpango wa kurejesha huduma unaoainisha taratibu za kukabiliana na majanga au matukio yasiyotarajiwa, kuwekeza katika vituo vya nje vya kuhifadhi taarifa kama vile vituo vya taarifa vya nje ya tovuti ambavyo vinaweza kurejesha haraka mifumo muhimu na taarifa iwapo kutatokea janga. Aidha, wanapaswa kutenga rasilimali kwa ajili ya kuandaa na kudumisha mpango wa uokoaji wa maafa na kituo cha kuhifadhi nakala na kuwaelimisha wafanyakazi wake kuhusu umuhimu wa kuokoa maafa na majukumu na uwajibikaji wao katika kutekeleza mpango wa kuokoa maafa.

3.5 Usimamizi wa Vihatarishi na Udanganyifu

Mwongozo wa kuandaa na kutekeleza Mfumo wa Usimamizi wa Vihatarishi vya Taasisi katika Sekta ya Umma wa mwaka 2012 uliotolewa na Wizara ya Fedha na Mipango juu ya Utekelezaji wa Usimamizi wa Vihatarishi katika taasisi uliwataka Maafisa Masuuli kuhakikisha usimamizi mzuri wa vihatarishi katika taasisi zao.

Kulingana na tathmini ya usimamizi wa vihatarishi iliyofanywa wakati wa ukaguzi, iligundulika kuwa taasisi 27 hazikuweza kutekeleza kwa ufanisi

usimamizi wa vihatarishi. Taasisi hizi zilikosa vipengele muhimu kama vile waratibu wa vihatarishi, sera za usimamizi wa vihatarishi, tathmini za vihatarishi, na usajili wa vihatarishi, ambazo ni muhimu kwa kutambua na kusimamia vihatarishi ambavyo vinaweza kuathiri shughuli za taasisi. Orodha ya taasisi zenye upungufu katika usimamizi wa vihatarishi iko katika **Kiambatisho Na. X**.

Usimamizi wa vihatarishi usiofaa ulihusishwa na Maafisa Masuuli ambao hawakuweka kipaumbele katika juhudi za kusimamia kwa ufanisi hatari zinazokabili taasisi zao. Mfumo thabiti wa usimamizi wa vihatarishi ni muhimu kwa mashirika kutambua ufanisi, kutathmini, na kusimamia vihatarishi. Bila mfumo huo, mashirika yanaweza kuwa hatarini zaidi kwa vihatarishi vitakavyotokea na haviwezi kuwa na ufahamu kamili wa hatarishi vinavyoweza kutokea kwa shughuli za taasisi . Kwa hiyo, wanaweza kufanya maamuzi yasiyo na taarifa sahihi na kushindwa kugawa rasilimali kwa ufanisi, ambayo inaweza kusababisha uharibifu wa sifa, hasara za kifedha, na matokeo mengine hasi.

Ikilinganishwa na tathmini ya mwaka uliopita, kuna ongezeko kutoka idadi ya taasisi 16 hadi taasisi 27 ambazo zilipatikana na upungufu wa usimamizi wa vihatarishi, ikionesha kuwa tatizo linaendelea.

Kwa mtazamo huu, ninapendekeza Maafisa Masuuli kuhakikisha usimamizi wa vihatarishi kwa kuandaa sera husika za vihatarishi, kuteua waratibu wa hatari, kufanya tathmini ya hatari kwa kutambua na kujibu hatari zilizotambuliwa na kuzirekodi katika daftari la vihatarisho.



SURA YA NNE

MAANDALIZI NA UTEKELEZAJI WA BAJETI

4.1 Utangulizi

Sura hii, inajadili bajeti ya mwaka wa Fedha 2021/22 ambayo ililenga kutekeleza vipaumbele muhimu kama vile kuchochea uchumi wa ushindani na shirikishi, kuimarisha uzalishaji katika viwanda, kuongeza thamani ya mazao ya kilimo, kukuza uwekezaji na biashara, pamoja na maendeleo ya rasilimali watu.

Bajeti ya Serikali iliainisha hatua za kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani ikiwa ni pamoja na kuboresha mazingira ya biashara ili kuvutia uwekezaji, kutumia mifumo ya TEHAMA katika ukusanyaji wa mapato ya Serikali za Mitaa, kutumia Mfumo wa Kielektroniki wa Malipo ya Serikali (GePG), kuimarisha usimamizi wa sheria za kodi ili kudhibiti ukwepaji wa kodi, na kuhamisha jukumu la kuweka alama za kemikali katika bidhaa za petroli kutoka kwa makampuni binafsi kwenda Shirika la Viwango Tanzania (TBS) ili kudhibiti ubora wa Mafuta yanayoagizwa kutoka nje ya Nchi na kudhibiti ukwepaji wa kodi unaotokana na ubadhirifu wa mafuta.

4.2 Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2021/22


Kwa mwaka wa fedha 2021/22, Serikali ilipanga kukusanya na kutumia Sh. trilioni 36.681. Hata hivyo, baada ya kupokea mkopo wa Sh. trilioni 1.311 (Dola za Marekani milioni 567.25) kutoka kwa Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) kwa ajili ya kutekeleza Mpango wa Kukabiliana na hali ya uchumi baada ya kupugua kwa Ugonjwa wa COVID-*19 "Tanzania COVID-19 Socio-Economic Response and Recovery Plan* (TCRP)", bajeti ilifanyiwa marekebisho hadi Sh. trilioni 37.992, ikiwa ni ongezeko la asilimia nne. Mikopo hiyo ilitengwa ili kutekeleza sekta Muhimu ikijumuisha; sekta za afya, elimu, maji, utalii, hifadhi ya jamii, nishati na uwezeshaji wa

kiuchumi. Bajeti iliyofanyiwa marekebisho ya Sh. trilioni 37.992 ilipelekea kuwa na ongezeko la asilimia tisa ya Bajeti ikilinganishwa na Sh. trilioni 34.879 za mwaka wa fedha 2020/21.

4.3 Mgawanyo wa Bajeti ya Matumizi ya Serikali

Katika mwaka wa fedha 2021/22, Serikali ilipanga kutumia Sh. trilioni 37.992 katika mgawanyo wa Sh. trilioni 14.989 kwa matumizi ya Maendeleo na Sh. trilioni 23.003 kwa matumizi ya kawaida. Mgawanyo wa matumizi kwa asilimia kama inavyooneshwa katika **Kielelezo Na. 1**.

Kielelezo Na. 1: Mgao wa Matumizi ya Serikali



Chanzo: *Sheria ya Matumizi ya Serikali ya mwaka, 2021*

4.4 Mwenendo wa Utendaji wa Bajeti

Katika mwaka wa fedha 2021/22, serikali ilikusanya Sh. trilioni 38.298, ikiwa ni zaidi ya bajeti ya Sh. trilioni 37.992 kwa Sh. bilioni 306 au ongezeko la 0.8%. Ikilinganishwa na Sh. trilioni 31.326 zilizokusanywa mwaka 2020/21, Nilibaini ongezeko la 22% sawa na Sh. trilioni 6.972. Tathmini na mwenendo wa makusanyo katika kila chanzo kilichoainishwa ni kama ifuatavyo;

i. Makusanyo ya Kodi

Makusanyo ya kodi ya Tanzania Bara yalikuwa Sh. trilioni 20.945 sawa na 96% ya bajeti ya Sh. trilioni 21.778; hivyo Serikali haikukusanya Sh. bilioni 833. Ikilinganishwa na makusanyo ya Sh. trilioni 17.598 za mwaka 2020/21, nilibaini ongezeko la makusanyo kwa Sh. trilioni 3.347 sawa na ongezeko la 19%.

ii. Makusanyo yasiyotokana na kodi

Makusanyo yasiyotokana na kodi yaliyokusanywa na Wizara, Idara na Sekretarieti za Mkoa na Taasisi nyinginezo yalikuwa Sh. trilioni 2.709 sawa na 89% ya bajeti iliyoidhinishwa ya Sh. trilioni 3.050 hivyo makusanyo ya Sh. bilioni 341 hayakukusanywa. Ikilinganishwa na makusanyo ya Sh. trilioni 2.023 ya mwaka 2021/21, nilibaini ongezeko la makusanyo yasiyotokana na kodi kwa Sh. bilioni 686 sawa na ongezeko la 34%.

iii. Makusanyo ya Serikali za Mitaa

Makusanyo ya Serikali za Mitaa yalikuwa Sh. bilioni 892 sawa na 103% ya bajeti iliyoidhinishwa ya Sh. bilioni 864, hivyo makusanyo ya Sh. bilioni 28 yalikusanywa zaidi. Ikilinganishwa na makusanyo ya serikali za Mitaa ya Sh. bilioni 698 ya mwaka 2020/21, nilibaini ongezeko la makusanyo kwa Sh. bilioni 194 sawa na 28%.

iv. Misaada

Katika mwaka wa fedha 2021/22 Misaada ya Sh. trilioni 1.305 sawa na 115% ya bajeti ya Sh. trilioni 1.138 ilikusanywa hivyo kiasi cha Sh. bilioni 167 zilikusanywa zaidi. Ikilinganishwa na Misaada ya Sh. bilioni 887 iliyopokelewa mwaka 2020/21, nilibaini kuongezeka kwa misaada kiasi cha Sh. bilioni 418 sawa na 47%.

v. Mikopo ya Ndani

Makusanyo yanayotokana na mikopo ya ndani ni pamoja na Ankara za Hazina, hati fungani na ufadhili wa ndani, jumla ya Sh. trilioni 6.489 ikiwa ni 30% zaidi ya bajeti iliyoidhinishwa ya Sh. trilioni 4.989 zilipokelewa. Ikilinganishwa na Mikopo ya Sh. trilioni 4.904 zilizokusanywa mwaka 2020/21 nilibaini ongezeko la mikopo ya ndani ya Sh. trilioni 1.585 sawa na ongezeko la 32%.

vi. Mikopo ya Nje Yenye Masharti Nafuu

Mikopo ya nje yenye masharti nafuu ya Sh. trilioni 4.149 iliyopokelewa katika mwaka wa fedha zaidi ya bajeti ya Sh. trilioni 3.128 kwa Sh. trilioni 1.021 sawa ogezeko la 33%. Ikilinganishwa na Mikopo ya Sh. trilioni 2.028 iliyopokelewa mwaka 2020/21 nilibaini ongezeko la mikopo ya nje yenye masharti nafuu kwa Sh. trilioni 2.121 sawa na ongezeko la 105%.

vii. Mikopo ya Nje isiyo ya masharti nafuu

Mikopo ya nje isiyo ya masharti nafuu ya Sh. trilioni 1.809 iliyopokelewa sawa na 59% ya bajeti ya Sh. trilioni 3.045 hivyo mikopo isiyo ya masharti nafuu ya Sh. trilioni 1.236 haikupokelewa. Ikilinganishwa na mikopo isiyo na Masharti nafuu ya mwaka 2020/21, nilibaini kupungua kwa mikopo isiyo ya masharti nafuu kwa 43% au Sh. trilioni 1.377 ikilinganishwa na Sh. trilioni 3.186 zilizopokelewa mwaka 2020/21. Mwenendo unaoonesha asilimia za makusanyo kutoka katika kila chanzo ni kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 16**.

Jedwali Na. 16: Mwenendo wa asilimia za Makusanyo kutoka kila chanzo kilichoainishwa

Mwenendo wa Bajeti na Makusanyo	2021/22 (Sh. Trilioni)	2020/21 (Sh. Trilioni)	2019/20 (Sh. Trilioni)
Bajeti	37.992	34.879	33.105
Makusanyo	38.298	31.326	31.519
Makusanyo katika %			
Kodi	55%	56%	57%
Makusanyo yasiyotokana na Kodi	9%	9%	8%
Mikopo ya Ndani	17%	16%	16%
Misaada na Mikopo ya Nje	19%	19%	19%


Chanzo: *Taarifa ya Ukaguzi wa Deni la Taifa na Mfuko Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2019/20 hadi 2021/22*

Makusanyo ya ndani, yanajumuisha 55% ya makusanyo ya kodi na 9% ya makusanyo yasiyotokana na kodi, ikiwa ni jumla ya 64% iliyotumika kufadhili matumizi ya serikali, wakati 36% ya matumizi ya Serikali yalifadhiliwa na 17% ya mikopo ya ndani na 19% ya Misaada na mikopo ya nje.

4.5 Mwenendo wa Makusanyo

Katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita, ikijumuisha mwaka wa Fedha 2019/20, 2020/21, na 2021/22, nimebaini kuwepo kwa ongezeko la makusanyo. Hata hivyo tofauti na miaka miwili ya awali ambapo makusanyo yamekuwa chini ya bajeti yaliyoidhinishwa, mwakusanyo ya mwaka 2021/22 yamekuwa zaidi ya bajeti kwa 0.8%, kama inavyooneshwa kwenye **Kielelezo Na. 2** hapo chini.

Kielelezo Na. 2: Mwenendo wa Makusanyo




Mwaka wa Fedha	2021/22	2020/21	2019/20
Bajeti	37.992	34.880	33.105
Makusanyo	38.298	31.326	31.519

Chanzo: *Taarifa ya Ukaguzi wa Deni la Taifa na Mfuko Mkuu kwa mwaka wa Fedha 2019/20 hadi 2021/22*

4.6 Mwenendo wa Makusanyo, Misaada na Mikopo

Makusanyo ya ndani yanayotokana na; kodi, makusanyo yasiyotokana na kodi na makusanyo ya Seikali za Mitaa yalikuwa Sh. trilioni 24.546, wakati misaada na mikopo ilikuwa Sh. trilioni 13.752 (Sh. trilioni 1.305 zilitokana na Misaada na Sh. trilioni 12.447 zilitokana na Mikopo). Mwenendo wa makusanyo, Misaada na Mikopo ilikuwa kama inavyooneshwa kwenye **Kielelezo Na. 3**.

Kielelezo Na. 3: Mwenendo wa Ufandili wa Bajeti



Mwaka wa Fedha	2021/22	2020/21	2019/20
Makusanyo ya Ndani	24.546	20.32	20.51
Misaada	1.305	0.89	1.12
Mikopo	12.447	10.12	9.89

Chanzo: *Ukaguzi wa Deni la Taifa na Mfuko Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2019/20 hadi 2021/22*

4.7 Utekelezaji wa Bajeti

4.7.1 Taratibu za Uhasibu katika Mfuko Mkuu

Ibara ya 135 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inataka makusanyo yote ya Serikali yapokelewe kwenye Mfuko Mkuu iliyopo Benki Kuu ya Tanzania na kusimamiwa na Mhasibu Mkuu wa Serikali. Makusanyo yanayotokana na vyanzo vya Kigeni, ikiwemo makusanyo ya washirika wa Maendeleo "*Development Pertners*", yanajumuisha makusanyo ya akaunti za pamoja "*Basket funds*", Msaada ya kibajeti, Fedha za Miradi zilizopewa idhini ya matumizi "*Exchequer*", pamoja na fedha za miradi zilizopelekwa moja kwa moja kwenye mradi (Fedha za Miradi zinazopewa idhini ya matumizi "*Exchequer*" baada ya kutumiwa) hupokelewa na Taasisi kwa utaratibu wa kupokea idhini ya matumizi "*Exhequer*" ama kupelekwa moja kwa moja kwenye utekelezaji wa Miradi kutoka kwa wafadhili.

Kati ya Sh trilioni 38.298 zilizokusanywa, Sh. trilioni 35.486 zilipokelewa Mfuko Mkuu, hivyo kiasi cha Sh. trilioni 2.812 hakikupokelewa Mfuko Mkuu. Tofauti hiyo inatokana na fedha zilizopelekwa moja kwa moja kwenye mradi kutoka kwa wafadhili, fedha za miradi zilizobaki katika akaunti miliki "*Holding account*", makusanyo ya TRA na makusanyo ya Mamlaka za Serikali

za Mitaa ambayo hayakuripotiwa katika Taarifa ya fedha ya mfuko mkuu hadi kufikia tarehe 30 Juni 2022. Ingawa fedha hizo hazikujumuishwa katika taarifa ya fedha ya mfuko mkuu zilitumika katika shughuli zilizokusudiwa. Aidha ni muhimu Mafungu husika pamoja na Mhasibu Mkuu wa Serikali kuhakikisha fedha hizo zinaripotiwa katika Taarifa za Fedha za Mfuko Mkuu. Maelezo zaidi ni kama yalivyoainishwa katika **Jedwali Na. 17**.

Jedwali Na. 17: Kusuluhisha Ukusanyaji Halisi wa Mapato na Amana katika Mfuko Mkuu wa Hazina (Kiasi katika Sh. Trilioni)

Maelezo	Bajeti	Makusanyo	Fedha zilizopokelewa Mfuko Mkuu	Tofauti	Sababu za uwepo wa Tofauti
Kodi	21.778	20.945	20.762	0.183	Makusanyo ya TRA ambayo hayakuletwa Mfuko Mkuu hadi 30 Juni 2022
Makusanyo yasiyotokana na Kodi	3.05	2.709	2.709	-	
Makusanyo ya Serikali za Mitaa	0.864	0.892	0.784	0.108	Makusanyo ya Serikali za Mitaa ambayo hayajaripotiwa Mfuko Mkuu
Misaada	1.138	1.305	1.267	0.038	Fedha za Miradi zilizopokelewa katika akauti za Wafadhili
Mikopo ya Ndani	4.989	6.489	6.489		
Mikopo ya Nje isiyo na masharti nafuu	3.045	1.809	1.809		
Mikopo ya Nje yenye masharti Nafuu	3.128	4.149	1.656	2.493	Fedha zilizopelekwa moja kwa moja kwenye Miradi

NATIONAL AUDIT OFFICE NAOT

Maelezo	Bajeti	Makusanyo	Fedha zilizopokelewa Mfuko Mkuu	Tofauti	Sababu za uwepo wa Tofauti
Makusanyo Mengine	-	-	0.01	(0.01)	Makusanyo mengine yaliyopokelewa Mfuko Mkuu
Jumla	**37.992**	**38.298**	**35.486**	**2.8118**	

Chanzo: *Ukaguzi wa Mfuko Mkuu*

4.7.2 Nakisi katika Mfuko Mkuu

Jumla ya Fedha zilizotolewa Mfuko Mkuu ili kufadhili miradi ya maendeleo na matumizi ya kawaida katika mwaka wa fedha 2021/22 zilikuwa jumla ya Sh. trilioni 36.063 dhidi ya fedha zilizopokelewa za jumla ya Sh. trilioni 35.486 hivyo kusababisha nakisi ya Sh. bilioni 577 katika mfuko mkuu hadi kufikia tarehe 30 Juni 2022. Maelezo kuhusu Makusanyo na matumizi ya fedha kutoka Mfuko Mkuu ni kama ilivyoainishwa katika **Jedwali Na. 18**.

Jedwali Na. 18: Makusnyo dhidi ya Matumizi yaliyofanywa katika Akaunti ya Mfuko Mkuu

Maelezo ya Makusanyo na Fedha zilizohamishwa	Kiasi Sh. Trilioni
Kodi	20.762
Makusanyo yasiyotokana na Kodi	2.709
Makusanyo ya Serikali za Mitaa	0.784
Misaada	1.267
Mikopo ya Ndani	6.489
Mikopo ya Nje	3.465
Makusanyo mengine	0.01
Jumla ya Makusanyo Mfuko Mkuu (A)	**35.486**
Fedha zilizotolewa kwa Wizara na Idara	36.871
Fedha zilizorudishwa kwa wahusika	0.009
Fedha zilizorudishwa	(0.817)
Fedha halisi zilizotolewa (B)	**36.063**
Nakisi katika Mfuko Mkuu (A-B)	**(0.577)**

Chanzo: *Ukaguzi Mfuko Mkuu*

4.8 Fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kwa Mashirika ya Serikali Kuu

Jumla ya fedha zilizotolewa Mfuko Mkuu kwa matumizi ya Serikali Kuu, ikijumuisha; Wizara, Wakala, Tume na Idara zilikuwa Sh. trilioni 29.350.wakati Sh. trilioni 7.521 zilitolewa kwa Matumizi Ofisi ya Raisi TAMISEMI pamoja na Tawala za Mikoa na serikali za mitaa, Taarifa za matumizi hayo zimechambuliwa katika Ripoti Kuu ya Mwaka ya Mamlaka za Serikali za Mitaa. Usimamizi wa bajeti, fedha zilizotolewa pamoja na matumizi yaliyofanyika ni kama yanavyoelezwa:

4.8.1 Makadirio Yaliyoidhinishwa na kutolewa kwa Hazina kwa Matumizi ya Kawaida


Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Wizara,Wakala na Idara ulibaini kuwa Sh. trilioni 17.754 sawa na 98% zilitolewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida dhidi ya bajeti yaliyoidhinishwa ya Sh. trilioni 18.090. Ikilinganishwa na fedha zilizotolewa mwaka 2020/21 Sh. trilioni 16.280, nilibaini ongezeko la fedha zilizo tolewa kwa matumizi ya Kawaida kwa Sh. trilioni 1.474 sawa na asilimia tisa.

4.8.2 Fedha Zilizotolewa na Matumizi Yaliyofanyika

Matumizi ya Kawaida yaliyofanywa na Wizara, Wakala na Idara yalikuwa Sh. trilioni 17.541 sawa na 99% ya fedha zilizotolewa kiasi cha Sh. trilioni 17.754 hivyo Sh. bilioni 213 hazikutumika na kurudishwa kwa mlipaji mkuu wa Serikali (PMG).Ikilinganishwa na matumizi ya Kawaida ya mwaka 2020/21 ya Sh. trilioni 16.247 nilibaini ongezeko la matumizi ya kawaida ya Sh. trilioni 1.294 sawa na asilimia nane.

Ni maoni yangu kuwa, uwepo wa bakaa ya fedha zisizotumika unamaanisha kutotekelezwa au utekelezaji hafifu wa shughuli zilizokusudiwa, ama uwezo hafifu wa Taasisi katika kutumia fedha zilizotolewa kwa wakati.Maelezo ni kama ilivyoainishwa katika **Kielelezo Na. 4**.

Kielelezo Na. 4: Makadirio, Fedha zilizotolewa na Matumizi halisi ya Fedha za Matumizi ya Kawaida kwa kipindi cha Miaka Mitatu



Mwaka wa Fedha	2021/22	2020/21	2019/20
Bajeti	18.090	17.460	16.185
Fedha zilizotolewa	17.754	16.281	15.899
Fedha zilizotumika	17.541	16.248	15.860

Chanzo: *Vitabu vya Bajeti, Taarifa ya Mabadiliko ya Bajeti na Taarifa ya Fedha zilizotolewa*

4.8.3 Udhibiti Usiotosheleza wa Usimamizi wa Bajeti

Kifungu cha 45 cha Sheria ya Bajeti, Sura ya 439 R.E 2020 kinampa mamlaka Maafisa Masuuli kusimamia matumizi ya serikali yanayotolewa Mfuko Mkuu, zaidi ya hayo, fedha zinazopelekwa kwenye Mafungu zinapaswa kulingana na matumizi na bajeti zilizoidhinishwa kulingana na upatikanaji wa fedha.

Nilibaini baadhi ya Mafungu yalipokea fedha chini ya bajeti iliyoidhinishwa, hata hivyo Mafungu saba yalipokea jumla ya Sh. bilioni 258.36 zaidi ya bajeti iliyoidhinishwa. Hii inashiria kutokuwepo kwa udhibiti wa ndani wa usimamizi wa bajeti.

Nilifahamishwa kwamba Wizara ya Fedha na Mipango ipo katika mchakato wa kuunganisha Mfumo wa Usimamizi wa Bajeti Kuu (CBMS) na MUSE ili kuwezesha fedha zinazotolewa kutumia Mfumo wa Bajeti (CBMS) ili kupunguza makosa yanayoweza kujitokeza. Maelezo ya Mafungu yaliyopokea fedha zaidi ya Bajeti ni kama ilivyo ainishwa katika **Jedwali Na. 19**.

Jedwali Na. 19: Fedha zilizotolewa zaidi ya Bajeti

Fungu	Taasisi	Bajeti ya Mwisho Sh.	Fedha zilizotolewa Sh.	Fedha zilizotolewa zaidi Sh.
52	Wizara ya Afya	1,183,656,385,983	1,406,909,874,583	223,253,488,599
40	Mahakama ya Tanzania	158,411,571,612	183,634,245,440	25,222,673,828
96	Wizara ya Habari Utamaduni na Michezo	37,057,329,846	41,637,114,445	4,579,784,599
71	Sekretarieti ya Mkoa wa Pwani	284,198,861,015	288,086,789,739	3,887,928,724
27	Msajili wa vyama vya Siasa	20,578,228,697	21,198,195,771	619,967,074
51	Wizara ya Mambo ya Ndani	35,527,789,569	36,018,949,451	491,159,883
24	Tume ya Maendeleo ya Ushirika	12,803,378,000	13,109,940,536	306,562,536
Jumla				258,361,565,243

Chanzo: *Ukaguzi wa Mfuko Mkuu kwa mwaka wa Fedha 2021/22*

Ni mapendekezo yangu kwa Wizara ya Fedha na Mipango kuimarisha udhibiti wa bajeti ya serikali na kuhakikisha Mfumo wa Usimamizi wa Bajeti (CBMS) na MUSE unaunganishwa ili kuzuia mapungufu katika utekelezwaji wa Bajeti.

4.8.4 Matumizi ya Kawaida Yaliyofanywa nje ya Bajeti

Kifungu cha 27 (4) cha Sheria ya Bajeti ya Mwaka 2015 kinaeleza baada ya Bajeti kuidhinishwa, inapaswa kutumika/kuelekezwa katika madhumuni yaliyokusudiwa na ndani ya mipaka iliyowekwa katika makadirio au bajeti. Nilibaini kuwa taasisi saba zilitumia jumla ya Sh. bilioni 1.46 katika matumizi ya kawaida nje ya madhumuni na bajeti iliyoidhinishwa na bila kupata kibali cha uhamisho na kuruhusu matumizi hayo kujumuishwa katika bajeti ya matumizi ya mwaka, jambo ambalo ni kinyume na utekelezaji wa bajeti ilizoidhinishwa hivyo kuzuia kufikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa na jambo linaliweza kupelekea usimamizi mbaya wa fedha zilizotolewa. Maelezo yanaoneshwa kwenye **Jedwali Na. 20**.

Jedwali Na. 20: Taasisi zenye Matumizi nje ya Bajeti Iliyoidhinishwa

Taasisi	Aina ya Taasisi	Kiasi (Sh.)
Mfuko wa Maendeleo ya Mifugo(LDF)	Mfuko	15,000,000
Hospitali ya Rufaa ya Musoma	Hospitali ya Rufa	77,290,000
Wizara ya Kilimo	Fungu 43	31,500,000
Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA)	Fungu 15	266,872,268
Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA)	Mamlaka	99,767,680
SUMA JKT – Kampuni ya Ulinzi	Taasisi nyingine	173,914,000
Shirika la Nyumbu (TATC)	Taasisi nyingine	799,402,000
Jumla		**1,463,745,948**

Chanzo: *Taarifa ya Ukaguzi ya mwaka 2021/22*

Ni mapendekezo yangu kwa Maafisa Masuuli wa Taasisi husika kuhakikisha kuwa matumizi yanayofanyika yanaendana na bajeti iliyoidhinishwa na kwamba uhamishaji wowote wa fedha unapitiwa na kuidhinishwa kabla ya utekelezwaji ili kuendana na Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015 kwa madhumuni ya kuongeza ufanisi katika usimamiwaji ya Bajeti na matumizi ya rasilimali ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.


4.8.5 Makadirio Yaliyoidhinishwa na Fedha Zilizotolewa kwa ajili ya matumizi ya Maendeleo

Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Wizara na Idara ulibaini Sh. trilioni 11.595 sawa na 99.5% zilitolewa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo dhidi ya bajeti iliyoidhinishwa ya Sh. trilion 11.653. Ikilinganisha na Sh. trilioni 9.267 za mwaka 2020/21, nilibaini ongezeko la Sh. trilioni 2.328 sawa na 25%.

4.8.6 Fedha zilizotolewa kwa Matumizi ya Maendeleo na Matumizi Halisi

Matumizi ya Maendeleo katika Wizara na idara yalikuwa Sh. trilioni 11.397 sawa na 98 % ya fedha zilizotolewa kiasi cha Sh. trilioni 11.595 hivyo bakaa ya Sh. bilioni 198 hazikutumika hadi mwisho wa mwaka na kurudishwa Mfuko Mkuu. Ikilinganishwa na matumizi ya maendeleo ya mwaka 2020/21 ya Sh. trilioni 9.032 nilibaini ongezeko la matumizi ya maendeleo kwa Sh. trilioni 2.365 sawa na 26%. Maelezo ni kama ilivyoainishwa katika **Kielelezo Na. 5**.

Kielelezo Na. 5: Makadirio, Fedha zilizotolewa na Matumizi Halisi ya Fedha za Maedeleo katika kipindi cha Miaka Mitatu



Mwaka wa Fedha	2021/22	2020/21	2019/20
Bajeti	11.653	10.942	10.588
Fedha zilizotolewa	11.595	9.267	7.011
Fedha zilizotumika	11.397	9.032	6.852

Chanzo: *Taarifa za fedha zilizokaguliwa za Wizara na Idara*

NAOT



SURA YA TANO

USIMAMIZI WA UKUSANYAJI WA MAPATO YA KODI, DENI LA TAIFA, HUDUMA ZA SERIKALI, UKAGUZI WA AWALI WA MAFAO YA WATUMISHI WALIOMALIZA MUDA KAZINI NA HESABU JUMUIFU ZA SERIKALI

5.1 Utangulizi

Sura hii inazungumzia masuala yanayohusu Usimamizi wa ukusanyaji wa Mapato, Deni la Taifa, Huduma za Serikali,Ukaguzi wa awali wa mafao ya watumishi waliomaliza muda kazini na Hesabu jumuifu za serikali.

5.2 Usimamizi wa Ukusanyaji wa Mapato Unaofanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania

Mamlaka ya Mapato Tanzania ilianzishwa kwa Sheria ya Bunge Na. 11 mwaka 1995 yenye jukumu la kusimamia bila upendeleo makusanyo yote ya kodi za ndani, ushuru wa forodha na tozo kwa niaba ya Serikali kuu. Mamlaka ya Mapato inaongozwa na Kamishina Mkuu. Inaundwa na idara nne za kiutendaji kati ya hizo idara tatu zinahusika moja kwa moja na ukusanyaji wa mapato ambazo ni Idara ya kodi za ndani, Idara ya walipakodi wakubwa na Idara ya Ushuru wa Forodha. Idara ya nne ni ya upelelezi wa kodi inayoshughulikia udanganyifu na ukwepaji wa kodi wa makusudi.

5.3 Ukusanyaji wa Mapato Tanzania

Kwa mwaka wa fedha 2021/22 Mamlaka ya Mapato ilikusanya jumla ya Sh. bilioni 20,944.67 kwa Tanzania Bara ukilinganisha na makisio yaliyowekwa ya Sh. bilioni 21,778.10, makusanyo hayo ni pungufu kwa kiasi cha Sh. bilioni 833.43 sawa na 3.8% ya makisio ya makusanyo. Pia, ilikusanya kiasi cha Sh. bilioni 359.19 kwa Zanzibari ukilinganisha na makisio yaliyowekwa ya Sh. bilioni 413.06. Makusanyo hayo ni pungufu kwa kiasi cha Sh. bilioni 53.87 sawa na 13.0% ya makisio ya makusanyo kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 21** na **Jedwali Na. 22**.

Jedwali Na. 21: Mchanganuo wa Makusanyo ya Mapato (Tanzania Bara)

Idara	Makisio (Sh. Bilioni)	Makusanyo halisi (Sh. Bilioni)	Makusanyo ziada (pungufu)	
			(Sh. Bilioni)	%
Kodi za ndani	4,336.19	3,977.71	(358.48)	(8.3)
Walipa kodi Wakubwa	9,007.40	9,216.32	208.93	2.3
Ushuru na Forodha	8,696.57	8,746.29	49.73	1.0
Jumla ya Makusanyo	**22,040.15**	**21,940.33**	**(99.82)**	**(0.5)**
Marejesho ya kodi na hamisho	262.05	995.66	733.61	280.0
Makusanyo kamili	**21,778.10**	**20,944.67**	**(833.43)**	**(3.8)**

Chanzo: *Taarifa za Makusanyo za Mapato zilizokaguliwa 2021/22*

Jedwali Na. 22: Mchanganuo wa Makusanyo ya Mapato (Zanzibar)

Idara	Makisio (Sh.Bilioni)	Makusanyo Halisi	Makusanyo ziada (pungufu)	
		(Sh. Bilioni)	(Sh. Bilioni)	%
Kodi za ndani	197.46	173.43	(24.03)	(12.2)
Ushuru na Forodha	215.61	185.76	(29.85)	(13.8)
Jumla ya Makusanyo	**413.06**	**359.19**	**(53.87)**	**(13.0)**


Chanzo: *Taarifa za Makusanyo za Mapato zilizokaguliwa 2021/22*

Utendaji wa idara ya Kodi za ndani katika ukusanyaji mapato uko chini ya makisio yaliyowekwa kwa mwaka 2021/22 wakati Idara ya Walipakodi wakubwa na Idara ya Ushuru na Forodha Ukusanyaji wa mapato upo juu ya makisio yaliyowekwa kwa mwaka 2021/22. Pamoja na mambo mengine, athari za vita nchini Ukraine ilikuwa ni miongoni mwa sababu zilizopelekea kushuka kwa makusanyo kwa Idara ya Kodi za ndani.

Ulinganifu wa idara (Tanzania Bara) unaonesha kuwa Idara ya Walipakodi Wakubwa ilichangia 42.0% ya makusanyo ikifuatiwa na Idara ya Ushuru na forodha iliyochangia 39.9% na Kodi za ndani 18.1%. Kiwango hiki hakihusishi makusanyo ya hati za misamaha kutoka Serikalini. Wakati ulinganifu wa idara (Zanzibari) unaonesha kuwa idara ya Ushuru na forodha ilichangia 51.7% na Kodi za ndani 48.3% ya makusanyo halisi. Ukusanyaji wa mapato


halisi kwa mwaka wa fedha 2021/22 na 2020/21 kwa idara unaoneshwa na **Kielelezo Na. 6** na **Kielelezo Na. 7.**

Kielelezo Na. 6: Ulinganifu wa Uchangiaji wa Makusanyo Halisi kwa Idara 2021/22 na 2020/21 (Tanzania bara)



Chanzo: *Taarifa za Mahesabu ya Mapato za Mamlaka zilizokaguliwa 2021/22 na 2020/21*

Kielelezo Na. 7: Ulinganifu wa Uchangiaji wa Makusanyo halisi kwa Idara 2021/22 na 2020/21 (Zanzibari)



***Chanzo**: Taarifa za Mahesabu ya Mapato za Mamlaka zilizokaguliwa 2021/22 na 2020/21*

Ulinganifu wa uchangiaji wa makusanyo halisi ya mapato kiidara kwa mwaka wa fedha 2021/22 na 2020/21 unaonesha makusanyo kwa Idara zote tatu yameongezeka ambapo Idara ya Walipakodi Wakubwa kwa 27.4%, Idara ya Kodi za ndani kwa 20.5% na Idara ya Ushuru na forodha kwa 19.9%. Aidha, ulinganifu unaonesha ukusanyaji wa mapato kwa idara ya kodi za ndani upo nyuma ya idara nyingine licha ya juhudi zinazochukuliwa na Mamlaka. Kwa ujumla, idara za Walipakodi Wakubwa na Ushuru na forodha ziliweza kufikia malengo yaliyopangwa wakati Idara ya Kodi za ndani haikuweza kufikia malengo yaliyopangwa kwa mwaka 2021/22.

5.3.1 Mwenendo wa Ukusanyaji wa Mapato

Mwenendo wa ukusanyaji wa Mapato wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miaka mitano umeoneshwa kwenye **Jedwali Na. 23**. Kwa miaka mitano iliyopita imeonesha makusanyo kuimarika kila mwaka kasoro kwa mwaka 2020/21 yalishuka kwa 0.2% ikilinganishwa na mwaka 2019/20.

Jedwali Na. 23: Mwenendo wa Ukusanyaji wa Mapato wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzia 2017/18 hadi 2021/22 (Tanzania Bara & Zanzibar)

Mwaka wa Fedha	Makisio (Sh. Bilioni)	Makusanyo Halisi (Sh. Bilioni)	Makusanyo ya Juu /(Chini)	%
2021/22	22,191.17	21,303.87	(887.30)	(4.0)
2020/21	20,709.32	17,897.86	(2,811.46)	(13.6)
2019/20	19,451.12	17,930.88	(1,520.25)	(7.8)
2018/19	18,332.67	15,764.66	(2,568.00)	(14.0)
2017/18	17,365.05	15,405.40	(1,959.65)	(11.3)

Chanzo: *Taarifa za Mahesabu ya Mapato za Mamlaka zilizokaguliwa 2017/18 hadi 2021/22*

Aidha, kwa mwaka wa fedha 2021/22 utendaji wa Mamlaka ulionesha kupanda kwa kiwango cha mapato ya kodi (uwiano wa kodi kwa Pato la Taifa) wa 12.5% ukilinganisha na 11.6% mwaka 2020/21, hata hivyo, kwa miaka minne iliyopita mwendo wa ukusanyaji mapato (uwiano wa kodi kwa Pato la Taifa) umeonekana ni wa kupanda na kushuka kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 24**.

Jedwali Na. 24: Uwiano wa kodi kwa Pato la Taifa kwa Tanzania na nchi nyingine za Afrika Mashariki kwa Miaka Mitano

Nchi	2017/18	2018/19	2019/20	2020/21	2021/22
Kenya	15.4%	15.5%	14.6%	13.7%	15.0%
Rwanda	15.6%	16.3%	15.9%	15.9%	15.8%
Tanzania	13.4%	11.4%	12.2%	11.6%	12.5%
Uganda	14.2%	15.1%	12.1%	13.0%	13.5%
Burundi	13.0%	14.8%	15.8%	16.5%	19.2%

Chanzo:*Kamati ya Kiufundi ya Mamlaka za Mapato za Afrika Mashariki*

Ni maoni yangu kwamba kuna ufanisi katika ukusanyaji wa kodi nchini Tanzania,kwenye makusanyo halisi na malengo kuongeza nafasi ya kuboreshwa kwa kuongeza juhudi katika kukusanya mapato kwa kuongeza wigo wa kodi, kuziba uvujaji wa mapato na kuhamasisha ulipaji wa kodi kwa hiari. Hatua hizi zote zitapunguza nakisi ya fedha ya nchi (fiscal deficit) na pengo la ufadhili wa deni.

5.3.2 Mapungufu katika Ukaguzi wa Bidhaa na Uhifadhi katika Bandari ya Zanzibar

Mapitio yangu ya ripoti ya matengenezo ya Kitambazo (Scanner) ya bandari ya Zanzibar ya mwaka 2021/22 yalibaini tatizo la kuharibika mara kwa mara Kitambazo cha mizigo ambapo ilipelekea Ukaguzi wa mizigo inayoingizwa na kusafirishwa nje ya nchi kufanyika bila kupita kwenye mashine (Manual Inspection), hivyo kupelekea mazingira magumu ya kufanya kazi. Aidha, ziara ya kutembelea bandari ilibaini kutokuwepo kwa eneo la kutosha kwa ajili ya ukaguzi, hivyo kupelekea ukaguzi wa mizigo na makontena kufanyika kwa sehemu tu, na sio kwa ukamilifu kama inavyohitajika kutokana na kutokuwepo kwa eneo la kutosha la ukaguzi na kuhifadhi bidhaa zinazosubiri kibali cha forodha. Kwa sababu ya ufinyu wa nafasi, sikuweza kuthibitisha kontena zilizokaa muda mrefu bandarini ambazo zilikabidhiwa kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania idara ya forodha na ushuru.

Naishauri Serikali kupitia Mamlaka ya Mapato; kubadilisha Kitambazo (scanner) katika eneo la bandari ya Zanzibar kwakuwa iliyopo imethibitika kuwa haiwezi kufanya kazi ipasavyo; kuruhusu kutolewa kwa moja kwa moja kwa bidhaa zenye mfanano (homogenous) kwenda

kwenye maghala ya wateja; na Kuweka utaratibu kufanya ukaguzi maalum wa bidhaa hizo.

5.3.3 Mafuta Yaliyokaa Muda Mrefu bila ya kutolewa kwenye Matanki ya Makampuni ya Mafuta (Oil Marketing Companies) yaliyoingizwa kwa Utaratibu wa Ghala la Dhamana (Bonded warehouse) yenye Kodi Iliyotathminiwa ya Sh. Bilioni 2.60

Nilibaini jumla ya lita 3,293,306 za mafuta yenye kodi iliyotathminiwa ya Sh. 2,602,504,091 yaliyoingizwa nchini chini ya utaratibu wa ghala la dhamana (Bonded warehouse-IM7 regime) na kuhifadhiwa kwenye matanki ya Makampuni ya uuzaji wa mafuta kwa muda wa zaidi ya miezi sita bila kibali cha nyongeza ya siku kutoka kwa Kamishna kama ilivyoainishwa chini ya Kifungu cha 57(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Ushuru na Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EACCMA, [Toleo la mwaka2 017]) au nia ya kubadilisha utaratibu na kuuzwa ndani ya nchi kwa mafuta yaliyokaa muda mrefu.

Naishauri Serikali kupitia Mamlaka ya Mapato ihakikishe; mafuta yote yaliyokaa muda mrefu yanatolewa na kwenda sehemu zinazotakiwa kwa wakati au yabadilishiwe utaratibu wa kuuzwa ndani ya nchi baada ya kulipwa kwa kodi stahiki ili kuepuka kuchelewa kwa ukusanyaji wa mapato ya serikali; Inaimarisha mfumo wa kodi za forodha (TANCIS) ili kutatua changamoto zinazowakabili waagizaji.

5.3.4 Kutokuwepo kwa Mfumo wa Ufuatiliaji wa Matukio/malalamiko kwa Watumiaji wa Nje wa Mifumo ya Mamlaka na kutotatuliwa kwa Wakati kwa Matukio/malalamiko Yaliyoripotiwa

Ukaguzi wangu ulibaini ukosefu wa mfumo kwa wateja wa nje ya Mamlaka (walipakodi) kwa ajili ya kutoa taarifa za matukio/malalamiko ya kimfumo pindi watumiapo mifumo husika, hususani mifumo mikuu kama mfumo wa kodi za forodha (TANCIS), mfumo wa kutolea risiti za kielektroniki (EFDMS), mfumo wa kielektroniki wa kuwasilisha ritani za kodi (e-filing), mfumo wa kusajili utambuzi wa walipakodi (TIN) n.k.

Pia Ukaguzi wangu ulibaini Kuchelewa au kuchukua muda mrefu katika kushughulikia matukio yaliyoripotiwa kwenye mfumo ambapo matukio ya kipaumbele yalitumia muda kati ya siku 3 hadi 365 na kwa kiwango sawa na

74% ikiwa ni matukio 9,729 kati ya 13,147 yaliyoripotiwa mpaka tarehe ya ukaguzi 30/9/2022.

Hii ilichangiwa na ukosefu wa kanzidata ya kina ya maarifa kwa matukio ya kielektroniki yaliyoripotiwa na kutatuliwa kwa ajili ya matumizi ya mrejeo.

Naishauri Serikali kupitia Mamlaka ya Mapato; Kuanzisha mfumo wa kuripoti matukio/malalamiko kwa watumiaji wa nje (Walipakodi) wa mifumo ya Mamlaka na uunganishwe na mfumo wa kuripoti matukio/malalamiko ya ndani kwa msingi wa maarifa, uangalizi na usimamizi wa matukio/malalamiko, na utatuzi wa matukio/malalamiko kwa wakati uliobainishwa/kuripotiwa kwenye tovuti ya Mamlaka kama sehemu ya msingi wa maarifa kwa wateja kwa kuanzisha mapitio ya kila siku na kila saa ya usimamizi wa matukio/malalamiko yaliyoripotiwa na utatuzi wa masuala ya kipaumbele hasa yale yanayohusiana na mifumo ya Kodi kama vile TANCIS, e-filing, n.k.

5.3.5 Kutofuata Sheria za Kodi kwa Walipakodi Waliosajiliwa kama Wajumuishi (Consolidators)

Nilipitia kampuni zinazofanya kazi kama wajumuishi (Consolidators), wanaunganisha mizigo kwa wasafirishaji wadogo wadogo wanaoagiza bidhaa kutoka nje kwa kiasi kidogo kwenye kontena moja, na kisha kuondoa bidhaa bandarini baada ya kulipa kodi na ushuru kama waagizaji. Hata hivyo, wajumuishi (Consolidators) wanakamilisha taratibu za forodha za kutoa bidhaa zilizoagizwa kutoka nje kwa kutumia utambulisho wao wa ulipakodi (TIN), kulipa kodi na tozo kwa majina yao wenyewe, na kutoa risiti za kielektroniki (EFD) kwa wateja wao ambayo inajumuisha kodi, ada nyinginezo na kamisheni ya huduma.

Zaidi ya hayo, nililinganisha marejesho ya kodi ya ongezeko la thamani (VAT) na taarifa za fedha za wajumuishi (Consolidators) nakubaini kuwa kamisheni ya huduma pekee ndio inayooneshwa kwenye taarifa za fedha, lakini si thamani ya ankara (Invoice) kama inavyoonekena kwenye stakabadhi za kielektroniki. Hii ina maana kwamba hakuna kodi ya ongezeko la thamani kwenye mauzo (Output tax) inayoripotiwa kwa ankara zinazotolewa kupitia mashine za EFD, wakati kwa upande mwingine wateja wanadai kodi zote za ongezeko la thamani kwenye manunuzi (Input tax)

kama zilivyooneshwa kwenye risiti. Pia ilibainika kuwa kodi za ongezeko la thamani kwenye manunuzi (Input tax) inayodaiwa na wateja inajumuisha Kodi la ongezeko la thamani na kodi nyingine ambazo wajumuishi walilipa kwa niaba ya wateja wao. Hili ni kinyume na Notisi ya Serikali Namba 337 ya mwaka 2018 inayosimamia uendeshaji wa biashara za ujumuishaji na inawataka wajumuishi kutangaza bidhaa zote zinazoingizwa nchini, kulipa kodi na tozo wenyewe.

Naishauri Serikali kupitia Mamlaka ya Mapato ihakikishe kuwa wajumuishi wote wanakuwa na mashine mbili za EFD, moja kwa ajili ya kutoa risiti kwa waagizaji na nyingine kwa ajili ya kutambua kamisheni kama mapato ili kupunguza mianya ya upotevu wa mapato.

5.3.6 Kodi Zilizoshikiliwa kwenye Mahakama za Rufani za Kikodi kiasi cha Sh. Trilioni 4.84

Katika ukaguzi wangu wa hesabu za Mamlaka ya Mapato kwa mwaka wa fedha 2021/22 nilibaini kuwepo kwa mashauri 904 ya kikodi katika mahakama za rufani za kikodi kwa muda mrefu yenye thamani ya Sh. trilioni 4.84 (inahusisha Dola za Marekani 15,713,232 zilizobadilishwa kwa Sh. 2,292.733/dola ya Marekani) kwa Tanzania Bara. Wakati Zanzibar ilikuwa na mashauri 34 ya kodi yenye thamani ya jumla ya Sh. bilioni 3.43 kama ilivyoainishwa katika **Jedwali Na. 25, Jedwali Na. 26, Jedwali Na. 27, Jedwali Na. 28** na **Jedwali Na. 29** mtawalia.

Jedwali Na. 25: Mashauri ya Kikodi yaliyopo kwenye Mahakama ya Rufani ya Tanzania (CAT) (Tanzania Bara)

Mwaka	Idadi ya kesi	Kiasi (Sh.)	Dola za Kimarekani
2020	4	107,394,526,329.70	-
2021	29	67,925,678,515.56	8,622,162.00
2022	22	57,585,495,328.97	3,972,164.00
Total	**55**	**232,905,700,174.23**	**12,594,326.00**

Chanzo: *Taarifa za hesabu Mamlaka ya Mapato mwaka 2021/22 na uhakiki kwa mahakama za rufani za kodi*

Jedwali Na. 26: Mashauri ya Kikodi yalipo Mahakama ya Rufaa ya Mapato ya Kodi

Mwaka	Idadi ya kesi	Kiasi (Sh.)	Dola za Kimarekani
2018	1	586,364,625.00	-
2019	1	28,831,566,835.03	-
2020	1	49,729,889,875.00	-
2020	98	302,054,644,621.10	-
2021	36	90,989,739,506.33	-
Total	137	**472,192,205,462.46**	-

Chanzo: *Taarifa za hesabu Mamlaka ya Mapato mwaka 2021/22 na uhakiki kwa mahakama za rufani za kodi*

Jedwali Na. 27: Kesi za Kikodi zilizopo Katika Bodi ya Rufani ya Mapato ya kodi

Mwaka	Idadi ya Kesi	Kiasi (Sh.)	Dola za Kimarekani
2016	3	18,282,472,925.09	-
2017	3	12,912,426,197.70	-
2018	11	60,945,372,214.27	-
2019	17	195,923,137,711.45	-
2020	80	607,988,096,474.86	-
2021	311	949,197,145,522.94	2,926,106.65
2022	287	2,250,000,247,715.26	192,799.80
Jumla	**712**	**4,095,248,898,761.57**	**3,118,906.45**

Chanzo: *Taarifa za hesabu Mamlaka ya Mapato mwaka 2021/22 na uhakiki kwa mahakama za rufani za kodi*

Jedwali Na. 28: Mashauri ya Kikodi yalipo Mahakama ya Rufaa ya Mapato ya

Mwaka	Idadi ya Kesi	Kiasi (Sh.)	Dola za Kimarekani
2019	1	10,700,323.54	-
2020	1	19,696,833.24	-
Jumla	**2**	**30,397,156.78**	**-**

Chanzo: *Taarifa za hesabu Mamlaka ya Mapato mwaka 2021/22 na uhakiki kwa mahakama za rufani za kodi*

Jedwali Na. 29: Kesi za Kikodi Zilizopo Katika Bodi ya Rufani ya Mapato ya kodi

Mwaka	Idadi ya kesi	Kiasi (Sh.)	Dola za Kimarekani
2019	3	553,356,111.84	-
2020	8	2,074,155,974.50	-
2021	20	558,652,753.69	-
2022	1	211,449,420.00	-
Jumla	**32**	**3,397,614,260.03**	**-**

Chanzo: *Taarifa za hesabu Mamlaka ya Mapato mwaka 2021/22 na uhakiki kwa mahakama za rufani za kodi*

Naishauri Serikali kupitia TRAB,TRAT na CAT kuharakisha usikilizwaji na uamuzi wa mashauri yaliyoyopo kwenye Mahakama za Rufani za kikodi.

5.4 Mapato Yasiyo ya Kodi

Sehemu hii inatoa muhutasari kwa maeneo yanayohusiana na usimamizi wa Makusanyo. Lengo kuu la ukaguzi wa makusanyo ni kuhakikisha makusanyo yanakusanywa kwa usahihi, ili kuhakikisha ufanisi katika udhibiti wa ndani katika makusanyo unapatikana, na kuhakikisha makusanyo yaliyokusanywa yanatambuliwa.

Malengo ya Taasisi yanaweza kufikiwa pale ambapo makusanyo yanakusanywa kikamilifu na kutumika katika utekelezwaji wa mikakati iliyokusudiwa. Kwakuwa rasilimali za umma ni chache, Serikali inapaswa kusimamia vizuri makusanyo yanayokusanywa, na kuhakikisha inatekeleza bajeti kwa ufanisi. Katika mwaka wa fedha 2021/22, nilitathmini uzingatiwaji wa Sheria, Kanuni na maagizo mbalimbali ya usimamizi wa Mapato na kubaini mapungufu katika ukusanyaji wa mapato kama inavyooneshwa katika aya zifuatazo:

5.4.1 Makusanyo Yaliyokusanywa bila ya kuwa na Kanuni Zinazosimamia Ukusanyaji wake Tume ya TEHAMA Sh. Milioni 786.44

Moja ya madhumuni ya kuanzishwa kwa Tume ya TEHAMA ni kutoa ushauri, mipango mkakati, utekelezaji, uwekezaji katika TEHAMA, kuratibu mipango ya Kitaifa ya TEHAMA, kuwajengea uwezo, kuwaidhinisha na kudhibiti ubora wa wataalamu wa TEHAMA;

Nilibaini, Tume ilikusanya Sh. milioni 786.44 kutoka katika vyanzo mbalimbali. Vyanzo vikuu vya mapato haya ni ada za maombi ya kitaaluma zinazotozwa kwa kiwango cha Sh. 20,000 kwa kila ombi, ada za usajili wa mwaka kwa wanachama Sh. 20,000 na ada za usajili za mwaka kwa wataalamu waliosajiliwa Sh. 75,000 kwa kila mwanachama na ada nyinginezo kwa viwango tofauti.

Hata hivyo, nilibaini kuwa Tume haina kanuni zinazosimamia na kuhalalisha viwango vinavyotumika katika makusanyo na msingi wa utekelezaji wake. Jambo linaloweza kusababisha kutokusanywa au kutofautiana kwa viwango vya utozwaji.

Ninapendekeza Tume ya TEHAMA iweke utaratibu ikiwa ni pamoja na kuweka sheria na/au kanuni za kusimamia makusanyo ili kupata uhalali wa ukusanyaji na kuongeza wigo wa ukusanyaji.

5.4.2 Kutosimamiwa kwa Muongozo wa Tozo ya Maendeleo ya Umwagiliaji na Tume ya Umwagiliaji

Kifungu cha 52(2) (g) cha Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji ya mwaka 2013 kinaeleza kuwa fedha zozote zinaweza kukusanywa katika Mfuko wa umwagiliaji kama itakavyoelekezwa na kupitishwa na Sheria au kama ilivyoidhinishwa na Tume, kupitia Kifungu cha 1.4.1(vi) cha Mwongozo wa Uendeshaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Umwagiliaji ya Agosti 2020 Tume inaidhinisha ukusanywaji wa tozo ya maendeleo ya umwagiliaji kwa Taasisi binafsi au watu wanaofanya shughuli za Umwagiliaji sawa na asilimia 0.3 ya mauzo.

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa Tume ilishindwa kusimamia ukusanywaji wa tozo ya maendeleo ya umwagiliaji kutoka taasisi binafsi zinazojihusisha na

kilimo cha umwagiliaji. Hii ilitokana na kushindwa kuwatambua wakulima wa sekta binafsi zinazojishugulisha na kilimo cha umwagiliaji na uelewa mdogo miongoni mwa wakulima. Hivyo kuifanya tume kushindwa kukusanya tozo kutoka kwa Taasisi binafsi au wakulima kama inavyotakiwa. Kutokusanywa kwa mapato yanayotokana na chanzo hiki kilichotambuliwa kunazuia ukusanywaji wa makusanyo ambayo yangeweza kutumika katika kugharamia shughuli nyingine za maendeleo ya Serikali.

Ni mapendekezo yangu kwa Tume kufanya uhakiki na kutambua Taasisi binafsi zinazojihusisha na shughuli za umwagiliaji na kutoa uelewa wa tozo ya maendeleo ya umwagiliaji ili kuhakikisha tozo ya umwagiliaji inakusanywa na kuboresha makusanyo ya Serikali.

5.4.3 Upotevu wa Mapato Unaotokana na Ukodishwaji wa Mitambo Usiofuata taratibu Sh. Milioni 919.60

Moja ya majukumu ya TEMESA ni kuandaa programu madhubuti ya huduma za kukodisha vifaa na kuhakikisha wakala unakuwa chanzo cha kuaminika cha huduma za ukodishwaji wa Mitambo na vifaa. (vifaa ni pamoja na magari na mitambo). Ili kutekeleza jukumu hilo Wakala anapaswa kuandaa programu madhubuti ya huduma za kukodisha vifaa, ambayo ni pamoja na kutunza rejista ya ukodishaji kwa kuzingatia Kanuni ya 261(2) na (3) ya Kanuni ya Fedha za Umma ya mwaka 2001. Madhumuni ya rejista ya ukodishaji ni kunakili tarehe ya kukodisha, taarifa za mteja aliyekodishwa, malipo ya kukodisha, na tarehe ambayo mtambo unapaswa kurejeshwa.

Nilibaini upotevu wa mapato kiasi cha Sh. milioni 919.60 uliotokana na kukodisha mitambo bila makubaliano ya kimkataba na kutokukusanywa kwa makusanyo ya ukodishaji kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2011 hadi 2022. Hali inayoonesha kukosekana kwa usimamizi na udhibiti katika ukodishaji wa mitambo hivyo kupelekea ubadhilifu wa makusanyo na mali za umma, matumizi mabaya ya mtambo na Wakala kushidwa kukusanya mapato ya ukodishwaji. Matokeo yake TEMESA ilitoa taarifa ya upotevu wa Mtambo wa kusaga kokoto hali inayopelekea upotevu wa mapato ambayo yangekusanywa kutokana na ukodishwaji wa mtambo huo.

Ni mapendekezo yangu kwa Wakala kufanya uchunguzi wa kina juu ya ubadhilifu uliofanyika wa Sh. milioni 919.60 na kuchukua hatua

madhubuti, aidha Wakala unapaswa kusimika mfumo wa kufuatilia ukodishwaji wa mitambo, kuweka makubaliano ya wazi ya kimkataba, sheria na masharti kwa kila ukodishaji, kuratibu ada za ukodishaji, na kuboresha mchakato wa ufuatiliaji na ukusanyaji wa malipo ili kuhakikisha ukodishaji wote umeidhinishwa na kutozwa hati za madai ipasavyo kwa lengo la kuongeza makusanyo yanayotokana na huduma za kukodisha mitambo.

5.4.4 Kutotozwa kwa Makusanyo ya Sh. Bilioni 8.43

Nilipitia usimamizi wa makusanyo kwa idara na Wakala mbalimbali na kubaini kiasi cha Sh. bilioni 8.43 hizikutozwa na Idara ya Zimamoto, Mahakama ya Tanzania na Wakala wa Majengo Tanzania licha ya kutolewa kwa huduma, kama ilivyoelezwa hapa chini;

a) Ada za Ukaguzi wa Usalama wa Moto kutoka Idara ya Zimamoto Sh. Milioni 223

Kupitia Kifungu cha 22(2) cha Sheria ya Zimamoto na Uokoaji cha mwaka 2021 kilichofanyiwa marekebisho na Kanuni ya 14(1) ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji (Ukaguzi wa Usalama) ya mwaka 2014 iliyofanyiwa marekebisho, inaitaka Idara ya Zimamoto kukagua usanifu wa majego kwa ajili ya usalama wa moto kabla ya kutolewa kwa kibali cha ujenzi na mamlaka husika na kukusanya tozo ya ukaguzi baada ya kukagua.

Nilibaini kuwa ofisi za zimamoto Mwanza na Dodoma hazikutoza ada ya ukaguzi kwa wamiliki wa majengo 55 yaliyokaguliwa kwa ajili ya usalama wa moto, hivyo kufanya tozo ya ukaguzi inayotakiwa kukusanywa ya Sh. milioni 223 kutokusanywa. Nilifahamishwa kuwa kushindwa kukusanywa kwa makusanyo hayo kumetokana na ubovu wa mfumo wa ukusanyaji, jambo ambalo linachelewesha ukusanyaji wa mapato ya Serikali ambayo yangeweza kutumika kugharamia shughuli nyingine zilizopangwa.

b) Tozo ya Riba Inayotokana na Kuchelewa Kulipa Kodi ya Wakala wa Majengo Tanzania katika Majengo ya Serikali yaliyopangishwa Sh. Bilioni 8.1

Kifungu 5.2 cha Mkataba wa upangishaji baina ya Mtendaji Mkuu - Wakala wa Majengo Tanzania na wapangaji wa nyumba za Serikali kinamtaka wakala

kukusanya malipo ya 20% kama riba ya ada kwa wapangaji watakaoshindwa kulipa Kodi kwa muda wa miezi mitatu mfululizo.

Nilibaini, Wakala anadai jumla ya kodi ya Sh. bilioni 40.51 kwa zaidi ya miezi mitatu, hata hivyo riba ya Sh. bilioni 8.1 kama malipo yanayotokana na ucheleweshwaji, haikutozwa kwa wapangaji husika kinyume na kifungu 5.2 cha mkataba wa upangaji. Kushindwa kutoza makusanyo yatokanayo na ucheleweshwaji wa malipo ya kodi kunahalalisha ukiukwaji wa mkataba wa upangishaji.

Nilifahamishwa kuwa Wakala yuko katika hatua za mwisho za kuboresha mfumo wake wa ukusanyaji wa kodi za majengo utakaowezesha kutoza tozo za moja kwa moja kama riba na kutuma hati ya madai moja kwa moja kwa wapangaji kupitia ujumbe wa simu ili kurahisisha utozwaji wa riba

c) Makusanyo ya kodi katika Jengo la Mahakama Lililopangishwa Sh. Milioni 109.7

Nilibaini, Mahakama ya Tanzania ilipangisha sehemu ya Ofisi yake kwa watoa huduma za kibenki na mgahawa kwa wapangaji watatu tofauti katika kipindi cha miaka miwili kuanzia tarehe 9 Novemba 2021 hadi tarehe 8 Novemba 2023. Wapangaji walitakiwa kulipa kodi ya kila mwezi kwa ajili ya matumizi ya Ofisi zilizopangishwa. Hata hivyo, ilibainika kuwa Mahakama haikutoza tozo za kodi zinazohitajika kiasi cha Sh. milioni 109.7 kwa zaidi ya miezi 15 kama ilivyoainishwa katika **Jedwali Na. 30**.

Jedwali Na. 30: Ada za Kukodisha Majengo Ambazo Hazijakusanywa

Ofisi iliyopangishwa	**Kiasi (Sh.)**
Kituo Jumuishi cha utoaji Haki Temeke	45,000,000
Kituo Jumuishi cha utoaji Haki Kinondoni	37,500,000
Mahakama Kuu Masijala Kuu	27,200,000
Jumla	109,700,000

Chanzo: *Taarifa ya Ukaguzi ya Mwaka 2021/22*

Ni mapendekezo yangu kwa Maafisa Masuuli wanaohusika kuhakikisha; Riba inatozwa kwa wapangaji wa Majengo ya Serikali wanaoshindwa kulipa kodi kwa wakati ili kuhimiza ulipwaji wa kodi. Afisa Zimamoto wa Mikoa wahakikishe mfumo wa ukusanyaji unafanya kazi ipasavyo na kuhakikisha wamiliki wa majengo wanalipa deni lao bila kuchelewa. Zaidi ya hayo, Mahakama ya Tanzania ikusanye kodi kwa wapangaji

waliokodisha ofisi katika Majengo yake na kukusanya kiasi ambacho hakijalipwa ili kuongeza mapato ya Serikali kwa shughuli za kijamii na maendeleo.

5.4.5 Kutokusanywa kwa Kodi za Nyumba Zilizopangishwa kwa Taasisi za Serikali Sh. Bilioni 13.104

Wakala wa Majengo Tanzania ilianzishwa kwa dhamira ya kutoa makazi bora kwa Serikali na watumishi wa umma. Wakala iliingia mikataba 125 na Taasisi mbalimbali za Serikali ili kutoa makazi kwa watumishi wa umma wa Taasisi husika ambapo Taasisi zinatakiwa kuilipa TBA kodi ya kila mwezi kama ilivyoainishwa kwenye mkataba wa upangaji.

Hata hivyo, nilibaini kuwa Taasisi za Serikali zinachelewa kulipa kodi inayotakiwa jumla ya Sh. bilioni 13.10 kwa mujibu wa mkataba wa upangaji kwa muda wa miezi 10 hadi 115, hivyo kupunguza ukusanyaji wa mapato kupitia chanzo hiki, fedha ambazo zingeweza kuelekezwa katika kutekeleza shughuli zilizopangwa, ikiwa ni pamoja na ujenzi wa nyumba mpya na ukarabati wa nyumba za Serikali zilizochakaa.

Ninapendekeza Wakala wa Majengo Tanzania kuhakikisha wapangaji wa Taasisi husika wanakumbushwa kulipa kodi ambazo hazijalipwa. Aidha, Wakala inashauriwa kuanzisha utaratibu wa makato ya kodi katika mishahara moja kwa moja kwa watumishi wa umma wanaokaa katika nyumba za serikali badala ya kutegemea malipo ya hiari kutoka kwa wapangaji.

5.4.6 Kushindwa Kuchukua Hatua dhidi ya Wanunuzi Waliokiuka Mkataba wa Mauzo ya Nyumba za Serikali Sh. Milioni 874.3

Kifungu cha 2.9 cha Mikataba ya Mauzo ya Nyumba za Serikali kati ya TBA na wanunuzi kinaelekeza kuwa wanunuzi (watumishi wa umma) wanapaswa kulipa 10% ya bei ya mauzo kama malipo ya awali wakati wa kusaini mkataba, wakati 90% iliyobaki italipwa kwa mujibu wa Jedwali la Malipo kama ilivyoainishwa katika Mkataba ndani ya miaka mitatu hadi saba. Aidha, mnunuzi akishindwa kufanya malipo ndani ya mwezi mmoja kutoka tarehe ya kumilikishwa kutapelekea malipo ya riba ya asilimia 16% ya malipo yaliyochelewa, aidha iwapo kutakuwa na ucheleweshaji wa mfululizo

unaozidi miezi sita toka kumilikishwa utapelekea kusitishwa kwa makubaliano.

Nilibaini kuanzia mwaka 2017 hadi 2020 TBA iliingia mkataba wa mauzo na wanunuzi nane wa nyumba za Serikali katika Mradi wa Bunju wenye thamani ya Sh. bilioni 1.1 mikataba ilihitaji malipo yakamilike ndani ya miaka mitatu. Hata hivyo, wanunuzi hao walikiuka makubaliano hayo kwa kutolipa kiasi cha Sh. milioni 874.3 ndani ya muda waliokubaliwa, wakati muda wa mkataba ukiwa umekwisha kwa zaidi ya kipindi cha mwezi 1 hadi miaka 5 na mkataba ya mauzo ukiwa bado haijasitishwa, hali inayoathiri ukwasi wa Wakala katika kufadhili shughuli nyingine za uwekezaji.

Wakala anapaswa kuchukua hatua dhidi ya utekelezaji wa makubaliano ya mauzo na kukusanya mapato ambayo hayajalipwa kutoka kwa wanunuzi wanaokiuka mikataba, Aidha tozo ya riba inapaswa kukusanywa kwa wanunuzi waliokiuka mikataba ya mauzo. Zaidi ya hayo, ushauri wa kisheria unapaswa kuzingatiwa ili kusitisha makubaliano ya mauzo yaliyokiuka mikataba na kuchelewa kulipa kwa zaidi ya miezi sita ili kuruhusu nyumba hizo ziuzwe kwa wanunuzi wanaotimiza wajibu wao wa kifedha katika mikataba ya mauzo.

5.4.7 Kutokusanywa kwa Ada ya usafirisha Mizigo iliyozidi ukubwa wa mzigo ulioidhinishwa Dola za Marekani 18,112,547 (Sh. Bilioni 41.48)

Kwa mujibu wa Kanuni ya 3 (1) (C) ya Kanuni za Jumuiya ya Afrika Mashariki inayohisiana na usafirishaji wa Mizigo (Mizigo Maalumu) ya mwaka 2018, mzigo wowote unaozidi uzito ulioidhinishwa unachukuliwa kuwa ni mzigo wenye uzito mkubwa na lazima usafirishwe kwa kibali maalumu pale unapopita katika mtandao wa Barabara Kuu na za Mikoa. Zaidi ya hayo, wasafirishaji wanapaswa kulipa ada ya ziada kwa mizigo iliyozidi uzito ulioidhinishwa wa gari. Kanuni hii iliwekwa ili kulinda usalama wa barabara na kupunguza uharibifu wa mtandao wa barabara.

Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi ilitoa vibali 13 vya usafirishaji wa mizigo maalumu kwa ajili ya kusafirisha mashine umba "*transformer*" na vinu vya umeme kwa ajili ya Mradi wa kuunganisha Umeme kati ya Kenya-Tanzania. Vibali hivyo vilihitaji malipo ya ziada ya Dola za Marekani 19,513,863.20

gharama ambazo zilionekana kuwa ni kubwa na kusababisha ongezeko kubwa la gharama za mradi. Hivyo TANESCO ililipa ada ya ziada ya Dola za Marekani 1,401,316 kwa niaba ya mkandarasi huku malipo ya ziada ya Dola 18,112,547 sawa na Sh. bilioni 41.48 hazikukusanywa kinyume na matakwa ya Kanuni 18 za Sheria ya Mizigo Maalumu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya 2018.

Kushindwa kulipa ada iliyobaki ya Dola za Marekani 18,112,547 sawa na Sh. bilioni 41.48 ijapokuwa mizigo hiyo yenye uzito mkubwa iliyosafirishwa kunazuia ukusanyaji wa mapato yaliyokusudiwa kufidia uharibifu wa miundombinu ya barabara wakati wa usafirishaji wa mizigo hiyo kati ya tarehe 30 Septemba 2021 na 4 Oktoba 2022.

Ni mapendekezo yangu kwa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kusisitiza umuhimu wa kuzingatia kanuni za usafirishaji wa mizigo maalum ili kulinda mtandao wa barabara na kupunguza uharibifu wa miundombinu ya barabara. Aidha, Wizara inatakiwa kukusanya malipo ya ziada ya Dola za Marekani 18,112,547 sawa na Sh. bilioni 41.48

5.4.8 Kusitishwa kwa Mkataba wa Ujenzi na Kusababisha Upotevu wa Mapato ghafi Sh. Milioni 974.37

Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) ilikabidhiwa jukumu la kutoa huduma bora za makazi kwa Ofisi kwa Serikali na watumishi wa Umma pamoja na kutoa huduma za ushauri kuhusiana na Ujenzi wa majengo ya Serikali.

Katika kufanya hivyo, TBA iliingia mkataba na Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Kakonko kwa ajili ya Ujenzi wa Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Kakonko Awamu ya Tatu kupitia mkataba namba LGA/139/HQ2018-2019/W/08 kwa muda wa miezi 18 kwa gharama ya Sh. bilioni 1.838. Kazi hiyo ilianza tarehe 1 Desemba 2018 na ilitarajiwa kukamilika tarehe 4 Novemba 2021.

Nilibaini kuwa Wakala ameshindwa kukamilisha mradi kulingana na muda wa mkataba licha ya kuongezewa muda na mwajiri mara kadhaa. Nilibaini zaidi kuwa utendaji duni ulisababisha mwajiri kusitisha mkataba wakati mwenendo wa kazi ulikuwa umefikia 47%. Hadi wakati wa kusitishwa TBA ilikuwa imekamilisha kazi zenye thamani ya Sh. milioni 864.063 na kushindwa kukamilisha kazi zilizobaki zenye thamani ya Sh. milioni 974.37.

Kushindwa kukamilisha kazi kwa wakati kumeinyima Wakala fursa ya kupata mapato ghafi ya Sh. milioni 974.37 na kuathiri uwezo wa kugharamia utekelezaji wa shughuli nyingine za uwekezaji.

Ninapendekeza TBA iimarishe mfumo wa udhibiti wa ndani ili kuhakikisha usimamizi bora wa miradi ya ujenzi kama chanzo cha makusanyo

5.4.9 Kutouzika kwa Vitalu 43 vya Uwindaji kwa Zaidi ya Miaka Minne na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania

Kifungu cha 38 (1) na (11), cha Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori, 2021 kinataka kuundwa kwa Kamati ya Ushauri ya Ugawaji na vitalu vya Uwindaji, ambayo itakuwa na jukumu la kumshauri Waziri kuhusu ugawaji wa vitalu vya uwindaji kwa njia ya mnada, zabuni au utaratibu mwingine wowote kwa uwazi na kuendana na misingi ya utawala bora.

Nilibaini Mamlaka ilikuwa na vitalu 111 vya kuwinda vilivyotakiwa kuuzwa katika mnada katika mwaka 2018 hadi 2022, hata hivyo Wakala alifanikiwa kupiga mnada vitalu 78 na kuuza vitalu 68 huku vitalu 43 vilivyobakia vikiwa havijauzwa kwa muda wa mwaka mmoja hadi minne. Nilifahamishwa kwamba vitalu vya uwindaji ambavyo havijauzwa vinachangiwa na mazingira yasiyofaa ya wanyamapori katika pori la akiba jambo linalosababishwa na shughuli za kibinadamu ikiwemo uvamizi na malisho ya mifugo.

Kutouzika kwa vitalu vya uwindaji kwa muda mrefu kunaathiri mifumo ya ikolojia ya wanyama na kuzuia kupatikana kwa mapato ya Serikali ambayo yangeweza kupatikana kupitia utalii wa picha.

Ninapendekeza Serikali na mamlaka zinazohusika zihakikishe mazingira mazuri ya usimamizi wa Vitalu vya Uwindaji kwa kuzuia shughuli za kibinadamu kwenye vitalu vya uwindaji vilivyotengwa na kuwavutia wazabuni wakati wa mchakato wa mnada.

5.4.10 Kutokodishwa kwa Nafasi za Wazi katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere zenye Thamani ya Sh. bilioni 3.72

Dhamira ya TAA ni kutoa huduma za hali ya juu katika uwanja wa ndege kwa usalama na ya ufanisi ufaao kwa watumiaji/wadau wa uwanja wa ndege ili kuchangia ukuaji wa kijamii na kiuchumi. Hivyo, Serikali imeongeza miundombinu ya jengo la abiria na viwanja vya ndege katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere hadi kufikia uwezo wa kuhudumia abiria milioni 8 kwa mwaka.

Ukaguzi ulibaini kuwa kwa sasa uwanja wa ndege una hudumia abiria milioni 3 badala ya uwezo uliopangwa wa abiria milioni 8 kwa mwaka na kusababisha matumizi duni ya miundombinu ya uwanja kwa abiria milioni 5 kwa mwaka, hali ambayo imepelekea kutokodishwa kwa baadhi ya miundombinu iliyotengenezwa kwa dhumuni hilo katika Majengo ya Uwanja kwa mita za mraba 1,330.05 ambazo zingeweza kukusanya Sh. bilioni 3.72 kwa mwaka.

Kushindwa kupata mwekezaji katika eneo la baadhi ya miundombinu iliyopo katika kiwanja kunainyima Mamlaka makusanyo ambayo yangeweza kutumika katika utekelezaji wa shughuli nyingine za maendeleo za Mamlaka.

Ni mapendekezo yangu kwa Mamlaka kuandaa mikakati ya masoko ili kuwashawishi wawekezaji, kuweka mazingira rafiki ya kibiashara ili kuvutia mashirika ya ndege na biashara nyinginezo.

5.4.11 Makusanyo Yaliyokusanywa nje ya Mfumo wa Sh. Bilioni 69.47

Serikali kupitia bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/22, ilipitisha sera, mikakati, na hatua mbalimbali za kiutawala ikiwa ni pamoja na matumizi ya Mfumo wa Kielektroniki wa Malipo wa Serikali (GePG). Zaidi ya hayo, Kifungu cha 7 cha Sheria ya Fedha za Umma, Sura ya 348 9 (Toleo la mwaka 2020) inahitaji pesa zote za umma kukusanywa kupitia mfumo wa GePG.

Hata hivyo, nilibaini kuwa katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2022, taasisi nne zilikusanya jumla ya Sh. bilioni 69.47 kama makusanyo yasiyo tokana na kodi nje ya mfumo wa malipo serikalini GePG, kinyume na Sheria ya Fedha za Umma. Aidha nilibaini kuwa 99% ya fedha zilizoripotiwa

zilitokana na jumuia 2631 za watoa huduma ya maji ngazi ya jamii (CBWSO) ambazo hazijajaunganishwa na mfumo wa ukusanyaji wa mapato bali zinategemea ukusanyaji wa fedha taslimu zinazotumiwa na vyombo hivyo katika uendeshwaji wa shughuli zake. Maelezo zaidi ni kama ilivyooneshwa katika **Jedwali Na. 31**.

Jedwali Na. 31: Makusanyo Yaliyokusanywa Nje ya Mfumo wa GepG

Jina la Taasisi	Kiasi(Sh.)
Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA)	68,239,841,453
Tume ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano	151,542,600
Shirika la Mzinga	181,902,250
Shirika la Magereza	900,688,851
Jumla	**69,473,975,154**

Chanzo: *Taarifa ya Ukaguzi ya Mwaka 2021/22*

Ni rai yangu kwamba, makusanyo taslimu bila kupitia mfumo wa GePG yanaweza kupelekea hatari za uvujaji na upotevu wa mapato, hivyo kuongeza kasi ya nakisi ya bajeti.

Hivyo basi, ninapendekeza Taasisi zote za Serikali zenye dhamana ya kukusanya mapato kutafuta ufumbuzi wa changamoto mbalimbali zinazoathiri ukusanyaji wa mapato kupitia mfumo, ili kuendana na mikakati ya Serikali, sera na hatua za kiutawala zilizobainishwa katika kusimamia ukusanywaji wa mapato kupitia mfumo wa GePG.

5.4.12 Kutokuwa na Uhakika wa Ukusanywaji wa Madai yaliyoripotiwa kwenye Taarifa za Fedha za TEMESA Sh. Bilioni 10.31

Nilibaini TEMESA iliripoti madai ya Sh. bilioni 53.76 katika taarifa za fedha hadi tarehe 30 Juni 2022, madai yaliyoripotiwa yalitokana na wateja mbalimbali ambao wamepewa huduma mbalimbali na Wakala ikiwa ni pamoja na: matengenezo ya magari yanayomilikiwa na Serikali, mitambo, umeme, elekitroniki/na TEHAMA, mifumo ya viyoyozi na majokofu katika majengo yote ya Serikali.

Nilifanya uthibitisho wa madai hayo kwa wadaiwa 25 wanaodaiwa jumla ya Sh. bilioni 14.67 na kubainisha kuwa taasisi husika zilithibitisha kudaiwa na Wakala kiasi cha Sh. bilioni 4.36 pekee hivyo kuleta sintofahamu ya kukusanya madai ya kiasi cha Sh. bilioni 10.31. Hali hiyo inachangiwa na

kutokuwepo kwa usuluhishi wa taarifa baina ya Wakala na wateja kuhusiana na huduma zinazotolewa, upatikanaji wa nyaraka za madai na ulipwaji wa madai. Aidha, kutokuwa na uhakika juu ya ukusanyaji wa madai ya Wakala kuna athiri mtaji wa Wakala katika utekelezaji wa shughuli zilizopangwa.

Ni pendekezo langu kwa Wakala kuhakikisha usuluhishi wa taarifa za madai unafanyika mara kwa mara baina ya Wakala na wateja ili kuhakikisha usahihi wa ankara ambazo hazijalipwa na kupunguza uwepo wa madai yaliyo katika sintofahamu ya ukusanywaji na kuimarisha uwezo wa kifedha wa Wakala.

5.4.13 Kutokusanywa kwa Makusanyo Yasiyotokana na Kodi ya Sh. Bilioni 397.34

Makusanyo yasiyotokana na Kodi ni makusanyo mengine isipokuwa makusanyo ya kodi. Yanaweza kujumuisha vyanzo mbalimbali kama vile faini, ada, mrabaha na vyanzo vinginezo vya makusanyo. Katika mwaka wa fedha 2021/22 makusanyo yasiyotokana na kodi yalikadiriwa kuchangia asilimia nane ya Bajeti ya Serikali ikiwa ni chanzo muhimu cha makusanyo ya Serikali.

Nilipitia taarifa za fedha za Wizara, Wakala na Taasisi mbalimbali na kubaini madai ya Sh. bilioni 397.34 yaliripotiwa kama madai ambayo hayakukusanywa baada ya huduma mbalimbali kutolewa. Aidha, sehemu kubwa ya makusanyo yaliyoripotiwa haijalipwa kwa zaidi ya miezi 12 na hivyo kuzuia mchango wake katika kugharamia matumizi ya Serikali. Maelezo ya Taasisi na madai husika ni kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 32**;

Jedwali Na. 32: Madai ya Makusanyo yasiyotokana na Kodi

Jina	Kiasi (Sh.)
Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano (NICTBB)	39,411,810,000
Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (FETA)	34,947,796
Wakala wa Ndege za Serikali (TGFA)	214,591,775,165
Wakala wa Mbegu za Kilimo (ASA)	1,529,457,845
Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA)	1,907,532,595
Jeshi la Polisi Tanzania	10,019,744,287
Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi	129,843,019,153
Total	**397,338,286,841**

Chanzo: *Taarifa ya Ukaguzi ya Mwaka 2021/22*

Ni mapendekezo yangu kwa Serikali na mamlaka zinazohusika kuandaa utaratibu wa kukusanya madai yasiyotokana na kodi ambayo hayajalipwa kwa madhumuni ya kuongeza ukwasi wa Taasisi na kugharamia bajeti ya Serikali kupitia makusanyo haya ambayo hayajakusanywa.

5.4.14 Kukosekana kwa Mchanganuo wa vyanzo vya Makusanyo yanayokusanywa katika Ushuru wa Kivuko cha Magogoni - Kigamboni na Ada ya Mlangoni katika Viwanja vya Benjamini Mkapa Sh. Bilioni 3.084

Ili kuongeza makusanyo na kugharamia bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2021/22 sera na mikakati mbalimbali iliandaliwa ili kuimarisha ukusanyaji wa mapato ikiwa ni pamoja na kusisitiza matumizi sahihi ya mifumo ya TEHAMA.

Kuzingatia sera hiyo Kituo cha Taifa cha Kuhifadhi taarifa za Mtandao cha Shirika la simu Tanzania (NIDC) kiliingia mkataba wa makusanyo na TEMESA ili kutoa mfumo wa kielektroniki wa tiketi za makusanyo katika kivuko cha Magogoni-Kigamboni kwa kamisheni ya asilimia nne kutoka katika makusanyo yatokanayo na mfumo huo.

Aidha, NIDC pia iliingia makubaliano na Wizara ya Habari, Utamaduni Sanaa na Michezo ili kutoa mfumo wa kielektroniki wa tiketi za makusanyo katika Viwanja vya Benjamin William Mkapa na Uhuru kwa kiwango cha kamisheni ya asilimia 5.5 kutoka katika makusanyo ya mfumo huo.

Katika Makubaliano hayo NIDC ilitakiwa kutoa taarifa za kina kwa kila robo mwaka na kutoa maelezo ya kiasi kilichokusanywa kama vile idadi na aina ya abiria na magari yanayovuka katika kivuko cha magogoni-kigamboni ili kupata idadi kamili ya abiria waliovuka na kiasi kinachopaswa kukusanywa pamoja na idadi ya watu waliohudhuria michezo kwenye Uwanja huo.

Nilibaini kuwa jumla ya Sh. bilioni 3.084 zilitumwa na NIDC kwa Taasisi hizo kama makusanyo kwa mwaka wa fedha 2021/22 ambapo; Sh. bilioni 2.8 zilitumwa TEMESA na Sh. milioni 284.14 zilitumwa kwa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Hata hivyo, NIDC ilishindwa kutoa taarifa za kina ikijumuisha; idadi na aina ya abiria na magari yanayovuka katika kivuko cha magogoni-kigamboni pamoja na idadi ya watu waliohudhuria michezo katika Uwanja wa Benjamini na Uhuru, badala yake taasisi hizo zilipewa haki ya kuangalia mwenendo wa makusanyo kwenye mfumo ambayo haikuweza kutoa mchanganuo wa makusanyo yote. Hivyo sikuweza kuthibitisha usahihi wa kiasi kilichokusanywa na kuripotiwa, hali inayoweza kuashiria hatari ya uvujaji wa makusanyo yaliyokusanywa.

Ni mapendekezo yangu kwa uongozi wa TEMESA na Wizara ya Habari, Utamaduni Sanaa na Michezo kuwasiliana na NIDC ili ripoti za robo mwaka zitolewe kwa mujibu wa makubaliano. Pia, TEMESA na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, kuhakikisha kuwa ripoti za makusanyo zinazotolewa na NIDC zinahakikiwa mara kwa mara ili kuhakikisha uwajibikaji na usimamizi wa mapato na kupunguza fursa za udanganyifu na ubadhirifu wa fedha za umma.

5.5 Usimamizi wa Deni la Serikali

Deni la Serikali linajumuisha madeni yote inayodaiwa Serikali ndani na nje ya nchi kupitia Serikali Kuu na wakala zake. Kwa madhumuni ya ufanisi katika usimamizi wa deni, Waziri wa Fedha na Mipango amepewa mamlaka ya kipekee ya kukopa kwa niaba ya Serikali mikopo ya nje na ndani, na kutoa dhamana kwa niaba ya Serikali kama ilivyobainishwa chini ya vifungu 3,6, na 13 vya Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada Na.30 ya mwaka 1974 kama ilivyorejewa mwaka 2004 na marekebisho yake mengine ya mara kwa mara.


5.5.1 Mchanganuo wa Deni la Serikali

Deni la Serikali kufikia tarehe 30 Juni 2022 lilikuwa Sh. bilioni 71,312.42 ikilinganishwa na Sh. bilioni 64,519.63 lililoripotiwa mwaka 2020/21. Kuna ongezeko la Sh. bilioni 6,792.79 (10.5%) ikilinganishwa na Sh. bilioni 7,762.93 (13.7%) kwa mwaka uliopita.

Deni la Serikali linajumuisha deni la ndani na nje Sh. bilioni 24,040.11 na Sh. bilioni 47,272.31 kwa mwaka wa fedha 2021/22 mtawalia, ikilinganishwa na Sh. bilioni 18,934.61 na Sh. bilioni 45,585.02 kwa mwaka

2020/21. **Kielelezo Na. 8** kinaonesha mwenendo wa ukuaji wa deni kwa mwaka 2019/20 hadi 2021/22.

Kielelezo Na. 8: Mwenendo wa Ukuaji wa Deni la Serikali



	2019/20	2020/21	2021/22
Jumla ya Deni	56,757	64,520	71,312
Deni la Nje	41,242	45,585	47,272
Deni la Ndani	15,515	18,935	24,040

Chanzo: *Hesabu za fedha fungu 22-deni la Serikali kwa mwaka 2019/20 hadi 2021/22*

5.5.2 Mwenendo wa Deni la Ndani

Kwa mwaka 2021/22 deni la ndani limeongezeka kwa Sh. bilioni 5,105.49 sawa na 27% ya deni la ndani lililoripotiwa mwaka 2020/21. Mwenendo wa ukuaji wa deni la ndani kuanzia mwaka 2019/20 hadi 2021/22 umeoneshwa kwenye **Jedwali Na. 33**.

Jedwali Na. 33: Mwenendo wa Deni la Ndani (Deni Halisi)

Mwaka wa fedha	Thamani ya deni	Ongezeko	
	(Sh. Bilioni)	(Sh. Bilioni)	Asilimia
2021/22	24,040	5,105	27
2020/21	18,935	3,420	22
2019/20	15,515	652	4

Chanzo: *Hesabu za fedha fungu 22-deni la Serikali kwa mwaka 2019/20 hadi 2021/22*

Vilevile, ukaguzi wangu ulibaini Serikali ilikopa jumla ya Sh. bilioni 8,555.63. Kati ya hizo, Sh. bilioni 1,757.75 (21%) zilikuwa mikopo ya muda

mfupi na Sh. bilioni 6,797.88 (79%) zilikuwa mikopo ya muda mrefu kama ilivyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 34**.

Jedwali Na. 34: Mwenendo wa Ukopaji wa Ndani (Thamani Halisi)

Ukopaji	2021/22		2020/21		2019/20	
	Sh. Bilioni	%	Sh. Bilioni	%	Sh. Bilioni	%
Muda mrefu	6,798	79	3,219	49	3,099	58
Muda Mfupi	1,758	21	3,331	51	2,236	42
Jumla	**8,556**	**100**	**6,550**	**100**	**5,335**	**100**

Chanzo: *Hesabu za fedha fungu 22-deni la Serikali kwa mwaka 2019/20 hadi 2021/22*

Ongezeko la deni la ndani linatokana na kukopa kwa malengo ya kulipia dhamana za Serikali zilizoiva na kufidia mapungufu ya kibajeti.

5.5.3 Mwenendo wa Deni la Nje

Deni la nje kufikia tarehe 30 Juni 2022 lilikuwa Sh. bilioni 47,272.29 ikiwa ni ongezeko la Sh. bilioni 1,687.29 sawa na asilimia nne ikilinganishwa na deni la Sh. bilioni 45,585 lililoripotiwa mwaka 2020/21 kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 35**.

Jedwali Na. 35: Mwenendo na Mseto wa Deni la Nje

Wakopeshaji	2021/22		2020/21		2019/20	
	Sh. Bilioni	%	Sh. Bilioni	%	Sh. Bilioni	%
Taasisi za Kimataifa	28,729	61	26,556	58	24,150	59
Nchi Marafiki	5,208	11	5,098	11	4,773	12
Benki za kuwezesha biashara ya Forodha	5,973	13	6,384	14	6,257	15
Wakopeshaji	7,363	16	7,547	17	6,062	15
Jumla	47,272	100	45,585	100	41,242	100
Ongezeko	1,687	4	4,343	10	3,001	8

Chanzo: *Jedwali la Mwenendo wa Deni la Serikali kwa Mwaka 2019/20 hadi 2021/22*

Nilibaini ongezeko la deni la nje lilitokana na ukopaji kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo pamoja na kushuka kwa thamani ya sarafu za wakopeshaji dhidi ya shilingi.

5.5.4 Uchambuzi wa Uhimilivu wa Deni

Katika mapitio yangu ya taarifa ya uchambuzi wa uhimilivu wa deni iliyoandaliwa na Wizara ya Fedha Novemba, 2022 nilijiridhisha kuwa deni la Serikali ni himilivu.

Uwiano wa thamani ya sasa (Present value) wa Deni la Serikali (deni la nje na deni la ndani) na Pato la Taifa (GDP) ni asilimia 32.5 ambayo ni chini ya kiwango ukomo/elekezi cha 55% kwa kipindi chote cha makadirio.

Hali kadhalika, uwiano wa thamani ya sasa (Present value) ya Deni la Nje (present value of Public and Publicly Guaranteed External Debt) na Pato la Taifa (GDP) ni 18.1% ikiwa pia ni chini ya kiwango ukomo/elekezi cha 40% kwa kipindi chote cha makadirio. Uwiano wa thamani ya sasa ya deni na mauzo ya nje (Exports) ni 119.6% chini ya kikomo 180%. Uwiano wa kulipa madeni (Debt service) na Mauzo ya Nje (Exports) ni asilima 13.5 chini kidogo ya kikomo cha asilimia 15 na uwiano wa malipo ya madeni na mapato ni asilimia 14.1 chini kidogo ya kikomo asilimia 18.

Hata hivyo katika uchanganuzi wa unyeti iwapo deni la serikali litakabiliwa na mshtuko, uwiano wa ukwasi wa malipo ya madeni kwa mauzo ya nje na malipo ya madeni kwa mapato ya ndani vilivuka kiasi kikomo kilichopo kwa makadirio ya muda mfupi, hata hivyo vilirudi chini ya ukomo katika makadirio ya muda mrefu. Licha ya kuimarika kwa kiasi kidogo kwa kiashirio cha nchi kuhimiri madeni ya Serikali katika mwaka kutoka 2.92 mwaka 2020/21 hadi 2.94 mwaka 2021/22, bado vihatarishi vya deni ni ya wastani katika ripoti ya sasa kama ilivyokuwa katika ripoti iliyopita.

Hii ilichangiwa na athari za janga la UVIKO-19, na uhafifu wa mauzo ya nje na kushuka kwa uchumi wa dunia kwa ujumla.

Naishauri Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango (a) kuboresha ukusanyaji wa mapato ya ndani na mauzo ya bidhaa nje ya nchi ili kusaidia kuboresha viashiria vya ukwasi katika usimamizi wa deni la

Serikali; (b) Kuchukua hatua za jumla kuhakikisha kiwango cha Nchi kimataifa kwenye usimamizi wa madeni kinapanda kurudi daraja la juu (c) Kuhakikisha mapato yatokanayo na mikopo ya kibiashara yanawekezwa katika miradi ya kimkakati yenye manufaa ya moja kwa moja kwenye ukuaji wa Pato la Taifa.

5.5.5 Mikopo Iliyosainiwa Bila Kupokelewa Kwa Muda Mrefu Sh. Bilioni 1,597

Ukaguzi wangu wa kanzidata ya deni ulibaini uwepo wa mikopo nane (8) yenye thamani ya Sh. bilioni 1,597 iliyosainiwa kati ya mwaka 1990 na 2017, lakini fedha zake hazikupokelewa hadi tarehe 30 Juni 2022.

Pia, nilibaini kwamba mikopo hii ilisajiliwa kwenye mfumo wa kuhifadhi taarifa za madeni ya Serikali (CS-DRMS) lakini hakuna miamala ya upokeaji fedha wala ulipaji inayohusiana na mikopo hiyo. Hii inachangiwa na uchelewaji wa Serikali katika kutimiza masharti ya awali ili kuruhusu utoaji wa fedha.

Naishauri Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango iboreshe utaratibu wa usuluhishi baina ya mikataba ya mikopo iliyosainiwa na upokeaji wa fedha zake; na kufuatilia kupitia kitengo cha Mipango ya Kitaifa na watekelezaji miradi ili kuhakikisha masharti ya awali yanatimizwa kwa wakati ili kuruhusu upokeaji wa fedha za mikopo.

5.5.6 Maandalizi Duni na Ufuatiliaji Hafifu wa Miradi Iliyofadhiliwa na Mikopo

Mapitio yangu ya Mihutasari ya vikao vya Kamati ya Kitaifa ya Kusimamia Madeni (NDMC) na taarifa za kutembelea miradi (CPPR na Aid de Memoire) iliyofanywa kwa ushirikiano kati ya wakopeshaji/wadai na vitengo vya usimamizi wa deni la Serikali yalibaini changamoto zinazofanana zinazoathiri utekelezaji mzuri wa miradi inayofadhiliwa na fedha za madeni. Mambo hayo ni pamoja na ucheleweshaji wa uidhinishaji wa fedha kupitia mfumo wa fedha zinazopelekwa moja kwa moja kwenye miradi (D-Fund) katika ngazi zote, Kutotimizwa kwa wakati kwa masharti yanayotakiwa ili kuufanya mkopo uwe tayari kusainiwa na mkopeshaji kuanza kuleta fedha, ucheleweshaji katika taratibu za manunuzi (Hii ni pamoja na kutoa notisi ya

Serikali (GN) kwa miradi yenye msamaha wa kodi) na changamoto katika ulipaji fidia kwa watu walioathiriwa na mradi (PAPs).

Changamoto hizi zinasababisha kupanda kwa gharama, kuchelewa kukamilisha miradi, malipo yasiyo ya lazima kwa wakopeshaji ikiwa ni pamoja na tozo za kutengewa fedha, kushuka kwa sifa ya Serikali kwa wakopeshaji na wananchi wake na kufutwa kwa mikopo kabla ya mradi kukamilika na kusababisha kutofanyika kwa miradi husika kwa viwango vilivyokusudiwa.

Ninapendekeza serikali ipunguze muda unaotumika katika michakato ya misamaha ya kodi na manunuzi. Izingatie matumizi bora ya mfumo wa fedha zinazopelekwa moja kwa moja kwenye miradi (Dfund) ili kuharakisha utekelezaji wa mradi badala ya kucheleweshe. Na kuwe na mipango thabiti ya kutimiza masharti ya awali kabla ya kusainiwa kwa mkataba wowote wa mkopo.

5.6 Usimamizi wa Huduma za Jumla

5.6.1 Kutokuwepo kwa Mfumo Rasmi wa Kushughulikia Malalamiko ya Wastaafu

Ufuatiliaji wa kitengo kidogo cha usajili ulibainisha kutokuwepo kwa mgawanyo wa wazi wa majukumu kati ya ofisi ya dawati la mbele la usajili (Front office) na ofisi ya nyuma ya usajili (Back office). Wastaafu uhudumiwa na mfanyakazi yeyote anayepatikana wakati huo na hakuna rejista ya malalamiko. Pamoja na jitihada za usimamizi wa kupokea malalamiko kwa njia ya barua, simu, wakati wa maonyesho mbalimbali ikiwemo ya sabasaba na kufika ofisi za pensheni kwa wastaafu, bado nina shaka na ufuatiliaji duni wa malalamiko yaliyopokelewa kutokana na kukosekana kwa chombo/utaratibu wa kurekodi na kufuatilia. Zaidi nilibaini uwepo wa tafiti za kufahamu malalamiko ya wastaafu/wateja hata hivyo hakuna kitengo maalum cha kufanya tafiti hizo. Tafiti za hivi karibuni zaidi zilikuwa za miaka ya 2010 na 2019 mtawalia. Ninaona kuwa ni kitambo kirefu sana kuwa na tafiti moja kwa miaka 9.

Napendekeza Wizara ya fedha na Mipango ianzishe mfumo rasmi wa uwazi wa kushughulikia malalamiko ya wastaafu katika ofisi zake zote na

izingatie kuwa na mwongozo wa vipindi vya kufanya utafiti wa malalamiko ya wastaafu.

5.7 Ukaguzi wa Hesabu Jumuifu

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (URT) ilirasimisha matumizi ya Kanuni za Uhasibu za Kimataifa katika Sekta ya Umma (IPSAS accrual basis of accounting) katika kuandaa hesabu kuanzia tarehe 1 Julai, 2012. Hivyo Serikali iliandaa hesabu jumuifu kwa mara ya kwanza kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2013 kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni za Uhasibu za Kimataifa katika Sekta ya Umma (IPSAS 35).Hata hivyo serikali bado inakabiliwa na changamoto zinazoathiri kufanikisha kwa ukamilifu utekelezaji wa taratibu za hesabu jumuifu kama nilivyoona katika ukaguzi wangu wa hesabu kwa mwaka wa fedha 2021/22. Changamoto hizo ni pamoja na:

5.7.1 Ulinganifu kati ya Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu Katika Sekta ya Umma 'IPSAS' na Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Hesabu 'IFRS' na Kutokuwepo kwa Taarifa ya wazi ya Mtazamo tofauti katika Hesabu Jumuifu

Aya 38 na 41 ya IPSAS 35 inaitaka taasisi inayodhibiti kuandaa Hesabu Jumuifu kwa kutumia sera za uhasibu moja kwa miamala iliyo sawa na matukio mengine yenye mazingira ya kufanana. Endapo kuna taasisi zinazodhibitiwa zinatumia sera za uhasibu tofauti na sera zinazotambuliwa na Hesabu Jumuifu marekebisho sahihi yanahitajika katika hesabu za taasisi zinazodhibitiwa wakati wa kutengeneza Hesabu Jumuifu ili kuhakikisha kuna ulinganifu wa sera za uhasibu za taasisi za kiuchumi.

Taasisi za Serikali zimekubali kutumia mbinu ya mfano wa gharama (cost model), baada ya utambuzi wa awali juu ya mali za uwekezaji ambazo umilikiwa kwa ajili ya kupata pango/kodi na/au kuongezeka thamani na Mali, Mimea na Vifaa (PPEs) zinatakiwa kutambuliwa kwa gharama ukitoa ongezeko la kushuka kwa thamani na ongezeko la uharibifu.

Mapitio ya mali za uwekezaji na Mali, Mimea na Vifaa (PPEs) zilizoripotiwa katika Hesabu Jumuifu na mfumo wa kuaanda taarifa hizo (GACS) nimebaini mapungufu yafuatayo;

5.7.1.1 Kutofautiana kwa Modeli ya Gharama 'Cost Model' dhidi ya Modeli ya Uthamini 'Revaluation Model' Zilizotumika katika Kupima Mali za Uwekezaji

Mali za uwekezaji na mabadiliko yanayohusiana katika Noti 85 ya Hesabu Jumuifu yameripoti utambuzi wa marekebisho ya uthamini ya Sh.139,302,281,000. Katika matumizi ya modeli wa uthamini 'revaluation model' kwa baadhi ya taasisi za Serikali, nimebaini faida ya thamani halisi "Fair value gain" kwenye mali za uwekezaji ya Sh. 100,514,601,000 ndani ya Noti 28 ambayo ni tofauti na kiasi cha Sh. 139,302,281,000 kilichoripotiwa katika Noti 85.

Nilibaini zaidi kuwa, jumla ya thamani ya mali za uwekezaji Sh. 305,852,270,720 katika sampuli 19 za taasisi nilizochagua kwa ajili ya ukaguzi hazikukatwa punguzo la thamani "depreciation" wakati taasisi husika zimekubali na kutumia modeli ya gharama "cost model" kinyume na matakwa ya IPSAS 16. Hii inachangiwa na matumizi ya modeli ya gharama "cost model" na modeli ya uthamini "revaluation model" kwa wakati mmoja katika Hesabu Jumuifu ambapo ni kinyume na sera ya uhasibu iliyopitishwa na takwa la IPSAS 35.

5.7.1.2 Kutofautiana kwa Modeli ya Gharama "cost model" dhidi ya Model ya Uthamini "revaluation Model" Zilizotumika katika Kupima Mali, Mimea, na Vifaa (PPEs)

Mapitio yangu ya Mali, Mmea na Vifaa (PPEs) na mabadiliko yanayohusu Noti 86 ya Hesabu Jumuifu kwa mwaka 2021/22 nimebaini marekebisho ya uthamini "revaluation adjustments" yaliyoijumuishwa kiasi cha Sh. 4,078,305,000 (2021; Sh. 1,622,997,039,000). Nilibaini zaidi kuwa, Taarifa ya jumuifu ya Mabadiliko ya Mali halisi na Mtaji imeripoti thamani ya ziada Sh. 1,755,023,000(2021: Sh.394,369,861,000) inayohusiana na sampuli tano za taasisi za Serikali nilizozichagua bila ya kufanya marekebisho ya miamala ili kulingana na modeli ya gharama (cost model) katika maandalizi ya hesabu jumuifu.

Wakati huo huo gharama za kushuka thamani (depreciation expenses) za Mali, Mimea na Vifaa (PPE) zikiripotiwa katika taarifa jumuifu ya kuonesha utendaji (consolidated financial performance) kiasi cha Sh. 3,557,660,074,000. Hii imechangiwa na baadhi ya taasisi ndani ya serikali kutumia modeli mbili ya IPSAS na IFRS ambapo haziendani na sera ya

kufunga hesabu jumuifu. Kuripoti thamani ya ziada na gharama za kushuka thamani kwa pamoja katika hesabu jumuifu kunapingana na matakwa ya Aya 38 ya IPSAS 35.

Ninapendekeza Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango kuhakikisha kuwa (a) marekebisho stahiki juu ya ziada ya uthamini/au vipimo vyovyote kulingana na mahitaji ya IFRS yanafanyika ili kuendana na mahitaji ya IPSAS (b) katika kuandaa Hesabu Jumuifu kuhakiki zinaendana na sera za uhasibu zilizokubalika na kuimarisha uwazi wa taarifa zilizoripotiwa kwa uwasilishaji bora na wa haki wa mizania

5.7.1.3 Kukosekana sifa kwa Mtaji wa ziada Uliojumuishwa katika Mfuko wa Fedha za Walipakodi 'Taxpayers fund' katika Hesabu Jumuifu Sh. bilioni 80.03

Mapitio yangu ya hesabu jumuifu na hesabu binafsi za taasisi za Serikali nilibaini kuwa, taarifa jumuifu inayoonesha Mabadiliko ya mali Halisi/Mtaji kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2022 imeripoti ongezeko la kiasi cha Sh. bilioni 1,058.37 ambacho kimejumuisha ongezeko la mtaji usiofaa katika mfuko wa fedha za walipakodi 'Taxpayers Fund' Sh. bilion 80.03 ambapo unaohusisha taasisi tatu (3) kama zilivyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 36**.

Jedwali Na. 36: Taasisi za Serikali Zilizojumuisha kiasi cha Mtaji Kisichostahili

Na	Jina la Taasisi ya Serikali	Kiasi kisichostahili kuripotiwa kama onezeko la mtaji katika hesabu jumuifu (Sh. bilioni)	Maelezo
1	Mfuko wa maendeleo ya jamii (TASAF)	75.18	Kiasi cha fedha kimejumuishwa kama ongezeko la mtaji katika katika hesabu jumuifu ambapo katika hesabu ya taasisi imeripotiwa kama kiasi cha mwanzo cha 'accumulated surplus'
2	Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira	1.73	Kiasi cha fedha kimeripotiwa katika hesabu za SHUWASA

Na	Jina la Taasisi ya Serikali	Kiasi kisichostahili kuripotiwa kama onezeko la mtaji katika hesabu jumuifu (Sh. bilioni)	Maelezo
	Mjini Shinyanga (SHUWASA)		kama hamisho la mali kutoka RUWASA
3	Shirika la Taifa la Maendeleo (NDC)	3.12	Kiasi hiki cha fedha hakikuweza kuonekana katika hesabu binafsi ya taasisi ya serikali
Jumla		**80.03**	

Chanzo:*Hesabu ya taasisi imeripotiwa kwa mwaka 2021/22*

Napendekeza Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango kuimarisha utaratibu madhubuti wa mapitio ya hesabu kwa uthibitishaji wa takwimu zilizoripotiwa katika hesabu jumuifu na kuimarisha kuwekwa wazi kwa takwimu hizo ili kuboresha uwasilishaji wa hesabu jumuifu.

5.7.2 Uondoshwaji usio Madhubuti wa Miamala ya Ndani ya Taasisi za Serikali "intra economic entities transactions" katika Hesabu Jumuifu

Aya ya 40 (a) hadi (c) ya IPSAS 35 inahitaji kuunganishwa kwa mali, madeni, mapato na gharama za taasisi inayodhibiti na zile za taasisi zinazodhibitiwa. Pia inahitaji kuondoa kwa ukamilifu mali zote za taasisi ya ndani ya uchumi, madeni, mali zote, mtaji, mapato, gharama na mtiririko wa pesa unaohusiana na miamala kati ya taasisi za kiuchumi. Madhumuni ya utaratibu ni kuondoa kuhesabu mara mbili na kuimarisha uhalisi wa matukio yaliyoripotiwa katika taarifa za fedha.

Mapitio yangu ya hesabu jumuifu na hesabu binafsi za taasisi za serikali zinazodhibitiwa yalibaini mapungufu yafuatayo:

5.7.2.1 Kuzidishwa kwa Madeni katika Hesabu Jumuifu Kutokana na Uondoshawaji Kidogo Sh. bilioni 407.72

Mapitio yangu ya hesabu jumuifu, taarifa ya uondoshwaji wa miamala (elimination schedules Noti 13) na taarifa ya mapato ambayo hayajapokelewa pamoja na madeni (Noti 77 na 93) kwenye hesabu jumuifu kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2022 nilibaini kuwa, Jumla ya Sh. bilioni 2,942.04 ya mapato ambayo hayajapokelewa yaliondolewa dhidi ya madeni kiasi cha Sh. bilioni 2,140.73 ambayo ni deni la Serikali na kiasi cha Sh. bilioni 801.304 kilichobaki kwenye mapato ambayo hayajapokelewa kiliondolewa dhidi ya madeni ambayo hayajalipwa. Hata hivyo madeni ambayo hayajalipwa yaliondolewa kwa kiasi cha Sh. bilioni 393.58 dhidi ya mapato ambayo hayajapokelewa na kusababisha kupunguzwa kwa uondoshwaji wa madeni ya Sh. bilioni 407.72.

5.7.2.2 Kuzidishwa kwa thamani ya Mali katika Hesabu Jumuifu Kutokana na Kutokuondolewa kwa Miamala inayostahili Kuondolwa Sh. bilioni 2,545.17

Mapato ya mikopo ambayo hayajapokelewa 'loan recevables'(Noti Na. 78) katika hesabu jumuifu inajumuisha mapato ambayo hayajapokelewa na Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGA) pamoja na Mashirika mengine ya Umma yenye jumla ya Sh. bilioni 2,545.17. (2021; Sh. bilioni 3,729.99) ambayo hayakuondolewa dhidi ya madeni mengine yaliyoripotiwa na mashirikia mengine ya umma.

Mapitio yangu zaidi ya maelezo Na. 78 ya hesabu jumuifu yalibaini kuwa Mikopo kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa na Mikopo kwa Mashirika mengine ya Umma yameainishwa kimakosa kuwa Mikopo kwa wahusika wengine nje ya taasisi za Serikali (loan to third parties) jambo ambalo linaleta shaka kuhusu usahihi na kuaminika "reliability" ya kiasi cha Sh. bilioni 5,185.10 (2021; Sh. bilioni 5,907.87) cha mapato ya mikopo ambayo hayajapokelewa kilichoripotiwa na Serikali

Napendekeza Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango iweke utaratibu madhubuti wa taasisi kuripoti miamala baina yake na taasisi nyingine za Serikali na Kutekeleza uthibitisho wa takwimu zilizoripotiwa kwenye mfumo ili kufanya uondoshaji (elimination) kikamilifu baina ya taasisi za ndani ya serikali na hatimaye kupata takwimu sahihi kwenye hesabu jumuifu.

5.7.3 Udhaifu katika Uchukuaji wa Nakala za Chelezo “backup copies” za Mfumo wa GACS

Serikali inatumia mfumo wa GACS (Government Accounting Consolidation System) katika maandalizi ya hesabu jumuifu . Hivyo, usimamizi wa mfumo wa taarifa, na uhifadhi wa taarifa muhimu na upatikanaji wa huduma endapo ikitokea uharibifu au hitilafu ya mfumo ni jambo muhimu sana. Mapitio yangu ya mpango wa kurejesha huduma baada ya majanga wa Wizara ya Fedha na Mipango nilibaini kuwa, GACS imewekwa katika kiwango cha pili “Level 2” na muda wa kurejea kwa huduma "Recovery Point Objective" (RPO) ya hadi masaa manne.

Hata hivyo, mapitio yangu kwa sampuli ya mwezi Januari na Februari 2023 nilizochagua yalionesha nakala za chelezo (backup) hazijafanyika kwenye kihifadhi taarifa za mifumo “server” ya kurejesha huduma kutokana na majanga kama ilivyoelezwa katika RPO. Hii ni kinyume na Sehemu 42-(a) ya Sheria ya Serikali mtandao “e-Government”, 2019 ambayo inahitaji taasisi zote za umma kuanzisha na kutekeleza mikakati sahihi ya chelezo na urejeshaji ili kuhakikisha kuendelea kwa kupatikana kwa huduma za mifumo yao ya TEHAMA.

Ninapendekeza Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango iboreshe mfumo wa ufuatiliaji ili kufuatilia mchakato wa nakala na kutoa tahadhari endapo kutatokea utofauti wa uchukuaji nakala tofauti na RPO iliyowekwa; kufanya majaribio ya mara kwa mara katika mpango wa kurejesha huduma kutokana na majanga ili kuhakikisha kuwa inakidhi RPO iliyowekwa na kuhakikisha upatikanaji wa huduma endapo kutatokea uharibifu au majanga katika mfumo.

5.7.4 Kutowekwa wazi kwa Miamala na Dhima Baina ya Taasisi za Serikali kwenye Hesabu za Taasisi husika Sh. Bilioni 1,512

Mapitio yangu ya ripoti za uondoaji (Elimination reports) katika hesabu jumuifu pamoja na sampuli 70 za hesabu binafsi za taasisi za serikali zilizotumika katika mchakato wa majumuisho nilibaini kuwa Sh. bilioni 2,638 ziliondolewa kwenye hesabu jumuifu kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2022. Nilibaini zaidi kuwa, taasisi za serikali 51 kati ya 70 sawa na asilimia 73 zenye miamala ya kiasi cha Sh. bilioni 1,521 hazikuwekwa wazi katika hesabu binafsi za taasisi hizo kama miamala iliyofanywa kwa

mashirika ya umma kinyume na Aya ya 3.12 ya Waraka wa Uhasibu Na. 1 wa 2021/22 kuhusu utayarishaji wa hesabu binafsi za taasisi za serikali.

Napendekeza Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango kuweka mkazo zaidi kwa Maafisa Masuuli katika kuzingatia waraka wa Uhasibu Namba 1 wa mwaka 2021/22 na kwa uhandaji wa hesabu zitakazo fanyika kwa kuhakikisha kuripotiwa kwa uwazi miamala ya taasisi katika taarifa zao za fedha ili kuongeza usahihi wa mchakato wa uondoaji wa miamala wakati wa utayarishaji wa hesabu Jumuifu.



SURA YA SITA

USIMAMIZI WA MATUMIZI

6.1 Utangulizi

Usimamizi wa matumizi serikalini ni kitu muhimu katika mfumo mzima wa usimamizi wa fedha za serikali. Ni eneo ambalo linahitaji umakini wa karibu ili kuhakikisha kuwa rasilimali zinatumika kwa ufanisi na ufasaha ili kufikia malengo ya taasisi za umma. Katika ukaguzi wangu, nilihakiki usimamizi wa matumizi ya taasisi za umma na kubaini masuala kadhaa muhimu ambayo yanahitaji umakini katika usimamizi. Maelezo muhimu ya masuala haya yameoneshwa hapa chini;

6.2 Usimamizi mbovu wa Fedha Zilizotolewa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa ajili ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi – Sh. Bilioni 26.04

Mnamo tarehe 8 Novemba 2021, Wizara ya Fedha na Mipango (Wizara ya Fedha) na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Wizara ya Ardhi) zilitia saini Mkataba wa Makubaliano (MoU). Wizara ya Fedha na Mipango ilitoa jumla ya Sh. bilioni 50 kama mkopo kwenda Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa ajili ya kupanga kupima na kumilikisha ardhi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kifungu cha IV cha makubaliano hayo kinaitaka Wizara ya Ardhi kulipa mkopo huo katika kipindi cha mwaka mmoja kuanzia tarehe ya makubaliano yaani kabla ya tarehe 8 Novemba 2022. Mnamo 6 Desemba 2021, Wizara ya Fedha ilitoa kiasi hicho kwa Wizara ya Ardhi .

Aidha, Desemba 2021, Wizara ya Ardhi ilitoa kiasi cha Sh. bilioni 41.14 kwa Halmashauri 54 na taasisi nyingine tano za Serikali. Fedha zilizobaki Sh. bilioni 8.86 zilihifadhiwa na Wizara kusaidia mradi huo katika ngazi ya Wizara. Pia Wizara ya Ardhi ilisaini mikataba na Halmashauri husika.

Ukaguzi ulibaini kuwa baadhi ya Halmashauri zilitumia vibaya fedha hizo kama ilivyofafanuliwa hapa chini:

a) Halmashauri tatu zilipokea jumla ya Sh. bilioni 4.96 kutoka Wizarani. Kati ya fedha hizo Halmashauri zilitumia jumla ya Sh. bilioni 2.35[3] kwa ajili ya shughuli zisizohusiana na kupanga, kupima na kumilikisha ardhi. Huu ni ukiukwaji wa Kifungu cha 4 cha makubaliano kati ya Wizara na Halmashauri husika, ambacho kilieleza kuwa fedha hizo zilipaswa kutumika tu kwa ajili ya kupima, kupanga na umilikishaji wa ardhi. Halmashauri ya Jiji la Dodoma ilitumia kiasi kikubwa cha Sh. bilioni 2.04 katika shughuli zisizohusiana na zoezi hilo.

b) Wizara ya Ardhi ilikopesha Sh. 3,003,723,748 kwa Halmashauri nne, ambazo ni Halmashauri ya Wilaya ya Musoma, Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga, Halmashauri ya Manispaa ya Tabora na Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara, kwa ajili ya kutekeleza shughuli za upimaji wa ardhi, mipango na umilikishaji. Kufuatia kukamilika kwa shughuli hizo za mradi, Halmashauri ziliingiza mapato ya jumla ya Sh. 2,023,937,637. Hata hivyo, Halmashauri hizo hazikulipa mkopo wa Wizara ya Ardhi na kutumia sehemu ya mapato hayo jumla ya Sh. 1,368,937,637 kwa ajili ya shughuli nyingine kinyume na matakwa ya Kifungu cha 7 cha makubaliano hayo, kinachoeleza kuwa fedha hizo zinapaswa kurejeshwa ndani ya miezi sita tangu tarehe ya makubaliano.

c) Pia niligundua kuwa kati ya fedha yote iliyotolewa na Wizara ya Ardhi kama mkopo (Sh. 41,138,956,800) kwa Halmashauri 54 na taasisi nyingine tano za Serikali, fedha iliyorejesha ni Sh. 15,100,000,000 tu . Hii ina maana kuwa bado kuna kiasi cha Sh. 26,038,956,800 (sawa na asilimia 63) hazijarejeshwa kinyume na Kifungu cha 7 cha makubaliano hayo kinachoeleza kuwa mkopo huo unatakiwa kulipwa Wizara ya Ardhi ndani ya miezi sita kuanzia tarehe ya makubaliano ambayo ilikuwa kuanzia tarehe 15 Desemba 2021 hadi tarehe 15 Juni 2022.

[3] Halmashauri ya Jiji la Dodoma Sh. Bilioni 3, Halmashauri ya Manispaa Shinyanga Sh. Bilioni 1.06, na Halmashauri ya Wilaya Shinyanga Sh. Millioni 900

d) Uchunguzi wangu ulibaini kuwa Kifungu cha IV cha makubaliano kati ya Wizara ya Fedha na Wizara ya Ardhi kinaitaka Wizara ya Ardhi kuhakikisha kuwa kiasi kilichokopwa cha Sh. Bilioni 50 kinalipwa kwa Wizara ya Fedha ifikapo tarehe 08 Novemba 2022. Hata hivyo, ulipaji ulikuwa haujafanyika, hadi wakati wa ukaguzi wangu tarehe 10 Februari 2023.

Maoni yangu ni kuwa kutorejeshwa kwa mkopo kunatokana na Wizara ya Ardhi kushindwa kufuatilia na usimamizi usioridhisha wa miradi inayotekelezwa na Halmashauri. Kushindwa kusimamia miradi kunaweza kusababisha malengo kutofikiwa, na uwezekano wa upotevu wa fedha za umma kutokana na matumizi mabaya na usimamizi mbovu. Pia, kuchelewa kwa ulipaji wa mikopo kumeinyima Serikali fursa ya kutumia fedha hizo kwa ajili ya shughuli nyingine za maendeleo.

Napendekeza Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi iimarishe ufuatiliaji na usimamizi, kutekeleza masharti ya makubaliano. Aidha, napendekeza Wizara ya Ardhi ichukue hatua za haraka kutimiza wajibu wake wa kulipa kiasi kilichokopwa cha sh. bilioni 50 kulingana na Kifungu cha IV cha MoU.

6.3 Malipo Yasiyo na Tija Sh. 68.60 billion

Kanuni Na. 21(2) ya Kanuni za Fedha za Umma, 2001, inaeleza kuwa "malipo yasiyo na tija" ni matumizi yasiyo ya kiuchumi ambayo yamelipwa kwa ubatili na ambayo yangeweza kuepukika endapo uangalifu unaofaa ungeweza kutumika.

Mwaka 2007, Serikali, kupitia Kampuni ya Air Tanzania Limited, ilisaini mkataba wa ukodishaji wa uendeshaji na Kampuni ya Wallis Trading Inc (Mmiliki) kwa ajili ya kukodisha ndege aina ya Airbus A320-310, kwa kipindi cha miezi 72, kwa malipo ya Dola za Marekani 315,000 kwa mwezi pamoja na akiba ya matengenezo. Majukumu ya Air Tanzania chini ya ukodishaji wa uendeshaji hapo yanatokana na dhamana iliyotolewa na Serikali tarehe 2 Aprili 2008.

Kuanzia mwaka 2007 hadi 2013, Serikali ilishindwa kuwasilisha ada ya ukodishaji kwa Kampuni ya Wallis Trading Inc na kusababisha kuongezeka kwa deni hadi kufikia Dola za Marekani 45,103,838.85. Mwakwa 2013 Serikali

iliingia makubaliano mapya na Wallis na kuwalipa Dola za Marekani 26,115,428.75, hivyo deni kubaki Dola za Marekani 18,988,410.10.

Mnamo mwaka wa 2017, Wallis Trading Inc ilifungua kesi ya madai ya dola za kimarekani 30,114,230.73 dhidi ya Serikali katika Mahakama Kuu ya Haki ya Uingereza na Wales. Msingi wa madai hayo ilikuwa ni Serikali kushindwa kulipa kulipa deni lililobaki pamoja na riba. Mnamo mwaka 2020 Mahakama iliamuru Serikali kulipa Wallis Trading Inc kiasi cha jumla cha Dola za Marekani 40,180,887.51, pamoja na riba iliyolimbikizwa.

Hata hivyo, Serikali haikukutekeleza agizo la mahakama, na mnamo Aprili 2021, Wallis Trading Inc iliwasilisha ombi katika Mahakama Kuu ya Haki ya Ontario nchini Canada ikitaka kutambuliwa na kutekelezwa kwa hukumu hiyo ya Mahakama ya Uingereza. Mnamo tarehe 29 Aprili 2021 Wallis Trading Inc ilikamata Ndege ya Serikali, De Havilland Canada Limited 8-402 Q400, ambayo ilikuwa ikiundwa nchini Canada.

Kutokana na hali hiyo, Serikali iliingia mkataba na Wallis Trading Inc tarehe 7 Julai 2021, na kuahidi kulipa jumla ya CAD 60,921,953.56 (sawa na USD 48,679,146.56) ifikapo tarehe 22 Julai 2021. Serikali ilitimiza wajibu wake chini ya Mkataba huo na kumlipa Walli Inc jumla ya sh. bilioni 112.47 (sawa na USD 48,679,146.56) tarehe 14 Julai 2021.

Tathmini yangu inaonesha kuwa Serikali imepata hasara ya Dola za Marekani 29,690,736.46 (sawa na Sh. bilioni 68.60) kutokana na kushindwa kulipa deni lililoiva la Dola za Marekani 18,988,410.10 mwezi Oktoba 2013 hivyo kusababisha ongezeko la riba na ada za kisheria la jumla ya Dola za Marekani 48,679,146.56.

Hasara iliyoipata Serikali ilichangiwa zaidi na kutofanya maamuzi ipasavyo kwa watendaji wenye dhamana ya kusimamia shughuli za Serikali na hivyo kusababisha mzigo mkubwa wa fedha kwa walipakodi. Malipo haya yasiyo na tija yangeweza kuepukwa na fedha hizo zingeweza kutengwa kwa mipango mbadala ya serikali.

Napendekeza kwamba Serikali ianzishe sera na taratibu madhubuti za usimamizi wa madeni. Pia ifanye mapitio ya mara kwa mara ya taratibu

za usimamizi wa fedha, ili kuhakikisha matakwa yote ya kimkataba yanatimizwa. Hii itazuia matukio kama hayo kujirudia katika siku zijazo.

6.4 Usimamizi wa Masurufu Sh. Billion 3.62

Masurufu hutolewa kwa wafanyakazi wa serikali ambao wanahitaji fedha kwa malipo ya haraka kwa madhumuni maalum. Hata kama ni kiasi kidogo kinachotolewa kwa gharama za kawaida, usimamizi wake lazima ushughulikiwe kwa tahadhari kwa sababu unaweza kuwa mwanya wa udanganyifu.

Hata hivyo, nilibaini kuwa Taasisi 10 zilikuwa na masurufu ambayo hayajarejeshwa ya jumla ya Sh. bilioni 3.62 kufikia tarehe 30 Juni 2022, hii ni ukiukwaji wa Kanuni Na. 103 ya Kanuni za Fedha za Umma, 2001. Kanuni hiyo inaelekeza kuwa masurufu yanapaswa kurejeshwa mara tu mahitaji hayo yanapokoma, na kwa vyovyote vile, ifikapo siku ya mwisho wa mwaka wa fedha iliyotolewa. Orodha ya taasisi zenye masurufu yasiyorejeshwa imeonyeshwa katika **Jedwali Na. 37**.

Jedwali Na. 37: Taasisi zenye Masurufu yasiyorejeshwa

Na.	Taasisi	Aina	Kiasi (Sh.)
1.	Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora (PO-PSM)	Fungu 32	37,471,828
2.	Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum	Fungu 53	75,775,000
3.	Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi	Fungu 48	276,839,190
4.	Wizara ya Afya	Fungu 52	124,735,689
5.	Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki	Fungu 34	2,655,971,025
6.	Kituo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Jamii	Taasisi Nyingine	16,738,736
7.	Chuo cha Uongozi wa Mahakama (IJA) - Lushoto	Taasisi Nyingine	6,148,340
8.	Baraza la Madaktari la Tanganyika (MCT)	Taasisi Nyingine	200,716,289
9.	Bodi ya Maji ya Bonde la Rufiji	BWB	215,500,820
10.	Programu ya Kisasa ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TMP)	Mamlaka	6,902,499
Jumla			**3,616,799,416**

Chanzo: *Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti 2021/22*

Zaidi ya hayo, nilibaini kuwa jumla ya Sh. milioni 646.43 hazikuwepo kabisa katika rejista ya masurufu ya taasisi mbili, jambo ambalo ni kinyume na Kanuni. 100(2) ya Kanuni za Fedha za Umma, 2001, ambayo inamtaka Ofisa anayesimamia masurufu kuwa na rejista inayoonyesha kiasi cha taarifa kamili za hati za malipo ya masurufu. Tazama maelezo katika **Jedwali Na. 38.**

Jedwali Na. 38: Taasisi ambazo Hazikuweka Taarifa za Masurufu kweye Rejista

Na.	Taasisi	Aina	Kiasi (Sh.)
1	Baraza la Madaktari Tanganyika (MCT)	Taasisi nyingine	178,288,848.50
2	Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali	Fungu 19	468,139,751.00
Jumla			**646,428,599.50**

Chanzo: *Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti 2021/22*

Aidha, kinyume cha Kanuni ya 98(2) ya Kanuni za Fedha za Umma, 2001, taasisi tatu zililipa jumla Sh. milioni 169.7 kama masurufu lakini malipo hayo yaliingizwa vitabuni kama matumizi badala ya kuingizwa kama masurufu ili baada ya kuwasilisha nyaraka za matumizi kuingizwa kama matumizi. Utaratibu huu unaweza kusababisha fedha za umma kutumika vibaya. Maelezo yanaoneshwa kwenye **Jedwali Na. 39** hapa chini

Jedwali Na. 39: Taasisi Zilizotoza Masurufu kama Matumizi

Na.	Taasisi	Aina	Kiasi (Sh.)
1	Baraza la Madaktari Tanganyika (MCT)	Taasisi nyingine	101,129,541.50
2	Taasisi ya Mafunzo ya Viwanda vya Misitu	Taasisi nyingine	49,426,210.00
3	Mamlaka ya Mapato Tanzania-Matumizi	Mamlaka	19,145,000.00
Jumla			**169,700,751.50**

Chanzo: *Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti 2021/22*

Udhaifu huu unasababishwa na udhaifu wa mfumo wa udhibiti wa ndani wa usimamizi wa masurufu, kukosekana kwa kumbukumbu za masurufu, sikuweza kuthibitisha uhalali wa gharama zilizofanywa na waliopewa masurufu hayo, na hivyo kuongeza uwezekano wa matumizi mabaya ya fedha za umma. Aidha, fedha zinazolipwa kama masurufu ambazo

hazijarejeshwa ipasavyo zinaweza kutumiwa vibaya na watumishi wasio waaminifu.

Napendekeza kuwa Maafisa Masuuli husika kuhakikisha kuwa masurufu yanarejeshwa mara tu baada ya madhumuni yaliyotolewa kukamilika; vinginevyo, kiasi kinapaswa kurejeshwa kwa kukatwa kutoka kwenye mshahara wowote au chanzo kingine chochote cha mtumishi husika. Pia napendekeza kwamba Maafisa Masuuli waandike na kuboresha rejista ya masurufu kwa mujibu wa Kanuni ya 100 (2) ya Kanuni za Fedha za Umma, 2001.

6.5 Bakaa ya Fedha kwenye Akaunti ya Matumizi ya Masurufu Sh. Bilioni 5.49

Aya ya 3.11 Waraka wa Serikali Na. 1 ya mwaka 2021/22 ya tarehe 7 Juni, 2022, iliyotolewa na Mhasibu Mkuu wa Serikali kuhusu uandaaji wa taarifa ya fedha na kufungwa kwa mwaka wa fedha 2021/22 unawakumbusha Maafisa Masuuli kuzingatia maelekezo yaliyotolewa na serikali kuhakikisha kuwa akaunti ya masurufu haina salio mwishoni mwa mwaka wa fedha.

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa Taasisi tano zilikuwa na bakaa ya Sh. bilioni 5.49 katika akaunti zao za matumizi ya masurufu hadi kufikia tarehe 30 Juni 2022 kinyume na waraka wa Serikali uliotajwa hapo juu. Tazama maelezo katika **Jedwali Na. 40**.

Jedwali Na. 40: Mfuko usiotumika katika Akaunti ya Matumizi

Na.	Taasisi	Aina	Kiasi (Sh.)
1	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Mawenzi	RRH	31,473,800.09
2	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Manyara	RRH	84,279,121.00
3	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Temeke	RRH	167,573,942.00
4	Hospitali ya Taifa ya Akili Mirembe	SH	1,314,813,444.03
5	Wakala wa Usambazaji Maji Vijijini (RUWASA)	Wakala	3,891,616,206.00
Jumla			**5,489,756,513.12**

Chanzo: *Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti 2021/22*

Maoni yangu ni kuwa kuwepo kwa fedha katika Akaunti matumizi ya masurufu baada ya mwaka kuisha kunaweza kusababisha matumizi mabaya ya fedha za umma.

Napendekeza kuwa Maafisa Masuuli, kwa kushirikiana na Mhasibu Mkuu wa Serikali, kuzielekeza benki za biashara kuhakikisha kuwa bakaa itakayokuwa katika akaunti ya benki ya matumizi ya masurufu mwishoni mwa mwaka wa fedha inahamishwa moja kwa moja kwenda kwenye Akaunti ya Ukusanyaji ya BOT na hatimaye kuhamishiwa kwenye mfuko mkuu wa serikali, badala ya kusubiri Maafisa Masuuli husika kufanya hivyo.

6.6 Malipo yenye Mapungufu Sh. milioni 602.59

Kanuni Na. 11 ya Kanuni za Fedha za Umma, 2001 inaagiza kuwa maafisa Masuuli wana jukumu la kusimamia na kulinda fedha na rasilimali za umma kwa ufanisi. Hivyo, ukaguzi wangu ulibaini kuwa Taasisi sita zilifanya malipo yasiyofaa jumla ya Sh. milioni 602.59, kinyume na matakwa ya kanuni tajwa hapo juu. Malipo haya yasiyofaa ni pamoja na malipo yasiyo stahiki kama malipo ya posho za wafanyakazi, malipo ya makandarasi, malipo ya kozi za mafunzo ambazo hazikubainishwa katika hati ya tathmini ya Mkataba wa Kugawana Bidhaa (PSA), na malipo ya shughuli ambazo hazikukusudiwa. Maelezo yanaoneshwa kwenye **Jedwali Na. 41**.

Jedwali Na. 41: Taasisi zenye Malipo Yenye Mapungufu

Na.	Taasisi	Aina	Kiasi (Sh)	Maelezo
1	Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA)	Wakala	60,946,311.88	Sh. 60,946,311.88 zilitengwa kwa ajili ya posho za nje na ndani kwa maofisa wa BRELA. Hata hivyo, nilibaini Sh. 31,426,311.88 zilitumika kwa posho za nje na Masurufu ya Safari kwa Maafisa kutoka Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara waliohudhuria mikutano ya ARIPO nchini Zimbabwe na Uganda na Sh. 29,520,000 zilitumika kuwezesha semina kwa Wabunge Wanawake. Shughuli hiyo haikuhusiana na Posho za nje kwa maafisa wa BRELA.
2	Wizara ya Madini	Fungu 100	157,698,835.30	Kiasi kilitengwa kwa ajili ya kupambana na shughuli za magendo, lakini ilibainika kuwa fedha hizo badala yake zilitumika kwa madhumuni mengine. Hasa, Sh. 61,400,000 zilitumika kwa honoraria, Sh. 49,758,835.30 zilitumika kwa posho za ndani, Sh. 16,000,000 zilitumika kukidhi gharama za vikao, na Sh. 30,540,000 zilitumika kwa shimiwi, hakuna hata moja ambayo ilikuwa inahusiana na kupambana na magendo.
3	Wizara ya Mkataba wa Kushiriki Uzalishaji wa Nishati (MEM-PSA)	Taasisi nyingine	270,219,297.76	Malipo ya kuhudhuria kozi za mafunzo ambazo zilikuwa nje ya kozi maalum ya tathmini ya PSA.
4	Taasisi ya Mafunzo ya Viwanda vya Misitu	Taasisi nyingine	11,380,000.00	Malipo yanayofanywa kwa ofisa wa umma badala ya mtoa huduma
5	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Maweni	RRH	68,400,000.00	Malipo ya Sh. 68,400,000 yanayohusiana na nyumba na simu na posho ya uwajibikaji yalilipwa kwa watumishi bila idhini ya Katibu Mkuu Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora (Establishments)
			10,738,733.36	Hospitali hiyo ililipa Sh. 102,803,733.36 kwa ajili ya urejeshaji wa mkopo kutoka NHIF chini ya makubaliano ya mkopo wa vifaa tiba. Hata hivyo, makubaliano hayo yalieleza kuwa hospitali hiyo ilitakiwa kulipa Sh. 92,065,000 pekee na kusababisha malipo ya ziada ya Sh. 10,738,733.36.
6	Mamlaka ya Mapato Tanzania	Mamlaka	23,204,171.00	Mamlaka iliilipa Kampuni ya Ujenzi ya SUMA JKT Ltd jumla ya Sh. 25,782,413 kwa cheti cha malipo ya muda, badala ya Sh. 2,578,241. Hii ilisababisha malipo ya ziada ya Sh. 23,204,171. 00.
Jumla			**602,587,349.30**	

Chanzo: *Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti 2021/22*

Nilibaini kuwa chanzo cha malipo haya yenye mapungufu ni udhibiti usioridhisha wa usimamizi wa fedha.

Ninapendekeza Maafisa Masuuli husika kuzingatia sheria, kanuni na miongozo ya serikali ya usimamizi wa fedha za umma na kuhakikisha kuwa idhini sahihi ya kimaandishi inapatikana wakati mapungufu yoyote ya kisheria yanapogunduliwa.

6.7 Malipo yaliyofanywa kwa kutumia vifungu visivyo sahihi Sh. Milioni 398.56

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa Taasisi tisa zilifanya malipo ya kiasi cha Sh. milioni 398.56 kwa kutumia vifungu vya matumizi visivyo sahihi, kinyume na Kanuni ya 46 (2) ya Kanuni za Fedha za Umma za mwaka 2001, ambazo zinaagiza kila malipo na kila chanzo cha mapato kiainishwe kwa usahihi kwa mujibu wa maelezo ya bajeti iliyoidhinishwa.

Kukosekana kwa udhibiti wa ndani juu ya matumizi ya bajeti iliyoidhinishwa ndio sababu ya malipo kufanywa kwa kutumia vifungu visivyo sahihi, na hali hii isipozibitiwa inaweza kupotosha madhumuni ya kupanga bajeti kwa kuongeza na kupunguza vifungu vya bujeti pamoja na kusababisha mizani isiyo sahihi ya uhasibu na matumizi zilizoripotiwa katika taarifa za kifedha. Orodha ya Taasisi zilizofanya malipo katika vifungu visivyo sahihi inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 42.**

Jedwali Na. 42: Malipo yaliyofanywa kwa kutumia vifungu visivyo sahihi

Na.	Taasisi	Aina	Kiasi (Sh.)
1.	Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora (TAMISEMI)	Fungu 32	43,961,400
2.	Tume ya Ukimwi Tanzania (TACAIDS)	Fungu 92	15,349,400
3.	Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya	Fungu 91	62,044,530
4.	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Singida	RRH	92,732,888
5.	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Dodoma	RRH	45,570,000
6.	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Maweni	RRH	18,408,500
7.	Ofisi ya Rais Tanzania Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC)	Wakala	73,411,930
8.	Programu ya Kisasa ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TMP)	Mamlaka	27,410,080
9.	Mfuko wa Udhamini wa Pembejeo za Kilimo (AGITF)	Mfuko	19,667,641
Jumla			**398,556,369**

Chanzo: *Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti 2021/22*

Napendekeza Maafisa Masuuli kujiepusha na kuidhinisha matumizi nje ya bajeti iliyoidhinishwa na Kanuni za Takwimu za Fedha za Serikali (GFS), iwapo itakuwa ni lazima kufanya hivyo ni muhimu, kutafuta hati ya uhamisho kwa mujibu wa kifungu cha 41 cha Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015.

6.8 Malipo bila kuomba Risiti za Kielekitroniki (EFD) Sh. Bilioni 15.31

Kifungu Na. 36 (1) cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi (TAA), Sura 438 (Toleo Lililorekebiswa 2019) na Kanuni ya 28(1) ya Kanuni za Kodi ya Mapato (Electronic Fiscal Devices) Kanuni 2012 zote zinaeleza kuwa mnunuzi na muuzaji, lazima watoe na kudai risiti za EFD.

Ukaguzi wangu ulibaini jumla ya malipo ya Sh. Bilioni 15.31 yalifanywa na Taasisi 21 bila kuwa na risiti za Kielekitroniki. **Jedwali Na. 43** linaonyesha orodha ya taasisi.

Jedwali Na. 43: Taasisi za Serikali zilizofanya malipo bila kuomba risiti za kielektroniki

Na.	Taasis	Aina	Kiasi (Sh)
1	Tume ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano	Taasisi nyingine	6,419,616.58
2	Nelson Mandela-Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Afrika (NM-AIST)	Taasisi nyingine	59,474,408.83
3	Mradi wa Mashine za Kilimo Suma JKT	Taasisi nyingine	15,489,803.00
4	Wizara ya Nishati	Fungu 58	11,861,999.84
5	Wizara ya Mawasiliano ya Habari na Teknolojia ya Habari	Fungu 68	30,274,300.00
6	Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya	Fungu 91	21,435,280.00
7	Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum	Fungu 53	146,400,500.00
8	Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki	Fungu 34	711,602,033.14
9	Mahakama ya Tanzania	Fungu 40	344,475,092.19
10	Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi	Fungu 51	292,084,716.00
11	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ya Amana	RRH	98,607,548.24
12	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Morogoro	RRH	11,355,730.40
13	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma	RRH	99,758,500.00

Na.	Taasis	Aina	Kiasi (Sh)
14	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Geita	RRH	43,120,000.00
15	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ya Maweni	RRH	1,541,996,692.52
16	Hospitali ya Rufaa ya Chato Zonal	ZRH	2,325,520,400.00
17	Hospitali ya Magonjwa ya Kuambukiza ya Kibong'oto	SH	88,244,995.09
18	Wakala wa Usambazaji Maji Vijijini (RUWASA)	Shirika la	9,439,832,523.00
19	Taasisi ya maji	Shirika la	17,803,700.00
20	Bodi ya Maji ya Bonde la Ziwa Tanganyika (LTBWB)	BWB	6,538,500.00
21	African Democratic Alliance (ADA-TADEA)	Chama cha Siasa	1,000,000.00
Jumla			**15,313,296,338.83**

Chanzo: Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti 2021/22

Malipo bila kuomba risiti za kielekroniki inachangiwa na kutokuwepo kwa jitihada za kutosha za Maafisa Masuuli katika kudai risiti hizo. Hivyo kunadhoofisha juhudi za Serikali za kukusanya kodi kwani wafanyabiashara wanaweza kutumia mwanya huu kukwepa kodi.

Nikirejea mapendekezo yangu ya awali, Maafisa Masuuli wanapaswa kufanya shughuli na wafanyabiashara ambao wana mashine za kielekroniki na kudai risiti za kielekroniki wakati wa kufanya malipo kwa mujibu wa Kifungu cha 36 cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi, 2015, na Kanuni Na. 28(1) ya Kanuni za Kodi ya Mapato (Vifaa vya Fedha vya Kielektroniki), 2012.

6.9 Kutokukata Kodi na Kutokuwasilishwa kwa Kodi Hiyo Mamlaka ya Mapato Tanzania sh. Milioni 749.53

Katika kipindi cha ukaguzi, nilibaini kuwa Taasisi 21 zilishindwa kuwasilisha kodi ya zuio jumla ya Sh. milioni 749.53 kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA). Kati ya kiasi hicho, taasisi 15 hazikukata kodi ya zuio ya jumla ya sh. milioni 713.70, huku taasisi sita zikizuia kodi lakini hazikuwasilisha sh. milioni 35.83 kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania. Hii ni kinyume na matakwa ya vifungu vya 83, 83A, na 84(1) vya Sheria ya Kodi ya Mapato, Cap 332 (Toleo Lililorekebishwa 2019), ambavyo vinaweka wajibu kwa Maafisa Masuuli kuzuia kodi kwenye ada za huduma, malipo ya mikataba, na bidhaa zilizonunuliwa, na kutuma fedha hiyo kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania

(TRA) ndani ya siku saba baada ya kumalizika kwa kila kalenda ya mwezi. **Jedwali Na. 44** latoa maelezo zaidi

Jedwali Na. 44: Taasisi ambazo Hazikuwasilisha Kodi ya Zuio

	Taaisisi ambazo hazikukata na kuwasilisha kodi ya zuio		
Na	**Taasisi**	**Aina**	**Kiasi (Sh.)**
1	Wakala wa Maendeleo ya Usimamizi wa Elimu (ADEM)	Wakala	3,478,050.00
2	Wakala wa Usambazaji Maji Vijijini (RUWASA)	Wakala	56,890,902.00
3	Wakala wa Huduma za Ununuzi Serikalini (GPSA)	Wakala	30,144,140.00
4	Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS)	Wakala	442,832,576.00
5	Wakala wa Mafunzo ya Mifugo (LITA)	Wakala	575,335.00
6	Tume ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano	Taasisi nyingine	1,459,791.52
7	Jitegemee (Shule ya Sekondari JKT	Taasisi nyingine	2,075,213.56
8	Kampuni ya Ujenzi ya SUMA JKT Ltd	Taasisi nyingine	162,076,305.13
9	Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO)	Fungu 18	3,063,767.42
10	Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo	Fungu 96	1,791,973.00
11	Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya	Fungu 91	1,998,521.50
12	Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi	Fungu 51	1,782,261.00
13	Bodi ya Maji ya Bonde la Ziwa Tanganyika (LTBWB)	BWB	1,585,929.63
14	Namtumbo WSSA	Usambazaji wa maji	3,911,500.00
15	Chama Cha Kijamii	Chama cha Siasa	32,600.00
	Jumla ndogo		**713,698,865.76**
	Taasisi zilizokata lakini hazikuwasilisha Kodi ya Zuio kwa TRA		
1	Wakala wa Maendeleo ya Usimamizi wa Elimu (ADEM)	Shirika la	6,044,912.76
2	Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara	Fungu 44	16,484,770.00
3	Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara	fungu 60	406,723.00
4	Muungano wa Mabadiliko na Uwazi (ACT -WAZALENDO)	PP	8,572,472.00
5	African Democratic Alliance (ADA-TADEA)	PP	344,000.00

	Taaisisi ambazo hazikukata na kuwasilisha kodi ya zuio		
Na	**Taasisi**	**Aina**	**Kiasi (Sh.)**
6	Baraza la Madaktari Tanganyika (MCT)	Taasisi nyingine	3,981,956.00
	Jumla ndogo		**35,834,833.76**
	Jumla kuu		**749,533,699.52**

Chanzo: *Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti 2021/22*

Serikali inapoteza mapato kutokana na kutokatwa kwa kodi ya zuio na kushindwa kuwasilisha kodi hiyo kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania, hivyo kuathiri shughuli zake zilizopangwa.

Napendekeza kuwa Maafisa Masuuli wahakikishe kuwa kodi ya zuio inakatwa na kupelekwa kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania kama inavyotekelezwa na Sheria ya Kodi ya Mapato.

NATIONAL AUDIT OFFICE
NAOT



SURA YA SABA

MENEJIMENTI YA RASILIMALI WATU, USIMAMIZI WA MISHAHARA NA MAFAO YA WASTAAFU

7.1 Utangulizi

Katika sura hii, nimeelezea matokeo yaliyoibuliwa wakati wa ukaguzi wa Menejimenti ya rasilimali watu, usimamizi wa mishahara na mafao ya wastaafu katika Taasisi za Serikali Kuu. Sura hii imebainisha mapungufu yaliyoonekana kwenye ukaguzi kama ifuatavyo:

7.2 Upungufu wa Idadi ya Watumishi wa Umma katika Taasisi za Serikali Kuu

Katika ukaguzi wa mwaka wa fedha 2021/22, nilibaini upungufu wa watumishi wa umma katika taasisi mbalimbali za serikali. Hii inaonesha kuwa jukumu la sekretarieti ya ajira katika utumishi wa umma halijatekelezwa ipasavyo kwa mujibu wa Kanuni Na. D.7 (1) na (4) za Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma za mwaka 2009 zinazoelezea kuwa ni jukumu la Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma kujaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kuajiri watumishi wapya na kusimamia zoezi la ajira.

Nilipitia taarifa za watumishi wa Umma zinazobainisha idadi ya watumishi wa Umma kwenye Taasisi za Serikali, nikabaini upungufu wa watumishi 16,525 katika Taasisi 86 za Serikali ikilinganishwa na upungufu wa watumishi 33,145 ulioanishwa kwenye ripoti yangu ya mwaka wa fedha 2020/21. **Jedwali Na. 45** na **Kiambatisho Na. XI** vinafafanua upungufu wa watumishi kwenye Taasisi za Serikali Kuu:


Jedwali Na. 45: Upungufu wa Watumishi kwenye Taasisi Serikali Kuu

Na	Maelezo ya Taasisi	Idadi ya Taasisi	Watumishi wanaohitajika	Watumishi Waliopo	Upungufu
1.	Wizara na Idara	13	14,311	6,651	7,660
2.	Wakala	6	2,047	1,190	857
3.	Taasisi nyingine	67	14,857	6,849	8,008
Jumla		**86**	**30,215**	**14,690**	**16,525**

Chanzo: *Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti 2021/2022*

Kwa mwaka wa fedha 2021/22, Serikali kupitia Ofisi ya Raisi Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ilipanga kuajiri watumishi wapya 10,829 na ajira zilizoidhinishwa zilikuwa 7,020. Hata hivyo, nilibaini kuwa Taasisi za Serikali Kuu ziliomba vibali vya kuajiri watumishi wapya 20,000 ambayo ni sawa na asilimia 185 ya ajira iliyopangwa. Aidha, kati ya vibali vilivyoombwa, ni vibali 7,020 tu vilivyotolewa na Utumishi, sawa na asilimia 35 ya maombi yote ya vibali. Mwenendo wa miaka mitatu kwa ajira mpya zilizopangwa, vibali vilivyoombwa na vibali vilivyotolewa, umeainishwa kwenye **Kielelezo Na. 9**.

Kielelezo Na. 9: Uchambuzi wa Mwenendo wa Ajira Zilizoidhinishwa, Ajira Zilizoombwa na Vibali Halisi Vilivyotolewa na Serikali



Chanzo: *Taarifa Za Watumishi Zilizotolewa Na Ofisi Ya Rais- Utumishi Na Utawala Bora*

Kutokana na uchambuzi uliofanywa kwenye kielelezo hapo juu,tatizo la upungufu wa Watumishi wa Umma bado ni kubwa na linasababishwa na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kushindwa kutoa vibali kwa wakati. Hii inapelekea Taasisi za Umma kutofikia malengo ya kiutendaji.

Ninapendekeza Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora iweke juhudi zaidi kuhakikisha wanafanyia kazi kwa haraka maombi ya taasisi za serikali ya kujaza nafasi zilizo wazi ili kushughulikia suala la uhaba wa watumishi.

7.3 Upungufu katika Maandalizi na Utekelezaji wa Mipango ya Mafunzo kwa Watumishi wa Umma katika Taasisi Serikali Kuu

Kanuni Na G 1 (7) na (8) za Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma ya mwaka 2009, zinaelekeza Taasisi za Serikali kuandaa mpango maalum wa ndani wa mafunzo ya watumishi kulingana na mahitaji yao. Mafunzo hayo yatawapatia ujuzi watumishi waliopo na wapya kwa kuwaongezea maarifa,dhana za msingi za kazi pamoja na sheria zinazohusu utumishi wa umma na usimamizi wa kazi. Kila Taasisi inatakiwa kutenga fedha kwenye mpango wa fedha wa mwaka kwa ajili ya kufanikisha mafunzo yaliyopangwa.

Wakati wa ukaguzi nilibaini mapungufu kadhaa kwenye uandaaji na utekelezaji wa mipango ya mafunzo kwa Watumishi wa Umma kama ifuatavyo:

a) Kutoandaliwa kwa Mpango na Tathmini za Mahitaji ya Mafunzo

Kwa mwaka wa fedha 2021/22, Taasisi 10 hazikuandaa mpango na tathmini za mahitaji ya mafunzo kwa watumishi wa umma, taarifa hizi ni muhimu kwani zinaainisha idadi ya watumishi wanaohitaji mafunzo, muda na wigo wa mafunzo. Ifuatayo ni rodha ya Taasisi ambazo hazikuandaa mpango na tathmini za mahitaji ya mafunzo.

i) Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi
ii) Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi
iii) Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania
iv) Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora
v) Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania
vi) Taasisi ya Sayansi na Teknoloji ya Nelson Mandela

vii) SUMA JKT- Kampuni ya Usafi na Unyunyuziaji Dawa
viii) Wakala wa Ununuzi wa Mafuta (PBPA)
ix) Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Mkoa, Chato
x) Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania

b) Kutokuendesha Mafunzo Elekezi kwa Waajiriwa Wapya

Pia nilibaini Wakala wa Huduma za Umeme Tanzania (TEMESA) na Hospitali ya Rufaa ya Kanda, Mtwara hazikufanya mafunzo elekezi kwa watumishi wapya 36 na 23 mtawalia. Mafunzo haya yanalenga kuwapatia ujuzi wa maarifa ya kutosha ya ufanisi, dhana za misingi ya utumishi na sheria zinazohusu utumishi wa umma na usimamizi wa kazi.

Upungufu katika uandaaji na utekelezaji wa mipango ya mafunzo unasababishwa na menejimenti kutotilia mkazo uandaaji na utekelezeji wa mipango. Pia, upungufu wa fedha zinazoletwa kwa ajili ya kutekeleza mipango ya mafunzo kwa waajiriwa wapya na waliopo. Maoni yangu ni kuwa kutofanya mafunzo kwa waajiriwa kunaweza kuathiri uzalishaji, utendaji, na uwezo wao wa kutoa huduma kama inavyotarajiwa.

Napendekeza Maafisa Masuuli waandae mipango ya mafunzo na kusimamia ipasavyo utekelezaji wake. Aidha, Wizara ya Fedha na Mipango itoe fedha za kutosha ili kutekeleza mipango ya mafunzo iliyopangwa.

7.4 Matumizi Yasiyoridhisha ya Mfumo wa Taarifa Shirikishi za Kiutumishi na Mishahara (HCMIS)

Mfumo wa Taarifa Shirikishi za Kiutumishi na Mishahara (HCMIS) ulianzishwa na Serikali mwezi Mei 2020 ili kuhakikisha mifumo yote ya Taasisi za Serikali inayohusiana na rasilimali watu na usimamizi wa mishahara inaunganishwa ili kukidhi matakwa ya Serikali kwenye kushughulikia masuala ya rasilimali watu na mishahara.

Ukaguzi ulifanyika ili kutathmini ufanisi na matumizi ya mfumo wa HCMIS katika kutunza na kuwasilisha taarifa za mishahara na rasilimali watu kwa usahihi. Pamoja na msisitizo wa kutumia mfumo huo ipasavyo, changamoto zinazohusiana na matumizi yake zilibainika wakati wa ukaguzi kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 46**:

Jedwali Na. 46: Taasisi zenye Changamoto kwenye Matumizi ya Mfumo wa HCMIS

Na	Changamoto Zilizobainishwa	Jina la Taasisi
1.	Baadhi ya watumishi kuwa na Tarehe inayofanana ya siku ya kuajiriwa,kupandishwa vyeo na kuthibitishwa kazini	Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu- Fungu 25
		Ofisi ya Waziri Mkuu-fungu 37
2.	Takwimu za wafanyakazi zinaonesha walithibitishwa kabla ya kuajiriwa	Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu fungu 25
		Ofisi ya Waziri Mkuu-fungu 37
		Tume ya Kuzuia Ukimwi -fungu 92
3.	Takwimu za mfumo zinaonesha tarehe ya kupandishwa vyeo ilikuwa kabla ya tarehe ya kuthibitishwa kazini kwa baadhi ya watumishi	Ofisi ya Waziri Mkuu-fungu 37
		Tume ya Kuzuia Ukimwi -fungu 92
4.	Namba ya Utambulisho wa wafanyakazi wa serikali kwa baadhi ya watumishi ilirekodiwa kwenye safu ya Vitambulisho vya Taifa (ID)	Tume ya Kuzuia Ukimwi -fungu 92
5.	Watumishi wanaopokea mishahara chini ya theluthi moja	Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari-fungu 68
		Tume ya Marekebisho ya Sheria-fungu 59
6.	Wafanyakazi wenye tarehe za uthibitisho zisizo sahihi na bila nambari ya faili	Tume ya Marekebisho ya Sheria-fungu 59

Chanzo: *Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti 2021/2022*

Ukosefu wa mafunzo ya kutosha kwa maafisa rasilimali watu unahusishwa na matumizi yasiyoridhisha ya mfumo huo. Hii inasababisha Taasisi za Serikali kushindwa kufikia lengo la mfumo ambalo ni kuunganisha Taasisi za Serikali na kupunguza changamoto zinazohusiana na rasilimali watu na usimamizi wa mishahara.

Napendekeza taasisi za serikali ziandae mipango ya kutosha ya mafunzo ya matumizi ya mfumo wa HCMIS .Pia Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ishughulikie kero zinazohusiana na ugumu wa matumizi ya mfumo huo ili kufanikisha kufikia lengo lake hatimaye kuongeza thamani ya fedha.

7.5 Wafanyakazi Wanaokaimu Nafasi za Juu kwa Zaidi ya Miezi Sita

Kanuni Na. D.24 (3) ya Kanuni za kudumu za Utumishi wa Umma ya mwaka 2009 inaelekeza Watumishi wa Umma kukaimu nafasi za juu kwa muda usiozidi miezi sita. Pia, inaelekeza mamlaka ya uteuzi kuhakikisha kuwa taratibu za kuthibitisha Watumishi wanaokaimu nafasi hizo zinakamilishwa katika muda unaotakiwa.

Ukaguzi wangu ulibaini taasisi 40 za Serikali zenye watumishi 258 wanaokaimu nafasi za juu zilizo wazi kwa zaidi ya miezi sita. Watumishi hao walikaimu nafasi hizo kwa muda kati ya miezi sita hadi 108, kama inavyobainishwa katika **Kiambatisho Na. XII** na **Jedwali Na. 47**.

Jedwali Na. 47: Taasisi zenye Watumishi Wanaokaimu zaidi ya Miezi Sita

Maelezo ya Taasisi	Idadi ya Taasisi	Idadi ya Watumishi Wanaokaimu
Wizara na Idara	6	57
Mashirika	7	123
Taasisi nyingine	27	78
Jumla	**40**	**258**

Chanzo: *Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti 2021/2022*

Suala hili limekuwa likiwasilishwa mara kwa mara kwenye ripoti za ukaguzi zilizopita, na linahusishwa na ucheleweshaji wa Taasisi inayohusika na kushughulikia maombi ya uthibitisho na uteuzi wa watumishi wanaokaimu nyadhifa mbalimbali. Kushindwa kuthibitisha na kuteua watumishi kwa wakati kunaweza kusababisha kupunguza uwezo wa kufanya maamuzi, uwajibikaji, na hatimaye kuathiri utendaji wa jumla wa Taasisi za Serikali.

Napendekeza Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora ichukue hatua katika kushughulikia tatizo hili kwa kuharakisha uteuzi wa watumishi wanaokaimu kwa muda mrefu na kuteua wafanyakazi wapya kwa nafasi za watumishi wanaokaimu ambao hawakidhi vigezo vinavyotakiwa.

7.6 Kutowasilisha Makato ya Mishahara katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na Taasisi Sh. Bilioni 1.60

Kifungu Na.18 na 19 cha Sheria ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ya mwaka 2018 vinaeleza wajibu wa waajiri kukata na kulipa michango kwa niaba ya wafanyakazi wao kwenye mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwa 20% ya mshahara wa mwezi wa kila mfanyakazi. Sheria hii inaendana na Kifungu Na. 84 (1) cha Sheria ya Kodi ya Mapato (Iliyorekebishwa mwaka 2012) na Kifungu Na.8 cha Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ambavyo vinataka Taasisi kuwasilisha makato kila mwezi, na kwamba kushindwa kuwasilisha makato hayo kwa wakati kutasababisha adhabu kwa taasisi husika.

Nilibaini kuwa Taasisi 17 hazikuwasilisha makato ya kisheria ya kiasi cha Sh. bilioni 1.60 kwa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ya (PSSSF na NSSF), Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kama ilivyoainishwa kwenye **Jedwali Na. 48**.

Jedwali Na. 48: Taasisi Ambazo Hazikuwasilisha Makato Ya Mishahara

Na	Taasisi	Kiasi (Sh.)
PSSSF (Makato ya Mafao ya uzeeni na mafao mengineyo)		
1.	Tume ya Kudhibiti Ukimwi Tanzania	11,862,680
2.	Baraza la Madaktari la Tanganyika	2,280,000
3.	Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi	17,577,200
4.	Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA)	6,000,000
5.	Mamlaka ya Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Handeni	12,325,000
6.	Mamlaka ya Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Chunya	7,883,200
7.	Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Tunduru	19,161,005
8.	Kampuni ya Ulinzi chini ya Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa	1,372,783,486
9.	Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi	12,006,750
NSSF (Makato ya Mafao ya Uzeeni na Mafao Mengineyo)		
10.	Baraza la Madaktari la Tanganyika	44,209,000
11.	Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula	36,328,800

Na	Taasisi	Kiasi (Sh.)
12.	Mamlaka ya Bomba Kuu la Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Handeni	2,465,000
NHIF (Kutowasilisha Makato ya Bima ya Afya)		
13.	Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania	18,180,000
14.	Baraza la Madaktari la Tanganyika	684,000
15.	Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi	23,749,020
TRA (Kutowasilisha Makato ya Kodi Kadri ya Kipato)		
16.	Baraza la Madaktari Tanganyika	2,316,000
17.	Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi	11,403,632
	Jumla	**1,601,214,773**

Chanzo: *Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti 2021/2022*

Kutowasilisha makato kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya na Mamlaka ya Mapato Tanzania, kunasababishwa na kutokuwa na utaratibu mzuri wa uwasilishaji wa makato hayo kwa wakati.

Kutowasilisha makato kunaathiri na kunaweza kuwakosesha watumishi haki na faida zinazotokana na kujiunga na mifuko ya Jamii na Afya. Pia,Taasisi zilizoshindwa kuwasilisha makato kwa wakati zinaweza kupata adhabu, hivyo kulipa malipo yasiyo na tija na kupata hasara.

Ninapendekeza Maafisa Masuuli wahakikishe kuna utaratibu mzuri unaosimamia uwasilishaji wa makato ya kisheria kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Taifa ya Jamii, Bima ya Afya na Taasisi nyingine.

7.7 Usimamizi wa Mafao ya Kustaafu kwa Watumishi wa Umma

Ukaguzi wa awali wa mafao ya watumishi waliomaliza muda kazini hufanyika kwa mujibu wa Ibara 143(2) (a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 (kama ilivyokuwa ikifanyiwa marekebisho mara kwa mara) ambayo inamtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuidhinisha malipo kutoka katika Mfuko Mkuu wa Serikali baada ya kujiridhisha kuwa Ibara ya 136 ya Katiba imezingatiwa.

Ukaguzi wa awali wa mafao ya watumishi waliomaliza muda kazini hufanyika kwa kuzingatia sheria za mafao ambazo ni pamoja na Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii katika Utumishi wa Umma Na.2 ya mwaka 2018; Sheria ya

Utumishi wa Umma Sura 298 ya mwaka 2022; Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii Sura 50 iliyorekebishwa mwaka 2018; Sheria ya Ulinzi wa Taifa Sura 439 iliyorekebishwa mwaka 2002; Sheria ya Utumishi wa Usalama wa Taifa Sura ya 406 ya mwaka 1996; Sheria ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kusimamia Sekta ya Hifadhi ya Jamii Sura ya 135 iliyorekebishwa mwaka 2015; Sheria ya Mafao ya Viongozi wa Kisiasa Sura ya 225 iliyorekebishwa mwaka 2015 na Sheria ya Kodi ya Mapato Sura ya 332 iliyorekebishwa mwaka 2019.

Lengo la ukaguzi huu ni kuhakiki usahihi wa mafao ili kuwezesha kutambua makosa mapema kabla ya malipo kufanyika. Makosa hayo ni, kipindi kisicho sahihi cha utumishi, mishahara isiyo sahihi iliyotumika kukokotoa mafao, michango ya watumishi isiyo sahihi na makosa ya majumuifu.

7.7.1 Mawanda ya Ukaguzi wa Awali

Ukaguzi wa awali wa mafao ya watumishi waliomaliza muda wao kazini unahusisha Watumishi wa Umma ambao mafao yao hulipwa kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali. Mafao hayo yanahusisha pesheni kwa Watumishi wa Umma; watoa huduma mchanganyiko; askari na maafisa wa jeshi; maafisa usalama; mafao kwa watumishi waliomaliza mikataba ya uongozi wa kisiasa; wageni toka nje; wastaafu waliorejeshwa kwenye utumishi; raia walioajiriwa wakiwa na umri wa zaidi ya miaka 45 na mafao kwa watumishi wasio kwenye masharti ya pesheni.

7.7.2 Utekelezaji Ukaguzi wa Awali

Ukaguzi wa awali ulianza na majalada 137 ambayo ni bakaa kutoka mwaka 2020/21 yakifuatiwa na majalada 3,095 yaliyowasilishwa kwa ajili ya ukaguzi katika kipindi cha mwaka 2021/22 hivyo kufanya jumla ya majalada 3,232. Kati ya hayo, majalada 2,867(88.7%) yenye mafao ya thamani ya Sh. bilioni 79.12 yalikaguliwa na kuidhinishwa kwa malipo. Majalada 216 (6.7%) yalihojiwa na kurudishwa kwa Maafisa Masuuli kwa marekebisho ambapo mpaka mwisho wa mwaka yalikuwa bado hayajarudishwa kwa ajili ya ukaguzi wa awali. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2022 majalada 149(4.6%) yalikuwa bado yakiendelea kukaguliwa katika Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 49**.

Jedwali Na. 49: Majalada ya Wastaafu Yaliyokaguliwa 2021/22

Maelezo	2021/22	2020/21
Majalada yaliyokuwepo tarehe 1 Julai-A	137	184
Majalada yaliyopokelewa-B	3095	2,092
Jumla ya majalada yaliyokuwepo kwa ukaguzi-C=A+B	3232	2,276
Majalada yaliyokaguliwa na kuidhinishwa-D	2867	1,880
Majalada yaliokaguliwa na kurejeshwa kwa waajiri yakiwa na hoja-E	216	259
Majalada yaliyosalia tarehe 30 Juni-F=C-D-E	149	137

Chanzo: *Mfumo wa Usimamizi wa ukaguzi wa awali wa mafao*

7.8 Matokeo ya Ukaguzi wa Awali kwa Majalada ya Mafao

Wakati wa ukaguzi wa awali wa majalada ya mafao ya watumishi waliomaliza muda kazini kwa mwaka wa fedha 2021/22 nilibaini mambo yafuatayo;

7.8.1 Waajiri Kukosea Ukokotoaji wa Mafao ya Wastaafu

Katika ukaguzi wa majalada ya mafao 2,867 niliyoyaidhinisha kwa malipo, nilibaini majalada 244 (8.5%) yalikokotolewa kimakosa. Makosa hayo yanatokana na kurekodi kipindi kisicho sahihi cha utumishi; kukokotoa mafao kwa kutumia mishahara na michango ya Watumishi isiyo sahihi na makosa ya majumuifu. Hata hivyo, makosa hayo yalirekebishwa na niliidhinisha malipo kwa majalada hayo.

Kati ya majalada 244 yaliyokototolewa kimakosa, majalada 208 (66.2%) yalikokotolewa zaidi ya kiwango stahiki kwa Sh. milioni 489.67 na majalada 106 (33.8%) yalikokotolewa kwa kiwango pungufu kwa Sh. milioni 274.15 kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 50**.

Jedwali Na. 50: Majalada ya Mafao Yaliyokokotolewa Kimakosa

Na.	Maelezo	Mafao yaliyozidi		Mafao yaliyopungufu	
		Idadi ya majalada	Kiasi (Sh. Milioni)	Idadi ya majalada	Kiasi (Sh. Milioni)
1	Kipindi cha utumishi kisicho sahihi	59	146.43	64	142.25
2	Mishahara ya iliyokosewa	25	109.41	11	25.48

Na.	Maelezo	Mafao yaliyozidi		Mafao yaliyopungufu	
		Idadi ya majalada	Kiasi (Sh. Milioni)	Idadi ya majalada	Kiasi (Sh. Milioni)
3	Makosa katika michango ya hifadhi ya Jamii	49	114.32	32	35.61
4	Makosa mbalimbali katika ukokotoaji	4	2.21		
	Jumla	**137**	**372.37**	**107**	**203.34**

Chanzo: *Fomu za malipo ya mafao na uhakiki wa ukaguzi*

Nashauri Serikali kupitia Maafisa Masuuli iwe na utaratibu ambao utahakikisha mafao ya Watumishi waliomaliza muda kazini yanakokotolewa kwa usahihi kabla ya kuwasilishwa kwa ukaguzi wa awali ili kuhakikisha wastaafu wanalipwa mafao yao kwa wakati. Hii itasaidia kupunguza hatari ya upotezaji wa fedha za Serikali endapo madai yatakayozidi kiwango stahiki hayatabainika na vile vile kuwalinda wastaafu wasilipwe pungufu ya stahiki zao kutokana na mapunjo katika mafao yao.

7.8.2 Kuchelewa kwa Uandaaji na Upelekaji wa Taarifa za Mafao

Kanuni ya 88 ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2022, inawataka waajiri na waajiriwa kutunza kumbukumbu za kiutumishi kwa lengo la kufanya marejeo wakati wa ukokotozi wa mafao ya hitimisho la kazi.

Pia, Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma ya mwaka 2009 ikisomwa pamoja na Kanuni ya 32(4) ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2022 zinamtaka mtumishi wa umma anayekaribia kustaafu, kutoa taarifa ya maandishi kwa mwajiri wake kupitia taratibu za kawaida, kwa kipindi cha miezi sita kabla ya kustaaafu.

Katika ukaguzi wa mwaka 2021/22, nilibaini ucheleweshwaji kwenye uandaaji na uwasilishwaji wa majalada ya mafao 727 kwa ajili ya ukaguzi wa awali kwa kipindi cha kuanzia mwaka 1 hadi miaka 30 kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na.8. Ucheleweshwaji huo unaathiri hali ya maisha ya wastaafu au wategemezi kwani wengi wao hutegemea mafao ya kustaafu kama pato la kuendesha maisha yao baada ya kumaliza utumishi wa umma.

Jedwali Na. 51: Majalada Yaliyocheleweshwa

Muda wa ucheleweshwaji wa majalada	Idadi ya majalada
Mpaka miaka 2	563
Mpaka miaka 5	117
Mpaka miaka 10	22
Mpaka miaka 20	18
Mpaka miaka 30	7
Jumla	**727**

Chanzo: *Fomu za malipo ya mafao na uhakiki wa ukaguzi*

Naishauri Serikali kupitia Maafisa Masuuli kuhakikisha mafao ya kustaafu yanaandaliwa na kuwasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa wakati ili kuzuia ucheleweshaji wa malipo hayo.

7.8.3 Kutorudisha Majalada yenye Hoja kwa Ajili ya Ukaguzi wa Awali

Mchakato wa ukaguzi wa awali wa majalada ya mafao ya wastaafu unahusisha vigezo vitatu, ambavyo ni uhalali, ukamilifu wa nyaraka na usahihi wa hesabu. Nikibaini makosa au hitilafu (hoja) yoyote, jalada lazima lirudishwe kwa mwaajiri kwa ajili ya kurekebisha hoja iliyobainika na kurejesha majibu ndani siku 21 kutoka tarehe ya kupokea kama inavyotakiwa na Kanuni ya 86(2) ya Ukaguzi wa Umma Sura ya 47 ya mwaka 2009.

Katika ukaguzi nilibaini makosa katika majalada 17 na kurudisha kwa waajiri kwa ajili ya marekebisho. Hata hivyo, Majalada husika hayakurudishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa ajili ya kuhakiki wa marekebisho yaliyofanywa kwa kipindi cha miezi mitano hadi miezi ishirini na moja kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2022. Barua za kuwakumbusha Waajiri (Maafisa Masuuli) husika kuwasilisha majalada hayo zilitumwa lakini hazikujibiwa. Ucheleweshaji uliokithiri wa kurudisha majalada yaliyohojiwa unasababisha kuchelewa kwa malipo ya mafao na kuathiri hali ya maisha ya wastaafu.

Naishauri Serikali kupitia Maafisa Masuuli kuhakikisha hoja za ukaguzi zinafanyiwa kazi kwa haraka na kurudisha majalada kwa wakati na pale inapobidi kuomba ufafanuzi kutoka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Pia, iwachukulie hatua stahiki Maafisa Utawala

wanaochelewesha kuandaa na kuwasilisha majalada ya wastaafu kwa ajili ya ukaguzi wa awali.

7.8.4 Majalada Yaliyoidhinishwa kwa Malipo Kurudishwa kwa Ukaguzi kwa Mara nyingine

Kifungu Na. 44 cha Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii katika Utumishi wa Umma Na.2 ya mwaka 2018 zinazuia mstaafu kupata mafao mara mbili kwa kazi hiyo hiyo na kipindi hicho hicho.

Katika ukaguzi wangu wa mafao, nilibaini majalada 53 yenye jumla ya Sh. milioni 778.23 yaliyorudishwa kwa mara ya pili ofisini kwangu japokuwa nilipitisha majalada hayo kwa malipo kipindi cha nyuma. Ninaamini kuwa, urudishaji wa majalada yaliyokwishwa lipwa ni kutaka kuisababishia Serikali hasara kwa kulipwa mara mbili.

Serikali kupitia Maafisa Masuuli inashauriwa kuhakikisha kuwa mafaili ya wastaafu yaliyokaguliwa na kupitishwa yanarekodiwa kwenye rejista kwa ajili ya ufuatiliaji ili kuepusha kuwasilishwa tena kwa faili lile lile wakati mstaafu ameshalipwa.Kadhalika, Serikali kupitia Maafisa Masuuli inatakiwa kuboresha mifumo ya malipo kwa ajili ya kugundua na kuzuia malipo ya mara ya pili.



SURA YA NANE

USIMAMIZI WA MALI NA MADENI

8.1 Utangulizi

Usimamizi wa mali na madeni ni muhimu ili kuwa na utendaji wenye ufanisi. Pia, kupunguza hatari ya Serikali kupata hasara kutokana na kutolipa madeni kwa wakati. Serikali inahitaji kuhakikisha kuwa mali zake zinatumika kikamilifu. Hii inaweza kufanikiwa kwa kufanya matengenezo na ukarabati wa mara kwa mara, kuhakikisha kunakuwa na uhifadhi sahihi wa mali pamoja na kuondoa mali zisizohitajika. Kwa upande mwingine, Serikali inahitaji kusimamia madeni yake ili kuleta ufanisi katika kupunguza hatari ya kushindwa kulipa na kupunguza riba na adhabu. Hii inaweza kufanikiwa kwa kuboresha mkakati wa usimamizi wa madeni, kufuatilia viwango vya deni mara kwa mara, na kujadili masharti mazuri ya kukopa.

Sura hii inaelezea masuala yanayohitaji kuzingatiwa kutokana na usimamizi usioridhisha wa mali za kudumu kama vile magari, majengo na ardhi. Malengo ya taasisi yanaweza kufikiwa tu ikiwa rasilimali zitasimamiwa na kutumiwa kwa ufanisi katika shughuli za mkakati. Maelezo ya udhaifu uliioonekana na mapendekezo yaliyotolewa yameainishwa hapa chini:

8.2 Kukosekana kwa Mpango wa Matengenezo ya Mali

Kanuni ya 137(4)(a) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013, kama ilivyorekebishwa na Kanuni ya 47 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma (Marekebisho) ya mwaka 2016, inaagiza kila Taasisi kutunza kumbukumbu za matengenezo na ukarabati wa kila chombo (gari, mitambo na vifaa), matengenezo na ufungaji wa vifaa vya umeme (viyoyozi na majokofu), na huduma za elektroniki. Utunzaji huu ni muhimu kwa ajili ya kukaguliwa na TEMESA, Wizara inayohusika na masuala ya umeme, mitambo, pamoja na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Aidha, Aya ya 14 ya

Mwongozo wa Serikali wa Usimamizi wa Mali (toleo la mwaka 2019) linamtaka kila Afisa Masuuli kuhakikisha kuwa mpango wa matengenezo wa mali umeandaliwa na kuzingatiwa. Pia, kuhakikisha huduma zinatolewa vizuri ili kuongeza faida kwa taasisi.

Kinyume na Mwongozo na Kanuni zilizotajwa hapo juu, taasisi 31 hazikuwa na mpango wa matengenezo ya mali, na taasisi 6 zilikuwa na mpango wa matengenezo ya mali lakini hazikutunza kumbukumbu za ukarabati na matengenezo kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Na. XIII**. Hili ni eneo muhimu sana linalohitaji uangalizi wa menejimenti ili kuhakikisha kuwa mali zinatunzwa vizuri na kutumiwa kwa ufanisi ili kufikia malengo ya Serikali. Ni muhimu pia, kuwa na mpango wa matengenezo ya mali ili kuepuka kupoteza thamani kabla ya wakati wake kutokana na kutofanyiwa matengenezo.

Ninapendekeza Wizara, Idara, Wakala na Taasisi nyingine kuandaa mpango wa matengenezo ya mali na kuweka kumbukumbu za kina za ukarabati na matengenezo. Hii itasaidia kuhakikisha mali za Serikali zinatunzwa vizuri kwa ajili ya kutoa huduma na kuzuia hasara zisizo za lazima

8.3 Magari, Mitambo na Vifaa vya Serikali Vilivyotelekezwa kwa Muda Mrefu.

Kanuni ya 254(1) na (2) ya Kanuni za Fedha za Umma za mwaka 2001 inaelekeza kuwa samani, magari, mitambo au vifaa ambavyo vimefikia mwisho wa kutumika kwa manufaa au havitengenezeki kwa sababu yeyote ile. Afisa Masuuli anatakiwa kuomba kibali kwa Mhasibu Mkuu wa Serikali ili kuvifuta, kuvigawa au kuviuza.

Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kuwepo kwa taasisi 58 zenye mali za kudumu 2800 (magari, pikipiki, mitambo na vifaa) ambazo hazitumiki kwa muda mrefu au kufanyiwa matengenezo. Mali hizi zimetelekezwa kwa muda mrefu kuanzia mwaka mmoja hadi miaka 22 bila kufanyiwa matengenezo yoyote muhimu au kuchelewa kupata idhini ya kuyaondoa au kuyauza kutoka kwa Mhasibu Mkuu wa Serikali tazama **Kiambatisho Na. XIV**.

Uwepo wa magari, mitambo na Vifaa vya Serikali vilivyotelekezwa kwa muda mrefu kunachangiwa na mchakato usio madhubuti wa kupata idhini

ya kuondosha mali chakavu, pamoja na ukosefu au upungufu wa fedha za kufanyia matengenezo. Ni muhimu kuchukua hatua za kukabiliana na masuala haya ili kupunguza kuwapo kwa mali zilizotelekezwa, kuboresha ufanisi wa uendeshaji, na kuzuia hasara kwa taasisi za Serikali.

Idadi ya mali za kudumu ambazo hazitumiki kwa muda mrefu zimeongezeka kutoka 489 za mwaka wa ukaguzi uliopita (2020/21) hadi 2827 kwa mwaka huu wa ukaguzi. Kati ya mali hizo 2837, magari ni 521 na mitambo, pikipiki na vifaa vingine ni 2306.

Maoni yangu ni kuwa kutelekezwa kwa magari, pikipiki, na vifaa visivyotumika kwa muda mrefu kunasababisha mali hizo kuzidi kuchakaa. Hivyo, huweza kupunguza mapato ambayo yangeweza kupatikana kama uamuzi wa kuyauza mapema ungezingatiwa.

Mapendekezo yangu ni kuwa serikali na taasisi husika zihakikishe zinauza haraka magari, pikipiki, mitambo na vifaa ambavyo havitumiki kwa muda mrefu kutokana na gharama kubwa za matengenezo. Kufanya hivyo kutapunguza gharama za kuendelea kuhifadhi. Pia, zihakikishe zinatoa kwa wakati kibali cha kufuta na kuondoa mali hizo ili kuepuka kupungua zaidi kwa thamani ya mali hizo.

8.4 Kutotumia Mfumo wa Taarifa wa Usimamizi wa Mali za Serikali (GAMIS)

Waraka Na. 2 wa mwaka wa fedha 2021/22 kutoka kwa Msajili wa Hazina unawataka Maafisa Masuuli kutumia mfumo wa Taarifa wa Usimamizi wa Mali za Serikali (GAMIS) kutunza kumbukumbu sahihi za mali na usimamizi. Mfumo huu unafanya kazi za kutunza taarifa za mali za kudumu, unawezesha kukokotoa gharama za uchakavu, na jumuisho la mali za kudumu kwa ngazi ya kitaifa.

Pia, waraka unataka nyongeza au uondoshaji wa mali yoyote, pamoja na uwekaji wa namba za utambulisho kupitia msimbo lazima ufanyike kwa ufanisi kupitia mfumo kuanzia mwaka wa fedha 2020/21 na kuendelea. Kinyume na maagizo ya waraka huu, ukaguzi wangu ulibaini kuwa taasisi 14 hazikutumia mfumo wa serikali ulioanzishwa kwa ajili ya kumbukumbu na usimamizi wa mali. **Jedwali Na. 52** linaonesha taarifa za taasisi zisizotumia mfumo wa GAMIS.

Jedwali Na. 52: Taasisi Zisizotumia Mfumo wa GAMIS

Na.	Taasisi	Kiasi ambacho hakijaripotiwa kwenye GAMIS (Sh.)
1.	Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (TPDF)	110,619,496,450
2.	Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa	Haijatambuliwa
3.	Idara ya Huduma za Magereza	650,752,896
4.	Wakala wa Ufundi na Umeme(TEMESA)	Hakijaripotiwa
5.	Tume ya Taifa ya UNESCO	106,067,571
6.	Hospitali ya Kanda,Chato	373,972,097
7.	Wizara ya Elimu,Sayansi na Teknolojia (MoEST)	351,240,342,561
8.	Shirika la Uzalishaji Mali la Magereza	Hakijaripotiwa
9.	Taasisi ya Kuthibiti Ubora wa Mbegu Tanzania (TOSCI)	Hakijaripotiwa
10.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka -Kasulu (Kuwssa)	2,858,764,168
11.	Tume ya Madini	28,682,031,811
12.	Shirika la Mzinga	50,632,447
13.	Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali	22,818,551,736
14.	Shirika la Nyumbu	32,609,562,000

Chanzo: *Ripoti za Ukaguzi mwaka 2021/22*

Udhaifu huu umesababishwa na kutofuata ipasavyo maagizo ya ufungaji hesabu kutoka kwa Mhasibu Mkuu wa Serikali (ACCGEN) na mafunzo duni kuhusu utumiaji wa mfumo wa GAMIS. Kutofuata waraka huu kunaweza kusababisha hesabu za mali za kudumu kutoandaliwa kwa usahihi kuhusu mali za kudumu.

Ninapendekeza maafisa masuuli katika taasisi husika watumie kikamilifu mfumo wa usimamizi wa mali na kuzingatia miongozo yote ya serikali ili kuhakikisha usimamizi thabiti wa kumbukumbu za mali za kudumu.

8.5 Majengo Yaliyochakaa Katika Vyuo Saba vya Walimu na Taasisi Nyingine

Kifungu cha 14 cha Mwongozo wa Usimamizi wa Mali za Umma wa mwaka 2019, kinamtaka Afisa Masuuli ahakikishe kuwa mpango wa matengenezo unaandaliwa na kufuatwa kwa mali zote za taasisi. Hii itasaidia kuhakikisha kuwa mali zinabaki na ubora wake, zinawezesha kutoa huduma, pamoja na

kuleta mafanikio ya kiuchumi. Kila mkuu wa kitengo anapaswa kuandaa mpango wa matengenezo na kutoa ripoti ya utekelezaji wake kwa afisa masuuli kila robo mwaka. Pia, ahifadhi rejista ya matengenezo ya mali.

Nilibaini kuwa kuna vyuo saba vya ualimu, ambavyo vina jumla ya nyumba 51 za wafanyakazi ambazo ziko katika hali mbaya. Vyuo hivyo ni Chuo cha Ualimu Ilonga, Chuo cha Ualimu Morogoro, Chuo cha Ualimu Nachingwea, Chuo cha Ualimu Vikindu, Chuo cha Ualimu Korogwe, Chuo cha Ualimu Bustani, na Chuo cha Ualimu Tukuyu. Nyumba hizi zina matatizo kama vile, paa kuvuja, ukungu ukutani, mfumo duni wa umeme, milango na madirisha yaliyoharibika, na uzio usiofaa. Aidha, mfumo wa maji safi na maji taka haufanyi kazi vizuri, hali inayosababisha hali mbaya kwa majirani kutokana na uvujaji wa maji taka.

Aidha, nimegundua kuwa majengo 1,934 katika maeneo saba tofauti yametelekezwa kwa miaka kadhaa. Majengo haya yana matatizo mbalimbali kama kuta zinazoporomoka, dari chakavu, na madirisha yaliyovunjika. Ukosefu wa matengenezo ya mara kwa mara umesababisha kuharibika kwa majengo hayo, hivyo kuweka hatari kwa wakazi na watu wanaopita karibu.

Ni muhimu kushughulikia masuala haya kwani yanaweza kuathiri ubora wa maisha ya wafanyakazi wanaoishi katika nyumba hizo. Aidha, ni lazima kufanyia matengenezo nyumba hizi ili kuhakikisha kuwa zinadumu kwa muda mrefu na kuzuia uharibifu zaidi.

Jedwali Na. 53: Maelezo ya Majengo Yasiyokarabatiwa

Na	Taasisi	Idadi ya majengo
1	Wizara ya Elimu, Sayansi, na Teknolojia (MoEST)	7
2	Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA)	16
3	Wakala wa Majengo Tanzania (TBA)	1867
4	Tume ya Taifa ya Mipango na Matumizi ya Ardhi	11
5	Jeshi la Polisi Tanzania (fungu 28)	33
Jumla		**1934**

Chanzo: *Taarifa za Ukaguzi mwaka 2021/22*

Udhaifu huu unatokana na kutofanyika kwa matengenezo ya kawaida ya majengo ya Serikali. Ili kuweza kufikia utendaji ulio bora kwa watumishi wa umma katika kutoa huduma zao, wanahitaji mazingira mazuri ya kufanyia

kazi na makazi. Hivyo, kufanya kazi katika majengo yaliyoharibika si tu kunapunguza morali ya kufanya kazi, bali pia ni hatari kwa wafanyakazi wanaofanyia kazi katika majengo hayo.

Napendekeza Maafisa Masuuli wa taasisi husika kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango wahakikishe kuwa fedha za kutosha zinatolewa kwa ajili ya ukarabati wa majengo yaliyoharibika.

8.6 Magari Yaliyolipiwa Lakini Hayajapokelewa Sh. Bilioni 4.06

Kanuni ya 242 (i) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 iliyorekebishwa mwaka 2016, inaeleza kuwa ambapo upokeaji wa bidhaa unacheleweshwa au unaonekana utacheleweshwa zaidi ya wakati uliowekwa katika mkataba, taasisi nunuzi lazima ipate ripoti na maelezo kutoka kwa wauzaji au mawakala wao. Pia, inaweza kuweka adhabu ya kikomo kama ilivyoelezwa katika mkataba.

Nimebaini kuwa Taasisi tisa zilinunua magari 21 kupitia Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini (GPSA). Hata hivyo, magari hayo bado hayajakabidhiwa kwa wamiliki husika.

Jedwali Na. 54: Magari Yaliyolipiwa ila Hayajapokelewa

Na.	Taasisi	Idadi	Kiasi cha mkataba (Sh)	Tarehe ya Malipo	Muda Uliochelewesh hwa
1	Baraza la Famasia	1	178,266,378	1 Aprili 2022	Miezi 5
2	Wizara ya Nishati	4	581,150,667	17 Machi 2022	Miezi 4
3	Wizara ya Madini	2	1,611,886,368	24 Desemba 2020	Miezi 20
4	Taasisi ya Mafunzo ya Misitu (FITI)	1	236,213,589	Aprili 2022	Miezi 6
5	Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora-Fungu 55	1	178,266,378	4 Novemba 2021	Siku 28
6	Ofisi ya Taifa ya Mashtaka (NPS (fungu 35)	3	439,923,375	15 Desemba 2021	Miezi 8
7	Mfuko wa Ukaguzi na Usimamizi wa Ushirika (ISCF)	6	588,489,806	10 Mei 2021 and 5 Januari 2022	Miezi 16
8	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa	1	92,346,913	29 Machi 2022	Miezi 5

Na.	Taasisi	Idadi	Kiasi cha mkataba (Sh)	Tarehe ya Malipo	Muda Uliochelewesh hwa
	-Mawenzi				
9	Wizara ya Afya	2`	151,749,924	7 Septemba 2020	Miezi 28
Jumla		**21**	**4,058,293,398**		

Chanzo: *Taarifa za Ukaguzi*

Maoni yangu ni kuwa, kuchelewa kukabidhi magari yaliyonunuliwa kunakwamisha kufikiwa kwa malengo yaliyotarajiwa, hivyo kuathiri shughuli za usimamizi na ufuatiliaji.

Napendekeza menejimenti za taasisi husika zifanye ufuatiliaji wa karibu kwa Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini (GPSA) ili kuhakikisha magari yanafikishwa kwa Taasisi nunuzi.

8.7 Viwanja vya Serikali ambavyo Havijaendelezwa

Nilibaini taasisi tatu zinamiliki viwanja ambavyo havijaendelezwa. Suala hili nililitolea taarifa katika ripoti zangu za miaka ya nyuma pia. Hata hivyo, inaonekana hakuna hatua za kulipatia ufumbuzi jambo hili kwani idadi imeongezeka kutoka viwanja vinne vilivyoripotiwa mwaka 2020/21 mpaka viwanja 862. Taarifa zaidi imeoneshwa katika **Jedwali Na. 55**.

Jedwali Na. 55: Viwanja vya Serikali ambavyo Havijaendelezwa

Na	Taasisi	Idadi ya viwanja	Maelezo
1	Jeshi la Kujenga Taifa (fungu 39)	1	Kiwanja kinatarajiwa kujengwa Chuo cha Mafunzo eneo la Kongwa Mkoa wa Dodoma kulingana na Mpango wa Matumizi ya Ardthi wa Agosti 2014.
2	Wakala wa Majengo Tanzania (TBA)	860	Viwanja idadi ya 850 havijaendelezwa takribani miaka nane na viwanja 10 vilivyopo Morogoro havijaendelezwa.
3	Chuo cha Ardhi Tabora (ARITA)	1	Kiwanja Na .49 kilichopo eneo la Cheyo “Mabatini” hakijaendelezwa.

Chanzo: *Taarifa za Ukaguzi*

Ninaamini kuwa ukosefu wa fedha za kutosha za kuendeleza viwanja hivyo ndio sababu ya viwanja vingi kutelekezwa.

Napendekeza kuwa taasisi husika zenye maeneo yasiyoendelezwa, waweke mipango ya utekelezaji na makadirio ya gharama za ujenzi na kuanza kutafuta fedha za kuendeleza viwanja hivyo.

8.8 Madeni ya Muda Mrefu

Kanuni ya 44 (1) ya Kanuni ya Ununuzi wa Umma, 2013 inaeleza kuwa 'kwa madhumuni ya kusaidia ukuaji wa makampuni ya ndani na kuwezesha makampuni hayo kutimiza wajibu wao wa kimkataba, taasisi zinazofanya ununuzi zitahakikisha kuwa malipo yanafanyika kwa wakati kwa wazabuni.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2022, Wizara, Idara, Wakala na Hospitali za Rufaa za Mikoa ziliripoti madeni ya jumla ya Sh. Trilioni 4.08. Kati ya madeni hayo, Sh. bilioni 509.21 (13%) ni madai ya watumishi, Sh. trilioni 3.40 (83%) ni madeni ya wazabuni na wakati Sh. Bilioni 170.29 (4%) ni madeni mengine.

Uchambuzi wangu zaidi ulibaini kuwa, Sh. Trilioni 3.19 (78%) yalikuwa ni madeni ya muda mrefu ambayo hayajalipwa kwa zaidi ya miezi 12. Madeni yanayodaiwa ndani ya miezi 12 yalifikia Sh. Bilioni 896.70 (22%), ambayo yasiposhughulikiwa kwa wakati yanaweza kusababisha madeni ya muda mrefu na kuathiri sifa ya Serikali na ari ya wauzaji bidhaa.

Ongezeko hilo la madeni linachangiwa na ucheleweshaji wa kutolewa kwa fedha kutoka Wizara ya Fedha na Mipango. Taasisi zenye madeni ambayo hayajalipwa ni kama inavyooneshwa katika **Kiambatisho Na. XV**.

Kushindwa kulipa madeni yanapofikia muda wa kulipwa kunatia dosari sifa ya serikali kwa wakandarasi, wasambazaji na watoa huduma. Hii imesababisha kuongezeka kwa gharama kutokana na riba na adhabu kwa madeni yaliyochelewa kulipwa na kuongezeka kwa bajeti.

Aidha, mapitio ya taarifa za fedha na barua yenye namba ya kumbukumbu CHA.226/446/06/07 ya tarehe 20 Oktoba, 2022 kutoka Wizara ya Afya yalibainisha kuwa hadi kufikia tarehe 30 Juni 2022, Wizara ya Afya (fungu 52) ilikuwa na madai ya jumla ya Sh. bilioni 9.21 ambayo hayajalipwa. Haya ni madai ya fedha za matibabu kutoka hospitali za rufaa nchini India.

Jedwali Na. 56: Madai ya Matibabu Kutoka Hospitali za Rufaa India

Na.	Taasisi	Madai ya Matibabu		Kiasi cha fedha (Sh.)
		Kiasi cha Fedha	Fedha	
1	Hospitali ya Indraprastha Apollo	131,331,783.94	INR	3,850,595,372
2	Hospitali ya Apollo Hyderabad	72,512,514.72	INR	2,126,037,927
3	Hospitali ya Chennai Apollo	51,647,854.83	INR	1,514,294,444
4	Hospitali ya Apollo Ahmedabad.	11,443,321.00	INR	335,513,594
5	Hospitali ya Apollo Bangalore	8,176,656.00	INR	239,736,283
6	Madras Medical Mission	495,410.00	USD	1,147,201,121
Jumla				**9,213,378,742**

Source: *Hesabu ya Wizara ya Afya ya Mwaka 20221/2022*

Changamoto ya kutolipa madai inatokana na aina ya bajeti ya Serikali, ambayo kimsingi inazingatia fedha taslimu wakati uhalisia wake upande wa matumizi ni kwa msingi usio wa fedha taslimu. Zaidi ya hayo, Serikali haijatenga fedha kwa ajili ya malipo ya madeni makubwa ambayo hayajalipwa, jambo ambalo limesababisha mlundikano wa madeni ya muda mrefu pamoja na riba na adhabu.

Kwa hiyo, napendekeza Serikali itoe fedha kwa mujibu wa bajeti iliyoidhinishwa. Pia, itoe kwa wakati ili kupunguza mlundikano wa madeni ambayo hayajalipwa kwa muda mrefu. Serikali pia inapaswa kujumuisha madeni ya sasa katika bajeti za kila mwaka. Mbinu hii itahakikisha kuwapo kwa fedha za kutosha za kulipia madeni yanayodaiwa, hivyo kuifanya Serikali isipate sifa mbaya kutoka kwa wasambazaji na wakandarasi. Vilevile, kutapunguza gharama zinazohusiana na riba na adhabu.

8.9 Madeni Tarajiwa (Kesi Ambazo Hazijafanyiwa Maamuzi) Sh. Trilioni 3.83

Madeni tarajiwa ni madeni ambayo yanaweza kujitokeza kutokana na tukio lisilo na uhakika la siku zijazo, kama vile matokeo ya maamuzi ya Mahakama kutokana na madai yaliyowasilishwa mahakamani. Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2022, taasisi 23 zilikuwa na kesi za kisheria zenye madai ya jumla ya Sh. 3,833,656,486,059 zikisubiri maamuzi ya mahakama dhidi ya mashirika

mbalimbali na watu binafsi. Orodha ya kina ya taasisi zilizo na kesi za kisheria ambazo hazijakamilika inaoneshwa katika **Kiambatisho Na. XVI**.

Kuna hatari ya kuingia katika matumizi yasiyo na faida kwa Wizara, Idara, na taasisi zingine za Serikali yatokanayo na faini ambayo itatakiwa kulipwa mahakamani iwapo taasisi hizi zitashindwa kesi. Aidha, wizara na taasisi zingine zinatumia kiasi kikubwa cha fedha katika ufuatiliaji wa kesi hizi.

Kwa hiyo, napendekeza kila wizara, idara na taasisi nyingine ziwe na mikakati inayofaa kusimamia madeni yanayoweza kutokea katika mazingira yao. Hii itahakikisha taasisi inakuwa katika mazingira mazuri ya kudhibiti hatari na madhara ya madeni kama vile kutozwa faini au adhabu. Pia, taasisi zitapunguza kiasi cha matumizi kinachohitajika kwa ufuatiliaji wa kesi za kisheria.

Zaidi ya hayo, napendekeza menejimenti ihakikishe kuwa wanasheria wanafuatilia kwa karibu kesi zinazoendelea na kutoa msaada wa kisheria unaohitajika kwa uamuzi unaofaa wa kesi hizo.

SURA YA TISA

UNUNUZI NA USIMAMIZI WA MIKATABA

9.1 Utangulizi

Serikali ya Tanzania inatambua umuhimu wa ununuzi na usimamizi mzuri wa mikataba ya umma kama dhana ya kuhakikisha matumizi bora, na uwajibikaji katika kusimamia rasilimali za umma. Kwa kufanya hivyo, Bunge limetunga Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 7 ya mwaka 2011 (kama ilivyorekebishwa 2016) na Kanuni zake za mwaka 2013 (kama zilivyorekebishwa 2016) ili kutoa mfumo wa kisheria unaosimamia uanzishaji wa taasisi na michakato ya manunuzi katika sekta ya umma.

Katika kutimiza majukumu yangu ya kisheria kama yalivyoainishwa katika kifungu cha 48 (3) cha Sheria hii, nimejumuisha katika sura hii tathmini na uchunguzi wa taratibu za ununuzi wa umma pamoja na kufuata sheria na kanuni za ununuzi. Zifuatazo ni dosari zilizobainika kutokana na ukaguzi wangu wa uzingatiaji wa Sheria ya Ununuzi wa Umma na Kanuni zake.

9.2 Ununuzi wa Magari Matatu ya Zimamoto kutoka kwa Mtengenezaji Asiyeidhinishwa yenye Thamani ya Sh. Bilioni 2.98

Kanuni ya 159 (1) ya Kanuni ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2013, kama ilivyorekebishwa na Kanuni ya 60 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma (sheria ya marekebisho) ya mwaka 2016, inaruhusu ununuzi kutoka chanzo kimoja katika mazingira maalumu. Mazingira haya ni pamoja na hitaji la dharura la bidhaa au huduma, haki za kipekee za mzabuni fulani kutoa bidhaa au huduma, manunuzi yanayohusisha ulinzi au usalama wa taifa, miradi inayoendelea, au sababu ya kununua vitu vya ziada kwa ajili ya kukamilisha utekelezaji. Hata hivyo, ununuzi huo wa chanzo kimoja lazima uidhinishwe na Bodi ya Zabuni.

Wakati wa ukaguzi wangu kuhusu usimamizi wa ununuzi, nilibaini kuwa tarehe 21 Desemba 2020, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi iliingia makubaliano Namba. 014/2019/2020/FRF/G/11 na Kituo cha Teknolojia ya Magari Tanzania (TATC) kwa ajili ya kuleta magari matatu ya zimamoto kwa jumla ya Sh. Bilioni 2.98 kwa kipindi cha miezi 15 kuanzia tarehe 21 Desemba 2020 hadi tarehe 21 Machi 2022. Hata hivyo iligundulika kuwa, TATC hakuwa muuzaji aliyeidhinishwa au mtengenezaji aliyeidhinishwa wa vifaa vya kuzima moto.

Hata hivyo, magari yenye injini za zimamoto yalikuwa bado hayajawasilishwa hadi kufikia wakati wa ukaguzi wangu mnamo Desemba 2022 (nilibaini ucheleweshwaji kwa miezi zaidi ya 24) licha ya ukweli kwamba muuzaji alikuwa amelipwa kiasi cha Sh. bilioni 2.23 Februari 2021 sawa na asilimia 75 na hakukuwa na makato yoyote ya ucheleweshaji wa kazi yaliyokatwa kulingana na matakwa ya Kanuni ya 243(5) (b) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma, 2013.

Nina maoni kwamba, kwa kununua magari kutoka TATC ambaye sio muuzaji au mtengenezaji aliyeidhinishwa, kunaweza kupelekea Wizara kutokuwa na dhamana ya huduma kwa kipindi fulani, vifaa kutokuwa na ubora halisi wa mtengenezaji na kusababisha kiwango katika utendaji wake ikilinganishwa na kama yangenunuliwa kutoka kwa muuzaji aliyeidhinishwa.

Ninapendekeza Wizara ya Mambo ya Ndani kuhakikisha kuwa katika siku zijazo, ununuzi wa magari yenye injini za zimamoto unafanyika kupitia muuzaji aliyeidhinishwa. Hata hivyo, wizara ihakikishe inafanya mawasiliano na TATC kuhakikisha kwamba magari hayo yanaletwa bila kuchelewa na pia kuhakikisha kuwa gharama za ucheleweshwaji zinadaiwa kulingana na masharti ya mkataba.

9.3 Dosari Zilizobainika katika Ununuzi wa Vishikwambi 300,000 Uliofanywa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

Mnamo Mwezi Machi 2022, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilipewa jukumu la kununua vishikwambi 300,000 kwa ajili ya Sensa ya Watu na Makazi iliyofanyika mwezi Agosti 2022. Kupitia zabuni Na. ME-024/2021-22/HQ/G/34, Wizara ilianzisha mchakato wa zabuni, ikialika wazabuni 14 kushiriki. Zabuni hiyo iligawanywa katika sehemu sita, kila moja ikiwa na vishikwambi 50,000. Wizara ilisaini mikataba na wazabuni watatu wa kuleta

vishikwambi 300,000 vyenye thamani ya Sh. Bilioni 123.78, (bei ya awali Sh. bilioni 104 na kodi ya ongezeko la thamani Sh. bilioni 18.992). Muda wa wazabuni kuwasilisha vishikwambi hivyo ulikuwa siku 40 baada ya kusaini mkataba. Ukaguzi wangu ulibaini dosari mbalimbali kama ilivyoainishwa kwenye **Jedwali Na. 57**.

Jedwali Na. 57: Kasoro Zilizobainika kwenye Ununuzi wa Vishikwambi

Na.	Suala	Maelezo
i.	Upitishwaji wa wazabuni usio wa haki	Wazabuni walichaguliwa bila ushindani; wajumbe wa bodi ya zabuni walipendekeza wazabuni 4 kati ya 14, 2 kati yao walishinda zabuni sio kazi ya Bodi ya zabuni kupendekeza wazabuni
ii.	Mabadiliko ya vigezo vya ubora	Bodi ya zabuni ilibadilisha vigezo vya ubora bila kuwasiliana na idara tumizi na kuondoa vifaa vya kutunzia umeme (power bank).
iii.	Bei za soko kutowekwa wazi	Idara ya manunuzi ya Wizara ilishindwa kuainisha bei za soko la vishikwambi. Hivyo huenda vimenunuliwa kwa bei ya juu ikilinganishwa na bei ya soko.
iv.	Muda wa zabuni usiotosheleza	Wazabuni walipewa siku 2 tu za kujibu nyaraka za zabuni badala ya 14, huku wazabuni 10 tu kati ya 14 wakiwasilisha kwa wakati.
v.	Kutofautiana kwa taarifa	Tofauti zilizopatikana kati ya bei za zabuni zinazojumuisha VAT katika taarifa ya ufunguzi wa zabuni na ripoti za tathmini ambapo zabuni hazikueleza hali ya VAT isipokuwa zabuni moja.
vi.	Dosari za kamati ya tathmini	Idara tumizi haikuhusika katika kamati na wajumbe waliteuliwa bila mapendekezo ya Idara ya ununuzi.
vii.	Kukosa hati dhamana ya ubora wa vishikwambi	Hakuna ushahidi wa hati ya udhamini uliotolewa kwa vishikwambi vilivyonunuliwa, kinyume na matakwa ya mkataba ulioainisha makubaliano ya hati ya miaka miwili .
viii.	Utunzaji usioridhisha wa vishikwambi	Wizara ilitoa vishikwambi 209,480 kwa Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) bila nyaraka sahihi au tarehe ya wazi ya makabidhiano na ripoti ya hali baada ya zoezi la sensa.

Chanzo: *Maelezo ya Mkataba*

Kasoro hizi zinaonesha kuwa mchakato wa ununuzi uliathiriwa na thamani bora ya fedha inaweza kuwa haijafikiwa.

Ninapendekeza kwamba Wizara ya Elimu, Sayansi na Tekinolojia izingatie miongozo ya ununuzi, kuweka bei za soko, kuhusisha idara za watumiaji katika michakato ya ununuzi, kudumisha kumbukumbu sahihi, na kutoa muda wa kutosha kwa wazabuni. Wizara na NBS pia wanapaswa

kutathmini hali ya vishikwambi vilivyotumika wakati wa sensa na kuvisambaza kwa walimu kama ilivyopangwa.

9.4 Dosari Zilizobainika kwenye Zabuni ya Loti namba 2, 4 na 6 kwa Kampuni ya Shenzhen Technology Company Limited kwa Usambazaji wa Vishikwambi 150,000

Kanuni ya 231 (1) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma, 2013 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2016 inaeleza kuwa, "Bodi ya Zabuni, kwa mujibu wa kifungu cha 75 cha Sheria, itaidhinisha mapendekezo ya timu ya tathmini na kumjulisha Afisa Masuuli kwa uamuzi wake wa tuzo ndani ya siku tatu za kazi baada ya kufanya uamuzi."

Mnamo tarehe 25 Juni 2022, Wizara iliingia mkataba na Kampuni ya Shenzhen Benton Technology Company Limited kwa uletaji wa vishikwambi 150,000 (kwa loti 2,4 na 6) vyenye thamani ya Mkataba wa Sh. bilioni 46.86 kwa kipindi cha siku 40 kuanzia tarehe ya kusaini mkataba (25 Juni 2022), ambapo vilipaswa kupokelewa tarehe 5 Agosti 2022.

Ukaguzi wa zabuni Na. ME-024/2021-22/HQ/G/34 kama ilivyoidhinishwa na Bodi ya Zabuni ya Wizara (MTB), ilibainisha kuwa Bodi ya Zabuni ya Wizara ilitia shaka kuhusu mzabuni aliyeshinda, M/s Shenzhen Technology Company Limited, kutokana na maoni hasi yaliyotokana na matokeo ya uchunguzi iliyofanywa na Ubalozi wa Tanzania nchini China. Bodi ya Wizara iliomba ushauri kutoka kwa Wakala Ununuzi Serikalini pamoja na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ambao walishauri hatua za tahadhari zichukuliwe ikiwa tuzo hiyo itatolewa kwa muuzaji. Licha ya ushauri wa kuingiza kifungu kinachoeleza malipo yatafanyika baada ya kupokelewa, Wizara ilisaini mkataba na mzabuni kwa masharti ya malipo ya awali ya asilimia 20 na malipo ya asilimia 80 wakati wa upokeaji wa bidhaa. Pia nilibaini kasoro zifuatazo:

i) Zabuni hiyo iliidhinishwa na wajumbe wawili tu wa Bodi ya zabuni ya Wizara badala ya akidi inayohitajika ya wajumbe wanne, ambayo ni ukiukwaji wa Sehemu ya 2 ya Sheria ya Ununuzi wa Umma, 2011 (kama ilivyorekebishwa mwaka 2016).

ii) Mzabuni huyo alijulishwa kushinda zabuni tarehe 22 Juni 2022, kabla ya zabuni hiyo kuidhinishwa na Bodi ya Zabuni ya Wizara iliyoidhinishwa tarehe 23 Juni 2022.

iii) Kampuni ya Shenzhen Benton Technology Company Limited na Wizara walisaini mkataba tarehe 25 Juni 2022 kwa ajili ya uletaji wa vishikwambi 150,000 kwa dola za Marekani Milioni 20.28 (sawa na Sh. bilioni 46.86). Hata hivyo, mkataba huo haukupelekwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa upekuzi kinyume na kanuni namba 59 ya mwaka 2013 (iliyorekebishwa 2016) inayotaka mikataba zaidi ya bilioni 1 kupekuliwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

iv) Mapitio ya faili la mkataba yalibainisha kuwa, mzabuni hakuwasilisha hati ya dhamana. Aidha, mapitio ya Masharti Maalum na masharti ya Jumla ya mkataba yalibainisha kuwa, vifungu hivyo havikuonesha sharti la kuwasilisha dhamana ya utendaji ili kuhakikisha utendaji wenye ufanisi wa mkataba kama ulivyoainishwa katika Kanuni za Ununuzi wa Umma. Kifungu hicho kingekuwa na umuhimu mkubwa, kulingana na uchunguzi wa kina uliofanywa tarehe 06 Aprili 2022 na mapendekezo kutoka kwa PPRA dhidi ya mzabuni, dhamana ya utendaji ingelinda maslahi ya Wizara kwa kuhakikisha Mzabuni anatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa mkataba.

v) Nilibaini kuwa, mzabuni Shenzhen Technology Company Limited, alishindwa kutimiza wajibu wa kimkataba kwa kuwasilisha vishikwambi katika tarehe ya mkataba (05 Agosti 2022) bila kuomba nyongeza ya muda kutoka kwa Wizara. Mzabuni alikamilisha kazi tarehe 29 Agosti 2022 hivyo kusababisha kuchelewa kwa siku 25. Masharti ya mkataba yalieleza kuwa fidia ya ucheleweshwaji itatozwa kwa kuchelewa kuleta vishikwambi kwa wakati. Hivyo, kiasi cha Sh. Milioni 540.25 kilipaswa kutozwa kwa mzabuni. Hata hivyo, Mzabuni hakutozwa fidia hiyo kwa ucheleweshwaji alioufanya.

Ninapendekeza menejimenti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ihakikishe akidi inayohitajika ya wajumbe inatimia wakati wa kufanya maamuzi ya bodi ya zabuni na kutoa taarifa/barua ya mzabuni aliyeshinda zabuni baada ya idhini ya bodi ya zabuni. Zaidi ya hayo, Wizara inapaswa kuhakikisha kwamba mikataba yote yenye thamani ya

Sh. bilioni 1 na zaidi inawasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Vilevile, Wizara inapaswa kuzingatia ushauri wa PPRA na Mwanasheria Mkuu wa Serikali pale unapotolewa. Aidha, katika zabuni zijazo makubaliano ya Mkataba yanapaswa kutekelezwa.

9.5 Ununuzi Mdogo Haujaripotiwa kwa Bodi ya Zabuni kiasi cha Sh. Bilioni 1.31

Kanuni ya 166 (7) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 (ilivyorekebishwa 2016) zinataka manunuzi yote madogo kuripotiwa kwenye bodi ya zabuni kila mwezi na mwenye mamlaka iliyokabidhiwa jukumu hilo, kwa kutumia fomu sahihi iliyotolewa na Mamlaka.

Hata hivyo, nilibaini kuwa taasisi 9 zilifanya ununuzi wa bidhaa zenye thamani ndogo kiasi cha Sh. bilioni 1.31 lakini hazikuripoti kila mwezi kwenye Bodi zao za Zabuni kulingana na matakwa ya Kanuni ya 166 (7) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma, 2013. Taasisi hizo ni pamoja na, Mafungu sita (Sh. milioni 672.72), Wakala wawili (Sh. milioni 577.78 na Taasisi nyingine mbili (Sh. milioni 60.55) kama ilivyoelezwa katika **Kiambatisho Na. XVII** cha ripoti hii.

Ni maoni yangu kwamba kushindwa kutoa taarifa za manunuzi madogo madogo kwa Bodi ya Zabuni kwa mujibu wa Kanuni za Ununuzi wa Umma 2013 (Iliyorekebishwa 2016) kunatoa fursa kufanyika manunuzi yasiyo ya kawaida bila umakini wa usimamizi na vikwazo katika uwazi.

Uchambuzi wangu unaonesha kuwa, kuna kupungua kwa kiasi cha kutofuata utaratibu kwa kiasi cha Sh. milioni 106.70 sawa na asilimia 7.5 (yaani Sh. bilioni 1.42 na Sh. bilioni 1.31 kilichoripotiwa mwaka 2020/21 na 2021/22 mtawalia.

Nina maoni kwamba Bodi za Zabuni za Wizara, Vitengo na Mamlaka husika, zina ukomo wa kutekeleza majukumu yake kulingana na matakwa ya Kanuni ya 166 (7) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma, 2013.

Ninapendekeza taasisi za ununuzi kuhakikisha vitengo vya Ununuzi vinaripoti kila mwezi manunuzi yote madogo madogo kwa Bodi ya Zabuni ili kuwezesha ufuatiliaji na udhibiti wa ununuzi katika taasisi za Serikali.

9.6 Kutofuatwa kwa Mipango ya Ununuzi ya Mwaka Kiasi cha Sh. Bilioni 2.72

Kifungu cha 69(7) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma, 2011 (kama ilivyorekebishwa mwaka 2016) kinataka Taasisi Nunuzi kuandaa mipango ya manunuzi ya mahitaji ambapo fedha za kutosha zimejumuishwa katika bajeti iliyoidhinishwa katika mwaka huo wa fedha au kama malipo yatatakiwa katika mwaka wa fedha unaofuata, basi malipo hayo yawe yametengewa bajeti.

Hata hivyo, nilibaini kuwa katika kipindi cha mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2022, Taasisi za Serikali zipatazo saba zilinunua bidhaa na huduma kiasi cha Sh. bilioni 2.72 ambapo hazikuwamo katika mipango ya manunuzi ya kila mwaka ya Taasisi husika. Ikiwa mipango ya kila mwaka ya Ununuzi ingeandaliwa vizuri kulingana na bajeti zilizoidhinishwa na Taasisi husika ingemaanisha kuwa manunuzi yote ambayo hayakujumuishwa katika mipango ya kila mwaka haikupangwa katika bajeti ambayo ni ukiukaji wa Sheria iliyotajwa hapo juu. Maelezo zaidi yanaonekana katika **Jedwali Na. 58**:

Jedwali Na. 58: Orodha ya Wizara, Vitengo na Wakala zilizokiuka Mpango wa Ununuzi wa Mwaka

Na.	Jina la Taasisi	Ununuzi	Kiasi (Sh.)
1.	Idara ya Jeshi la Magereza	Ununuzi wa sare	338,786,159.32
2.	Wizara ya Nishati	Ununuzi wa Magari	581,150,667.17
3.	Chuo cha Taifa cha Utalii	Ununuzi wa Magari	461,407,308.66
4.	Mamlaka ya Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Mafinga	Usambazaji wa mita za maji za ndani zilizolipiwa kabla na baada ya kulipwa na Usambazaji wa mabomba ya maji	430,276,375.00
5.	Mamlaka ya Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Uwanda wa Makonde (MPWSSA)	Ukarabati wa pampu za maji.	280,518,300.00
6.	Bodi ya Maji Ziwa Tanganyika (LTBWB)	Ujenzi wa mradi wa maji	79,296,481.38

Na.	Jina la Taasisi	Ununuzi	Kiasi (Sh.)
7.	Bodi ya Maji ya Bonde la Ruvuma Kusini mwa Pwani (RSCBWB)	Ununuzi wa bidhaa na huduma na usimamizi wa mikataba	546,918,432
Jumla			**2,718,353,723.53**

Chanzo: *Taarifa za Ukaguzi za mwaka wa fedha 2021/22*


Napendekeza, Menejimenti ya Taasisi za Serikali kuandaa makadirio halisi ya bajeti ambayo hutumika kwa ajili ya maandalizi ya mipango ya manunuzi ya kila mwaka kwa kuhusisha utafiti wa kina wa soko pamoja na kuweka sera na taratibu za wazi za ununuzi.

9.7 Taasisi 22 Zilishindwa Kutekeleza kwa Ufanisi Mpango wao wa Ununuzi kwa kiasi cha Sh. Trilioni 3.14

Kanuni ya 69 (7) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 inazitaka Taasisi Nunuzi kuandaa mipango ya manunuzi ya mahitaji na kutenga fedha za kutosha kwenye bajeti. Vilevile, kifungu cha 49(1&2) cha Kanuni za Ununuzi za Umma, 2011 kinataka mpango wa manunuzi wa kila mwaka uidhinishwe na Mamlaka Stahiki ya bajeti na Taasisi Nunuzi kufuatilia mipango hiyo ya manunuzi iliyoidhinishwa.

Mapitio ya utekelezaji wa mipango ya manunuzi ya mwaka wa fedha 2021/2022 yalibainisha kuwa taasisi nunuzi 22 zilipanga kununua bidhaa na huduma zenye thamani ya Sh. trilioni 3.52 lakini hadi mwisho wa mwaka Taasisi hizo ziliweza kununua bidhaa na huduma zenye thamani ya Sh. bilioni 380.69 sawa na asilimia 10 ya mpango wa ununuzi usiotekelezwa wenye thamani ya Sh. trilioni 3.14 sawa na asilimia 10 kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 59** na **Kielelezo Na. 10.**

Kielelezo Na. 10: Uwiano wa Utekelezaji wa Mipango ya Manunuzi ya Mwaka ya Taasisi za Serikali



Source: *Ripoti za Ununuzi*

NATIONAL AUDIT OFFICE
NAOT

Jedwali Na. 59: Uchambuzi wa utekelezaji wa Mpango wa Ununuzi wa Mwaka

Na.	Jina la Taasisi	Bajeti iliyopangwa (Sh)	Kiasi halisi (Sh)	Bakaa (Sh)	Asilimia (%)
1	Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA)	10,500,979,629	5,280,158,529	5,220,821,100	50
2	Bodi ya Maji ya Bonde la Pangani	2,658,000,000	2,218,000,000	440,000,000	84
3	Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania	4,293,333,260	3,077,629,260	1,215,704,000	72
4	Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere	7,885,513,968	7,648,343,968	237,170,000	97
5	Wakala wa Barabara Tanzania	2,914,813,070,000	700,000	2,914,113,070,000	0
6	Wakala wa Barabara Tanzania (Ofisi za Mikoa)	135,797,309,665	104,910,980,700	30,886,328,965	77
7	Bodi ya Filamu Tanzania-Fungu-TR.173	424,729,000	140,854,950	283,874,050	33
8	Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania	25,000,000,000	-	25,000,000,000	0
9	Uongozi Institute	1,004,999,000	-	1,004,999,000	0
10	Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara – (Fungu 44)	34,427,696,118	5,854,470,244	28,573,225,874	17
11	Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara – (Fungu 44)	56,357,006,578	20,443,981,235	35,913,025,343	36
12	Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo - Fungu 96	185,226,159,495	170,241,159,475	14,985,000,020	92
13	Wakala wa Uzito na Vipimo (WMA)	2,930,578,134	1,630,369,234	1,300,208,900	56
14	Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi	57,051,867,667	37,632,170,091	19,419,697,576	65
15	Taasisi ya Mafunzo ya Misitu	952,184,550	1,643,511,550	691,327,000	173
16	Chuo cha Taifa cha Utalii	5,044,942,180	2,499,169,373	2,545,772,806	50
17	Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA)	22,893,727,457	5,621,630,393	17,272,097,064	25
18	Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo- Fungu -TR 77	639,158,000	408,488,581	230,669,419	64
19	Kampuni ya Huduma za Majini	10,506,373,023	-	10,506,373,023	0
20	Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA)	10,500,979,629	5,280,158,529	5,220,821,100	50
21	Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara – (Fungu 44)	34,427,696,118	5,854,470,244	28,573,225,874	17
22	Mfuko wa Dhamana ya Kilimo (AGITF)	601,901,308	299,624,677	302,276,631	50
Jumla		**3,523,938,204,779**	**380,685,871,033**	**3,142,553,033,745**	

Kwa kuzingatia hayo, nina maoni kwamba, ucheleweshwaji wa shughuli za ununuzi kumepelekea ucheleweshwaji wa huduma pamoja na kutofikiwa kwa malengo ya Taasisi.

Ninapendekeza kwamba Taasisi za Serikali ziandae mpango halisi wa ununuzi na kuhakikisha unatekelezwa kwa ufanisi kwa mwaka mzima. Hii itahakikisha kuwa shughuli za ununuzi zinaendana na malengo ya Taasisi, na kwamba muda na rasilimali za kutosha zinatengwa kwa kila shughuli ya ununuzi. Kwa kufuata mchakato wa ununuzi uliopangwa vizuri, Taasisi zinaweza kuongeza uwazi na uwajibikaji, kukuza ushindani, na kuhakikisha kuwa bidhaa na huduma zinatolewa kwa wakati na kwa gharama nafuu.

9.8 Ununuzi wa Vifaa na Huduma bila kuidhinishwa na Bodi ya Zabuni Kiasi cha Sh. bilioni 13.27

Kwa mujibu wa kifungu cha 31 (1) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma, 2011 isipokuwa kama imeelezwa vinginevyo katika Sheria au kanuni hizi, kila Taasisi ya Umma inatakiwa kuwa na Bodi ya Zabuni ya Ununuzi wa bidhaa, huduma na uondoaji wa mali za Umma kwa njia zabuni. Aidha, kifungu cha 33 cha Sheria hiyo hiyo kinatoa majukumu kwa Bodi ya Zabuni ikiwa ni pamoja na kuidhinisha manunuzi yote na uondoaji wa mali kwa utaratibu za zabuni.

Katika mwaka wa fedha 2021/22 taasisi 12 zilinunua bidhaa na huduma kiasi cha Sh. bilioni 13.27 bila kupata kibali kutoka Bodi ya Zabuni, kinyume na kifungu cha 33 cha Sheria ya Ununuzi wa Umma, 2011. Hii imeoneshwa katika **Jedwali Na. 60** hapo chini:

Jedwali Na. 60: Orodha ya Taasisi vilizonunua bidhaa na huduma bila idhini ya Bodi ya Zabuni

Na.	Jina la Taasisi	Thamani ya Ununuzi (Sh.)
1.	Mamlaka ya Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira ya Kishapu	26,567,000
2.	Mamlaka ya Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Maganzo	12,910,814
3.	Mamlaka ya Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Makonde Plateau (MPWSSA)	280,518,300

Na.	Jina la Taasisi	Thamani ya Ununuzi (Sh.)
4.	Mamlaka ya Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Mwanhuzi	184,218,518
5.	Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Fungu 62)	14,123,500
6.	Mamlaka ya Udhibiti na Utekelezaji wa Dawa za Kulevya (Fungu 91)	34,641,140
7.	Wizara ya Mifugo na Uvuvi- (Sekta ya Uvuvi)-Fungu 64	67,200,000
8.	Wizara ya Afya	38,864,874
9.	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Tumbi	317,646,273
10.	Shirika la Magereza Pekee	11,892,423,009
11.	Kitengo cha Udhibiti Fedha Haramu	277,410,000
12.	Mradi wa Mashine za Kilimo Suma JKT	126,068,100
Jumla		**13,272,591,528**

Chanzo: *Taarifa za Ukaguzi za Wizara, Wakala na Vitengo kwa Mwaka wa Fedha 2021/22)*

Nina maoni kwamba kufanya manunuzi bila kupata idhini ya Bodi ya Zabuni ni ukiukwaji wa kifungu cha 33(1) (d) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma, 2011 (kama ilivyorekebishwa mwaka 2016), jambo ambalo linaweza kusababisha ununuzi wa bidhaa zisizo na ubora na kwa bei ya juu pamoja na Bodi ya Zabuni kushindwa kusimamia ununuzi.

Napendekeza Menejimenti za Wizara, Wakala na Taasisi nyingine kuhakikisha kuwa Bodi za Zabuni zinaidhinisha ununuzi na uondoaji wa vifaa kabla ya kutekelezwa kwa shughuli za ununuzi.

9.9 Kuchelewa kupokea Vifaa na Huduma zilizonunuliwa Kiasi cha Sh. bilioni 18.75

Kanuni ya 242 (2) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma ya mwaka 2013 inaeleza kuwa pale ambapo upokeaji wa bidhaa unachelewa au kuna uwezekano wa kucheleweshwa zaidi ya muda uliowekwa katika mkataba, Taasisi Nunuzi itatafuta taarifa na maelezo kutoka kwa wauzaji au mawakala wao inaweza kutoza gharama ya ucheleweshaji kulingana na matakwa ya mkataba.

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa utoaji wa bidhaa na huduma zenye thamani ya Sh. bilioni 18.75 kwa Taasisi zipatazo 16 ulicheleweshwa zaidi ya muda uliokubaliwa kwa kipindi cha kuanzia wiki 5 hadi miezi 27. Ucheleweshwaji ulisababishwa hasa na usimamizi usioridhisha wa mchakato wa ununuzi, pamoja na mawasiliano duni baina ya Taasisi Nunuzi na wauzaji. Pia nilibaini kuwa baadhi ya mikataba ya manunuzi haikuwa na vipengele vya kufuatilia na kusimamia ratiba ya utoaji huduma. Maelezo zaidi yameonekana katika **Kiambatisho Na. XVIII.**

Ni maoni yangu kwamba kuchelewa kwa utoaji wa bidhaa na huduma kunaweza kusababisha gharama za ziada kwa taasisi nunuzi, pamoja na kuvuruga shughuli za ununuzi na hivyo kupelekea uwezekano wa upotevu wa mapato.

Napendekeza taasisi husika ziboreshe ufuatiliaji na usimamizi wa mikataba ya ununuzi na zijumuishe katika mikataba kipengele cha ratiba za utoaji na athari za matokeo ya ucheleweshaji wa kuleta bidhaa/kutoa huduma.

9.10 Kuchelewa kukamilika kwa miradi ya ujenzi yenye thamani ya Sh. Bilioni 197.36 katika Taasisi za Serikali.

Kanuni ya 242 (2) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma ya mwaka 2013 inaeleza kuwa pale ambapo upokeaji wa bidhaa unachelewa au kuna uwezekano wa kucheleweshwa zaidi ya muda uliowekwa katika mkataba, Taasisi Nunuzi itatafuta taarifa na maelezo kutoka kwa wauzaji au mawakala wao inaweza kutoza gharama ya ucheleweshaji kulingana na matakwa ya mkataba.

Katika mapitio yangu ya taarifa za utekelezaji wa miradi pamoja na kufanya ziara katika miradi mbalimbali katika vipindi tofauti, nilibani ucheleweshaji mkubwa wa kukamilika kwa miradi 26 yenye thamani ya na Sh. bilioni 197.36 inayotekelezwa na Taasisi mbalimbali za Serikali nchini kwa kipindi cha kuanzia mwezi 1 hadi miezi 96. Miradi iliyocheleweshwa imefafanuliwa kwa kina katika **Kiambatisho Na. XIX** cha ripoti hii. Taasisi zilizochelewesha zaidi miradi ni pamoja na Wakala wa Ujenzi Tanzania (miezi 96), Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (miezi 84) na Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru (miezi 18)
Pia nilibaini kuwa ucheleweshaji mradi umekuwa ukichangiwa na sababu mbalimbali ikiwemo ukosefu wa fedha za miradi ambapo wakandarasi

wamekuwa wakilipwa sehemu ya malipo na sababu nyingine mahususi za kitaasisi. Hata hivyo, hakuna hatua zozote zilizochukuliwa na menejimenti kuhusu namna ya kukabiliana na changamoto hii.

Kwa maoni yangu, kuchelewa kukamilika kwa miradi kunaweza kuwa na athari mbaya kwa mipango ya Serikali na inaweza kusababisha gharama kubwa kuwa zaidi ya makadirio ya awali, kwani bei za vifaa zinaweza kuongezeka. Pia, ucheleweshaji huo unaweza kusababisha miundombinu iliyopo kuchakaa zaidi kabla ya miradi kukamilika na kutumika.

Naishauri Serikali kuboresha usimamizi wa miradi kwa kusimamia wakandarasi kwa karibu wa wakandarasi ili kuhakikisha kuwa miradi inakamilika ndani ya muda uliokubaliwa. Pia, napendekeza fedha za kutosha zitengwe ili kukamilisha miradi iliyocheleweshwa, ili kupata thamani ya fedha na kuzuia miradi isitumike.

9.11 Michakato ya Ununuzi Iliyofanywa Nje ya Mfumo wa Ununuzi kwa njia ya mtandao (TANePs) Sh. Bilioni 46.15

Kanuni ya 342 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013, kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2016, inazitaka Taasisi Nunuzi kutekeleza ununuzi kwa njia ya kielektroniki katika mfumo wa Ununuzi wa Umma. Aidha, Mwongozo Na.4 wa mwaka 2019 iliyotolewa na Wizara ya Fedha na Mipango inazitaka taasisi nunuzi kutumia mfumo wa TANePS katika ununuzi wa bidhaa na huduma kuanzia tarehe 1 Januari 2020. Kwa hiyo, Serikali ya Tanzania hivi karibuni ilipitisha na kwa sasa inatumia Mfumo wa Taifa wa Ununuzi kwa njia ya mtandao (TANePs) ulioanza kutumika tangu mwaka wa fedha 2020/21 kwa mujibu wa Taarifa ya Umma ya Mamlaka ya Udhibiti Ununuzi wa Umma (PPRA).

Katika mwaka ulioishia 30 Juni 2022, taasisi 36 zilinunua bidhaa na huduma zenye thamani ya Sh. Bilioni 46.15 bila kutumia mfumo wa Ununuzi kwa njia ya mtandao (TANePS) kinyume na kanuni iliyotajwa hapo juu. Maelezo zaidi yameoneshwa katika **Kiambatisho Na. XX** cha ripoti hii.

Taasisi kushindwa kutumia mfumo wa Ununuzi kwa njia ya mtandao (TANePs) katika manunuzi, kunaweza kusababisha kutofikiwa malengo ya Serikali katika kuongeza ufanisi na kupunguza muda wa ununuzi, kupunguza hatari, na kuboresha uwazi na haki katika ununuzi wa umma kupitia mfumo

wa kielekitroniki yanaweza yasifikiwe. Pia kutofuata kanuni ya 342 ya Sheria ya Kanuni za Ununuzi wa Umma (Pamoja na Marekebisho ya mwaka 2016) na Mwongozo 4 wa mwaka 2019 uliotolewa na Wizara ya Fedha na Mipango.

Napendekeza Wizara, Wakala na Vitengo kuongeza matumizi ya Mfumo wa Ununuzi kwa njia mitandao katika ununuzi kulingana na matakwa ya Kanuni ya 342 (1) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 kama ilivyorekebishwa na Kanuni ya 6 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2016 na Mwongozo Na 4 wa mwaka 2019 uliotolewa na Wizara ya Fedha na Mipango.

9.12 Ununuzi Uliofanywa bila Ushindani Kiasi cha Sh. Bilioni 1.23

Kanuni ya 163 (1) ya kanuni za Ununuzi wa Umma ya mwaka 2013 inaitaka bodi ya zabuni kuidhinisha na kukaribisha ushindani kupitia maombi ya nukuu za bei (quotations) katika ngazi ya kimataifa au kitaifa endapo bidhaa zitakazonunuliwa zitakuwa na utofauti mkubwa kiasi kwamba haitakuwa na maslahi ya kibiashara kwa muuzaji yeyote mmoja kutoa zabuni kwao; au bidhaa zinapatikana kwa urahisi nje ya rafu au bidhaa za vipimo vya kawaida.

Nilibaini kuwa Taasisi 10 za Serikali zikiwemo Wizara tatu, Mamlaka ya Maji moja, Taasisi nyingine tatu, na Mfuko mmoja, zilinunua bidhaa na huduma zenye thamani ya Sh. bilioni 1.23 kutoka kwa wazabuni na watoa huduma bila kutumia ununuzi wa Ushindani. Katika Ukaguzi huu nilibaini kupungua kwa manunuzi hayo ikilinganisha na mwaka wa fedha uliopita ambapo taasisi 21 zilihusika kununua bidhaa na huduma zenye thamani ya Sh. bilioni 3.57. Maelezo ya taasisi zinazohusika yanapatikana katika **Jedwali Na. 61** cha ripoti.

Jedwali Na. 61: Orodha ya Taasisi ambazo zilifanya manunuzi ya bidhaa na huduma pasipo ushindani

Na.	Jina la Taasisi	Kiasi (Sh.)
1.	Bodi ya Maji ya Bonde la Wami-Ruvu (WRBWB)	21,764,964
2.	Mamlaka ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya (Fungu 91)	93,971,508
3.	Wizara ya Afya	124,348,700
4.	Mamlaka ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA)	23,187,000
5.	Taasisi ya Mafunzo ya Viwanda vya Misitu	16,329,974
6.	Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru	671,975,434

Na.	Jina la Taasisi	Kiasi (Sh.)
7.	Chuo cha Mafunzo ya Viwanda vya Misitu	16,329,974
8.	SUMA JKT -Kilimo	124,120,000
9.	SUMA JKT - Upishi	102,424,498
10.	Mfuko wa Ukaguzi na Usimamizi wa Ushirika (ISCF)	32,460,000
	Jumla	**1,226,912,052**

Chanzo: *Taarifa za Ukaguzi za Wizara, Wakala na Vitengo kwa Mwaka wa Fedha 2021/21*

Nina maoni kwamba ukiukwaji wa Sheria na Kanuni za manunuzi unaweza kusababisha matumizi mabaya ya fedha za Umma. Utaratibu huu unazinyima Taasisi hizo kupata bei nzuri.

Ninapendekeza menejimenti za Wizara, Wakala na Vitengo wakati wa kufanya ununuzi: (a) kutafuta nukuu za ushindani wa bei kwa wazabuni walioidhinishwa kabla ya malipo kufanyika kuathiriwa (b) kuzingatia Sheria na Kanuni za ununuzi ili kupata thamani ya fedha iliyokusudiwa.

9.13 Bidhaa zenye thamani ya Sh. Bilioni 3.03 Zilizopokelewa na Kutumika Bila Hati za Kamati ya Ukaguzi na Mapokezi

Kanuni ya 244 (1) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma, 2013 inataka Bidhaa zitakazo nunuliwa zitakaguliwa, kupimwa na taasisi nunuzi na hazitakubaliwa kama ziko chini ya viwango vilivyoainishwa katika mkataba. Ukaguzi wangu ulibaini kuwa bidhaa zenye thamani ya Sh. bilioni 3.03 zilinunuliwa na kupokelewa na Wizara, Wakala na Vitengo zipatazo 17 na kuanza kutumika bila kuwa na hati kutoka Kamati ya Ukaguzi na mapokezi ya bidhaa. Maelezo zaidi yametolewa katika **Kiambatisho Na. XXI** cha ripoti hii.

Nina maoni kwamba kupokea bidhaa bila kukaguliwa kunaweza kusababisha kupokelewa kwa bidhaa zisizofaa kwa matumizi yaliyokusudiwa pia bidhaa/huduma hizo kutokidhi vigezo au ubora unaohitajika.

Nashauri Wizara, Wakala na Vitengo zihakikishe kwamba bidhaa zinakaguliwa na kukubalika kabla ya kuanza kutumika ili kuhakikisha kwamba zinakidhi viwango na ubora unaotakiwa na zinafaa kwa matumizi. Hii inapunguza hatari ya upotevu, uharibifu, na hatari za kiusalama kama inavyotakiwa na Kanuni ya 244 (1) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma, 2013.

9.14 TEMESA ilifanya Manunuzi yenye thamani ndogo ndogo zaidi ya Ukomo Ulioidhinishwa Kiasi cha Sh. Bilioni 7.35.

Kanuni ya 66(2) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma, 2013 inaeleza kuwa "Bila kujali kanuni ndogo ya (1), pale ambapo kuna umuhimu wa ununuzi, na bila kukusudia haukujumuishwa katika mpango wa manunuzi wa mwaka lakini uko ndani ya mamlaka ya Afisa Masuuli na upo ndani ya bajeti ya Taasisi Nunuzi, thamani ya ununuzi huo haitazidi ukomo wa manunuzi madogo madogo ulioainishwa katika jedwali la Sita na Kumi kwenye Kanuni hizi".

Baada ya kupitia taarifa ya manunuzi madogo madogo kila mwezi zilizowasilishwa Bodi ya Zabuni ya TEMESA Dodoma pamoja na ya kituo cha Kivuko cha Kigongo-Busisi, ilibainika kuwa katika mwaka wa fedha 2021/22, vituo hivi vilikuwa vimefanya manunuzi madogo madogo zaidi ya kiwango kilichoidhinishwa cha Sh. milioni 300 kama ilivyoainishwa katika jedwali la sita. Jumla ya manunuzi madogo madogo yaliyofanywa zaidi ya kikomo hiki yalikuwa Sh. Bilioni 7.35, ambapo TEMESA Dodoma ilifanya manunuzi ya Sh. Bilioni 4.57, na Kituo cha Kivuko cha Kigongo-Busisi ilifanya manunuzi ya Sh. bilioni 2.78.

Kwa kuzingatia udhaifi huo, nina maoni kuwa, kulikuwa na ukiukwaji wa Kanuni ya 66(2) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma, 2013 na inaweza kusababisha kukosekana kwa uwazi na uwajibikaji, kupungua kwa ushindani na uwezekano wa kununua bidhaa na huduma zisizo na ubora.

TEMESA inashauriwa kuhakikisha manunuzi yote madogo madogo yaliyofanywa katika kipindi cha mwaka yanakuwa ndani ya ukomo unaoruhusiwa kwa mujibu wa jedwali la sita na saba la Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 na hatua stahiki zichukuliwe ili kuzuia ukiukwaji siku za baadaye na kuhakikisha uzingatiaji wa kanuni za manunuzi.

9.15 Manunuzi kwa kutumia Chanzo Kimoja pamoja na Njia ya manunuzi ya Umma bila Uhalali Sh. Bilioni 6.01

Kwa mujibu wa Kanuni ya 159 (1) ya Kanuni ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2013 kama ilivyorekebishwa na Kanuni ya 60 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma 2016, kwa mujibu wa idhini ya Bodi ya Zabuni, Taasisi Nunuzi inaweza kununua kwa kutumia chanzo kimoja kwa mujibu wa kanuni ndogo ya 3 chini

ya mazingira yaliyoainishwa ikiwa ni pamoja na yafuatayo: kuna uhitaji wa haraka wa bidhaa au huduma; bidhaa au huduma zinapatikana tu kutoka kwa mzabuni pekee ambaye ana haki za kipekee kuhusiana na bidhaa au huduma; ununuzi unaohusisha Majeshi ya Ulinzi au Usalama wa Taifa; ulikuwa mradi unaoendelea, au uhitaji wa vitu vya ziada kwa ajili ya kukamilisha utekelezaji wa mradi.

Aidha Kanuni ya 152 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma, 2013 inahitaji Taasisi Nunuzi kuzuia matumizi ya zabuni maalum ikiwa kuna ulazima wa bidhaa, ujenzi au huduma na kama hakutakuwa na muda wa kutosha kwa Taasisi Nunuzi kushiriki katika kufungua zabuni za kitaifa na kimataifa na kulikuwa na mazingira yaliyopelekea kushindwa kutabiri umuhimu huo mapema katika Taasisi Nunuzi.

Katika ukaguzi wangu wa usimamizi wa manunuzi, nilibaini kuwa Taasisi za Serikali zipatazo saba zilitumia njia ya ununuzi kwa mzabuni mmoja na kuzuia ununuzi maalumu kwa bidhaa na huduma zilizonunuliwa zenye thamani ya Sh. bilioni 6.01 bila uhalali wa kimaandishi kulingana na matakwa ya Kanuni ya 159 (3) na 152 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma, 2013. Maelezo yapo katika **Jedwali Na. 62** la ripoti hii.

Jedwali Na. 62: Orodha ya Taasisi ambazo zilifanya manunuzi kwa kutumia njia ya chanzo kimoja

Na.	Jina la Taasisi	Mkataba Na.	Maelezo ya ununuzi	Kiasi (Sh.)
1.	Jeshi la Magereza	ME 014/2021/2022/PR/G/10	Ununuzi wa sare	338,786,159.32
2.	Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA)	NFRA/2021/2022/HQ/LPO/13	Ugavi wa nyaraka za uwajibikaji	57,536,160.00
3.	Wakala wa Majengo Tanzania (TBA)	AE/012/2021-22/HQ/G/20 LOT II	Usambazaji wa Saruji kwa ajili ya ujenzi wa nyumba 150 za watumishi wa umma Dodoma	1,785,950,000.00
4.	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Tumbi	Kim Yung Engineering Company Ltd	Ukarabati wa kitengo cha kusafisha damu	410,978,455.40

Na.	Jina la Taasisi	Mkataba Na.	Maelezo ya ununuzi	Kiasi (Sh.)
5.	Bodi ya Maji ya Bonde la Ziwa Tanganyika (LTBWB)	Nguvu Kazi	Ununuzi wa vifaa vya MUSE	40,285,000.00
6.	Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (Fungu 24)	IE/TCDC/HQ /2021-2022/G/05/01	Utoaji wa usambazaji wa pikipiki mia moja thelathini na saba	397,300,000.00
7.	Mfuko wa Dhamana ya Kilimo (AGITF)	AE/062/2021 /2022/HQ/N /9	Utoaji wa huduma ya uchapishaji	5,590,722.00
8.	Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi (MOHA)	014/2019/2020/FRF/G/11	Usambazaji wa magari matatu ya injini ya zimamoto	2,977,500,000
	Jumla			**6,013,926,496.72**

Chanzo: *Taarifa za Ukaguzi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022*

Ninaamini kuwa matumizi ya njia ya ununuzi wa chanzo kimoja bila maelezo ya kuhalalisha njia ya ununuzi yanaweza kupunguza ushindani na kushindwa kupata bidhaa zenye ubora wa hali ya juu kwa bei ya chini na inaweza kusababisha udanganyifu na mfumuko wa bei za bidhaa na huduma, jambo ambalo linadhoofisha usimamizi mzuri wa rasilimali.

Napendekeza kuwa Wizara, Wakala na Vitengo na vizingatie kikamilifu Sheria za Manunuzi kwa kuangalia uhalali sahihi wakati wa kutumia ununuzi wa chanzo kimoja ili kuongeza ushindani kwenye manunuzi.

9.16 Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) ilitoa mikataba zaidi ya kiwango cha bajeti yake kiasi cha Sh. Milioni 661.51

Kanuni ya 16 (2) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 inataka Taasisi Nunuzi kutoingia katika zabuni inayozidi bajeti zilizopo iliyopo.

Hata hivyo, mapitio yangu ya mpango wa manunuzi na mikataba katika mwaka wa fedha 2021/22, nilibaini kuwa TANROADS ilitoa mikataba mitatu ambayo inazidi bajeti iliyoidhinishwa kwa kiwango cha Sh. Milioni 661.51 kinyume na Kanuni iliyotajwa. Maelezo yako katika **Jedwali Na. 63**:

Jedwali Na. 63: Mikataba Iliyotolewa Zaidi ya Bajeti

Mkataba Na.	Maelezo	Jumla ya Mkataba (Sh.)	Bajeti (Sh.)	Kiwango zaidi Bajeti (Sh.)
TRD/HQ /1037/2021/22	Mkataba wa huduma za ushauri wa utafiti wa kiuchumi, tathmini ya athari za mazingira na kijamii, muundo wa kina wa uhandisi na uandaaji wa nyaraka za zabuni za ukarabati wa barabara ya Singida - Shelui (km 110)	1,223,307,500	700,000,000	523,307,500
TRD/HQ /1039/2021/22	Mkataba wa utoaji wa leseni ya 'sophos' ya ulinzi wa mifumo (full guard plus firewall)	155,287,165	26,000,000	129,287,165
TRD/HQ /1056/2021/22	Mkataba wa usambazaji wa vifaa vya michezo kwa Siku ya Mei 2022	19,670,000	10,750,000	8,920,000
Jumla		**1,398,264,665**	**736,750,000**	**661,514,665**

Chanzo: *Mpango wa Unuunuzi wa Mwaka na Rejista ya Mikataba*

Ni maoni yangu kuwa, utoaji wa zabuni zinazozidi bajeti unaathiri utekelezaji wa shughuli nyingine zilizopangwa.

Ninapendekeza mchakato wa manunuzi wa Wakala wa barabara ufuatiliwe kwa karibu ili kuhakikisha kuwa zabuni zinatolewa kulingana na bajeti iliyotengwa. Hii inawezekana kwa kuandaa mipango mizuri na na usimamizi mzuri wa mchakato wa ununuzi.

9.17 Miradi iliyotekelezwa ikiwa na Dhamana ya Benki iliyoisha muda wake Sh. Bilioni 151.03

Kifungu cha 60 cha masharti ya jumla ya mkataba kinataka mwajiri atoe uhakika wa mtekelezaji wa mradi kwa tarehe iliyowekwa katika barua ya kukubaliwa na iliyotolewa, kwa kiasi na fomu inayokubalika kwa benki au uhakika unaokubalika kwa mwajiri. Usalama huo utakuwa halali hadi tarehe 28 tangu tarehe ya kutolewa kwa hati ya cha kukamilika kazi kwa dhamana ya Benki na mwaka mmoja tangu tarehe ya hati ya ukamilishaji wa kazi katika utekelezaji mradi.

Baada ya kufanya mapitio ya nyaraka za mkataba katika taasisi mbalimbali za Umma, nimebaini kuwa miradi ipatayo 32 yenye thamani ya Sh. bilioni 151.03 imefanyika pasipokuwa na dhamana ya benki katika utekelezaji miradi au iliyoisha muda wake (performance bank guarantee) hadi wakati wa ukaguzi mwezi Novemba 2022. **Jedwali Na. 64** linaonesha maelezo kamili.

Jedwali Na. 64: Orodha ya Taasisi ambazo miradi ilitekelezwa kwa Dhamana ya Benki ya Utendaji iliyoisha muda wake

Na.	Jina la Taasisi	Idadi ya Miradi	Kiasi (Sh.)
1.	Wakala wa Barabara Tanzania	26	140,795,058,609.41
2.	Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania	1	47,178,144.30
3.	Mamlaka Kuu ya Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Handeni	1	1,113,964,181.00
4.	Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA)	3	982,435,165.10
5.	Wizara ya Afya	1	8,089,141,900.00
Jumla		**32**	**151,027,777,999.81**

Chanzo: *Taarifa za ukaguzi za mwaka wa fedha 2021/2022*

Kwa kuzingatia hayo, nina maoni kwamba hali hii inaweza kusababisha hasara ya fedha za Umma endapo wakandarasi watashindwa kutekeleza miradi.

Napendekeza Taasisi zihakikishe kuwa dhamana za benki katika utekelezaji wa mikataba zinahuishwa mara tu baada ya kumalizika kwa muda wake ili kuwa na uhakika wa utekelezaji mradi kwa muda wa mkataba uliobaki.

9.18 Taasisi zilizotekeleza Miradi Kabla ya Kupata Hati ya Tathmini ya Athari za Mazingira na Kijamii kutoka Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC) - Sh. Bilioni 547.02

Sehemu ya 81 (3) ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 inaeleza kuwa, kibali au leseni ya utekelezaji wa mradi wowote au kufanya kwa mujibu wa sheria yoyote iliyoandikwa haitampa haki mtetezi au masanifu wa programu kufanya au kusababisha kufanyika kwa mradi au shughuli bila cheti cha tathmini ya athari za mazingira kilichotolewa chini ya Sheria hii. Aidha, Kifungu cha 81 (4) kinasema kwamba, mtu yeyote anayekiuka kifungu kidogo cha (3), anatenda kosa.

Kinyume na mamlaka iliyotajwa hapo juu, ilibainika kuwa, Taasisi zilitekeleza miradi katika mwaka wa fedha 2021/22 kabla ya kupata Hati ya Tathmini ya Athari za Mazingira kutoka NEMC. Pia, hadi wakati wa ukaguzi mwezi Novemba 2022, Wakala wa Taifa wa Barabara ilikuwa bado haijapata huduma hiyo kwa miradi hiyo kutoka NEMC. Rejea **Kiambatisho Na.** XXII.

Nina maoni kwamba Taasisi husika zinaweza kutakiwa kulipa faini kutokana na kutenda kosa kwa mujibu wa kifungu cha 81 (4) cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004. Pia, mabadiliko ambayo yangeweza kufanyika kabla ya kuanza kwa mradi yanaweza kuwa yamepuuzwa na kupelekea ucheleweshaji wa ripoti ya usanifu.

Napendekeza menejimenti za Taasisi husika zizingatie Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 kwa kuhakikisha kuwa Tathmini ya Athari kwa Mazingira inafanyika kabla ya kuanza utekelezaji wa miradi.

9.19 Miradi Iliyotekelezwa bila Bima ya Mradi wenye thamani ya Sh. bilioni 4.27.

Kifungu cha 17.1 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba kati ya Wakala Taifa wa Barabara (TANROADS) na Wakandarasi kinamtaka mkandarasi, kwa pamoja yaani mwajiri na mkandarasi, kutoa bima kuanzia tarehe ya mwanzo hadi mwisho wa kipindi cha matazamio, kwa kiasi na makato yaliyotajwa katika Masharti maalum ya Mkataba. Hii ni kwa matukio ambayo yanatokana na hatari ya mkandarasi. Sera na vyeti vya bima vinatakiwa kukabidhiwa na mkandarasi kwa meneja wa mradi kwa ajili ya kuidhinishwa kabla ya tarehe ya kuanza. Aidha, kifungu cha 17.3 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba kinataka endapo mkandarasi hatatoa sera na vyeti vyovyote vinavyotakiwa, mwajiri anaweza kukata bima iliyotakiwa na mkandarasi na kurejesha malipo ambayo mwajiri amelipa au kama hakuna malipo yanayostahili, malipo yatakuwa kwenye madeni ya mkandarasi.

Ukaguzi wa majalada ya Mkataba, mihtasari ya vikao eneo la mradi, nilibaini kuwa wakandarasi walikuwa wakitekeleza miradi inayofikia thamani ya Sh. Bilioni 4.27 bila kuwa na bima kinyume na kifungu cha 17.1 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba. Maelezo ya miradi hiyo yameoneshwa katika **Jedwali Na. 65**.

Jedwali Na. 65: Orodha ya Taasisi zilizotekeleza Mikataba pasipokuwa na Bima

Na	Taasisi	Namba ya Mkataba	Maelezo ya Mkataba	Thamani ya mkataba (Sh.)
1.	TANROADS	AE/001/2021-22/KG/W/24	Ujenzi katika mto wa Malagarasi - Buhigwe - Kitanga - Kumsenga	99,541,150.00
		TRD/SG/W/2021-2022/32	Loti No. 1: Kazi za matengenezo ya Mara kwa mara; Lot No. 2: Kazi za kawaida na matengenezo ya mara kwa mara; Lot No. 3: Ujenzi wa daraja); na Loti Na 4: matengenezo ya kuimarisha daraja la Kinyamshindo - Kititimo barabara ya Mkoa isiyopitika (R 463).	221,231,800.00

Na	Taasisi	Namba ya Mkataba	Maelezo ya Mkataba	Thamani ya mkataba (Sh.)
		TANROADSS/RK/2021-22/W/01	Matengenezo ya maalum ya kawaida, kuboresha sehemu korofi, Barabara ya Matai-Kasesya.	462,030,300.00
		TANROADSS/RK/2021-22/W/09	Kazi ya Matengenezo ya Mara kwa Mara na Uboreshaji wa barabara Kizitwe – Mkima.	418,658,100.00
		TRD/RM/MBY/2021-22/W/21	Ukarabati wa barabara ya Ilongo –Usangu Narco (Km 24+000 hadi Km 28+500 hadi km 32+900 na Igulusi Utengule –Luhanga	382,001,800.00
		TRD/RM/MBY/2021-22/W/16	Ukarabati mkubwa wa daraja kando ya barabara ya Mbalizi-Shigamba.	314,925,600.00
		AE/001/2021-22/IR/W/27	Kazi ya Matengenezo ya kilomita 42.62 na ukarabati wa viwango vya changarawe barabara za Mkoa Ihawaga- Kasanga-Igowole (km 3.0)	190,000,000.00
2.	Wizara ya Afya	ME/007/2021-22/HQ/W/12	Ujenzi wa Kituo cha Afya	2,184,592,221.17
Jumla				**4,272,980,971.17**

Chanzo: *Rejista ya MIkataba ya Taasisi husika*

Kwa maoni yangu, kukosekana kwa bima kunaweza kupelekea Taasisi mbalimbali kuingia hatarini endapo kutatokea hasara au uharibifu wakati wa ujenzi.

Ninapendekeza menejimenti za Taasisi husika kuhakikisha miradi inakuwa na bima ili kuepuka ucheleweshaji wa utekelezaji wa miradi na upotevu wa rasilimali za umma.

9.20 Kushindwa kwa Mkandarasi Kuleta na Kufunga Taa za Barabarani za Mitaani zenye thamani ya Sh. Milioni 67.5 Kulingana na Masharti ya Mkataba

Tarehe 30 Juni 2022, TANROADS ilitoa hati ya kukamilika kwa mradi kupitia barua yenye kumbukumbu namba AE/299/373/01A/ ikionesha kuwa mradi huo ulikamilika kikamilifu na kuainisha kazi ndogo mbili ikiwemo kazi za kuweka alama za barabarani ambazo zilikubaliwa kukamilika ndani ya kipindi cha matazamio kuanzia tarehe 02 Juni 2022 hadi tarehe 02 Juni 2023.

Hata hivyo, tarehe 21 Septemba 2022, nilitembelea mradi na nilibaini kuwa baadhi ya kazi za mkataba yaani, usambazaji na ufungaji wa taa zinazotumia mwanga wa jua za barabarani kama zinavyoonekana kwenye Jedwali zilikuwa hazijakamilika na hazikuwa katika orodha ya kazi zilizotakiwa kukamilishwa kipindi cha muda wa matazamio licha ya mkandarasi kulipwa kiasi cha Sh. milioni 67.5 kwa ajili ya kazi hiyo.

Jedwali Na. 66: Orodha ya Kazi ambazo hazikukamilika (Taa za barabarani)

Na.	Mgawanyo	Orodha ya Kazi ambazo hazikutekelezwa hadi wakati wa ukaguzi 21 Septemba 2022.	Kiasi (Sh.)
1.	Sehemu ya I	Uwekaji wa taa za barabarani ikiwa ni pamoja na usimikaji wa nguzo za chuma betri za nishati ya jua, aina ya 120W, betri ya sanduku la kudhibiti N120Ah 14 Nos kwa Sh. 3,750,000.	52,500,000
2.	Sehemu ya II	Uwekaji wa taa za barabarani ikiwa ni pamoja na usimikaji wa nguzo za chuma betri za nishati ya jua, aina ya 120W, betri ya sanduku la kudhibiti N120Ah 4 Nos kila moja Sh. 3,750,000.	15,000,000
Jumla			**67,500,000**

Chanzo: *Majalada ya Mikataba*

Ni maoni yangu kwamba, kutoa hati ya kukamilisha kazi bila kukamilisha baadhi ya kazi ni dalili ya kukosa uadilifu katika usimamizi wa mikataba.

Ninashauri TANROADS kuhakikisha hati ya kukamilisha kazi inatolewa pale kazi zote za mkataba zinapokuwa zimetekelezwa kikamilifu.

Mkandarasi ambaye ameshindwa kuleta na kufunga taa za barabarani za mitaani zenye thamani ya Sh. 67.50 milioni aagizwe kukamilisha kazi sawa na vigezo na masharti ya mkataba.

9.21 Mkandarasi alitelekeza Mradi Wenye Thamani ya Sh. Milioni 903. 60 (Ujenzi wa Daraja la Mkombo)

Kampuni ya Tanjo Builders Company Limited iliingia mkataba na Wakala wa wa Barabara Tanzania (TANROADS) – Mkoa wa Rukwa kwa ajili ya ukarabati mkubwa wa Madaraja ya Kikoma, Kipala , daraja la Mkombo na daraja la Ulumi, Kaenges-Mwimbi, Laela - Mwimbi - Kizombe, Kalepula - Mwambenkonswe na Mishindwe Mambwekenya kwa mkataba Na. TANROADS/RK/2021-22/W/19 wenye thamani ya Sh. milioni 903.60 (Iliyofanyiwa marekebisho hadi kufikia Sh. bilioni 1.09) uliotegemewa kutekelezwa kwa muda wa siku 180, kuanzia tarehe 11 Oktoba 2021 hadi 28 Juni 2022 ambayo iliongezwa hadi tarehe 28 Juni 2022.

Hata hivyo, nilibaini kuwa mkandarasi alitelekeza mradi huo kwa kipindi cha kuanzia siku 19 hadi 21 bila TANROADS Rukwa kuchukua hatua zozote dhidi ya mkandarasi kulingana na makubaliano ya mkataba. Nilitembelea mradi huo tarehe 3 Septemba 2022, nilibaini kuwa maendeleo ya kazi yalikuwa chini ya asilimia 40, wakati muda uliopangwa ulikuwa umepitiliza kwa asilimia 167 na mkandarasi alikuwa tayari amelipwa kiasi cha Sh. milioni 109.54. Pia, vifaa pamoja na wafanyakazi hawakuwepo kwenye eneo la mradi wakati nilipotembelea mradi.

Naamini kuwa, kulingana na matakwa ya mkataba endapo mkandarasi atatelekeza mradi kwa zaidi ya siku 28, inachukuliwa kama uvunjaji wa mkataba, na kusitishwa kwa mkataba kunaweza kuiingizia serikali gharama za ziada.

Menejimenti ya Wakala wa barabara inashauriwa kufanya tathmini ya kutosha ya mtiririko wa fedha kabla ya kusaini mikataba ili kuepuka ucheleweshaji wa mradi kutokana na ukosefu wa rasilimali fedha.

9.22 TANROADS Haijalipa Fidia kwa Watu 236 Walioathiriwa na Miradi Sh. Bilioni 3.76

Kanuni ya 13 (1-3) ya Kanuni ya Ardhi (Tathmini ya Thamani ya Ardhi kwa ajili ya Fidia) ya mwaka 2001 inaeleza kuwa "kiasi ambacho kitalipwa kama fidia kiwe cha haki, cha kutosha na kilipwe haraka ndani ya miezi sita kuanzia tarehe ya uthamini, vinginevyo riba kiwango kinachotolewa na benki za biashara kwenye amana za kudumu kitatozwa hadi fidia hizo zitakapolipwa".

Nilibaini kuwa watu 275 wenye madai ya fidia ya jumla Sh. bilioni 4.74 ambao waliidhinishwa na Mthamini Mkuu wa Serikali tarehe 3 Februari 2021 kwa ajili ya malipo kwa mujibu wa Taarifa ya Uthamini wa Mali zilizopo kando ya eneo la mradi wa ujenzi wa Kituo cha Pamoja cha Ukaguzi katika eneo la Idofi, Halmashauri ya Mji wa Makambako. Hata hivyo, kati ya waathirika wa mradi 275, ni waathirika 39 walilipwa jumla ya Sh. milioni 870.18 na kuacha fidia ya Sh. bilioni 3.76 kwa waathirika 236 ikiwa bado haijalipwa hadi wakati wa ukaguzi mnamo mwezi Septemba 2022, ambao ni ucheleweshaji wa malipo kwa muda wa mwaka mmoja na miezi saba tangu taarifa ta tathmini kuidhinishwa.

Nina shaka kuwa kuchelewa kulipa fidia kwa waathirika wa mradi zaidi ya miezi sita kama inavyotakiwa na Kanuni za Ardhi (Tathmini ya Thamani ya Ardhi kwa ajili ya Fidia) za mwaka 2001 zinaweza kusababisha malipo ya ziada yanayotokana na riba za ucheleweshaji malipo.

Ninapendekeza TANROADS kuhakikisha kuwa madai ya fidia ya waathirika waliopisha mradi wapatao 236 yenye jumla ya Sh. bilioni 3.76 yanalipwa kwa wakati ili kuepusha malipo ya riba.

9.23 Kasoro zilizobainika kwenye Mkataba wa Uboreshaji wa Sanzate – Nata Kiwango cha Lami (Km 40) wenye thamani ya Sh. bilioni 22.72

Tarehe 2 Aprili 2020, Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) aliingia mkataba Na.TRD/HQ/1042/2019/20 na Mkandarasi China Railway Seventh Group Co. Ltd kwa ajili ya kuboresha barabara ya Makutano – Nyamuswa - Ikoma Gate kwa kiwango cha lami ya kilometa 135Km: Kipande cha pili cha Sanzate- Nata chenye urefu wa kilomita 40 kwa bilioni Sh.39.47. Mkataba

huu ulipaswa kukamilika tarehe 6 Julai 2022. Hadi wakati wa ukaguzi wangu Desemba 2022, mkandarasi alikuwa ameshalipwa Sh. bilioni 11.64 ikijumuisha malipo ya awali ya Sh. Bilioni 5.74. Aidha, TANROADS Engineering Consulting Unit (TECU) ilipewa jukumu la kuwa mshauri wa mradi kwa kusimamia mkataba wa ujenzi na pamoja na kupitia usanifu wa mradi huo.

Mapitio yangu ya ripoti ya TECU iliyowasilishwa TANROADS tarehe 30 Septemba 2021, yalibainisha kuwa Mshauri alibaini mapungufu kadhaa katika makisio ya gharama za kazi (Bills of Quantities). Ili kukabiliana na mapungufu hayo, mshauri alipendekeza gharama ya ziada ya Sh. bilioni 22.72, ambayo ni ongezeko la asilimia 58 kutoka kiwango cha mkataba wa awali, kama ilivyoainishwa hapa chini:

- Mshauri alibainisha kuwa kipengele Na. 45.01 (a) cha makisio ya gharama za kazi ambacho kinahusu uso wa barabara. Makisio ya awali yalionesha kuwa eneo la barabara ni mita za mraba 46,480 tu, wakati eneo halisi lilikuwa ni mita za mraba 396,245. Hivyo kusababisha upungufu wa mita za mraba 349,765. Ili kukabiliana na upungufu huo, makisio ya gharama za kazi kwa kipengele hicho yaliongezeka kwa Sh. Bilioni 16.53 hivyo kufanya jumla ya gharama kwa kipengele hicho kuwa Sh. Bilioni 19,88 kutoka Sh. Bilioni 3.35 ya makisio ya awali.

- Aidha, mshauri ilibainisha maeneo yaliyokumbwa na mafuriko na kuhitaji kuongezwa kwa mifereji 12 kwenye mifereji 70 iliyokuwepo kwenye muundo wa awali. Mshauri pia alipendekeza kazi za ziada za kudhibiti mmomonyoko mkubwa ambazo hazikujumuishwa katika muundo wa awali. Kazi hizi za ziada zilichangia kuongezeka kwa gharama ya Sh. bilioni 3.01.
- Pia, Mshauri alibainisha kuwa kazi za ziada zilizopendekezwa hapo juu zilikuwa na athari kwenye kazi nyingine za ardhini hivyo kuhitaji ongezeko Sh. Bilioni 1.48. Mshauri pia ilipendekeza kuongeza kiasi kilichotengwa kwa ajili ya kufidia tofauti ya bei kwa Sh. bilioni 1.70 ili kuzingatia tofauti katika wigo wa mradi.

Hata hivyo, katika ukaguzi wangu uliofanyika Desemba 2022, nilibaini kuwa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) ilikuwa bado haijaidhinishwa mapendekezo yaliyowasilishwa na Mshauri licha ya kupita miezi 14 tangu

kuwasilishwa kwa mapendekezo hayo mnamo tarehe 30 Septemba 2021. Hata hivyo, muda wa kukamilisha mkataba uliisha tarehe 06 Julai 2022, na hakuna nyongeza ya muda iliyotolewa licha ya ombi la mkandarasi kuongezewa muda tangu tarehe 21 Aprili 2022.

Kwa mujibu wa menejimenti ya TANROADS ni kwamba, kwa sasa wapo kwenye majadiliano na mkandarasi ili kupunguza bei ya bidhaa kabla ya kufanya maamuzi ya kuidhinisha kibali hicho. Hata hivyo, kasoro hizi kimsingi zilisababishwa na usanifu wa mradi usioridhisha wa makisio ya gharama za kazi kabla ya kutolewa kwa zabuni. Kushindwa kushughulikia kasoro hizi kwa wakati kunaweza kuchelewesha kukamilika kwa mradi na usumbufu kwa watumiaji wa barabara.

Napendekeza TANROADS iimarishe mfumo wake wa udhibiti wa ndani katika uandaaji na uhakiki wa usanifu wa miradi na makisio ya gharama za kazi kabla ya kutolewa kwa Umma kwa madhumuni ya zabuni. Pia, TANROADS inapaswa kuimarisha usimamizi wake wakati wa uandaaji na usanifu wa mradi ili kupunguza gharama za ziada zinazotokana na miundo duni wa mradi.

9.24 Utoaji wa Zabuni zaidi ya moja kwa Mkandarasi ambaye ana Uhaba wa Watumishi Muhimu na Vifaa Sh. Bilioni 6.16

Kanuni ya 224 (9) ya Kanuni ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2013 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2016 inaelekeza taasisi nunuzi kuweka ukomo wa idadi au jumla ya thamani ya tuzo zinazotolewa kwa mzabuni iwapo rasilimali za mzabuni zinaweza kuwa hazitoshi kwa mzabuni kuweza kuwa na kadhia za ziada ambazo zinaweza kutokana na mkataba unaopendekezwa.

Nilipitia Taarifa za Tathmini ya Zabuni pamoja na rejista ya mikataba kwa mwaka 2021/22 na kubaini kuwa TEMESA ilitoa zabuni/mikataba saba kwa Kampuni ya Songoro Marine Transport Limited bila kuzingatia uwezo wa mkandarasi kuhusu uwezo wa mitambo na watumishi muhimu. Kwa mfano, zabuni saba ambazo zilitolewa kwa Kampuni ya Songoro Marine Ltd kati ya Machi na Mei 2022 mkandarasi aliwasilisha orodha hiyo hiyo ya watumishi muhimu na vifaa kwa ajili ya mikataba yote ambayo ipo katika maeneo tofauti ya kijiografia (yaani, Mwanza na Dar es Salaam) na mikataba hiyo ilipangwa kuanza na kukamilika ndani ya kipindi kilekile.

Zaidi ya hayo, nilibaini kuwa miradi miwili kati ya saba aliyopewa kandarasi M/s Songoro Transport Marine Limited yenye jumla ya Sh. bilioni 6.16 zilitolewa bila kuzingatia kadhia ya ukomo kwa mujibu wa Kanuni ya 224 (9) ya Kanuni ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2013 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2016. Kutokana na hilo, mkandarasi amechelewa kumaliza baadhi ya shughuli zilizopangwa kwa miradi kwa kipindi cha miezi sita hadi nane. Mkandarasi amelipwa jumla ya Sh. bilioni 1.91 kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 67**.

Jedwali Na. 67: Uchambuzi wa Maelezo ya Mkataba na Malipo kwa Mkandarasi Ambaye ana Upungufu wa Watumishi Muhimu na mitambo

Namba ya Vocha	Maelezo ya Malipo	Bei ya Mkataba (Sh.)	Kiasi Kilicholipwa (Sh.)
Mkataba Na. AE/006/2021-2022/HQ/W/CN-25	Malipo ya awali kwa ajili ya ukarabati wa MV. Kazi kinachotembea kati ya Magogoni –Kigamboni	1,735,560,000	173,556,000
AE/006/2021-22/HQ/W/CN-04	Ukarabati mkubwa wa MV. Nyerere mkoani Mwanza.	4,427,224,064	1,735,560,000
Jumla		**6,162,784,064**	**1,909,116,000**

Chanzo: *Mikataba ya Ujenzi*

Nina maoni kwamba kutoa zabuni zaidi ya moja kwa mkandarasi mmoja ambaye ana uhaba wa mitambo na watumishi/wataalam muhimu kumeathiri utekelezaji wa miradi kwa wakati.

Napendekeza menejimenti ya TEMESA kuhakikisha tathmini ya zabuni inafanyika ipasavyo na ripoti za tathmini ya bodi ya zabuni kabla ya kutoa zabuni kwa makandarasi kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 224 (9) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 zilizofanyiwa marekebisho ya mwaka 2016.

9.25 Malipo ya Awali ya Sh. bilioni 2.82 yaliyotolewa kwa Wakandarasi zaidi ya kiwango kilichoainishwa katika nyaraka za zabuni Sh. bilioni 2.82

Kanuni ya 227(1) za Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 (marekebisho ya mwaka 2016) inaitaka bodi ya zabuni kuidhinisha mpango wa majadiliao kabla ya mazungumzo yoyote kufanyika. Aidha, Kifungu cha 23 cha Karatasi ya Takwimu za Zabuni (TDS) na Maelekezo ya Zabuni (ITT) na Kifungu cha 59.1 cha nyaraka za zabuni kinataka malipo ya awali yawe ya kiwango cha asilimia 10 hadi kiwango cha juu cha asilimia 20 ya kiasi cha mkataba na kulipwa katika kila Hati ya Malipo ya Muda na kumalizika pale ambapo thamani ya kazi iliyofanyika imefikia asilimia 80.

Ukaguzi wangu wa wa Mfumo wa Ununuzi wa Umma kwa njia ya mtandao (TANePS) kuanzia Julai 2021 hadi Juni 2022 ulibaini kuwa mmojawapo wa Wakandarasi alikuwa na mikataba sita yenye thamani ya Sh. bilioni 19.41 na alikuwa na haki ya kulipwa kiasi cha Sh. bilioni 3.88 kama malipo ya awali kwa kiwango cha asilimia 20 ya gharama za mkataba. Aidha, nilibaini kuwa TEMESA ililipa malipo ya awali ya Sh. bilioni 6.70, sawa na asilimia 35 ya gharama za mkataba, ikizidi kiwango cha malipo kinachoruhusiwa kwa Sh. bilioni 2.82 na kukiuka vipengele vilivyotajwa hapo juu.

Nina maoni yangu kuwa kulipa malipo ya awali kwa mkandarasi zaidi ya kikomo kinachohitajika kunaifanya TEMESA kuwa katika hatari ya kupoteza fedha za mradi iwapo mkandarasi atashindwa kutekeleza kazi.

Ninapendekeza uongozi wa TEMESA kuhakikisha kuwa malipo ya awali yanafanyika kulingana na kiwango kilichotajwa katika mkataba.

9.26 Mapungufu yaliyobainishwa Katika Mradi wa ununuzi wa Vivuko vipya,na Ukarabati mkubwa wa Vivuko na Ujenzi wa Maengesho ya Kivuko

Kanuni ya 69 (4) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013, ambayo ilitangazwa katika Gazeti la Serikali Na. 446, inaelekeza kwamba "Kulingana na kanuni ndogo ya (3), utabiri wa muda wa utekelezaji na umalizaji kazi utajumuisha makadirio ya muda unaofaa wa kipindi cha mwezi mmoja. Ukaguzi huu ulibaini mapungufu yafuatayo:

(a) Ucheleweshaji Mkubwa wa Kuanza Kazi Sh. bilioni 23.46

Katika mwaka wa fedha 2021/22, tulipitia majalada ya mikataba na nyaraka nyingine zinazohusiana na Kituo cha Kivuko cha Magogoni na Kigamboni na kubaini kuwa TEMESA ilisaini mikataba mitatu na Kampuni ya Songoro Marine Transport Ltd na mkataba mwingine na Kampuni ya KL Heavy IND. Jumla ya gharama ya mikataba yote ni Sh. bilioni 23.46 na Dola za Marekani kiasi cha Sh. milioni 1.65. Mkataba mmoja ulisainiwa mwezi Aprili 2022 na mikataba miwili mingine ilisainiwa mwezi Mei 2022. Hata hivyo, nilibaini kuwa hadi kufikia muda wa ukaguzi mwezi Agosti 2022, hakukuwa na kazi zozote zilizotekelezwa kwa mikataba yote minne iliyosainiwa.

(b) Utekelezaji wa Kazi Usioridhisha

Nimepitia ripoti za maendeleo ya miradi 22, ikiwa ni pamoja na miradi mitano ya ununuzi wa vivuko vipya, miradi 12 ya ukarabati mkubwa wa vivuko na miradi mitano ya ujenzi wa maengesho ya vivuko. Nilibaini kuwa miradi minne kati ya mitano ya ununuzi wa vivuko vipya bado haijaanza licha ya kusainiwa tangu mwezi Aprili na Mei 2022. Kwa upande mwingine, mradi mmoja ulikuwa umechelewa kwa asilimia 17.

Wakati wa ukaguzi, niligundua kuwa miradi mitatu kati ya 12 ya ukarabati mkubwa wa vivuko ilikuwa imesimama bila ya utekelezaji kwa kipindi cha miezi 14. Aidha, miradi mingine tisa ilionesha hali ya uchelewaji kwa kiwango cha wastani wa asilimia 12. Aidha, nilibaini kuwa miradi mingine mitano ya ujenzi wa maengesho ya vivuko ilionesha hali ya uchelewaji kwa kiwango cha wastani cha kuanzia asilimia 20 hadi 30.

Ninaamini kuwa kuchelewa kuanza kwa kazi za ujenzi na maendeleo yasiyoridhisha ya ujenzi vinazuia wananchi kupata huduma za vivuko kwa wakati, hivyo kuongeza malalamiko yao kwa Serikali. Aidha, ucheleweshaji huo una athari kwa bei za vifaa vya ujenzi zinazoendelea kupanda.

Napendekeza menejimenti ya TEMESA kuimarisha usimamizi wa utekelezaji wa miradi na kuboresha mipango ya miradi ili iweze kutekelezwa kwa wakati unaofaa. Pia, ni vyema kuendelea kuwasiliana na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa ushirikiano na Wizara ya Fedha na Mipango ili kuhakikisha fedha zinatolewa kwa wakati unaofaa. Hii

itasaidia kupunguza ucheleweshaji wa utekelezaji wa miradi na hivyo kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma za vivuko kwa umma.

9.27 Kasoro zilizopatikana katika Mkataba wa Ushauri wa Ujenzi wa Jengo la Tume ya Utumishi wa Mahakama Dodoma wenye thamani ya Sh. Milioni 746.4 5

Kanuni ya 75(1) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 (Iliyorekebisha mwaka 2021) zinataka Taasisi Nunuzi kuhakikisha fedha zinatengwa au kukasimiwa kabla ya kuanza taratibu za ununuzi.

Aidha, Kanuni 111(1) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 (zilizorekebishwa 2021) inawataka Maafisa Masuuli kuongeza muda wa mkataba, na sababu hizo ni lazima ziandikwe kikamilifu katika kumbukumbu za utekelezaji wa mkataba.

Tarehe 1 Julai 2021, Tume ya Uongozi wa Mahakama ilisaini Mkataba Na. IE/007/2020/2021/HQ/C/O1 na Mkandarasi Arqes Africa Limited kwa ajili ya kutoa huduma za ushauri wa usanifu na usimamizi wa kazi katika ujenzi wa Jengo la Tume ya Uongozi wa Mahakama Dodoma kwa bei ya mkataba wa Sh. milioni 746.45 kwa kipindi cha miezi 12 kuanzia tarehe 16 Julai 2021 hadi tarehe 15 Julai 2022.

Nilibaini kuwa maendeleo ya ujenzi wa jengo hilo yalikuwa asilimia 49.90 kufikia kipindi cha ukaguzi tarehe 7 Septemba 2022, wakati mkataba wa mshauri ulikuwa umemalizika tarehe 15 Julai 2022. Niligundua pia kwamba mkataba ulikuwa na awamu mbili, ya kwanza ikiwa katika hatua ya usanifu na ya pili ikiwa katika hatua ya usimamizi. Awamu ya kwanza ilikuwa imekamilika, na Sh. milioni 373.22 (sawa na asilimia 50 ya bei ya mkataba) ilikuwa tayari imelipwa kwa mshauri. Nilipitia majalada ya utekelezaji wa mkataba na kubaini kasoro zifuatazo:

i. **Bei ya Mkataba wa Mshauri ilikuwa zaidi ya Bajeti iliyoidhinishwa kiasi cha Sh. milioni 496.45.**
   Baada ya kupitia Bajeti ya Tume ya Utumishi wa Mahakama, nilibaini kuwa Sh. milioni 250 zilitengwa kwa ajili ya huduma za ushauri katika usanifu na usimamizi wa ujenzi wa Jengo la Tume ya Utumishi wa Mahakama jijini Dodoma. Aidha, Tume iliingia mkataba na Mshauri aitwaye Arqes Africa Limited kwa mkataba wenye thamani ya Sh.

milioni 746.45 ambayo ilizidi bajeti iliyotengwa kwa Sh. milioni 496.45. Hii ni kinyume na kanuni iliyotajwa hapo juu na hakuna ushahidi wa chanzo cha ziada cha fedha kilichotolewa wakati wa ukaguzi.

ii. **Utekelezaji wa Kazi ya Ushauri katika Muda wa Mkataba ulioisha muda wake**

1.	Taasisi za serikali	1,721,503,618
2.	Taasisi binafsi	78,823,977
3.	Watu binafsi	107,205,000
Jumla		**1,907,532,595**

Chanzo: *Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti*

Ni maoni yangu kuwa, madai haya kukaa kwa muda mrefu bila kukusanywa kumechangiwa na ufuatiliaji usioridhisha wa RUWASA na wadaiwa kukosa uwezo wa kulipa madeni yao.

Ni dhahiri kuwa madai ya muda mrefu kutoka kwa taasisi za serikali yanaikosesha RUWASA mapato na kuathiri utendaji wa kitengo cha uchimbaji.

Ninapendekeza RUWASA ichukue hatua za haraka za kukusanya madai kutoka kwa wateja wote, ikiwa ni pamoja na taasisi za Serikali, taasisi binafsi, na watu binafsi. Ili kufanikisha hili, RUWASA inaweza kufikiria kutekeleza masharti na adhabu kali kwa wanaochelewesha malipo, na kushirikisha Wizara ya Fedha na Mipango kama wakala wa ukusanyaji wa maduhuli kwa taasisi za Serikali kwa kukata moja kwa moja kiasi chochote kinachodaiwa kutoka kwenye ruzuku iliyotengwa kwa taasisi hiyo.

10.4.3 Miradi ya Maji Isiyo Endelevu Yenye Vituo 16,806 vya Kuchotea Maji

Mapitio ya taarifa kutoka kwenye Mfumo wa Utoaji na Usimamizi wa Huduma za RUWASA (RSDMS) kwa mikoa 20 kati ya 25 ambako RUWASA inafanya kazi yalibaini kuwa kati ya vituo 215,980 vya kuchotea maji, 16,806 sawa na asilimia nane havikuwa endelevu. Kati ya vituo hivyo visizo endelevu, 10,565 sawa na asilimia tano havifanyi kazi, 4,886 sawa na asilimia mbili vinahitaji ukarabati na 1,355 sawa na asilimia moja vimetelekezwa. Hali ya utendaji kazi wa vituo vya kuchotea maji inaoneshwa katika **Jedwali Na. 76**.

Jedwali Na. 76: Hali ya Utendaji Kazi wa Vituo vya Kuchotea Maji kwenye Miradi ya Maji

Na.	Hali ya Vituo	Idadi ya Vituo vya Kuchotea Maji	Asilimia
1.	Vilivyotelekezwa	1,355	1
2.	Visivyofanya kazi	10,565	5
3.	Vinavyohitaji ukarabati	4,886	2
Jumla ya vituo visivyoendelevu		16,806	
4.	Vinavyofanya kazi	199,174	92
Jumla ya vituo vya maji		**215,980**	**100**

Chanzo: *RSDMS Imepatikana tarehe 31 Januari 2023*

Katika ukaguzi wangu, nilibaini sababu za kuathirika kwa uendelevu wa vituo vya kuchotea maji kwenye miradi ya RUWASA ni pamoja na matengenezo yasiyoridhisha, ukosefu wa fedha za kutosha, ukosefu wa mipango sahihi, na utekelezaji duni wa miradi.

Kwa maoni yangu, vituo vya kuchotea maji visivyo endelevu vinaweza kusababisha kupungua kwa upatikanaji wa maji safi na salama, na kuongezeka kwa gharama za ukarabati na matengenezo.

Ninapendekeza RUWASA ifanye matengenezo na ukarabati wa mara kwa mara kwenye vituo vya usambazaji maji ili kuhakikisha uendelevu wake. Katika siku zijazo, RUWASA inapaswa kutenga fedha za kutosha na kuweka kipaumbele katika upangaji na utekelezaji sahihi wa miradi ya maji. Aidha, RUWASA inapaswa kufanya kazi ya kuboresha mfumo wa usimamizi wa takwimu ili kuwa na taarifa sahihi za miradi ya maji iliyotelekezwa na thamani ya fedha ya miradi hiyo ili kuwezesha kupata thamani sahihi ya uchakavu na kuchukua hatua stahiki.

10.4.4 Visima 57 Visivyo na Tija

Ukaguzi wa bajeti ya RUWASA ya mwaka 2021/22 na ripoti ya utekelezaji ya robo ya nne kuhusu Sehemu ya Uchimbaji ulibaini kuwa kati ya visima 250 vilivyopangwa kuchimbwa, visima virefu 57 sawa na asilimia 23 havikuwa na tija, visima virefu 44 sawa na asilimia 18 vilichimbwa lakini havikufanyiwa majaribio ya kusukuma maji, na visima virefu 40 sawa na asilimia 16 havikuchimbwa. Maelezo yanaoneshwa katika **Jedwali Na. 77.**

Jedwali Na. 77: Hali ya Visima Vilivyopangwa Na Vilivyochimbwa

Na.	Aina ya Visima	Idadi ya Visima
1.	Visima vilivyochimbwa lakini havina maji ya kutosha.	5
2.	Visima vilivyochimbwa lakini havijapatikana na maji.	44
3.	Visima vilivyochimbwa na kutelekezwa.	8
Jumla		**57**

Chanzo: *Bajeti iliyoidhinishwa na taarifa ya utekelezaji ya robo ya nne*

Kwa mtazamo wangu, Sehemu ya Kuchimba visima ya RUWASA haikufanya tafiti za kutosha za kijiolojia kwa kutumia zana za kisasa kabla ya kuchimba

visima, jambo ambalo limesababisha visima visivyo na tija na ukosefu wa vipimo vya kusukuma maji.

Ni maoni yangu kuwa uwepo wa visima visivyo na tija unawanyima watumiaji fursa ya kupata maji safi na salama, na pia husababisha upotevu wa gharama zilizotumika kuchimba visima hivyo.

Naishauri RUWASA kufanya tafiti za kijiolojia kwa kutumia zana za kisasa kabla ya kuchimba visima ili kupunguza hasara zinazotokana na kuchimba visima ambavyo havina maji.

10.4.5 Udhibiti na Ufuatiliaji Usioridhisha wa CBWSOs Zilizokusanya Sh. Bilioni 68.2

Vifungu vya 34 na 41 (1) vya Sheria ya Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira, 2019 vinaipa RUWASA jukumu la kufuatilia na kusimamia shughuli za Chombo cha Watoa Huduma ya Maji Ngazi za Jamii (CBWSO) ili kuhakikisha utoaji wa huduma endelevu za maji. Hii ni pamoja na wajibu wa kufuatilia utendaji wake wa kazi, usimamizi wa fedha, na uanzishwaji wa kanuni za maadili, pamoja na uundaji na uidhinishaji wa Katiba au Mkataba wa Makubaliano wa CBWSOs. Aidha, Kifungu cha 7 cha Sheria ya Fedha za Umma Sura ya 348 fedha zote za umma kukusanywa kupitia Mfumo wa Kielektroniki wa Malipo ya Serikali (GePG).

Nilipitia Mfumo wa Utoaji na Usimamizi wa Huduma za RUWASA (RSDMS) na kubaini kuwa Vyombo 2,631 vya Watoa Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii (CBWSOs) vilikusanya jumla ya Sh. bilioni 68.2 nje ya Mfumo wa Kielektroniki wa Malipo ya Serikali (GePG). Mapato haya hayajaonekana katika taarifa za fedha za RUWASA. Aidha, hakuna utaratibu wa uhifadhi wa fedha ili kuhakikisha uendelevu wa miradi ya maji. Licha ya mapato yanayokusanywa na CBWSO, jukumu la matengenezo na uendelevu wa miradi ya maji liko katika Ofisi za Wilaya za RUWASA.

Aidha, ukaguzi wangu katika Ofisi za RUWASA Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Lindi, Mbeya, Morogoro, Njombe na Pwani ulibaini udhaifu katika usimamizi na ufuatiliaji wa CBWSOs kama vile kutoandaa na kuwasilisha taarifa zinazotakiwa kwa RUWASA, kushindwa kuanzisha na kuzingatia viwango na kanuni za maadili zinazohitajika, mahudhurio ya mafunzo yasiyotosheleza,

pamoja na kushindwa kuandaa taarifa za fedha, ufuatiliaji usioridhisha wa ubora wa maji na ukosefu wa uanzishwaji wa kamati za maji. Masuala haya yaliripotiwa katika ripoti zangu za ukaguzi za miaka ya nyuma, na hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa kuyashughulikia.

Maelezo ya mapato yanayokusanywa na CBWSOs katika mikoa 25 na masuala yaliyobainishwa katika usimamizi wa CBWSOs yanaoneshwa katika **Jedwali Na. 78** na **Jedwali Na. 79**.

Jedwali Na. 78: Makusanyo ya mapato ya CBWSO

Na.	Mkoa	Idadi ya CBWSO	Jumla ya Makusanyo (Sh.)
1	Kilimanjaro	43	17,403,530,911
2	Tabora	63	6,616,132,781
3	Arusha	110	6,202,982,209
4	Shinyanga	35	3,942,936,267
5	Morogoro	70	3,418,070,057
6	Manyara	217	3,233,042,381
7	Dodoma	347	3,223,529,491
8	Mwanza	75	2,973,297,651
9	Tanga	132	2,620,540,943
10	Kagera	150	2,281,169,018
11	Singida	144	2,037,632,786
12	Lindi	186	1,941,601,441
13	Mtwara	77	1,608,854,297
14	Geita	47	1,444,604,718
15	Iringa	64	1,402,923,366
16	Simiyu	59	1,305,589,262
17	Kigoma	122	1,283,348,559
18	Ruvuma	98	935,395,526
19	Mbeya	78	852,050,344
20	Katavi	40	758,038,148
21	Pwani	88	696,607,528
22	Njombe	171	614,651,007
23	Mara	89	583,343,361
24	Songwe	85	452,239,726
25	Rukwa	41	407,729,675
Jumla		**2631**	**68,239,841,453**

Chanzo: *Mfumo wa Utoaji na Usimamizi wa Huduma za RUWASA*

Jedwali Na. 79: Udhaifu Uliobainishwa katika Usimamizi wa CBWSO

Mkoa	Maelezo
RUWASA Arusha	Haikuwa imeandaa viwango na kanuni za maadili kwa CBWSO na watumiaji kwa ujumla
	RUWASA Arusha ina CBWSOs 97 ambapo hakuna iliyoandaa na kusaini Katiba/MoA kama inavyotakiwa na Kifungu cha 34 cha Sheria ya Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira, 2019.
	Hakuna CBWSO iliyoandaa na kuwasilisha ripoti kwa RUWASA kama inavyotakiwa chini ya Kifungu cha 34.
RUWASA Kilimanjaro	RUWASA Kilimanjaro haikuwa imeandaa viwango na kanuni za maadili kwa CBWOs na watumiaji kwa ujumla.
	RUWASA Kilimanjaro ina CBWSO 47, kati ya hizo CBWSO iliyoandaa na kusaini Katiba/MoU kama inavyotakiwa na Kifungu cha 34 cha Sheria ya Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira, 2019.
	Ni CBWSO tatu tu (asilimia 6) kati ya CBWSO 47; Lossa_KIA, Uroki-Bomang'ombe, Hedaru – Same na Lembeni waliandaa na kuwasilisha ripoti RUWASA
RUWASA Lindi	Jumla ya miradi 88 ya maji inafanya kazi katika vijiji 136 bila Kamati ya Maji ambayo inatoa huduma ya usambazaji maji na usafi wa mazingira
RUWASA Morogoro	Ufuatiliaji ulifanyika Wilaya ya Morogoro pekee kati ya Wilaya 7.
	Miradi 40 ya maji inayofanya kazi bila Kamati ya Maji ambayo inatoa huduma za usambazaji maji na usafi wa mazingira
RUWASA Njombe	Hakuna viwango na kanuni za maadili kwa CBWOs ziliandaliwa
	CBWSOs zote za RUWASA Njombe zimeandaa na kusaini Katiba kama inavyotakiwa na Sheria, 2019
	Hakuna CBWSO yeyote katika RUWASA Njombe aliyeandaa na kuwasilisha ripoti kwa RUWASA kama inavyotakiwa chini ya Kifungu cha 34.
RUWASA Pwani	CBWSOs zote 30 hazijawahi kuandaa taarifa za kifedha tangu kuanzishwa.
	CBWSOs 20 zilikuwa hazihudhurii mafunzo kinyume na mpango wa mafunzo ya RUWASA Mkoa wa Pwani
RUWASA Mbeya	RUWASA haijafanya utafiti kwa ajili ya utawala na usimamizi wa CBWSO kinyume na matakwa ya Kifungu cha 41 (1)(c)
	RUWASA Mbeya haikuandaa viwango na kanuni za maadili kuhusiana na CBWSO kinyume na matakwa ya Kifungu cha 41 (1) (a).
	Ufuatiliaji wa ubora wa maji haukuthibitishwa kufanyika kinyume na matakwa ya Kifungu cha 41 cha Sheria ya Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira, 2019.
	Katika kipindi cha mwaka 2021/22 makubaliano ya utendaji kati ya CBWSO na RUWASA hayakusainiwa.

Chanzo: *Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti*

Ni maoni yangu kwamba, kushindwa kukusanya mapato kupitia mfumo wa GePG na kukosekana kwa utaratibu wa uhifadhi fedha kunaweza kusababisha upotevu wa mapato ya Serikali na ukosefu wa uendelevu wa miradi ya maji. Ufuatiliaji usioridhisha wa CBWSOs pia umechangia usimamizi mbovu na utunzaji duni wa miradi ya maji, jambo ambalo linaathiri utoaji wa huduma za maji kwa jamii.

Ninatoa wito kwa Vyombo vya Watoa Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii (CBWSOs) kutumia mfumo wa GePG kukusanya mapato, na kuanzisha utaratibu wa kuhifadhi fedha ili kuhakikisha uendelevu wa miradi ya maji. Ofisi za Mikoa za RUWASA pia ziboreshe ufuatiliaji wao wa CBWSOs ili kuhakikisha usimamizi na utunzaji madhubuti wa miradi ya maji. Aidha, serikali ihakikishe kuwa mapato yote yanayokusanywa na CBWSOs yanaonekana katika taarifa za fedha ili kuepuka upotevu wa mapato ya serikali.

10.5 Mamlaka za Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Daraja la III

Wakati wa tathmini yangu, nilibaini masuala kadhaa yanayohusu usimamizi wa usambazaji wa maji, ambapo matano yalionekana kuwa muhimu kama yalivyoelezwa katika aya ya 10.5.1 hadi 10.5.5.

10.5.1 Upotevu wa Mapato Kiasi cha Sh. Bilioni 9.32 Uliosababishwa na Upotevu wa Maji

Maji Yasiyo ya Mapato (NRW) ni kiasi cha maji ambacho Mamlaka ya Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira inazalisha au kununua kwa ajili ya kuuza lakini hupotea kabla ya kuwafikia wateja. Kwa mujibu wa viwango vya EWURA, kiwango kinachokubalika cha NRW kwa Mamlaka za Maji ni sawa au chini ya asilimia 20 ya maji yote yanayozalishwa.

Nilibaini kuwa kiwango cha maji yasiyo ya mapato ni kikubwa sana hadi kufikia asilimia 84 kwa badhi ya mamlaka, kipimo ambacho kinazidi ukomo unaokubalika wa asilimia 20 uliowekwa na EWURA kwa mamlaka za maji. Hii ni sawa na upotevu wa Sh. bilioni 9.32 kutoka mamlaka za maji 30, kama inavyooneshwa katika **Kiambatisho Na. XXVI.**

Tathmini yangu imebaini kuwa kiwango kikubwa cha maji yasiyo ya mapato ni miundombinu iliyochakaa.

Ninaishauri Serikali na mamlaka husika kuimarisha usimamizi wa rasilimali maji kupitia utekelezaji wa miundombinu ya kisasa inayopunguza uvujaji wa maji.

10.5.2 Wateja Wasiofungiwa Mita za Maji

Kifungu cha 21 (c) na (d) cha Sheria ya Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira, 2019 kinaitaka mamlaka ya maji kufunga mita za maji kwa wateja wake kwa lengo la kupima kiasi halisi cha maji kilichosambazwa kwa mlaji; na kutoza ada kwa huduma iliyotolewa.

Nilibaini kuwa katika mwaka wa fedha 2021/22, mamlaka za maji tisa zilikuwa na wateja 26,730, kati ya hao wateja 6,515 sawa na asilimia 24 hawakuwa na mita kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 80**. Hii imesababisha kupungua kwa uwezo wa mamlaka kuongeza mapato yake ya ndani.

Jedwali Na. 80: Orodha ya Mamlaka za Maji zenye Wateja Wasiofungiwa Mita za Maji

Na.	Jina la Mamlaka	Jumla ya Wateja	Wateja Wenye Mita	Wateja Wasio na Mita	Asilimia
1.	Mamlaka ya Maji Itumba-Isongole	1,664	782	882	53
2.	Mamlaka ya Maji Kasulu	3,312	1,610	1,702	51
3.	Mamlaka ya Maji Lushoto	1,753	958	795	45
4.	Mamlaka ya Maji Maswa	4,701	3,455	1,246	27
5.	Mamlaka ya Maji Mombo	723	202	521	72
6.	Mamlaka ya Maji Namtumbo	11,819	10,961	858	7
7.	Mamlaka ya Maji Songe-Kilindi	598	455	143	24
8.	Mamlaka ya Maji Vwawa Mlowo	2,160	1,792	368	17
Jumla		**26,730**	**20,215**	**6,515**	

Chanzo: *Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti*

Tathmini yangu ilibaini kuwa sababu kuu ya kuwa na idadi kubwa ya wateja wasiofungiwa mita za maji ni mamlaka za maji kukosa rasilimali fedha za kufunga mita za maji na kutunza miundombinu ikiwemo mita na vifaa vinavyohusiana.

Kwa kutowafungia wateja mita za maji sahihi, kunazuia utozwaji wa gharama za maji kwa wateja kulingana na matumizi halisi ya maji, na kusababisha upotevu wa mapato au utoaji wa bili zisizo sahihi. Hii pia inaweza kusababisha mamlaka kukosa hamasa ya kuwekeza katika kupanua miundombinu yake na kuboresha huduma kutokana na mapato kidogo.

Ninapendekeza mamlaka za maji kuweka kipaumbele katika ufungaji wa mita za maji kwa wateja wote ambao hawajafungiwa. Hii itawezesha mamlaka kutoza wateja kulingana na matumizi yao halisi, jambo ambalo litaongeza ukusanyaji wa mapato na kusaidia mamlaka kuwa na fedha za kutosha. Mamlaka za maji pia zizingatie utekelezaji wa mpango wa matengenezo ya mara kwa mara wa mita hizo ili kuhakikisha zinakuwa sahihi na zinafanya kazi vizuri.

10.5.3 Gharama kubwa za Umeme kwa Mamlaka za Maji katika Kusambaza Huduma ya Maji

Kifungu cha 15 (1) cha Sheria ya Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira, 2019 kinaitaka mamlaka ya maji kutoa huduma ya maji kwa ufanisi na kiuchumi kulingana na leseni iliyotolewa na EWURA.

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa, katika kipindi cha mwaka wa ukaguzi mamlaka za maji tatu zilitumia Sh. milioni 239.96 kwa ajili ya gharama za umeme sawa na asilimia 34 ya mapato yote ya Sh. milioni 698.07 yaliyokusanywa kwa mwaka kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 81**.

Jedwali Na. 81: Gharama kubwa za umeme kwa Mamlaka za Maji katika Kusambaza Huduma ya Maji

Na.	Jina la Mamlaka	Jumla ya Mapato Yaliyokusanywa (Sh.)	Gharama za Umeme (Sh.)	Asilimia
1.	Mamlaka ya Maji Chunya	140,456,330	78, 408,500	56
2.	Mamlaka ya Maji Gairo	476,828,178	215,612,296	45

Na.	Jina la Mamlaka	Jumla ya Mapato Yaliyokusanywa (Sh.)	Gharama za Umeme (Sh.)	Asilimia
3.	Mamlaka ya Maji Songe-Kilindi	80,789,860	24,350,000	30
Jumla		**698,074,368**	**239,962,296**	**34**

Chanzo: *Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti*

Tathmini yangu imebaini kuwa gharama za umeme zimekuwa zikiongezeka kwa kiasi kikubwa huku ukusanyaji wa mapato ukiendelea kuwa hafifu kutokana na upotevu wa maji na mauzo ya maji yasiyo kusanywa.

Nina maoni kuwa, malipo haya makubwa ya umeme yanaweza kusababisha ugumu wa kukidhi gharama nyingine za uendeshaji wa shughuli za mamlaka kwa ufanisi na malengo yaliyokusudiwa.

Ninapendekeza mamlaka za maji kuangalia namna ya kuongeza ukusanyaji wa mapato ili kukidhi gharama kubwa za umeme. Hii inaweza kujumuisha kuanzisha vyanzo vipya vya kuzalisha mapato, au kushirikiana na Wizara ya Maji na RUWASA ili kupata mapato ya ziada.

10.5.4 Mapato Yasiyokusanywa Kutokana na Mauzo ya Maji Sh. Bilioni 1.55

Kanuni ya 57 (2) ya Kanuni ya Fedha za Umma, 2001 inawataka Maafisa Masuuli kuhakikisha kuwa wanaodaiwa mapato wanaarifiwa kupitia bili, hati ya madai, au aina nyingine zinazofaa za madai. Aidha, kuwakumbusha mara kwa mara juu ya madeni yoyote yaliyosalia, na hatua stahiki zichukuliwe dhidi ya wadaiwa, ikiwa ni pamoja na hatua za kisheria pale inapobidi.

Ukaguzi wangu ulibainisha kuwa, kati ya Sh. bilioni 8.75 za mauzo ya maji kwa wateja katika mamlaka za maji 22, ni Sh. bilioni 7.2 tu zilizokusanywa na kuacha mapato yasiyokusanywa kiasi cha Sh. bilioni 1.55 kama inavyoelezwa katika **Kiambatisho Na. XXVII**.

Tathmini yangu ilibaini kuwa sababu kuu ya kutokusanywa mapato yatokanayo na mauzo ya maji ni uwepo wa bili au mita zisizo sahihi, hivyo kusababisha migogoro na ucheleweshwaji wa malipo. Aidha, sababu zingine zilizochangia mapato yasiyokusanywa ni udhaifu wa mifumo na taratibu za

ukusanyaji wa mapato, ikiwa ni pamoja na miundombinu duni ya utoaji wa bili, ukusanyaji, pamoja na ukosefu wa mikakati na sera madhubuti za ukusanyaji.

Mapato ya mauzo ya maji yasiyokusanywa kiasi cha Sh. bilioni 1.55, yanaonesha kuwa mamlaka za maji hazijaweza kukusanya mapato yote zinayodai. Hii inaweza kuwa na athari mbaya kwenye hali ya kifedha ya mamlaka, kwani wanaweza kukabiliwa na ugumu katika kutimiza majukumu ya kifedha, kama vile kulipa mishahara, kununua vifaa, na kuwekeza katika uboreshaji wa miundombinu na hatimaye kuathiri ubora wa huduma zinazotolewa kwa wateja.

Ninaziomba mamlaka za maji kuimarisha mfumo wao wa madai na ukusanyaji mapato kwa kuhakikisha wateja wote wanatozwa kwa usahihi na kwamba hati za madai zinawasilishwa kwa wakati. Pia wanapaswa kuwa na mfumo wa kufuatilia madai ya muda mrefu na kuhakikisha kuwa wateja wanafahamu madhara ya kutolipa. Aidha, naziomba mamlaka za maji kuimarisha udhibiti wa ndani ili kuzuia udanganyifu na kuhakikisha mapato yote yanatunzwa ipasavyo.

10.5.5 Uwezo Usioridhisha kwa Mamlaka za Maji Kusambaza Huduma za Maji katika Eneo la Mamlaka yao

Kifungu cha 13 (1) cha Sheria ya Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira, 2019 kinaitaka mamlaka ya maji kutumia njia zote muhimu ili kutoa huduma ya usambazaji maji na usafi wa mazingira katika eneo lililo chini ya mamlaka yake.

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa mahitaji ya maji kwa maeneo ya utawala wa mamlaka za maji 16 kwa mwaka 2021/22 yalikuwa ni mita za ujazo 37,031,917. Hata hivyo, uwezo wao wa uzalishaji kwa mwaka ulikuwa ni mita za ujazo 15,384,511 tu na hivyo kusababisha upungufu wa mita za ujazo 21,647,406 ambao ni sawa na upungufu wa asilimia 58. Upungufu huo kwa baadhi ya mamlaka za maji ulikuwa wa hali ya juu hadi kufikia asilimia 86 kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 82**.

Jedwali Na. 82: Mamlaka za Maji Zenye Uwezo Mdogo wa Kusambaza Maji

Na.	Chombo	Mahitaji ya kila mwaka	Uzalishaji wa kila mwaka	Upungufu	Asilimia
1.	Mamlaka ya Maji Biharamulo	1,134,241	388,111	746,130	66
2.	Mamlaka ya Maji Chunya	918,340	395,660	522,680	57
3.	Mamlaka ya Maji Itumba-Isongole	620,500	476,690	143,810	23
4.	Mamlaka ya Maji Kasulu	2,265,555	932,575	1,332,980	59
5.	Mamlaka ya Maji Loliondo	530,430	147,201	383,229	72
6.	Mamlaka ya Maji Mafinga	2,850,862	996,085	1,854,777	65
7.	Mamlaka ya Maji Maganzo	241,083	91,958	149,125	62
8.	Mamlaka ya Maji Namanyere	1,075,089	496,400	578,689	54
9.	Mamlaka ya Maji Namtumbo	1,420,992	704,520	716,472	50
10.	Mamlaka ya Maji Orkesument	574,226	133,545	440,681	77
11.	Mamlaka ya Maji Rombo	12,045,000	7,462,473	4,582,527	38
12.	Mamlaka ya Maji Ruangwa	1,593,590	858,480	735,110	46
13.	Mamlaka ya Maji Rujewa	2,331,360	734,760	1,596,600	68
14.	Mamlaka ya Maji Tunduma	5,624,285	880,745	4,743,540	84
15.	Mamlaka ya Maji Tunduru	1,475,280	203,265	1,272,015	86
16.	Mamlaka ya Maji Turiani	1,267,200	311,040	956,160	75
17.	Mamlaka ya Maji Ushirombo	1,063,884	171,003	892,881	84
Jumla		**37,031,917**	**15,384,511**	**21,647,406**	**58**

Chanzo: *Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti*

Tathimini yangu imebaini kuwa, sababu ya msingi ya uwezo usioridhisha wa mamlaka za maji kutoa huduma za maji katika maeneo yao ni miundombinu

ya maji iliyochakaa ambayo inasababisha upotevu mkubwa wa maji na mapato kutokana na kuvuja kwa maji.

Ukosefu wa maji ya kutosha unaweza kusababisha uhaba wa maji, ambao unaweza kuathiri vibaya mahitaji ya maji kwenye kaya, biashara, kilimo, na mfumo wa ikolojia.

Ninazishauri mamlaka za maji kuangalia namna ya kuongeza uwezo wao wa uzalishaji ili kukidhi ongezeko la mahitaji ya maji katika maeneo yao. Hii inaweza kuhusisha kuwekeza katika miundombinu mipya, kuboresha miundombinu iliyopo, au kutumia teknolojia mpya ili kuboresha usambazaji wa maji. Pia, kushirikiana na mamlaka nyingine za maji kwa kugawana rasilimali, miundombinu na utaalamu vinaweza kuboresha upatikanaji wa maji na kuhakikisha uendelevu wa rasilimali za maji.



SURA YA KUMI NA MOJA

UKAGUZI WA WAKALA ZA SERIKALI, MIFUKO MAALUMU YA FEDHA, NA TAASISI NYINGINE

11.1 Utangulizi

Sura hii inaelezea matokeo ya ukaguzi wa Wakala za Serikali 30, Mifuko Maalumu ya Fedha 19, Taasisi Nyingine za Serikali 68.

Katika Sura hii nimeonesha masuala mahususi na mtambuka yanayohitaji kufanyiwa kazi na Serikali, Bunge, Bodi za Ushauri za Wizara na Menejimenti za taasisi husika ili kuhakikisha ufanisi katika utendaji wa shughuli za taasisi hizo.

Katika ukaguzi wa mwaka wa fedha 2021/22 wa Wakala za serikali ambazo zimeanzishwa chini ya Sheria ya Wakala [Sura ya 245], nimebaini mapungufu kadhaa kuhusu uendeshaji na usimamizi wa kifedha wa Wakala hizo. Aidha, nimeangalia ni jinsi gani Wakala zinasimamia mipango iliyowekwa ya ufuatiliaji wa maendeleo ya miradi inayosimamia. Yafuatayo ni masuala muhimu yaliyobainika katika ukaguzi wa Wakala wa Serikali.

11.2 Wakala wa Majengo Tanzania (TBA)

Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) ni wakala wa Serikali chini ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Lengo kuu la TBA ni kutoa makazi bora kwa Serikali na Watumishi pamoja na kutoa ushauri katika masuala ya Ujenzi kwa Serikali. Ukaguzi kuhusu uendeshaji wa TBA ulibaini upungufu ufuatao:

11.2.1 Riba Iliyosababishwa na Ucheleweshaji wa Ulipaji wa Madai ya Mshirika katika Uwekezaji wa Jengo la Chimara – dola za Marekani milioni 5.22 (Sh. Bilioni 11.99)

Tarehe 06 Agosti 2007, TBA na M/s Royale Orchard Inn Ltd (ROIL) waliingia mikataba miwili ya ubia (Nambari: TBA/JVA/DSM/ROI/001 na TBA/JVA/DSM/ROI/002) kwa ajili ya uendelezaji na umiliki wa kudumu wa pamoja wa mali zilizopo katika viwanja Na. 45 na 46 vilivyopo Barabara ya Chimara, Dar es Salaam kwa ajili ya makazi. Kulingana na makubaliano, majengo mawili ya ghorofa 15 kila moja yalipangwa kujengwa kwenye eneo hilo, ambapo baadaye yalibadilishwa na kuwa ghorofa 18 kwa kila jengo. Ilikubaliwa na pande zote kuwa TBA itamiliki asilimia 25 ya hisa, ambayo ni thamani ya ardhi, wakati ROIL itamiliki hisa asilimia 75 ya hisa. Ujenzi huo ulikamilika Mei 2011.

Kufuatia kukamilika kwa ujenzi huo mnamo mwezi Mei 2011, Serikali ilichukua vyumba 11 kwenye ghorofa ya 17 na 18 (vinavyomilikiwa na ROIL) kwa sababu za usalama. Pia, Mei 2012, serikali iliiagiza TBA kutoa nyumba 32 (zinazomilikiwa na Wakala) vikiwa na samani za kujitosheleza, kwa ajili ya wajumbe wapya wa Kamati ya Bunge ya katiba. Kufuatia maagizo hayo, TBA ilinunua samani hizo kutoka ROIL kwa ajili ya nyumba 32 na ikakubali kulipa Dola za Marekani 35,000 kwa samani hizo kwa kila nyumba (jumla ya Dola za Marekani 1,120,000) ndani ya siku 90. Kukosa kufanya malipo ndani ya muda uliowekwa kungeweza kusababisha riba ya asilimia 2 kwa mwezi.

Hata hivyo, nilibaini kuwa miaka mitano baadaye, ROIL ilifungua kesi ya Ardhi (Kesi ya Ardhi Na. 14 ya mwaka 2016 kati ya Royale Orchard Inn Ltd na TBA) ya tarehe 09 Machi 2016, dhidi ya TBA kwa kutokulipa kodi ya nyumba 11 zinazokaliwa na maafisa wa Serikali pamoja na samani zilizotolewa kwa ajili ya nyumba 32 vya wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Katiba. Katika hukumu ya tarehe 14 Juni 2019, Mahakama Kuu ya Tanzania iliamuru TBA kulipa kodi ya nyumba hizo 11, pamoja na riba ya 18% kwa mwaka. TBA pia iliagizwa kulipia gharama za samani zilizonunuliwa na kuwekwa kwenye nyumba 32, riba ya asilimia mbili kwa mwezi, pamoja na malipo ya huduma na maji kwenye nyumba hizo.

Kutokana na hukumu hiyo ya mahakama, nilibaini kuwa TBA ilifanya malipo ya dola za Marekani 12,158,182.50 kwa ROIL tarehe 12 Mei 2022, kwa

kutumia nambari ya vocha ya malipo 00S40000D2201464. Malipo haya yalijumuisha deni halisi la Dola za Marekani 6,609,464.81, riba ya Dola za Marekani 5,216,158.69 kwa kucheleweshwa kwa malipo, na kodi ya ongezeko la thamani ya dola za Marekani 332,559. Hata hivyo, ni maoni yangu kuwa riba iliyotozwa ya dola za Marekani 5,216,158.69 (Sh. 11,994,296,099.72), sawa na asilimia 79 ya deni halisi, imesababisha mzigo mkubwa wa gharama kwa walipakodi. Mzigo huu ungeweza kuepukwa, na fedha hizo kutumika kwa shughuli nyingine za maendeleo.

Ninapendekeza TBA ihakikishe kuwa inafanya malipo ya madeni yake kwa wakati ili kuepuka riba za ucheleweshaji malipo. Aidha, serikali ifanye uchunguzi ili kubaini iwapo kulikuwa na uzembe uliosababisha serikali kulipa kiasi kikubwa cha riba. Iwapo uzembe au utovu wa nidhamu utabainika, hatua stahiki zinapaswa kuchukuliwa dhidi ya waliohusika ili kuzuia hali kama hiyo kutotokea katika siku zijazo.

11.3 Wakala wa Ndege za Serikali (TGFA)

Wakala wa Ndege za Serikali (TGFA) ni wakala ambao hutoa huduma za ndege kwa watu mashuhuri (VIP) kwa maafisa wa serikali. Pia, TGFA inasimamia ndege zote za serikali ya Tanzania. Ukaguzi wa shughuli za TGFA ulibaini upungufu ufuatao:

11.3.1 Kutokulipwa kwa Gharama za Kukodisha Ndege za Serikali na ATCL – Sh. Bilioni 188.19

Wakala wa Ndege za Serikali Tanzania (TGFA) na ATCL (Shirika la Ndege Tanzania) waliingia mikataba mitatu ya ukodishaji na miwili ya nyongeza za mikataba hiyo (addendum) mnamo tarehe 03 Oktoba 2016, 10 Desemba 2018, na 24 Julai 2018. Mikataba hii ilikuwa na madhumuni ya kukodisha ndege 11 za aina tatu tofauti zikiwemo Bombardier Dash 8 - Q400, Airbus A220-300, na Boeing B787-8. Kifungu cha 4 na 11.10 cha mikataba hii kinamtaka mkodishwaji (ATCL) kulipa ada za kila mwezi za kukodisha ndege na fedha za matengenezo kwa viwango vilivyoainishwa kwenye mikataba husika.

Katika ukaguzi wa makubaliano hayo nilibaini kuwa, TGFA ilitoa bili kwa ATCL za kiasi cha Sh. 191,185,465,739.20, ikiwa gharama ya kukodi ndege na fedha ya akiba ya matengenezo kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2016 hadi

2022. Hata hivyo, TGFA ilipokea jumla ya Sh. 3,000,225,100.32 kutoka ATCL, huku jumla ya Sh. 188,185,240,638.88 ikiwa haijalipwa hadi kufikia tarehe 30 Juni 2022. Kiasi hicho ambacho hakijalipwa kinajumisha Sh. 111,162,778,092.14 ya gharama za kodi na Sh. 77,022,462,546.74 ya fedha za akiba za matengenezo.

Kutolipwa kwa Sh. 188,185,240,638.88 na ATCL kunahatarisha sana uendeshaji wa TGFA, kwani inaweza kuifanya TGFA kushindwa kugharamia shughuli zake za uendeshaji za kila siku na kushindwa kuhakikisha ATCL inafanya matengenezo makubwa (C checks) kwenye ndege hizo baada ya kufikisha masaa ya kuruka yanayohitajika chini ya muongozo wa mpango wa matengenezo ya ndege. Kushindwa kufanya matengenezo baada ya ndege hizo kufikisha muda unaotakiwa kunaweza kusababisha ndege hizo kuzuiliwa kuruka, jambo ambalo litakuwa na madhara makubwa katika sekta ya ndani ya anga, ukizingatia ushawishi mkubwa wa ATCL ndani ya sekta hiyo.

Ili kutatua hali hiyo, TGFA ilieleza kuwa Serikali imechukua hatua kwa kuteua timu huru mnamo tarehe 29 Agosti 2022. Timu hii ilitakiwa kupitia upya masharti ya mikataba ya ukodishaji kati ya ATCL na TGFA, kuchunguza changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa mikataba hiyo, na kutoa mapendekezo ya utekelezaji wa mikataba hiyo.

Hivyo, naishauri Serikali kuhakikisha ATCL inaweka utaratibu utakaowezesha Shirika hilo kulipa deni tajwa la kiasi cha Sh. 188,185,240,638.88 na kuharakisha mchakato wa kupitia upya viwango vilivyopo kwa mujibu wa mikataba husika.

11.4 Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA)

Wakala ilianzishwa chini ya mamlaka ya Sheria ya Wakala za Serikali (Sura ya 245) kwa ajili ya kutoa huduma za Umeme, Mitambo na Elektroniki, Huduma za vivuko pamoja na Ukodishaji Mitambo kwa taasisi za serikali na Umma kwa ujumla. Ukaguzi nilioufanya juu ya shughuli za TEMESA ulibaini upungufu ufuatao:

11.4.1 Upotevu wa Mapato Unaotokana na Utoaji wa Idhini ya Matengenezo ya Magari ya Serikali kwenye Karakana Binafsi – Sh. Bilioni 4.58

Kifungu Na. 3.3 cha Wakala (Wakala wa Huduma za Umeme, Mitambo na Elekitroniki Tanzania), Agizo la Uanzishwaji la mwaka, 2005 linaeleza kuwa dhamira ya TEMESA ni kutoa huduma za uhandisi wa Umeme, Mitambo na Kieletroniki kwa taasisi za Serikali na Umma kwa ujumla, kwa ufanisi na kuongeza tija.

Hata hivyo, nilivyopitia taarifa za utendaji kazi wa Wakala kuanzia tarehe 1 Julai 2021 hadi 30 Juni 2022 nilibaini kuwa Ofisi za TEMESA Mkoa wa Dodoma na Tabora zilipokea jumla ya maombi 5,771 ya matengenezo ya magari kutoka taasisi mbalimbali za Serikali. Kati ya maombi hayo, TEMESA iliweza kufanya matengenezo ya magari 4,210, huku matengenezo ya magari 1,561 yenye thamani ya Sh. 4,582,734,851.12 yalielekezwa kwenye karakana binafsi.

Aidha, nilibaini kuwa sababu ya kuhamisha matengenezo ya magari ya serikali kwa karakana za kibinafsi ilisababishwa na uhaba wa vifaa vya kiufundi katika karakana za TEMESA, idadi ndogo ya mafundi wa magari, elimu duni ya kiufundi katika kufanya matengenezo magari ya kisasa yenye teknolojia ya juu, na ongezeko kubwa la madeni ya wasambazaji wa vipuri, hali ambayo imeweka ugumu kwa Wakala kupata vipuri kwa mkopo. Kwa maoni yangu, uamuzi wa kuidhinisha matengenezo ya magari 1,561 kwenye karakana binafsi ulisababisha hasara ya Sh. 4,582,734,851.12 kwa TEMESA. Upotevu huu wa mapato unaweza kusababisha wakala kushindwa kujiendesha na kutegemea zaidi ruzuku ya serikali.

Ninapendekeza TEMESA kushughulikia changamoto za kiutendaji kwa kuhakikisha karakana zinakuwa na vifaa vya kutosha vya kiufundi; wataalamu wa kutosha wa ufundi wa magari; kuwaongezea ujuzi wa kiufundi wafanyakazi ili kuendana na maendeleo ya kiteknolojia katika tasnia ya magari; na kulipa madeni ya wasambazaji kwa wakati ili kusaidia kujenga uhusiano mzuri.

11.4.2 Hatari Zinazohusishwa na Kushindwa Kushughulikiwa kwa Mapungufu Katika Uendeshaji wa MV Pangani Yaliyoripotiwa na TASAC

Kanuni ya 20 (2) ya Kanuni za Usafirishaji wa Meli, 2006 inaitaka TASAC kufanya uchunguzi au kipimo na kutoa cheti cha kubainisha uzito na muundo wa meli na maelezo mengine yanayoelezea utambulisho wa meli.

Kwa mujibu wa mamlaka iliyotajwa hapo juu, TASAC ilipitia uendeshaji wa MV Pangani tarehe 19 Agosti 2021. Katika mapitio haya, masuala kadhaa muhimu yalibainishwa ambayo yanahatarisha usalama wa abiria na wafanyakazi kama ifuatavyo:

a) Kivuko kimekuwa kikifanya kazi bila Cheti cha Kuthibitisha Usalama Baharini (Sea Worthiness Certificate), hivyo usalama wa kivuko hauwezi kuthibitishwa, na inaiweka kivuko kwenye hatari ya ajali, hitilafu ya vifaa na hatari nyinginezo za uendeshaji.
b) Mabaharia wote wanaoendesha kivuko hicho walishindwa kuonesha vyeti vyao, na hili linathibitisha kuwa wafanyakazi wa kivuko hicho huenda hawana taaluma ya uendeshaji vivuko.
c) Jenereta mbili zilizokuwemo kwenye kivuko hazikuwa zikizalisha umeme wa kutosha kuendesha injini za propela za Azimuth, na hivyo kusababisha chombo kushindwa kujiendesha jinsi ilivyokusudiwa, jambo ambalo linaweza kusababisha ucheleweshaji, ufanisi mdogo na hatari za kiusalama.
d) Magati mawili ya kushukia na kuegesha Kivuko yanafanya kazi kwa kutegemea nguvu kazi ya mikono na sio kwa njia ya umeme, na kuifanya iwe vigumu kuinua na kushusha magati kwa usawa unaofaa kutegemea na ujazo wa maji katika sehemu ya maegesho. Magati haya yaliwekwa katika sehemu isiyobadilika iliyo chini ya usawa wa chini wa Kivuko, ambapo inahatarisha usalama wa uendeshaji wa Kivuko.
e) Vyumba vinavyounda sehemu kuu ya chini ya Kivuko havikutenganishwa mara mbili, vilikua vikubwa na havikugawanywa kupunguza athari ya eneo kubwa la wazi kama itatokea athari ambayo haitambuliki.

Hata hivyo, tarehe 12 Agosti 2022, nilifanya ziara ya kikaguzi katika kituo cha Feri, Pangani na kubaini kuwa TEMESA haikuwa imechukua hatua yoyote kushughulikia udhaifu wa uendeshaji wa MV. Pangani ulioripotiwa na TASAC.

Udhaifu huu umesababisha hatari kubwa ya usalama wa abiria na wafanyakazi kwa kipindi cha mwaka mzima tangu ripoti ya TASAC ilipotolewa na bado athari hiyo inaendelea kuwapo mpaka TEMESA itakapochukua hatua stahiki. Kulingana na ukaguzi wangu, inaonekana kuwa kuchelewa kwa TEMESA kutatua madhaifu hayo kulisababishwa na kutokuwepo kwa hatua mahususi za usalama kwenye vivuko. Ikiwa hatua za haraka hazitachukuliwa, kuna hatari kubwa ya kupoteza maisha ya abiria na mabaharia.

Ninapendekeza TEMESA kuchukua hatua za haraka kushughulikia udhaifu ulioripotiwa na kuboresha hatua za usalama kwenye vivuko. Ni muhimu pia kwamba TEMESA itengeneze mpango wa kina wa kushughulikia masuala yoyote ya usalama yatakayobainishwa katika siku zijazo na kufuatilia mara kwa mara ili kuhakikisha usalama endelevu kwa abiria na wafanyakazi wote.

11.4.3 Matumizi Yasioridhisha ya Magari Maalumu ya Karakana Yaliyonunuliwa Sh. Milioni 494.81

Tarehe 28 Februari 2020, Wakala wa Huduma za Umeme, Mitambo na Elektroniki (TEMESA) iliingia mkataba Na. AE/006/2019-2020/HQ/G/CN-25 na M/s TATA Africa Holdings (T) Ltd kwa ajili ya kusambaza magari sita yenye karakana kwa bei ya mkataba ya Sh. 494,814,000. Magari haya yaliwekwa kifaa maalumu (canopy) kwa ajili ya zana za matengenezo, vilainishi, na vifaa ili kurahisisha huduma za matengenezo kwa wateja walio mbali bila kuhitaji kupeleka magari yao kwenye karakana za TEMESA. Mzabuni aliwasilisha magari hayo yenye karakana tarehe 18 Januari 2021, na yalisambazwa katika ofisi sita za mikoa ya Mbeya, Tabora, Dodoma, Mwanza, Arusha na Mtwara.

Katika ukaguzi wangu nilioufanya mwezi Agosti 2022, nilibaini kuwa kati ya magari sita yenye karakana yaliyowasilishwa na M/s TATA Africa Holdings (T) Ltd kwa TEMESA mnamo mwezi Januari 2021, matano kati ya hayo yalikuwa hayajatumika kwa muda wa mwaka mmoja na nusu. Huku, ni gari moja tu, ambalo lilipelekwa katika ofisi ya Mwanza, ndilo ambalo lilifanya kazi mara mbili tu katika kipindi hicho na kuingiza makusanyo ya Sh. 300,000 pekee. Hii ikimaanisha magari haya yenye karakana hayakutumika kama ilivyokusudiwa.

Aidha, nilibaini kuwa sababu za kutotumika kwa magari hayo yenye karakana ni kutokana na TEMESA kushindwa kufanya uchambuzi wa uwekezaji ili kutathmini gharama na faida kabla ya kununua magari hayo. Kukosekana kwa uchambuzi huo wa kina, TEMESA inaweza kupata hasara ya Sh. 494,814,000 ambazo tayari zimewekezwa katika mradi huo. Pia, bila ya hatua za haraka kuchukuliwa, TEMESA inaweza kupata hasara zaidi kutokana na uchakavu wa magari hayo yenye karakana kwa muda ambao yanaendelea kukaa bila kutumika kikamilifu.

Ninapendekeza TEMESA kufanya uchambuzi wa kina wa uwekezaji kabla ya kununua mitambo na mashine. Pia, kuandaa mpango wa matumizi na ratiba za matengenezo ya mara kwa mara, na kutathmini matumizi mbadala ya magari haya ikilazimika.

11.5 Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS)

Wakala ulianzishwa ili kutengeneza, kudumisha na kusimamia mtandao wa barabara kuu na za mikoa kwa gharama nafuu, salama na mazingira endelevu sambamba na mkakati wa kupunguza umaskini na sera nyingine za Serikali kupitia nguvu kazi yenye uwezo na motisha. Katika ukaguzi wa TANROADS nilibaini mapungufu kadhaa katika usimamizi wa miradi ya ujenzi wa barabara kama ilivyoainishwa hapa chini

11.5.1 Hasara Iliyotokana na Kutorekebisha Hitilafu za Mapema za Barabara katika Barabara ya Ndundu – Somanga (Km 60) – Sh. Bilioni 7.24

Tarehe 30 Juni 2008, Wizara ya Ujenzi (iliyokuwa Wizara ya Maendeleo ya Miundombinu) iliwapatia mkataba M/s Mohamed Abdulmohsin Al-Kharafi na Wana wa Safat – Kuwait, kwa ajili ya kuboresha Barabara ya Ndundu – Somanga (Km 60) kwa jumla ya mkataba wa Sh. 75,727,952,725.56. Mkataba ulikamilika kwa kiasi kikubwa tarehe 26 Februari 2015, na Kipindi cha uangalizi kilipangwa kumalizika tarehe 26 Februari 2016 (cheti cha ukamilishaji wa kazi za ujenzi hakijatolewa hadi sasa). Huduma ya usimamizi wa mkataba huu ilitolewa na M/s Engineering Systems Group (K.S.C.C) ya Kuwait kwa kushirikiana na M/s Mouchel ParKman Services Ltd na M – Konsult Ltd ya Tanzania, hadi mshauri alipojiondoa mnamo tarehe 08 Juni 2014.

Katika mwaka wa fedha wa 2018/19, nilibaini kuwa mkandarasi aliyetajwa hapo juu alikuwa kwenye eneo la mradi akifanya kazi za kurekebisha hitilafu za mapema za barabara zilizojitokeza katika kipindi cha matazamio. Ukaguzi wangu wa ripoti ya uchunguzi iliyotolewa na Maabara Kuu ya Vifaa vya Ujenzi (CML) nilibaini kuwa hitilafu za mapema za barabara zilitokana na sababu mbalimbali kama vile ubovu wa lami, mchanganyiko wa lami usiokidhi vigezo, matumizi ya kokoto za kiwango duni katika tabaka la chini, na tabaka la lami kushindwa kustamili.

Hata hivyo, katika ukaguzi wangu mwezi Novemba 2022, niligundua kuwa mkandarasi husika alitelekeza kazi ya kurekebisha hitilafu hizo mnamo mwezi Desemba 2019, licha ya kupokea jumla ya Sh. 75,727,952,725.56 kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo ambayo ilibainika kuwa chini ya kiwango. Kutokana na hali hiyo, TANROADS ililazimika kumpatia mkandarasi mpya, Mtwivila Traders & Construction Ltd, kazi ya kukamilisha marekebisho yaliyobakia kwa gharama ya Sh. 7,821,306,000 kwa kutumia fedha za Bodi ya Mfuko wa Barabara (RFB). Hadi wakati wa ukaguzi wangu mwezi Novemba 2022, TANROADS ilimlipa mkandarasi huyu mpya jumla ya Sh. 7,242,684,717.98.

Kutokana na madhaifu hayo, ninaamini kuwa usimamizi hafifu wa mradi katika utekelezaji wa kazi za ujenzi na urekebishaji wa hitilafu zilizobainika ulisababisha kwa kiasi kikubwa ujenzi usiokidhi vigezo na kutelekezwa kwa kazi za marekebisho ya hitilafu za ujenzi duni na mkandarasi husika. Hivyo, kusababishia walipakodi kupata hasara ya Sh. bilioni 7.24 katika malipo yaliyotolewa kwa mkandarasi mpya ili kumalizia kazi za marekebisho ya hitilafu hizo. Hasara hii ingeweza kuepukwa kama kungekuwepo na usimamizi mzuri kuanzia mwanzo wa mradi.

Kwa kuzingatia hayo hapo juu, napendekeza TANROADS kurejesha gharama ya ukarabati wa hitilafu za barabara kutoka kwa mkandarasi na mshauri mwelekezi aliyehuska na ujenzi ulio chini ya kiwango. Zaidi ya hayo, kuimarisha udhibiti wa ndani wa usimamizi wa mikataba ili kuzuia upotevu kama huo wa fedha za walipa kodi katika siku zijazo.

11.5.2 Kutorejeshwa kwa Malipo ya Ziada Kutoka kwa Mkandarasi – Sh. Bilioni 1.4

Tarehe 14 Desemba 2017, TANROADS (Ofisi ya Mkoa wa Manyara) ilisaini mkataba (AE/001/2016/2017/MNR/CONT/W/33) na Kampuni ya M/s China Railway Seventh Group, kwa ajili ya Ujenzi wa Daraja la Magara (mita 84.0) na barabara zake (kilomita 4.0) kando ya Barabara ya Mbuyu wa Mjerumani Mbulu, kwa bei ya mkataba wa Sh. 12,772,704,234.27 (iliyoongezwa). Kipindi cha uangalizi wa mkataba huu kilimalizika tokea tarehe 20 Mei 2021.

Wakati wa mapitio ya Hati za Malipo ya Muda (IPCs) na Vocha ya Malipo Na.00009939 ya tarehe 23 Februari 2022 kuhusiana na mkataba hapo juu, nilibaini kuwa TANROADS ilimlipa mkandarasi malipo ya ziada ya Sh. bilioni 1.4 ambayo yalitokana na riba ya ucheleweshaji wa malipo pamoja na marekebisho ya bei za mradi kutokana na mabadiliko ya muda (price adjustment). Malipo haya ya ziada ni kama yalivyoelezewa hapa chini:

- Kwa kuzingatia Kifungu cha 17 cha Masharti Maalumu ya Mkataba, kiwango cha riba kitakachotumika kwa ucheleweshaji wa malipo kinapaswa kuwa kiwango cha jumla cha riba ya amana kwa miezi mitatu kutoka Benki Kuu ya Tanzania (BOT) kutoka muda ulioainishwa kwaajili ya malipo. Hata hivyo, baada ya kupitia Hati za Malipo ya Muda Na. 1 mpaka 9 nilibaini kuwa mkandarasi alilipwa tozo ya riba ya Sh. 2,263,907,362.88 kwa kucheleweshа malipo yake ambapo riba hii ilipatikana kwa kutumia kiwango cha riba ya jumla ya ukopeshaji kutoka BOT.

  Hata hivyo, kiasi hicho kilicholipwa kinatofautiana na sharti la Kifungu cha 17 la kutumia kiwango cha riba ya amana ya muda wa miezi mitatu kutoka BOT, ambacho kingetumika kingesababisha mkandarasi kulipwa Sh. 966,921,619.14, na tofauti hiyo ilisababisha malipo ya ziada ya Sh. 1,296,985,743.74.

- Zaidi ya hayo, Kifungu cha 20 cha Masharti Maalumu ya Mkataba kinasema kuwa Mkataba unaruhusu marekebisho ya bei kutokana na muda (price adjustment) kwa mujibu wa Kifungu cha 49 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba. Hata hivyo, ukaguzi wangu wa Hati ya Malipo ya Muda Na. 10 (IPC) ulibaini kuwa TANROADS ilimlipa mkandarasi

gharama za marekebisho ya bei ya Sh. 910,779,863.18 kwa kutumia takwimu za bei zisizo sahihi badala ya Sh. 810,037,784.44 ambazo zingeweza kulipwa kwa kutumia takwimu sahihi, hivyo basi kusababisha malipo ya ziada ya Sh. 100,742,078.74.

Kutokana na malipo hayo ya ziada, TANROADS imekiri kuwa malipo hayo yalitokana na makosa ya mapitio ya hati za malipo na imemuelekeza mkandarasi kurejesha kiasi hicho. Hata hivyo, nina mashaka kuwa TANROADS inaweza kushindwa kurejesha kiasi cha malipo ya ziada kwa vile muda wa matazamio ya kasoro kwenye mkataba umeisha tangu tarehe 20 Mei 2021, ikiashiria kukamilika kwa mradi. Tatizo hili kimsingi limesababishwa na uhakiki usiotosheleza wa hati za malipo ya muda yaliyowasilishwa na mkandarasi, jambo ambalo linaweza kusababisha upotevu wa fedha za walipakodi.

Ninapendekeza TANROADS iimarishe udhibiti wa ndani wa uhakiki wa hati za malipo ya muda kabla ya kufanya malipo. Pia, kuhakikisha kiasi cha malipo ya ziada kinarejeshwa kutoka kwa Mkandarasi husika.

11.5.3 Riba Iliyotokana na Kuchelewa kwa Malipo ya Wakandarasi na Washauri katika Miradi ya Ujenzi wa Barabara – Sh. Bilioni 36.86

Kwa mujibu wa Kifungu cha 54 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba, Mwajiri analazimika kumlipa Mkandarasi kiasi kilichoidhinishwa na Meneja wa Mradi ndani ya siku 28 kuanzia tarehe ya kila Hati ya Madai. Katika mikataba chini ya muundo wa FIDC, tarehe ya malipo inaongezwa hadi siku 56 baada ya kuwasilishwa kwa madai ya mkandarasi. Ikiwa Mwajiri amechelewesha malipo, Mkandarasi ana haki ya kupokea riba kwa ucheleweshaji malipo hayo, ambayo yatajumuishwa katika hati ya madai inayofuata.

Hata hivyo, mapitio yangu ya hati za malipo na bili za madai nilibaini kuwa wakandarasi na washauri kadhaa wamedai riba ya malipo yaliyocheleweshwa, ambayo ni Sh. 36,860,022,478.59 hadi kufikia tarehe 30 Juni 2022. TANROADS tayari imelipa jumla ya Sh. 18,850,878,721 kati ya deni hilo, huku kiasi kilichobaki cha Sh. 18,009,236,260.22 hakikulipwa hadi tarehe 30 Juni 2022. Riba hii ambayo haijalipwa inaendelea kuongezeka mpaka pale tu malipo yatakapofanyika.

Katika ripoti yangu ya mwaka wa fedha 2020/21 nilionesha kuwa ucheleweshaji wa kulipa madeni hayo umetokana na upatikanaji usioridhisha wa fedha kutoka serikalini na zaidi kwa miradi inayofadhiliwa moja kwa moja au kiasi na Serikali. Tatizo hili linaendelea kuwaongezea mzigo walipa kodi, mpaka pale hatua za haraka zitakapochukuliwa kutokomeza riba hizo.

Hivyo, narudia pendekezo langu la mwaka uliopita kuwa Wizara ya Fedha na Mipango, itengeneze mikakati na sera za kuhakikisha kuwa madeni hayo yanalipwa ndani ya muda uliokubaliwa kimkataba. Zaidi ya hayo, ni muhimu kwa Serikali kuweka kipaumbele katika kulipa madeni ya nyuma kabla ya kuingia kwenye miradi mipya.

11.5.4 Kushindwa Kutoa Zabuni za Miradi ya Ujenzi wa Barabara – Sh. Trilioni 2.91

Kifungu cha 49(1 na 2) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma, 2011 kinataka Mpango wa Manunuzi wa Mwaka uidhinishwe na mamlaka ya kuidhinisha bajeti na taasisi zinazofanya manunuzi kuzingatia mipango iliyoidhinishwa ya manunuzi ya mwaka.

Kwa mujibu wa Mpango wa Manunuzi wa Mwaka ulioidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2021/22, TANROADS ilipanga kutekeleza miradi 88 ya barabara kwa kutumia bajeti iliyotengwa ya Sh. 2,914,813,070,000 inayofadhiliwa na serikali. Hata hivyo, hadi kufikia tarehe 30 Juni 2022, TANROADS ilitoa zabuni kwa kandarasi moja tu huku ikiacha zabuni za miradi 87 ya barabara yenye thamani ya Sh. 2,914,113,070,000 (99.9%) hazijatolewa kama ilivyoainishwa kwenye mpango wa mwaka wa manunuzi.

Aidha, nilibaini kuwa sababu kuu ya dosari hii ni kuchelewa kwa mchakato wa manunuzi, pamoja na kuchelewa kupata kibali cha kutangaza zabuni ya miradi husika kutoka Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Ujenzi). Ninaamini kuwa kushindwa kutangaza na kutoa zabuni za miradi hii kunanyima fursa walipakodi kupata miundombinu ya barabara.

Napendekeza TANROADS kuharakisha mchakato wa ununuzi na uidhinishaji ili kuhakikisha utekelezaji wa miradi ya barabara kwa wakati.

11.5.5 Matengenezo na Uboreshaji wa Barabara Ambazo Zipo Nje ya Mamlaka ya TANROADS – Sh. Bilioni 10.75

Agizo 3.1 la Agizo la Wakala wa Utendaji (Wakala wa Barabara Tanzania) (Uanzishwaji) (Marekebisho) 2020, linaeleza kuwa "lengo la TANROADS ni kusimamia matengenezo na uendelezaji wa gharama nafuu wa Mtandao wa Barabara kuu, Mikoa na Viwanja vya Ndege, ili kusaidia maendeleo endelevu ya kiuchumi Tanzania. Utekelezaji wa shughuli zake utaongozwa na lengo hili".

Hata hivyo, niligundua kuwa TANROADS imekuwa ikifanya matengenezo na uboreshaji wa barabara 49, zikiwemo barabara za Wilaya, barabara za Mjini, barabara za Miji, na barabara za jamii, ambazo haziko kwenye mamlaka yake kinyume na matakwa yaliyotajwa hapo juu ya kusimamia tu barabara kuu na za mikoa. Kutokana na hali hiyo, katika mwaka wa fedha 2021/22, TANROADS ilitumia fedha za matengenezo jumla ya Sh. 10,747,118,104 kufanya matengenezo na uboreshaji wa barabara 49 ambazo hazikuwa chini ya mamlaka yake. Hatua hii imekuwa na athari kubwa katika utekelezaji wa shughuli zilizoidhinishwa za matengenezo ya barabara kuu na za mikoa, kwani fedha zilizotolewa na Bodi ya Mfuko wa Barabara (RFB) zilihamishwa kwa shughuli zisizohusiana.

Kwa kuzingatia hayo, TANROADS imekiri kuwa suala la kufanya shughuli za matengenezo ya barabara ambazo haziko chini ya mamlaka yake limefikishwa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi – Ujenzi kwa ajili ya kupatiwa mwongozo. Hata hivyo, naamini kuwa TARURA, kama taasisi yenye dhamana, ina rasilimali za kutosha kwa upande wa wafanyakazi na fedha za kusimamia matengenezo ya barabara 49, TANROADS inapaswa kusitisha shughuli zake za matengenezo ya barabara hizo na kutenga fedha husika kwa ajili ya shughuli za matengenezo ya barabara kuu na za mikoa zilizoidhinishwa.

Napendekeza TANROADS na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Ujenzi) kusitisha matengenezo ya barabara 49 ambazo hazipo chini ya mamlaka ya TANROADS. Aidha, kuwasiliana na Wizara ya Fedha na Mipango ili kuhakikisha kuwa kiasi cha Sh. bilioni 10.75, ambacho kilitumika kwa ajili ya matengenezo ya barabara hizo ambazo ziko nje ya mamlaka ya

TANROADS, kinarejeshwa, na kupelekwa katika shughuli za matengenezo ya barabara zilizoathirika na ukosefu wa fedha.

11.5.6 Usimamizi Usioridhisha wa Uendeshaji wa Vituo vya Mizani ya Kupima Uzito wa Magari

Agizo 3.6 (e) la Wakala wa Utendaji (Wakala wa Barabara Tanzania) (Uanzishwaji) (Marekebisho) Agizo la 2020 linaipa TANROADS mamlaka ya kuanzisha na kuendesha mizani na kutekeleza udhibiti uzidishaji wa uzito wa mizigo katika mtandao wa barabara ulio chini ya mamlaka yake. Wakati wa mapitio ya shughuli za mizani, nilibaini madhaifu kadhaa yanayohitaji umakini wa usimamizi, ikiwa ni pamoja na:

(a) Wasafirishaji 153 Walitumia Kibali Kimoja Maalumu kwa Safari Zaidi ya Moja

Kanuni ya 15 (1) (a) ya Kanuni za Udhibiti wa Uzidishaji wa Mizigo ya Magari ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (Mizigo Maalumu) ya mwaka 2018 inaeleza kuwa mtu atatenda kosa kwa mujibu wa Sheria na Kanuni hizi iwapo atasafirisha mzigo wowote maalumu bila kibali halali. Pia, Kifungu cha 9 (3) cha Sheria ya Udhibiti wa Mizigo ya Magari ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2016 kinataka gari linalobeba mizigo yoyote iliyoainishwa katika kifungu kidogo cha (1) bila kibali maalum kusimamishwa na kuzuiliwa na afisa aliyeidhinishwa.

Hata hivyo, nilivyopitia taarifa za kielektroniki za mizani kutoka vituo vya Himo 2, Mikumi, na Mikese kuanzia tarehe 1 Julai 2021 hadi 30 Juni 2022, nilibaini kesi 153 ambapo wasafirishaji walikuwa wametumia vibali vinavyofanana (nambari za kumbukumbu zinafanana) kwa zaidi ya safari moja.

(b) Magari 119,899 Yalipita Kwenye Mizani Bila Kupimwa Kutokana na Usimamishaji wa Shughuli za Mizani Mara kwa Mara

Kifungu cha 8 (1) cha Sheria ya Udhibiti wa Mizigo ya Magari ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2016 kinamtaka msafirishaji anayeendesha gari lenye uzito wa kilogramu 3,500 au zaidi atawasilisha gari hilo kupimwa katika kila kituo cha mizani kilichopo kwenye Mtandao wa Barabara ambao gari husika linapita.

Hata hivyo, nilibaini kuwa kuanzia tarehe 01 Julai 2021 hadi 30 Juni 2022, vituo 13 vya mizani vilifungwa mara kwa mara, kwa jumla ya siku 612. Hivyo kusababisha magari 119,899 yenye uzito wa zaidi ya kilogramu 3,500 kupita vituo vya mizani bila kupimwa.

(c) Magari 27 Yaliyozidisha Uzito Yaliachiwa Bila Kulipia Tozo Stahiki ya Kuzidisha Uzito na Bila Kupunguza Uzito Uliozidi – Sh. milioni 98.12

Kanuni ya 13 (1) ya Kanuni za Udhibiti wa Mizigo kwenye Magari ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (Hatua za Utekelezaji) za mwaka 2018 inataka gari lililokuwa limepakia uzito wa ziada kuzuiliwa na kuwekwa kizuizini hadi msafirishaji atakapolipa ada ya uzidishwaji wa mizigo.

Hata hivyo, nilibaini kuwa kuanzia tarehe 1 Julai 2021 hadi 16 Septemba 2022, TANROADS Tanga iliachia magari 27 yaliyozidisha uzito bila kukusanya tozo ya uzidishaji uzito ya kiasi cha Sh. 98,125,374. Zaidi ya hayo, wasafirishaji hao waliozidisha uzito hawakutakiwa kupunguza uzito wa ziada kabla ya kuendelea na safari.

Nilibaini kuwa madhaifu yaliyoelezewa hapo juu yametokana na uendeshaji usioridhisha wa mizani pamoja na hitilafu katika vifaa vya kupimia uzito. Kuruhusu udhaifu huu kuendelea kunaweza kusababisha uharibifu mkubwa katika tabaka la lami la barabara na madaraja.

Napendekeza TANROADS iboreshe usimamizi na ufuatiliaji wa shughuli za mizani, kutunza vifaa vya kupimia mizani, kuhakikisha uendeshaji endelevu wa vituo vya mizani, kushikilia magari ya wasafirishaji wanaotumia kibali maalumu kwa safari zaidi ya moja, kushikilia magari yaliyozidisha uzito hadi ada zilipwe na mzigo wa ziada kupunguzwa, na kuwa na mfumo wa kufuatilia matumizi ya vibali maalum

11.6 Wakala wa Ununuzi wa Mafuta kwa Pamoja (PBPA)

PBPA ni Wakala wa Serikali ulioanzishwa chini ya Sheria ya Wakala Tendaji kupitia GN. Namba 423 ya tarehe 25 Septemba 2015. Kama ilivyoainishwa kwenye kanuni, Wakala umepewa mamlaka ya kusimamia uingizaji wa

bidhaa za petroli nchini. Ukaguzi wangu wa shughuli za PBPA nilibaini mapungufu yafuatayo:

11.6.1 Gharama ya Ziada Iliyotokana na Ucheleweshaji wa Kupakua Mafuta kutoka kwenye Meli (Demurrage) zinazoathiri Watumiaji wa Mwisho – Dola za Marekani milioni 13.91 (Sh. Bilioni 32.07)

Demurrage ni ada inayotozwa kwa mnunuzi wa mzigo kama amesababisha uchelewaji wa ushushaji wa mzigo kwenye meli kuendana na muda ulioainishwa kwenye mkataba. Pia, Demurrage inaweza tozwa kwenye shirika la meli au msambazaji kama ndio aliyehusika kwenye ucheleweshaji wa ushushaji wa mzigo kwenye meli.

Kifungu cha 17.1 cha mikataba kati ya Wakala wa Ununuzi wa Mafuta kwa Pamoja (PBPA) na Wazabuni kinataka muda wa kushusha mafuta uwe ni saa 72 na saa 36 kwa shehena nzima itakayotolewa kwenye SBM, Dar es Salaam na KOJ, mtawalia kutoka kwa Notisi ya utayari wa zabuni.

Aidha, kifungu cha 18.1 cha mkataba kinamtaka msambazaji awe na haki ya kutoza malipo ya chini ya Dola za Marekani 22,000 na Dola za Marekani 18,000 kwa siku kwa mafuta. Gharama za kucheleweshaji ushushaji wa mafuta hutozwa kwa mwagizaji bidhaa isipokuwa kama zimesababishwa na Kampuni za Uuzaji wa Mafuta (OMCs) au mtoa huduma.

Mapitio yangu ya ripoti ya ucheleweshaji wa ushushaji wa mafuta ya mwaka wa fedha 2021/22 yalionesha kuwa mzabuni alitoza waagizaji mafuta jumla ya Dola za Marekani 13,916,834.34 (Sh. 32,067,118,193.94) kama ada ya kusababisha uchelewaji wa ushushaji wa mafuta. Hata hivyo, mapitio zaidi yalibaini kuwa tozo hizo ni moja ya mambo yanayozingatiwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) wakati wa kuainisha bei ya kikomo ya mafuta. Kutokana na hali hiyo, ongezeko la bei za mafuta iliyotokana na ucheleweshaji wa ushushaji wa mafuta kwa jumla ya Dola za Marekani 13,916,834.34 (Sh. 32,067,118,193.94) ulihamishiwa kwa watumiaji wa mwisho, yaani umma kwa ujumla.

PBPA ilieleza kuwa tozo hizo za ucheleweshaji wa ushushaji wa mafuta kwenye Mfumo wa Mafuta ya Pamoja, imesababishwa zaidi na miundombinu duni ya kupokea bidhaa za petroli kutoka kwenye meli. Licha ya ongezeko

la mahitaji ya mafuta kutoka kiwango cha juu cha tani 250,000 mwaka 2012 hadi viwango vya mahitaji ya sasa ya tani 650,000, miundombinu imebaki vile vile. Zaidi ya hayo, mabomba ya petroli yanayotumiwa kusafirisha mafuta yamechakaa, na hivyo kulazimika kupunguzwa kwa nguvu ya kusukuma mafuta ili kuzuia uharibifu mkubwa. Sababu nyingine inayochangia ni muda unaochukuliwa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) kufanya uhakiki wa ubora wa mafuta katika mikoa ya Tanga na Mtwara ambao ni kati ya saa 12 hadi 24. Ucheleweshaji huu pia unazingatiwa katika muda unaotumiwa na vyombo vya usafiri wa majini kusafirisha mizigo kulingana na Mkataba.

Kwa hiyo, napendekeza Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Uchukuzi) kupunguza changamoto za uendeshaji wa ushushaji wa mafuta ya petroli na kuboresha miundombinu ili kupunguza tozo za ucheleweshaji wa ushushaji wa mafuta.

11.7 Wakala wa Mbegu za Kilimo (ASA)

ASA ilianzishwa chini ya Sheria ya Wakala za Serikali [Sura.245]. Wakala ilizinduliwa Juni 2006 kama chombo kinachojiendesha chini ya Wizara ya Kilimo. Lengo la kuanzisha ASA ni kuhakikisha mbegu bora za kilimo zinapatikana kwa wakulima na kwa bei nafuu. Wakati wa ukaguzi wa ASA, nilibaini mapungufu yafuatayo:

11.7.1 Kutotumika kwa Ardhi Yenye Rutuba kwa Uzalishaji wa Mbegu - Hekta 7,528.67

Kwa mujibu wa Aya ya 2.2.1 ya Mpango Mkakati wa Wakala, Wakala wa Mbegu za Kilimo (ASA) unaendesha shughuli za uzalishaji wa mbegu Tanzania nzima kwa kutumia mashamba yake 10 yaliyopo Kanda zote za Kilimo-Ekolojia, yenye jumla ya hekta 13,206.6, kati ya hizo hekta 10,193.6 ndizo zinarutuba ikiwa ni asilimia 77 ya eneo lote la ardhi.

Hata hivyo, nilivyopitia Taarifa ya Utendaji wa Uzalishaji kwa mwaka fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2022, nilibaini kuwa ni hekta 2,664.93 tu za mashamba ndio inayotumika kwa ajili ya uzalishaji wa mbegu, na zilizosalia hekta 7,528.67 (sawa na asilimia 74 ya mashamba yenye rutuba) haitumiki. Ninaamini kuwa uhaba wa rasilimali fedha unasababisha kutotumika kwa

ardhi hii na inaweza pia kusababisha jamii kuvamia ardhi hiyo ya Wakala kwa matumizi binafsi.

Ninapendekeza kuwa ASA ichukue hatua madhubuti kuhakikisha kuwa hekta 7,528.67 zilizosalia zinatumika katika uzalishaji wa mbegu ili kuepuka uvamizi, migogoro ya ardhi na upotevu wa rasilimali.

11.8 Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA)

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) ilianzishwa kwa kifungu cha 4(1) cha Sheria ya Mamlaka ya Hali ya Hewa. Ikiwa na jukumu la kuratibu, kudhibiti na kutoa huduma za hali ya hewa zinazopatikana katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ukaguzi wangu kuhusu uendeshaji wa TMA umebaini mapungufu yafuatayo:

11.8.1 Kuchelewa kwa Ugavi, Usimikaji, Upimaji na Kamisheni ya Rada ya Hali ya Hewa - Dola za Marekani milioni 4.99 (Sh. Bilioni 11.43)

Tarehe 10 Aprili 2019, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) iliingia mkataba na Mzabuni, kwa ajili ya Ugavi na usimikaji wa Rada ya Hali ya Hewa katika miji ya Mbeya na Kigoma. Mkataba huo ulikuwa na bei ya Dola za Marekani 4,994,230 (Sh. 11,434,634,686.29) na ulitarajiwa kukamilika ifikapo tarehe 30 Novemba 2022 (kuboreshwa).

Hata hivyo, uhakiki wangu umebaini kuwa mzabuni bado hajawasilisha na kusimika rada hiyo, licha ya muda wa mkataba kuisha. Ucheleweshaji huu umetokana na usimamizi duni wa mkataba na unaweza kuathiri utekelezaji wa lengo lililokusudiwa kwa wakati.

Ninapendekeza Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania kuchukua hatua za kimkataba dhidi ya mzabuni kwa kuchelewa kuleta na kusimika Rada ya Hali ya Hewa. Aidha, Mamlaka inapaswa kuboresha usimamizi na ufuatiliaji wa mikataba ili kuhakikisha ufanisi katika miradi ya baadaye.

11.9 Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS)

Wakala iliundwa kwa madhumuni ya kuhakikisha: kuwapo kwa usimamizi madhubuti na wenye ufanisi na tija wa rasilimali za misitu na nyuki; kuongeza ubora na thamani ya kifedha katika kutoa huduma kwa umma; na

kuendelea kukuza na kuboresha uwezo wa kutoa huduma kwa umma. Katika ukaguzi wa shughuli za TFSA nilibaini mapungufu yafuatayo:

11.9.1 Kutofanya Kazi kwa Boti Zilizonunuliwa kwa Kushindwa Kukidhi Mahitaji ya Viwango vya TASAC – Sh. Milioni 404

Katika ukaguzi wangu, nilibaini kuwa mwaka 2019, Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) ilinunua boti mbili za Fiber Glass, MV Mafia yenye Namba ya Usajili TSC/DAR104 na MV Nyamisati yenye Nambari ya usajili NYST/L34, kutoka kwa M/S Sam & ANZAI Boat Builders Co. Ltd kwa gharama ya Sh 404,000,000. Nia ilikuwa boti hizo zitumike kusafiri kati ya Mafia na Rufiji. Hata hivyo, nilibaini kuwa boti hizo hazijatumika tangu ununuzi wake mnamo mwaka 2019, ambapo ni kinyume na madhumuni ya ununuzi.

Kuhusiana na hayo hapo juu , nilibaini kuwa wakala ilisitisha matumizi ya boti hizo baada ya Shirika la Wakala wa Meli Tanzania (TASAC) kuonesha kuwa haziko salama kwa matumizi katika sehemu ya bahari yenye kina kirefu. Hata hivyo, ni maoni yangu kuwa Wakala ilifanya ununuzi wa boti hizo mbili bila kuzingatia viwango vinavyotakiwa. Hili limetokana na mahitaji ya boti hizo kutoidhinishwa na Shirika la Wakala wa Meli Tanzania (TASAC) kabla ya manunuzi. Hivyo, kuna uwezekano kuwa boti hizo hazifai kutumika kwa madhumuni yaliyokusudiwa.

Napendekeza TFS iangalie upya taratibu zake za manunuzi ili kuhakikisha kuwa zinafuata viwango na kanuni zinazotakiwa. Aidha, TASAC kufanya tathmini ya kina ya boti husika ili kubaini uwezo wake wa kutumika katika sehemu ya baharí yenye kina kirefu iwapo itabainika si salama au hazifai kwa madhumuni yaliyokusudiwa, hatua stahiki zichukuliwe, kama vile kuzirudisha kwa msambazaji au kuzirekebisha ili kufikia viwango vinavyohitajika.

11.9.2 Uvamizi katika Hifadhi za Misitu

Kifungu cha 33 (1) cha Kanuni ya Misitu ya mwaka 2004 kinakataza mwenye leseni ya uchimbaji madini au leseni ya utafutaji madini kuingia sehemu yoyote ya mamlaka au eneo au hifadhi ya ardhi ya kijiji kwa ajili ya shughuli za uchimbaji madini au utafutaji wa madini isipokuwa kama amepata kibali kutoka Mkurugenzi au Afisa Mtendaji Mkuu. Hata hivyo, wakati wa ukaguzi, niliona ongezeko la uvamizi katika hifadhi za misitu kama ifuatavyo:

- Hifadhi ya Msitu wa Mafuta Morogoro iliundwa kwa Tangazo la Serikali (GN) namba 204 la tarehe 17 Julai 1953, na mpango namba JB Namba 152 wa tarehe 2 Februari 1953. Hifadhi hii ina ukubwa wa hekta 12,950 na inasimamiwa na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania chini ya Sheria ya Misitu ya mwaka 2002 [Sura ya 323], iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2016. Hata hivyo, tangu mwaka 2010, baadhi ya wanakijiji wamevamia hifadhi kwa kuanzisha makazi na kuendesha shughuli za kilimo na ufugaji ndani ya eneo lililotengwa.

- Zaidi ya hayo, katika ziara yangu mnamo mwezi Desemba 2022 kwenye shamba la Msitu wa Silayo, niliona uwepo wa kundi la wachimbaji wadogo wadogo wanaokuja kwa wingi kuvamia ardhi bila idhini kutoka kwa wakala kwa lengo la kutafuta madini.

Kuhusiana na tatizo hilo, Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) ulieleza kuwa Wizara ya Maliasili na Utalii ilitenga eneo la ekari 5,113 za misitu kwa wavamizi hao ambao utekelezaji wake unaendelea kwa sasa. Hata hivyo, ni maoni yangu kuwa ustahimilifu huu wa Wakala juu ya uvamizi wa hifadhi za msitu unaweza kusababisha uharibifu mkubwa wa msitu, jambo ambalo litasumbua mfumo wa ikolojia na kusababisha hasara ya mapato ya Serikali kutokana na kutokusanywa kwa mirabaha ya misitu.

Ninapendekeza Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) kuchukua hatua za kukabiliana na vitendo haramu, kushirikiana na mamlaka nyingine za serikali kuzuia uvamizi, kuandaa mfumo wa ufuatiliaji wa kina, kuongeza kampeni za uhamasishaji kwa umma, na kutenga rasilimali za kutosha kwa ajili ya ulinzi wa misitu.

11.10 Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA)

Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) ina jukumu la uandikishaji na utoaji wa vitambulisho vya taifa kwa wananchi na wakazi wanaotambulika kisheria. Wakati wa ukaguzi wa shughuli za NIDA nilibaini mapungufu yafuatayo:

11.10.1 Mapungufu katika Utoaji wa Vitambulisho vya Taifa

Baada ya kufanya tathmini ya shughuli za NIDA katika utoaji wa Vitambulisho vya Taifa, nilibaini kuwepo kwa upungufu ufuatao:

i. **Utoaji wa Nambari za Vitambulisho vya Taifa kwa Wageni na Wakimbizi 53 bila ya Kuwapo kwa Nyaraka.**
Kanuni ya 5(3) (b) (iii) ya Kanuni ya Usajili na Utambulisho wa Watu ya mwaka 2014 inabainisha kuwa taratibu za usajili wa mkazi mgeni zinamtaka mwombaji kutoa kibali cha ukaazi na kuhusiana na mkimbizi, hitaji ni Kadi ya kitambulisho cha Mkimbizi. Hata hivyo, nilibaini kuwa NIDA ilisajili na kutoa Nambari za Vitambulisho vya Kitaifa (NINs) kwa wakazi 53 wa kigeni bila nyaraka zinazohitajika kama vile vibali vya ukaaji au nambari za vitambulisho vya mkimbizi.

ii. **Utoaji wa Nambari za Vitambulisho vya Taifa kwa Watu walio Chini ya Umri wa Miaka 18**
Kanuni ya 4(2) ya Kanuni ya Usajili na Utambulisho wa Watu, 2014 inamtaka kila mtu ambaye ametimiza masharti yaliyotajwa kwenye sheria, kufanya maombi ya usajili ndani ya siku tisini baada ya kufikisha umri wa miaka 18. Hata hivyo, nilibaini kuwa NIDA ilikuwa imetoa Nambari za Vitambulisho vya Taifa (NINs) kwa watu 15 ambao walikuwa na umri chini ya miaka 18 au miaka yao ya kuzaliwa ni zaidi ya mwaka wa 2023.

Tatizo hili limechangiwa na kasoro katika uandikishaji wa taarifa za siku ya kuzaliwa za wahusika kwenye mfumo wa usajili wakati wa usajili. Kwa mfano, NIDA ilitoa nambari za usajili; 20430101654160000124, 20490401655180000119, na 20320701655050000127 inayoonesha kuwa watu hao walizaliwa mnamo mwaka 2043, 2049 na 2032 mtawalia.

iii. **Watu 21 Walitumia Cheti Kimoja cha Kuzaliwa kwa Usajili wa Nambari ya Kitambulisho cha Taifa (NIN).**
Kanuni ya 5(5) (b) (i) ya Kanuni ya Usajili na Utambulisho wa Watu ya mwaka 2014 inamtaka kila mtu anayeomba kusajiliwa kuwasilisha cheti cha kuzaliwa au ushahidi wa maandishi wa kuzaliwa kwa afisa wa usajili. Hata hivyo, nilipitia tarifa za usajili wa NIDA na nilibaini

kuwa Nambari za Vitambulisho vya Taifa (NINs) za watu 21 zilitolewa kwa kutumia cheti cha kuzaliwa kimoja chenye namba 292/2010 pekee.

iv. **Kushindwa Kutengeneza Vitambulisho vya Taifa 7,188,098**
Kifungu cha 2(1) cha Sheria ya Uanzishwaji wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) ya mwaka 2008 kinaitaka Mamlaka kutoa vitambulisho vya Taifa kwa raia wa Tanzania wanaostahili, wakazi halali na wakimbizi. Kwa mujibu wa Ripoti ya Mwaka ya Usimamizi wa Vitambulisho (IDM), NIDA ilipanga kuzalisha vitambulisho 10,043,868 katika mwaka wa fedha 2021/22. Hata hivyo, ripoti hiyo ilionesha kuwa, ni vitambulisho 2,855,770 pekee vilivyozalishwa katika kipindi hiki, hivyo kuacha lengo la uzalishaji wa vitambulisho vya Taifa 7,188,098 kutofikiwa (sawa na asilimia 72).

Madhaifu yaliyobainika katika Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) kimsingi yalisababishwa na udhibiti wa ndani usioridhisha wa kuthibitisha taarifa zinazoingizwa kwenye mfumo. Pamoja na ukosefu wa kadi ghafi za kizazi cha pili uliosababisha upungufu katika uzalishaji wa vitambulisho. Endapo masuala haya hayatashughulikiwa kwa haraka, NIDA inakabiliwa na hatari ya kusajili wahamiaji haramu na kushindwa kutoa vitambulisho kwa wananchi wanaostahili.

Ninapendekeza NIDA kuboresha udhibiti wa ndani kwa ajili ya kuhakiki usahihi wa taarifa zilizoingizwa katika mfumo wa usajili. Aidha, NIDA inapaswa kuhakikisha kwa haraka upatikanaji wa kadi ghafi za kizazi cha pili ili kuhakikisha upatikanaji wa vitambulisho vya kutosha kwa raia wanaostahili, wakazi halali na wakimbizi.

11.11 Wakala wa Nishati Vijijini (REA)

Wakala wa Nishati Vijijini (REA) wana jukumu kuu la kukuza na kuwezesha upatikanaji bora wa huduma za nishati ya kisasa katika maeneo ya vijijini ya Tanzania Bara. REA ilianza kufanya kazi mnamo Oktoba 2007. Mapitio ya uendeshaji wa REA nilibaini mapungufu yafuatayo kama yalivyoelezwa hapa chini:

11.11.1 Gharama Zisizo za Ulazima Zitokanazo na Kurudiwa kwa Majukumu kati ya REA na Wakala wake – Sh. Bilioni 12

Kifungu cha 23(1) & (3) cha Sheria ya Nishati Vijijini ya mwaka 2005 kinaitaka Bodi ya Wakurugenzi ya REA kuteua Wakala wa Udhamini ambaye atawajibika kwa ulipaji wa malipo ya ruzuku, usimamizi wa malipo ya ruzuku ikijumuisha utoaji wa fedha, uhakiki na ufuatiliaji wa miradi. Tarehe 13 Desemba 2019, REA iliingia mkataba na Muungano wa Benki ya CRDB PLC na Interfini Consultants Limited kufanya kazi kama Wakala wa Udhamini kwa muda wa miaka mitatu, mpaka tarehe 13 Desemba 2022. Majukumu ya Wakala wa Dhamana ni pamoja na kufuatilia maendeleo ya utekelezaji wa mradi Tanzania Bara na kuhakikisha yanaendana na matakwa ya ruzuku. Ili kutekeleza majukumu haya, Wakala wa Dhamana alitarajiwa kufanya ziara za kutembelea miradi kwa wastani wa umbali wa kilomita 84,000 kwa mwaka.

Kwa kuzingatia hayo hapo juu, nilibaini kuwa REA ilimlipa Wakala dhamana jumla ya Sh. 2,078,465,750 kufuatilia na kusimamia miradi ya REA kuanzia mwaka 2020 hadi 2022. Hata hivyo, ilibainika kuwa REA pia imetumia Sh. 12,006,572,740 katika kipindi hicho kufanya shughuli za ufuatiliaji na usimamizi, ikionesha kuwa REA iliingilia kazi ya Wakala wa Dhamana na kusababisha kuingia gharama zisizo za lazima za Sh. bilioni 12.

Kwa maoni yangu, kama REA ina uwezo wa kufuatilia na kusimamia miradi, inaweza kuwa nafuu zaidi kuelekeza fedha katika kuimarisha jukumu la ufuatiliaji na usimamizi ndani ya REA badala ya kushirikisha Wakala wa Dhamana.

Ninapendekeza REA kutathmini umuhimu wa nafasi ya Wakala wa Udhamini na kufanya uamuzi iwapo kuendelea kumtumia Wakala wa Udhamini katika jukumu la kufuatilia na kusimamia miradi au kusimamisha mkataba na wakala na kurudisha jukumu la kusimamia miradi kwa REA.

11.12 Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (TAWA)

Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (TAWA) chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii ni taasisi ya umma inayojiendesha ambayo ilianzishwa kwa Agizo la Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori la mwaka 2014. Ina jukumu la kufanya uongozi na usimamizi endelevu wa uhifadhi wa rasilimali za wanyamapori na viumbe hai nje ya Hifadhi za Taifa na Hifadhi ya Ngorongoro. Hii inajumuisha kusimamia jumla ya eneo la kilomita za mraba 169,553 (asilimia 79 ya eneo lote la maeneo ya hifadhi nchini) linalojumuisha Mapori ya Akiba, Mapori Tengefu na maeneo ya wazi. Ukaguzi wa utendaji kazi wa TAWA ulibaini yafuatayo:

11.12.1 Waongoza watalii wanaofanya kazi katika Hifadhi ya Akiba ya Grumeti Bila Kulipia Ada za Kuingia kwenye Hifadhi – Sh. Milioni 241.23

Kanuni ya 16 (1) na (2)(a) (I-XX) za Kanuni ya Uhifadhi wa Wanyamapori, 2016, zinataka shughuli yoyote inayofanyika katika eneo la uhifadhi kama ilivyoainishwa chini ya kanuni hii lazima iambatane na ada. Ada zitakazotozwa kama ilivyoainishwa chini ya kanuni hii ni pamoja na ada za kuingia, ada za kuingia kwa gari, na ada za waongoza watalii walioajiriwa na serikali.

Wakati wa ukaguzi wa TAWA, nilibaini kuwa kuna kampuni iitwayo M/s Grumeti Reserve Ltd imekuwa ikifanya shughuli za utalii ndani ya Hifadhi ya Akiba ya Grumeti, iliyopo Serengeti. Hata hivyo, baada ya ukaguzi wa kina, nilibaini kuwa waongoza watalii 2053 wanaoshirikiana na M/s Grumeti Reserve Ltd wamekuwa wakiingia ndani ya pori la akiba bila kulipa ada ya kiingilio, ambayo ni jumla ya Sh. milioni 241.23.

TAWA ilieleza kikao cha menejimenti kilichofanyika tarehe 16 Septemba 2020 kiliamua kusamehe ada za serikali kwa kampuni ya Grumeti Reserves Ltd wakati wakifanya shughuli ndani ya eneo la hifadhi. Hata hivyo, ni maoni yangu kuwa uamuzi huu wa msamaha kutoka kwa menejimenti ya TAWA ulikuwa kinyume na kanuni zilizotajwa hapo juu, na ulisababishia hasara serikali.

Napendekeza Wizara ya Maliasili na Utalii ifanye uchunguzi wa kina kuhusu sababu ya uamuzi wa kuisamehe M/s Grumeti Reserve LTD kulipa

mapato ya Serikali. Pia, kutambua mapato yaliyopotea tangu kuanza kwa shughuli za kampuni hiyo na kuchukua hatua zinazohitajika kurejesha kiasi hicho.

11.13 Tume ya Madini

Tume ya Madini ilianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Madini ya mwaka 2010 iliyorekebishwa na Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali ya mwaka 2017. Tume ilianzishwa kupitia Tangazo la Serikali namba 27 la tarehe 07 Julai 2017. Lengo la Tume ni kuimarisha usimamizi wa Sekta ya Madini na kuhakikisha kuwa Serikali inanufaika na mapato yanayopatikana kwa njia endelevu. Nimebaini mapungufu yafuatayo katika ukaguzi wa Tume ya Madini:

11.13.1 Wachimbaji Wadogo Wadogo Wanaendesha Mitambo 206 ya Kuchenjua Madini Kinyume na Sheria

Kifungu cha 6(1) cha Sheria ya Madini [Sura ya 123] inahitaji shughuli zozote za uchechuaji wa madini zinazofanywa katika ardhi yoyote ambayo Sheria inatumika lazima iidhinishwe na leseni ya madini iliyotolewa au inayochukuliwa kuwa imetolewa chini ya Sheria. Kutozingatia masharti haya kunaweza kusababisha Tume kutaifisha vifaa na madini, ambavyo vitapigwa mnada kupitia taratibu husika za mnada wa mali za serikali, kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (4). Zaidi ya hayo, Kifungu cha 7(1) cha Sheria kinaainisha aina za leseni za madini zinazoweza kutolewa, ambazo ni pamoja na leseni za uchenjuaji, leseni za kuyeyusha na kusafisha.

Hata hivyo, wakati wa ukaguzi wa Tume ya Madini (Ofisi ya Geita), nilibaini kuwa kuna mitambo 206 inayoendeshwa na wachimbaji wadogo kati ya mwaka 2014 na 2022 bila leseni ya uchakataji wa madini, kama inavyoainishwa katika Kifungu cha 7(1)(i) cha Sheria ya Madini [Sura ya 123]. Ukaguzi wangu zaidi ulibaini kuwa tatizo hilo limetokana na Tume kutofanya ufuatiliaji wa kutosha ili kubaini na kuchukua hatua za kuchukua dhidi ya wahusika, kama inavyofafanuliwa katika Kifungu cha 6(1) cha Sheria ya Madini.

Mitambo ya uchechuaji inayoendeshwa kinyume cha sheria inaweza kusababisha uharibifu wa mazingira, uchimbaji usio salama na upotevu wa mapato ya serikali, katika suala la ada na mrabaha. Zaidi ya hayo,

kukosekana kwa hatua za ufuatiliaji kwa Tume ya Madini kunamaanisha udhaifu wa usimamizi, ambao unaweza kusababisha uvunjifu wa sheria zaidi na shughuli za uchimbaji haramu.

Napendekeza Tume ya Madini iimarishe udhibiti wake wa ufuatiliaji na uchukuzi wa hatua madhubuti ili kuhakikisha kuwa Sheria ya Madini [Sura 123] inafuatwa, hasa kuhusu matakwa ya leseni za uchechuaji wa madini. Aidha, Tume ichunguze njia za kuongeza uelewa kwa wachimbaji wadogo kuhusu upatikanaji wa leseni za madini na madhara ya kutofuata.

Masuala yaliyojitokeza katika Ukaguzi wa Mifuko Maalumu

Mifuko maalumu ilianzishwa na serikali kwa ajili ya kukusanya fedha ambazo zitatumika kwa shughuli maalumu. Pia, Mifuko maalumu inahakikisha uwajibikaji na kutoa ukweli kwa walipa kodi kwamba fedha zao zinatumika katika shughuli zilizokusudiwa. Nilipitia shughuli za Mifuko na kubaini masuala muhimu ambayo yanahitaji uboreshaji kama ilivyoelezwa hapo chini:

11.14 Bodi ya Mfuko wa Barabara (RFB)

Bodi ya Mfuko wa Barabara (RFB) ina jukumu la kufadhili na kusimamia mipango ya ukarabati na maendeleo ya barabara nchini. Bodi ilianzishwa mwaka 2001 chini ya Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta, ambayo ililenga kutengeneza utaratibu endelevu wa ufadhili wa mtandao wa barabara nchini Tanzania. Ukaguzi wangu juu ya shughuli za Mfuko umebaini yafuatayo:

11.14.1 Fedha za Ongezeko la Tozo ya Mafuta Iliyoanzishwa na Serikali Haikupelekwa na Kusimamiwa na Bodi ya Mfuko wa Barabara (RFB) – Sh. Bilioni 330.33

Kifungu cha 4 (1) cha Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta [Sura ya 220] kinasema kwamba “itaanzishwa Mfuko utakaojulikana kama Mfuko wa Barabara ambao utalipwa fedha zote zinazokusanywa kama tozo ya mafuta katika dizeli na petroli, ada za usafiri, leseni za magari makubwa, ada za tozo za kuzidisha uzito wa mizigo katika magari, au kutoka chanzo kingine chochote kwa kiwango au viwango vitakavyoamuliwa na Bunge mara kwa mara”.

Aidha, Kifungu cha 5 (4) cha Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta (Sura 220) kinaeleza kuwa kazi ya Bodi ya Mfuko wa Barabara itakuwa: kutumia fedha zilizowekwa kwenye Mfuko kwa madhumuni yaliyoidhinishwa na Bunge; kuhakikisha ukusanyaji na uhamishaji wa tozo za barabara na mafuta zilizokusanywa kwenye akaunti ya Mfuko; kupeleka fedha kutoka Mfuko kwenda kwa watekelezaji; na kufuatilia matumizi ya fedha zinazotolewa kwa watekelezaji kwa madhumuni ya malengo ya Mifuko.

- Tarehe 01 Julai 2021, Kifungu cha 4A cha Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta (Sura 220) kilifanyiwa marekebisho na kifungu cha 42 cha Sheria ya Fedha, 2021 na kuanzisha tozo ya ziada ya Sh. 100 kwa lita itakayotozwa kwenye petroli au dizeli ambayo ingeongeza tozo ya mafuta kutoka Sh. 263 kwa Lita hadi Sh. 363 kwa Lita. Aidha, kifungu cha 4A inabainisha kuwa tozo hiyo ya ziada ya Sh. 100 kwa lita itakayotozwa kwa petroli au dizeli itahamishwa kwenda kwa Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA).

- Kutokana na hayo, nilibaini kuwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (kwa niaba ya Mfuko) ilikusanya jumla ya Sh. 330,332,843,270.22 kuanzia tarehe 1 Julai 2021 hadi 30 Juni 2022 kama nyongeza ya tozo ya mafuta (Sh. 100 kwa Lita). Kiasi kilichokusanywa kiliwekwa kwenye Akaunti ya Mfuko wa Barabara ya BOT Namba 9921169779, ambayo iko chini ya Wizara ya Fedha na Mipango. Hata hivyo, ukaguzi zaidi umebaini kuwa Wizara ya Fedha na Mipango ilishindwa kuhamisha makusanyo hayo kwenda Bodi ya Mfuko wa Barabara, jambo ambalo ni kinyume cha Kifungu cha 5 (4) cha Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta (SURA 220). Kifungu hiki kinaiagiza Bodi kuhakikisha ukusanyaji wa tozo za barabara na mafuta na kuzipeleka kwenye akaunti ya Mfuko kwa ajili ya kusambazwa kwa watekelezaji.

- Aidha, nimebaini kuwa Wizara ya Fedha na Mipango imekuwa ikihamisha moja kwa moja fedha zilizokusanywa kutokana na tozo ya ziada ya mafuta kwenda TARURA. Hata hivyo, ni maoni yangu kuwa Wizara ya Fedha na Mipango haina mamlaka ya kupeleka fedha hizo moja kwa moja TARURA, na utaratibu huo unakwenda kinyume na Kifungu cha 5 (4) (g) cha Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta. Kifungu hichi kinaeleza kwa uwazi kwamba jukumu la kutoa fedha hizo ni la Bodi ya Mfuko wa Barabara (RFB). Aidha, kukosekana kwa ufuatiliaji kutoka RFB

juu ya uhamishaji wa fedha za jumla ya Sh. bilioni 330.33 moja kwa moja kwenda TARURA na Wizara ya Fedha na Mipango unakinzana na Kifungu cha 5 (4) kinachoitaka RFB kufuatilia matumizi ya fedha zilizotolewa.

Kutokana na ukaguzi wangu, mapungufu katika usimamizi wa fedha zilizokusanywa kupitia tozo ya mafuta ya nyongeza inatokana na kutofuatwa kwa sheria zilizowekwa na Wizara ya Fedha na Mipango. Ukiukaji huu unaweza kuwezesha usimamizi duni na matumizi mabaya ya fedha, kwa kuwa hakuna mipango na ufuatiliaji wa kutosha wa matumizi ya tozo hiyo.

Napendekeza Wizara ya Fedha na Mipango kuzingatia Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta (Sura ya 220) na kuhakikisha kuwa fedha zinazokusanywa za tozo ya mafuta zinahamishwa kwenda Bodi ya Mfuko wa Barabara, kama inavyotakiwa na Kifungu cha 5 (4) (g). Aidha, napendekeza Mamlaka za Uchunguzi za Serikali kufanya uchunguzi wa kina kuhusu matumizi ya fedha hizo zenye thamani ya Sh. bilioni 330.30 ambazo zilihamishwa moja kwa moja kwenda TARURA. Endapo usimamizi mbaya wowote utabainika, hatua stahiki zichukuliwe dhidi ya waliohusika.

11.15 Mfuko wa Dhamana wa Pembejeo za Kilimo (AGITF)

Malengo ya msingi ya Mfuko wa Pembejeo za Kilimo (AGITF) ni; (a) kutoa mikopo kwa ajili ya kugharamia uingizaji na usambazaji wa pembejeo za kilimo kwa kuzingatia kanuni na masharti yaliyowekwa na Bodi; (b) huduma za ushauri wa kifedha na usaidizi wa kiufundi kuhusiana na upatikanaji, usambazaji na matumizi ya pembejeo za kilimo; na (c) kulipia gharama za usimamizi wa Hazina. Kulingana na ukaguzi wangu kuhusu shughuli za Mfuko, nilibaini makosa yafuatayo:

11.15.1 Hasara Itokanayo na Mikopo Chechefu – Sh. Bilioni 19.49

Kutokana na ukaguzi wangu wa uendeshaji wa AGITF nilibaini kuwa Mfuko ulitoa mikopo ya jumla ya Sh. 26,422,092,101 kwa wakopaji 1,091 ambayo ilikuwa haijalipwa hadi tarehe 30 Juni 2022. Hata hivyo, niligundua kuwa AGITF imefuta mikopo chechefu yenye thamani ya Sh. 19,490,052,568 kati ya kiasi cha mikopo ambayo ilikuwa bado haijalipwa.Hatua hii ilichukuliwa

kwa sababu AGITF ilifanya tathmini na kubaini kuwa Mfuko hautaweza kukomboa mikopo hii kutoka kwa waliokopeshwa.

Kwa mfano, nilibaini kuwa AGITF imefuta mikopo ya jumla ya Sh. 807,389,632 ambayo ilikuwa imetolewa kwenda benki kadhaa. Benki hizi zilifungwa na Benki Kuu ya Tanzania (BOT) kutokana na kasoro za kiutendaji na kuwekwa chini ya Bodi ya Bima ya Amana (DIB) kwa ajili ya kufilisiwa. Pia, nilibaini kuwa AGITF ilifuta mikopo chechefu yenye thamani ya Sh. 11,371,413,858 ambayo ilitolewa kuwezesha ununuzi wa matrekta mapya, ikiwa ni asilimia 58 ya jumla ya mikopo iliyofutwa na AGITF.

Aidha, ukaguzi wangu wa ziada umebaini kuwa sababu kuu ya hasara hiyo ilitokana na AGITF kutokuwa na usimamizi wa kutosha wa utoaji na urejeshaji wa mikopo hiyo. Kwa hivyo, umesababisha athari kwenye uwezo wa AGITF kuendelea kufanya shughuli zake kwa muda mrefu siku za mbeleni. Aidha, walipakodi wameelemewa na gharama za hasara hiyo, ambazo zingeweza kutumika kugharamia shughuli nyingine za kimkakati.

Ninapendekeza Mamlaka za Uchunguzi za Serikali kufanya uchunguzi wa kina kuhusu michakato ya utoaji na urejeshaji wa mikopo ya AGITF iliyosababisha hasara ili kubaini kama kuna uzembe wowote ulifanyika na kuchukua hatua za kisheria kwa wahusika. Aidha, napendekeza AGITF iimarishe udhibiti wake wa ndani juu ya ukusanyaji wa mikopo ambayo haijarejeshwa ili kuzuia hasara zaidi.

11.16 Mfuko wa Kukopesha Watumishi wa Serikali (AF)

Lengo kuu la Mfuko wa Maendeleo ni kuimarisha ustawi wa watumishi wa umma kwa kutoa msaada wa kifedha kwa ajili ya upatikanaji na matengenezo ya vyombo vya usafiri, pamoja na ununuzi wa vifaa vya nyumbani. Ukaguzi wangu kuhusu uendeshaji wa Mfuko ulibainisha udhaifu ufuatao:

11.16.1 Kutorejeshwa kwa Mikopo Kulikosababishwa na Kushindwa Kuhifadhi Taarifa za Makato ya Mishahara ya Wanufaika – Sh. Milioni 198.55

Tarehe 17 Agosti 2019, Kamati ya Mikopo ya Hazina ilifikia uamuzi kuhusu makato ya kila mwezi ya mkopo. Kulingana na uamuzi huo, Maafisa Masuuli lazima waanzishe makato katika mfumo wa "Lawson" kabla ya kutoa mkopo kwa mnufaika. Ili kutekeleza uamuzi huu, Mfuko unahitaji kutuma barua kwa Afisa Masuuli husika. Barua hiyo inapaswa kuomba idhini ya kukatwa makato ya mkopo kwenye mfumo wa Lawson kabla ya kurejeshwa kwenye Mfuko kwa ajili ya kutoa mkopo huo.

Hata hivyo, nilibaini kuwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/20 hadi 2021/22, jumla ya mikopo 120 yenye thamani ya Sh. 198,553,392.66, ilitolewa kwa wanufaika. Hata hivyo, mpaka muda wa ukaguzi 07 Desemba 2022, Mfuko ulikuwa bado haujaingiza taarifa za makato kwenye mfumo kwa kipindi cha kuanzia mwaka mmoja mpaka mitatu kinyume na muongozo uliyotolewa na Kamati ya Mfuko.

Zaidi ya hayo, nilibaini kuwa sababu ya msingi ya mikopo kutorejeshwa ilitokana na utoaji wa fedha kwa wanufaika kabla ya Kuhifadhi taarifa za makato ya mishahara yao. Basi ni maoni yangu kuwa kuna hatari ya idadi kubwa ya wafanyakazi kushindwa kunufaika na Mfuko kwa sababu ya kutorejeshwa au kuchelewa kurejeshwa kwa mikopo waliyopewa ya Sh. 198,553,392.66.

Ninapendekeza Mfuko wa Mikopo chini ya Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali kuhakikisha uboresahaji wa udhibiti ili kuhakikisha makato yanafanyika kwa wakati, kuweka ufuatiliaji wa mara kwa mara wa marejesho ya mikopo.

11.17 Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo (CDCF)

CDCF ni Mfuko ulianzishwa kwa lengo la kuchochea maendeleo ya majimbo ya uchaguzi ya Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Sheria Na. 16 ya Mwaka 2009 ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo.

11.17.1 Utoaji wa Fedha za Mfuko kwenye Akaunti za Benki Ambazo Hazihusiani na Wanufaika – Sh. Milioni 313.97

Kifungu cha 5(4)(a) cha Sheria ya Mfuko wa Maendeleo ya Majimbo [Sura ya 96, Toleo la 2015] kinataka fedha zilizotengwa kwa kila eneo la majimbo kuhamishwa moja kwa moja na Hazina hadi kwenye akaunti husika za Majimbo. Akaunti hii inapaswa kufunguliwa kwa kufuata sheria za kifedha za serikali ya mtaa.

Katika ukaguzi wangu, nilibaini kuwa Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo (CDCF) ulifanya malipo ya Sh. 313,976,694.85 kwa majimbo matatu - Halmashauri ya Wilaya ya Kusini, Halmashauri ya Mji wa Kati, na Halmashauri ya Manispaa ya Magharibi B huko Zanzibar. Hata hivyo, nilibaini kuwa fedha hizo zilikuwa zimeingizwa kwenye akaunti za benki ambazo hazihusiani na majimbo hayo.

Udhaifu huu unaonesha ukosefu wa udhibiti madhubuti wa ndani wa fedha. Kwa hiyo, inaleta mashaka kuhusu uwazi na uwajibikaji wa CDCF katika kusimamia fedha za umma. Pia, majimbo yaliyoathirika yanaweza kuwa hayajapata fedha zilizokusudiwa, hivyo kusababisha ucheleweshaji au hata kufutwa kwa miradi iliyopangwa.

Ninapendekeza CDCF iimarishe udhibiti wa ndani wa fedha ili kuhakikisha usimamizi mzuri wa fedha za umma. Pia, kufanya uchunguzi wa kina ili kubaini sababu ya utoaji fedha usio sahihi na kuchukua hatua stahiki kwa wahusika wa tukio hilo.

11.18 Mfuko wa Udhamini wa Ukimwi (ATF)

Mfuko wa Udhamini wa UKIMWI ni Mpango wa Kifedha wa Ndani ulioundwa na Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania kupitia Sheria ya TACAIDS (Marekebisho) namba 6 ya mwaka 2015. Lengo lake kuu ni kuongeza mipango ya ufadhili wa VVU na UKIMWI, hivyo kukuza uendelevu wa Taifa katika kupambana na janga hilo.

11.18.1 Kuchelewa Kuhamisha Fedha kwenda MSD kwa ajili ya Ununuzi wa Dawa za Waathirika wa VVU – Sh. Milioni 600

Niligundua kuwa Wizara ya Fedha na Mipango (MoFP) ilitoa Sh. 600,000,000 mnamo tarehe 30 Mei 2022 kwa Mfuko wa Udhamini wa Ukimwi (ATF) ili kuwezesha ununuzi wa dawa kwa watu wanaoishi na virusi vya ukimwi. Fedha hizo zilitarajiwa kupelekwa Bohari ya Dawa (MSD) na ATF kwa ajili ya kusimamia mchakato wa manunuzi. Hata hivyo, kipindi cha ukaguzi mwezi Agosti 2022, ATF ilikuwa bado haijapeleka fedha MSD na hivyo kusababisha kuchelewa kwa ununuzi wa dawa hizo kwa muda wa miezi mitatu.

Kwa maoni yangu, ucheleweshaji wa fedha kutoka Mfuko wa Udhamini wa Ukimwi (ATF) kwenda Bohari ya Dawa (MSD) ulisababishwa na usimamizi wa fedha usioridhisha. Ucheleweshaji huu unaweza kuwa na madhara makubwa, kwani unaweza kusababisha uhaba wa dawa na vifaa muhimu kwa watu wanaoishi na VVU/UKIMWI. Hii inaweza kusababisha matokeo mabaya ya kiafya, pamoja na kuongezeka kwa ugonjwa, kulazwa hospitalini, na hata vifo.

Napendekeza Mfuko wa Udhamini wa Ukimwi kuweka kipaumbele katika kupeleka fedha kwenye Bohari ya Dawa na kuhakikisha kuwa ununuzi wa dawa na vifaa unaharakishwa. Zaidi ya hayo, ATF inapaswa kupitia udhibiti na taratibu zao za ndani ili kubaini masuala yoyote ambayo huenda yamesababisha ucheleweshaji huo na kuchukua hatua za kurekebisha.

11.19 Mfuko wa Taifa wa Usimamizi wa Maafa

Mfuko ulianzishwa kwa malengo ya kufanya maombi maalumu au ya jumla kwa taifa kwa ajili ya kuchangia kwa njia ya fedha au mali kwa ajili ya kuokoa maisha, mali, na kupunguza athari au kurudisha hali ya kawaida kwa jamii iliyoathirika na majanga. Kwenye ukaguzi wa opersheni za Mifuko Maalumu nilibaini yafuatayo:

11.19.1 Kutorejeshwa kwa Fedha zilizotolewa kwa Halmashauri ili Kukabiliana na Uhaba wa Chakula – Sh. Milioni 471.49

Nilibaini kuwa kati ya mwaka 2011 hadi 2015, Mfuko wa Taifa wa Kukabiliana na Maafa, chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu (Ofisi ya Waziri Mkuu), ulitoa msaada wa chakula kwa halmashauri mbalimbali kwa ajili ya kuwauzia wananchi

kwa bei ya chini kuliko viwango vya soko ili kukabiliana na uhaba wa chakula. Halmashauri zilitarajiwa kukusanya fedha hizo na kuzirejesha kwenye akaunti ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Hata hivyo, katika ukaguzi wangu tarehe 15 Desemba 2022, nilibaini kuwa halmashauri 18 bado hazijarejesha kiasi cha Sh. 471,492,185.69 kwa kipindi cha kati ya miaka saba hadi 11, na zinaonesha kushindwa kufanya malipo yaliobakia. Maelezo ya Halmashauri zenye mikopo ambayo haijalipwa yanaoneshwa kwenye **Jedwali Na. 83**:

Jedwali Na. 83: Halmashauri ambazo Hazijarejesha Mkopo

Na.	Jina la Halmashauri	Kiasi (Sh.)
1	Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa	22,567,957.00
2	Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni	6,762,100.00
3	Halmashauri ya Wilaya ya Chemba	17,650,000.00
4	Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu	89,991,859.00
5	Halmashauri ya Wilaya ya Liwale	24,323,813.00
6	Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro	24,750,000.00
7	Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa	73,376,000.00
8	Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa	38,500,000.00
9	Halmashauri ya Wilaya ya Hanang'	8,800,000.00
11	Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi	10,000,000.00
12	Halmashauri ya Wilaya ya Maswa	1,004,600.00
13	Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi	19,348,492.00
14	Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe	3,600,000.00
15	Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba	105,798,378.00
16	Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa	4,500,000.00
17	Halmashauri ya Wilaya ya Karangwe	5,000,000.69
18	Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu	15,518,986.00
Jumla		**471,492,185.69**

Chanzo: *Ripoti za ukaguzi 2021/22*

Kwa maoni yangu, kutorejeshwa kwa fedha zilizotolewa na Mfuko wa Taifa wa Kukabiliana na Maafa kwa Halmashauri kunaweza kuchangiwa na kutofuatiliwa ipasavyo na menejimenti ya Ofisi ya Waziri Mkuu na pia halmashauri kushindwa kurudisha fedha hizo ambazo inawezekana zilitumika katika matumizi mengine. Kushindwa kwa halmashauri kurejesha fedha hizo kwenye akaunti ya PMO kunaweza kusababisha uhaba wa fedha za Mfuko wa Taifa wa Kukabiliana na Maafa, jambo ambalo linaweza kuathiri uwezo wao wa kutoa msaada wakati wa majanga.

Napendekeza menejimenti ya Ofisi ya Waziri Mkuu ianzishe taratibu thabiti za ufuatiliaji ili kuhakikisha kuwa halmashauri zinarejesha fedha zilizokopwa ndani bila kuchelewa.

11.19.2 Kutorejeshwa kwa Fedha Zilizokopwa na Wizara – Sh. Milioni 323.11

Kanuni 62 (4) ya Kanuni ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 inatamka kuwa hakuna mtu ataruhusiwa kukopa au kuazima au kusababisha ukopaji wa fedha zilizokusanywa chini ya kanuni hii kwa namna au malengo yoyote.

Hata hivyo, katika kipindi cha ukaguzi wa shughuli za Mifuko maalumu, nilibaini kuwa wizara mbali mbali zilikopa jumla ya Sh. 323,110,130 kutoka mifuko maalumu mitatu bila ya kurudisha kiasi hicho kama ilivyoelezewa kwenye Jedwali hapo chini

Jedwali Na. 84: Fedha zilizokopwa na Wizara

Na.	Jina la Mfuko	Kiasi Kilichokopwa (Sh)	Mkopaji
1	Mfuko wa Uwezeshaji wa Maendeleo ya Madini (EMDF)	223,110,130	Wizara ya Madini
2	Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake (WDF)	100,000,000	Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu
	Jumla	**323,110,130**	

Chanzo: *Ripoti za Ukaguzi 2021/22*

Ni maoni yangu kuwa, kutokurudishwa kwa fedha zilizokopwa na Wizara kunaweza kuhatarisha shughuli za Mifuko Maalumu na kusababisha malengo ya bajeti kutofikiwa

Ninashauri Wizara kuhakikisha kuwa kiasi kilichokopwa kinarudishwa kwenye Mifuko husika. Pia, Seikali iandae mwongozo utakaosaidia kuzuia ukopaji wa Wizara kwenye Mifuko.



SURA YA KUMI NA MBILI

UTENDAJI KATIKA UENDESHAJI WA HOSPITALI ZA RUFAA ZA MIKOA NA HOSPITALI MAALUMU

12.1 Utangulizi

Katika sura hii, ninawasilisha matokeo ya ukaguzi kuhusu huduma za matibabu na changamoto za mfumo wa afya katika Hospitali za Rufaa za Mikoa, kanda, na hospitali maalumu.

Hospitali hizi ziko chini ya usimamizi wa moja kwa moja wa Wizara ya Afya, na uendeshaji wake madhubuti ni muhimu katika kukuza ustawi wa wananchi na maendeleo ya taifa. Matokeo ya ukaguzi wangu, yanaonesha kuwa sekta ya afya inaendelea kukabiliwa na changamoto zinazohusiana na rasilimali, ikiwa ni pamoja na uhaba wa watumishi wenye ujuzi, ufinyu wa bajeti , mazingira duni ya kazi, miundombinu duni, uhaba wa dawa na vifaa tiba.

Pamoja na jitihada za Serikali katika kuhakikisha kuna mafanikio makubwa ya upatikanaji wa huduma za afya ya msingi, bado kuna changamoto, hasa kwa wananchi wa kawaida wanaotafuta huduma bora za afya. Sura hii inabainisha maeneo muhimu ambayo yanahitaji jitihada zaidi katika usimamizi na kupendekeza hatua ambazo Serikali na wadau wengine wanapaswa kuzingatia ili kuboresha huduma za kitabibu.

12.2 Utoaji wa Huduma za Rufaa Usioridhisha katika Hospitali za Rufaa za Mikoa

Wakati wa ukaguzi wangu wa Hospitali za Rufaa za Mikoa, nilibaini kuwa hospitali 20 hazikuweza kutoa huduma sahihi za rufaa kwa wagonjwa kutokana na uhaba wa madaktari na vifaa tiba maalumu.

Hii ni kinyume na mwongozo wa kiutendaji uliotolewa na Wizara ya Afya mwezi Juni 2019, ambao unataka hospitali za rufaa kuwa na wataalamu maalumu wa matibabu, dawa na vifaa tiba vya kutosha.

Aidha, hali imekuwa hairidhishi ukilinganisha na mwaka wa fedha 2020/21, ambapo kuna ongezeko la hosipitali 14 ambayo ni sawa na asilimia 233 kwa Hospitali ambazo zinazotoa huduma za rufaa zisizokidhi viwango. Hii inaaashiria kuwa mapendekezo ya awali hayakutekelezwa ipasavyo. Orodha ya hospitali zenye upungufu wa utoaji wa huduma za rufaa zimeoneshwa katika **Kiambatisho Na. XXVIII**.

Nina maoni kwamba utoaji wa huduma duni katika hospitali za rufaa za mikoa unaweza kuzuia kufanikiwa kwa malengo ya utoaji wa huduma za kitabibu za afya katika ngazi ya mkoa.

Kwa hiyo, napendekeza Serikali itenge fedha za kutosha katika sekta ya afya ili kuhakikisha kwamba hospitali za rufaa za mikoa na maalumu zinakuwa na wataalamu na vifaa vya kutosha vya matibabu ili kuboresha huduma za afya ya jamii.

12.3 Fedha za Hospitali Kiasi cha Sh. Bilioni 20.66 Zinashikiliwa na Bohari Kuu ya Dawa Bila Kusambaza Dawa na Vifaa Tiba

Kanuni ya 140(3) na 141(3) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma (2013) zinaitaka Bohari Kuu ya Dawa (MSD) kununua na kusambaza vifaa vya katalogi na visivyo vya katalogi ambavyo vinahitajika mara kwa mara kwa kipindi fulani. Hata hivyo, mapitio yangu ya taarifa ya akaunti ya Bohari Kuu ya Dawa kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2022 nilibaini kuwa hospitali za rufaa za mikoa 15 zilikuwa na salio la Sh. bilioni 20.66 zilizo shikiliwa na Bohari Kuu ya Dawa kwa kipindi cha zaidi ya mwaka mmoja kwa ajili ya ununuzi wa dawa na vifaa tiba.

Hali hii inasababishwa na kukosekana kwa makubaliano ya kisheria ambayo yatalazimisha Bohari Kuu ya Dawa kusambaza vifaa vya katalogi na vitu visivyo vya katalogi ambavyo vimekosekana kwa niaba ya hospitali kwa kutumia fedha zilizotengwa.

Kwa kuzingatia hayo hapo juu, kiasi kikubwa cha fedha kinachoshikiliwa na Bohari Kuu ya Dawa kwa zaidi ya mwaka mmoja kinaweza kukwamisha

upatikanaji wa dawa na vifaa tiba kwa hospitali zilizokusudiwa, hivyo kukwamisha utoaji wa huduma na hivyo kuwa vigumu kutoa huduma stahiki za matibabu.

Aidha, salio la fedha za dawa Bohari Kuu ya Dawa limeongezeka kwa Sh. Bilioni 6.56, ambayo ni sawa na asilimia 47 ikilinganishwa na mwaka wa fedha uliopita wa 2020/21. Hii inaashiria kuwa mapendekezo niliyokuwa nimeyatoa awali kuhusu suala hili hayakutekelezwa ipasavyo." Hospitali zenye salio kubwa la fedha zinazoshikiliwa na Bohari Kuu ya Dawa zimeorodheshwa katika **Jedwali Na. 85**.

Jedwali Na. 85: Orodha ya Hospitali zenye Kiasi kikubwa cha Fedha Kinachoshikiliwa na Bohari Kuu ya Dawa

Na.	Jina la hospital ya Rufaa ya mkoa na Hospitali Maalum	Kiasi (Sh.)
1	Chato ZRH	4,495,768,664
2	Iringa	793,321,205
3	Morogoro	602,581,632
4	Mwananyamala	1,196,467,755
5	Singida	16,479,430
6	Sokoine	724,794,728
7	Geita	1,013,621,383
8	Kibong'oto	930,816,394
9	Katavi	7,797,145,766
10	Shinyanga	335,488,094
11	Temeke	631,342,559
12	Mirembe	711,849,053
13	Mtwara	304,682,392
14	Tabora	177,191,945
15	Tanga	933,249,465
Jumla		**20,664,800,464**

Chanzo: *Barua za Mapungufu kwa Menejimenti za 2021/22*

Ili kukabiliana na suala hili, napendekeza Serikali na uongozi wa hospitali husika za rufaa za mikoa ziweke makubaliano ya kisheria na Bohari Kuu ya Dawa. Aidha, endapo kutatokea ukosefu wa dawa Bohari Kuu ya Dawa inapaswa kurejesha salio lote lililobaki kwa hospitali husika.

12.4 Wataalamu wa Afya Ambao Wanatoa Huduma Bila Kuwa na Leseni Halali.

Kifungu Na. 52(3) cha Sheria namba 11 ya Madaktari wa binadamu, meno na wataalam wa afya shirikishi ya mwaka 2017 kinamtaka mtu yeyote anayejihusisha na kazi za kitaalamu za matibabu ya afya ya binadamu, meno na magonjwa mengine bila kusajiliwa au kuwa na leseni halali ya kufanyia kazi hizo, atakuwa anatenda kosa.

Pia, kifungu cha 16(1) cha Sheria ya Famasia, ya mwaka 2011 na Viwango vya Msingi vya Vituo vya Afya kwa Hospitali za ngazi ya I na II iliyotolewa na Wizara ya Afya mwaka 2017, wafamasia wanapaswa kusajiliwa na kuwa na leseni halali ya taaluma yake na kutambuliwa na baraza lao la kitaaluma. Hata hivyo, ukaguzi wangu ulibaini kuwa wataalamu wa afya **289** katika hospital za rufaa za mikoa 10 walikuwa wakifanya taaluma zao bila kusajiliwa na Baraza husika na hivyo kutokuwa na leseni za kitaaluma kinyume na sheria kama ilivyoelezwa katika **Jedwali Na. 86.**

Jedwali Na. 86: Hospitali za Rufaa zenye Wataalamu wa Afya Wasio na Leseni za Kufanya Taaluma zao

Na.	Jina la Hospitali ya Rufaa	Idadi ya wataalamu
1	Chato	14
2	Mbeya	16
3	Mbeya ZRH	107
4	Morogoro	39
5	Geita	23
6	Shinyanga	20
7	Mirembe	26
8	Bukoba	19
9	Tabora	10
10	Tanga	15
Jumla		**289**

Chanzo: *Ukaguzi wa wataalamu wa Afya katika Hospitali ya Rufaa 2021/22*

Hii ilitokana na ufuatiliaji usioridhisha wa uongozi wa hospitali husika na watu binafsi kushindwa kujisajili katika baraza la wataalamu.

Licha ya ripoti yangu ya mwaka uliopita kuonesha upungufu huo, kumekuwa na uboreshaji hafifu katika eneo hili, ikilinganishwa na mwaka uliopita kuna upungufu wa wataalamu 10 wasiokuwa na leseni kufanya taaluma zao, sawa

na asilimia 8. Pasipokuwa na leseni halali, ubora wa huduma zinazotolewa hauwezi kufikia kiwango kinachotakiwa, na endapo kutakuwa na ubadhirifu, uongozi wa hospitali utashindwa kumwajibisha mfanyakazi.

Hivyo basi, ninapendekeza kuwa Afisa Masuuli wa Wizara ya Afya aweke mikakati ya kufuatilia na kuhakikisha kuwa wanataaluma wote wanaofanya kazi wana leseni halali ya kufanya kazi hiyo.

12.5 Msamaha wa Sh. Milioni 703 Uliotolewa kwa Wagonjwa Wasiostahili

Wakati wa ukaguzi wangu kuhusu utoaji wa misamaha wa gharama za matibabu kwa wagonjwa katika hospitali za rufaa za mikoa, nilibaini kuwa hospitali zilikuwa zimetoa misamaha ya jumla ya Sh.milioni 703 kutoka hospitali za rufaa za mikoa 10 bila kufanya tathmini ya kina au kupata taarifa zote muhimu kama vile historia ya matibabu ya mgonjwa, barua ya rufaa na historia ya familia kama inavyotakiwa na aya 5.5.1 (e) ya mwongozo wa kisheria wa gharama za matibabu katika hospitali za rufaa za mikoa.

Hii ilitokana na ukweli kwamba wajibu wa afisa ustawi wa jamii ambapo ni usajili wa wagonjwa, kupitia mapendekezo, uthibitisho, ugawaji wa huduma za matibabu, na kuidhinisha matibabu ulikuwa ukitekelezwa na afisa mmoja bila kuwapo kwa mgawanyo wa majukumu. Aidha, ukaguzi niliofanya katika mfumo wa huduma za Afya (AfyaCare System) nilibaini kuwa, mfumo huo haukuwa na uwezo wa kuambatanisha nyaraka zinazohitajika ili kuhalalisha misamaha iliyotolewa.

Kutokana na tathmini hiyo ambayo inaonyesha kuwepo kwa utaratibu usioridhisha, kuna hatari kwamba misamaha inaweza kutolewa kwa wagonjwa wasiostahili, hivyo kusababisha upotevu wa mapato kwa hospitali husika. Orodha ya hospitali zilizotoa msamaha wa gharama za matibabu usio stahili kwa wagonjwa inaoneshwa kwenye **Jedwali Na. 87**.

Jedwali Na. 87: Msamaha kutolewa kwa Wagonjwa Wasiostahili

Na.	Jina la Hospitali za Rufaa na Maalumu	Kiasi kilicho samehewa (Sh.)
1	Kibongoto SRH	150,621,095
2	Ligula RRH	5,284,100
3	Mawenzi RRH	163,678,400

Na.	Jina la Hospitali za Rufaa na Maalumu	Kiasi kilicho samehewa (Sh.)
4	Singida RRH	12,146,900
5	Shinyanga RRH	43,124,120
6	Sumbawanga RRH	31,558,858
7	Bukoba RRH	75,138,145
8	Njombe RRH	13,637,860
9	Tabora	83,074,837
10	Meru	125,170,100
	Jumla	**703,434,415**

Chanzo: *Barua za Mapungufu kwa Menejimenti za 2021/22*

Napendekeza Wizara ya Afya ishirikiane na hospitali husika kuhakikisha kwamba tathmini sahihi zinafanyika na kwamba ushahidi sahihi unapatikana kabla ya kutoa misamaha.

12.6 Upotevu wa Mapato Kutokana na Kukataliwa kwa Madai ya Bima ya Afya ya Sh. 7.8 bilioni

Kifungu cha 27(2) cha Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya, 1999 kinaeleza kuwa mfuko unaweza kukataa au kupunguza malipo ya madai ya uongo au yasiyo sahihi au pale mdaiwa anaposhindwa kufuata sheria au kanuni za malipo ya madai yaliyotolewa chini ya Sheria hii.

Tathmini yangu katika hospitali za rufaa za mikoa, hospitali maalumu na hospitali za kanda nilibaini kuwa madai ya jumla ya Sh.bilioni 7.8 kutoka hospitali za rufaa za mikoa 32 yalikataliwa kutokana na kasoro mbalimbali kama vile uthibitisho usio sahihi, nambari za magonjwa zisizo sahihi, na kutofuata mwongozo wa matibabu.

Nilibaini kuwa kati ya Sh. bilioni 60.63 zilizodaiwa, ni bilioni 52.83 (87%) ya fedha zilizodaiwa zilikubaliwa na kurejeshwa, ikasababisha upotevu wa Sh. bilioni 7.8 (13%) kwa hospitali. Ukilinganishwa na mwaka uliopita madai yaliyokataliwa yameongezeka kwa Sh. bilioni 4.62 ambayo ni sawa na asilimia 145%, hii inaonesha kuwa mapendekezo yangu ya awali hayakutekelezwa kikamilifu. Orodha ya hospitali zenye kasoro zilizobainishwa zinaonekana katika **Kiambatisho Na. XXIX**. Ni maoni yangu kuwa, upotevu wa mapato unaojitokeza unaweza kuathiri sana utekelezaji

wa malengo ya hospitali za rufaa na uwezo wao wa kutoa huduma bora za afya kwa jamii.

Ninapendekeza kwamba Serikali kupitia Wizara ya Afya ianzishe programu ya mafunzo maalumu kwa watumishi wa afya ili kuwajengea uwezo wa kujaza fomu za madai ya bima ya afya kwa usahihi.

12.7 Hasara Iliyopatikana Kutokana na Dawa Zilizoisha Muda Wake Sh. Bilioni 2.24

Kanuni ya 254 sheria ya Fedha za Umma ya Mwaka 2001, inataka kwamba wakati maghala, magari, mitambo au vifaa vinakuwa havifai kutumika, vinapaswa kuhifadhiwa hadi kiasi kinachotosha kinakusanyika ili kuomba Bodi ya Uharibifu kufanya ukaguzi. Afisa wa Uhasibu lazima atayarishe orodha ya vitu hivyo pamoja na maelezo ya umri na thamani yao, na kuwasilisha nakala nne za orodha hizo kwa Mhasibu Mkuu kuomba kwamba Bodi iteuliwe kufanya ukaguzi na kutoa mapendekezo kuhusu uharibifu na utupaji.

Kanuni ya 10 ya Sheria ya Tanzania ya Chakula, Dawa na Vipodozi (Uainishaji wa Dawa) ya Mwaka 2015 inataka Mkuu wa kituo au daktari wa meno kuamuru kuharibu bidhaa zisizofaa.

Hata hivyo, wakati nilipochunguza rejista za dawa za matibabu zilizoisha muda wake, nilibaini kuwa hospitali za rufaa za mikoa 17 zilikuwa zimehifadhi dawa za matibabu zilizoisha muda wake kwa wastani wa muda miezi mitatu hadi miaka 10 zenye thamani ya Sh. Bilioni 2.24. Rejea **Jedwali Na. 88** kwa maelezo.

Jedwali Na. 88: Hasara Iliyopatikana Kutokana na Dawa zilizoisha Muda wake

Na.	Jina la Hospitali za Rufaa na Hospitali Maalumu	Kiasi (Sh.)
1	Benjamin Mkapa	245,172,201
2	Chato ZRH	21,037,595
3	Ligula RRH	67,039,048
4	Mtwara ZRH	769,932
5	Mbeya ZRH	104,402,937
6	Iringa	13,077,378
7	Mawenzi RRH	10,105,184
8	Morogoro	81,183,653

Na.	Jina la Hospitali za Rufaa na Hospitali Maalumu	Kiasi (Sh.)
9	Songea	587,750,116
10	Katavi	305,662,766
11	Simiyu	63,091,690
12	Temeke	650,436,836
13	Sekou Toure	24,971,235
14	Njombe	40,364,956
15	Tabora	3,292,058
16	Tanga	10,158,337
17	Meru	10,281,687
	Jumla	**2,238,797,609**


Chanzo: *Barua za Mapungufu kwa Menejimenti za 2021/22*

Mlundikano wa dawa zilizoisha muda wake umetokana na ununuzi au upokeaji wa dawa zenye muda mfupi wa matumizi kutoka Bohari Kuu ya Dawa (MSD) na kukosekana kwa utaratibu unaohakikisha kuwa akiba ya dawa iliyopo inatolewa kwa msingi wa inayokaribia kuisha muda wa matumizi inatolewa Kwanza (First Expiry First Out-FEFO).

Kushindwa kuteketeza dawa zilizoisha muda wake kunaweza kusababisha hatari kwa umma iwapo zitatumika kwa bahati mbaya au kuangukia mikononi mwa watu wasio waaminifu.

Kwa kulinganisha na mwaka uliopita (2020/21) nilibaini kuwa dawa zilizoisha muda wake zimeongezeka kwa Sh. milioni 610, sawa na asilimia 37, hivyo inamaanisha kuwa mapendekezo ya ukaguzi wa miaka iliyopita hayakuzingatiwa ipasavyo na Hospitali za Rufaa husika. Kielelezo Na. 11 kinaonyesha ulinganisho wa hasara iliyopatikana kwa sababu ya dawa zilizo kwisha muda wake.

Kielelezo Na. 11: Ulinganisho wa Hasara Kutokana na Dawa zilizoisha Muda Wake



Chanzo: *Barua za Mapungufu kwa Menejimenti za 2021/22*

Ili kukabiliana na suala hili, napendekeza hospitali za rufaa za mikoa kuteketeza dawa zilizoisha muda wake kulingana na matakwa ya sheria. Zaidi ya hayo, wanapaswa kuepuka kupokea dawa zenye muda mfupi wa matumizi ili kuzuia kumalizika mapema kwa muda wa matumizi ya dawa na vifaa tiba.

12.8 Ununuzi wa Dawa na Vifaa Tiba bila Kuthibitisha Upatikanaji wake Kutoka Bohari Kuu ya Dawa Sh. Bilioni 1.75

Kwa mujibu wa Kanuni ya 140(5) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013, na Aya ya 2.4 ya Mwongozo wa Uendeshaji wa Hospitali za Rufaa za Mikoa uliotolewa mwezi Juni mwaka 2019 na Wizara ya Afya, endapo vitu vilivyotakiwa havipatikani katika Bohari Kuu ya Dawa, taarifa ya kutopatikana lazima itolewe kwa taasisi husika ndani ya siku moja.

Hata hivyo, wakati wa ukaguzi wa hospitali za rufaa za mikoa, nilibaini kuwa hospitali tano zilinunua dawa na vifaa tiba vyenye thamani ya Sh. bilioni 1.75 kutoka kwa wauzaji binafsi bila Bohari Kuu ya Dawa kudhibitisha kutokuwepo kwa dawa hizo kama inavyohitajika na kanuni za ununuzi wa umma. Rejea maelezo katika **Jedwali Na. 89**.

Jedwali Na. 89: Orodha ya Hospitali Zenye Ununuzi wa Dawa bila Uthibitisho Kutoka Bohari Kuu ya Dawa

Na.	Jina la hospitali	Kiasi Sh.
1	Benjamini Mkapa SRH	410,081,100
2	Iringa RRH	263,691,390
3	Mawenzi RRH	189,418,075
4	Morogoro RRH	7,400,000
5	Musoma RRH	876,414,914
Jumla		**1,747,005,479**

Chanzo: *Barua za Mapungufu kwa Menejimenti za 2021/22*

Utaratibu huu unaweza kusababisha gharama kubwa ikilinganishwa na Bohari Kuu ya Dawa na hatimaye kusababisha hasara kwa Serikali, na inaweza kusababisha ubadhirifu katika ngazi ya hospitali.

Aidha, ikilinganishwa na ripoti yangu ya awali ya mwaka wa fedha 2020/21 ununuzi wadawa na vifaa tiba bila kuthibitisha upatikanaji wake kutoka Bohari Kuu ya Dawa umeongezeka kwa kiasi cha Sh bilioni 1.44, ambayo ni ongezeko la matumizi ya fedha kwa asilimia 461. Hii inaonesha kuwa Serikali haijashughulikia ipasavyo suala hili.

Mapendekezo yangu kwa Serikali, Hospitali zihakikishe kuwa manunuzi yote ya dawa na vifaa vingine vya hospitali hayafanywi kutoka kwa wasambazaji binafsi pasipokuwa na uthibitisho wa ukosefu wa dawa kutoka Bohari Kuu ya Dawa, kulingana na kanuni.

12.9 Kucheleweshwa kwa Upokeaji wa Dawa na Vifaa vya Matibabu Vilivyolipiwa, Vyenye Thamani ya Sh. Bilioni 16.85

Kanuni ya 114 (a) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma, 2013 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2016, inataka taasisi nunuzi kuwa na jukumu la usimamizi madhubuti wa ununuzi wowote wa bidhaa, huduma au kazi ambazo inafanya na itafuatilia gharama na upokeaji wa bidhaa na huduma kwa wakati na kwa kiwango sahihi na ubora ulioainishwa katika kila mkataba.

Katika kipindi cha ukaguzi wa malipo yaliyofanywa na hospitali za rufaa za mikoa dhidi ya manunuzi ya dawa na vifaa tiba, niligundua kuwa hadi tarehe 30 Juni, 2022 wazabuni hawakuwa wamepeleka dawa na vifaa tiba vyenye thamani ya Sh. bilioni 16.85 kwa hospitali za rufaa za mikoa 18. Hii

ilisababishwa na ununuzi wa dawa na vifaa tiba kutoka kwa wasambazaji wenye uzoefu duni na uwezo mdogo wa usambazaji.

Ni maoni yangu kwamba, kutosambaza dawa na vifaa tiba huathiri uwezo wa hospitali kutoa huduma bora za afya kwa jamii. Orodha ya hospitali za rufaa za mikoa zenye changamoto hii iko katika **Kiambatisho Na. XXX**.

Ninapendekeza Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Hospitali husika kuandaa mikakati itakayohakikisha kuwa dawa na vifaa vya matibabu vinawasilishwa na wazabuni ili kuimarisha utoaji huduma katika vituo hivyo. Zaidi ya hayo, wazabuni ambao wamezidisha muda uliokubalika wa utoaji wa dawa na vifaa vya matibabu wafutiwe mikataba, na malipo yoyote yaliyofanywa kwao, pamoja na uharibifu uliopatikana, yarejeshwe kwa wakati.

12.10 Vifaa vya Matibabu vyenye Thamani ya Sh. Bilion 4.56 Vimenunuliwa Lakini Havitumiki.

Katika ukaguzi wangu, nilibaini kuwa hospitali za rufaa za mikoa 12 zilinunua vifaa tiba vyenye jumla ya thamani ya Sh. bilioni 4.56, lakini vifaa hivyo havikuanza kutumika kama ilivyokusudiwa kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na ujenzi usiokamilika wa jengo linalohitajika kufunga vifaa hivyo na ukosefu wa wataalamu wa kutumia vifaa hivyo. Huu ni ukiukwaji wa kanuni za 87(1)(h) za Kanuni za Fedha za Umma za mwaka 2001 ambazo zinataka vifaa vilivyonunuliwa viwezekutumika mara moja. **Kiambatisho Na. XXXI** kinaonesha orodha ya hospitali zenye vifaa tiba na majengo yasiyotumika.

Ucheleweshaji huu unaonesha kuwa mchakato wa ununuzi haukuzingatia mahitaji halisi, bali ilifanyika kwa kubashili. Zaidi ya hayo, ikiwa vifaa hivyo bado havitumiki kwa muda mrefu, vinaweza kupitwa na wakati hivyo kutofaa kutokana na maendeleo ya kiteknolojia.

Napendekeza hospitali za rufaa za mikoa zifanye manunuzi ya vifaa baada ya kubaini mahitaji yao halisi na kuzingatia mambo ya kimazingira na kiteknolojia. Pia, Afisa Masuuli ahakikishe anatatua changamoto zilizobainishwa kiasi kwamba vifaa vilivyonunuliwa vinatumika bila kuchelewa zaidi.

12.11 Kuchelewa Kukamilika kwa Ujenzi wa Majengo ya Hospitali za Rufaa za Mikoa yenye Thamani ya Sh. Bilioni 74.15

Katika kutathmini utekelezaji wa miradi katika hospitali za rufaa za mikoa, nilibaini kuwa miradi ya hospitali, ikiwa ni pamoja na ujenzi wa wodi, majengo ya radiolojia, ICU, na nyumba za watumishi zenye thamani ya jumla ya Sh. bilion 74.15, zilikuwa zinajengwa, lakini kulikuwa na ucheleweshaji mkubwa wa ukamilishaji wake.

Tathmini yangu, kulingana na ripoti za utekelezaji wa ujenzi, nakufanya ziara katika miradi, na tathmini ya mikataba, nilibaini kuwa ujenzi wa majengo ulikuwa unachukua miezi mitatu hadi miaka mitatu zaidi kuliko ilivyotarajiwa. Sababu za kuchelewa kwa ujenzi huo ni pamoja na kuchelewa kutoa fedha kwa wakati kutoka Wizara ya Afya kwenda hospitalini, kuchelewa kwa usambazaji wa vifaa vya ujenzi na uhaba wa watumishi wa kiufundi, ufadhili usioridhisha na hali mbaya ya hewa. Orodha ya hospitali za rufaa zilizochelewa kumaliza ujenzi wa majengo ya hospitali iko katika **Kiambatisho Na. XXXII**.

Kutokana na kuongezeka kwa idadi ya hospitali za rufaa za mikoa zenye miradi ya ujenzi iliyocheleweshwa kufikia 15 ambayo ni sawa na asilimia 214 ikilinganishwa na mwaka uliotangulia, kuna hatari kubwa kwamba Serikali inaweza kushindwa kufikia malengo yake ya kuanzisha hospitali hizo kama ilivyoelezwa katika Dira ya Maendeleo ya Tanzania ya mwaka 2025.

Ninapendekeza Afisa Masuuli wa Wizara ya Afya kwa kushirikiana na uongozi wa hospitali husika katika ujenzi wa majengo ya hospitali nchini, kuchukua hatua za kuanzisha mikakati ambayo itahakikisha miradi inatekelezwa ndani ya muda uliokubaliwa, hivyo kufikia malengo yaliyokusudiwa.

12.12 Vifaa na Mashine za Hospitali Kutofanyiwa Matengenezo na Kutotumika kabisa

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa hospitali za rufaa za mikoa zinamiliki mali mbalimbali ikiwa ni pamoja na vifaa na mashine ili kuongeza ubora wa utoaji huduma za afya, matibabu na kuhakikisha kuwa thamani ya fedha inapatikana katika matumizi ya mashine hizo.

Katika ukaguzi wangu wa usimamizi wa matumizi ya vifaa na mashine za hospitali, nilibaini kuwa hospitali za rufaa tano zina mashine na vifaa ambavyo havitumiki na vingine kutofanya kazi kabisa. Sababu kuu ya suala hili ni kutokana na kukosekana kwa wataalamu na fedha za kununua vifaa vya kutosha na kufanya ukarabati mkubwa. **Jedwali Na. 90** linaonyesha vifaa na mashine za hospitali zinazohitaji ukarabati.

Jedwali Na. 90: Vifaa na Mashine za Hospitali Kutofanyiwa Matengenezo na Kutotumika Kabisa.

Na.	Jina la hospitali	Hoja	Maelezo
1	Mbeya ZRH	Vifaa tiba na mashine visivyo fanyiwa matengenezo na havijaondolewa	Wakati wa ukaguzi, nilibaini kuwepo kwa vifaa tiba mbalimbali visiyoweza kutumika kama vile vifaa vya uchambuzi wa kemia, mchanganuo wa hematolojia, incubator na mengine ambayo havijaondolewa.
2	Musoma RRH	Vifaa na mashine visivyo fanyiwa matengenezo na havijaondolewa.	Nilibaini kuwepo kwa vifaa tiba na mashine mbalimbali visiyofanyiwa matengenezo kama vile vitanda vya hospitali, viti vya ofisi, viti vya magurudumu, sinki la kunawa na mengine ambayo havijaondolewa mpaka wakati wa kuhitimisha ukaguzi mnamo Septemba 2022.
3	Geita	Kutofanya kazi kwa baadhi ya vifaa tiba muhimu vya Huduma ya afya	Ukaguzi wa utoaji huduma za afya uliofanywa hospitali ya rufaa ya mkoa Geita nilibaini kuwa baadhi ya vifaa tiba muhimu vya hospitali kwa ajili ya utoaji wa huduma havifanyi kazi ipasavyo hivyo kusababisha kukosekana kwa huduma za kawaida za matibabu. Pia baadhi ya vifaa vinakosa baadhi ya vipengele muhimu kwa ajili ya kufanya kazi vizuri.
4	Tumbi	Vifaa tiba visivyofanya kazi	Mapitio ya ufanisi wa mashine na vifaa tiba vya hospitali nilibaini kwa baadhi ya vifaa havifanyikazi kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo huduma na kukosa vipuri.
5	Tanga	Vifaa tiba ambavyo havifanyi kazi	Kwenye ukaguzi wa matumizi ya vifaa tiba vya hospitali nilibaini kuwa kuna vifaa havifanyikazi kama vile Oxygen Concentrator, Suction Mashine na Patient Monitor.

Chanzo: : *Taarifa ya ukaguzi kwa menejiment 2021/22*

Hali hii inaweza kusababisha kutoaminika kwa mfumo wakutoa huduma za afya kwa wagonjwa, na kusababisha jamii kupunguza matumizi ya mfumo wakutoa huduma za afya. Aidha, kutokana na mabadiliko ya kiteknolojia, yanaweza kufanya mashine kupitwa na wakati kabla ya kutumika kikamilifu na hivyo kutopata thamani ya fedha katika matumizi ya vifaa tiba.

Ili kukabiliana na tatizo hili, napendekeza Serikali kupitia Wizara ya Afya itenge fedha za kutosha kuwezesha huduma za ukarabati mkubwa wa vifaa tiba na mashine za hospitali.

12.13 Mtiririko wa Taarifa Zisizoendana Kati ya Mfumo wa Malipo wa Serikali (GePG) na Mifumo ya Kielectroniki ya GoT-HoMIS, Afyacare na eHMIS

Katika kupitia mifumo ya TEHAMA inayosaidia uendeshaji wa hospitali za rufaa za mikoa, nilibaini kuwa kulikuwa na tofauti kwenye mtiririko wa takwimu na taarifa kati ya mifumo ya GoT-HoMIS, Afyacare na GePG kinyume na kifungu Na. 26(1) ya Sheria ya Serikali Mtandao, 2019. Mifumo hii hutumiwa na hospitali kusajili wagonjwa na hati za madai, na imeunganishwa na GePG kwa ajili ya ukusanyaji wa mapato.

Zaidi ya hayo, nilibaini kuwa hakujafanyika usuluhishi wa Sh. bilioni 14.1 kati ya taarifa ya mfumo wa malipo wa Serikali (GePG) na taarifa za makusanyo kutoka mifumo ya kielectroniki ya GoT-HoMIS, eHMIS na Afya Care kutoka hospitali za rufaa tisa kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 91.**

Jedwali Na. 91: Orodha ya Hospitali za Rufaa Zenye Makusanyo Yasiyolingana na Taarifa za Mfumo

Na.	Jina la Hospitali	Makusanyo katika mfumo wa malipo wa Serikali (Sh.)	Jumla ya Mkusanyo kwa GoT-HoMIS/eHMS & Afyacare (Sh.)	Tofauti (Sh.)
1	Iringa RRH	293,854,848	117,984,376	175,870,472
2	Morogoro	1,082,653,065	1,326,363,663	243,710,598
3	Kibong'to	1,124,458,326	255,291,036	869,167,290
4	Simiyu	570,511,530	392,117,790	178,393,740
5	Manyara	62,833,098	54,699,749	8,133,349
6	Temeke	2,178,715,327	2,321,543,870	142,828,543
7	Njombe	881,002,966	1,170,544,689	289,541,723
8	Tabora	788,728,764.00	1,761,565,073	972,836,309

Na.	Jina la Hospitali	Makusanyo katika mfumo wa malipo wa Serikali (Sh.)	Jumla ya Mkusanyo kwa GoT-HoMIS/eHMS & Afyacare (Sh.)	Tofauti (Sh.)
9	Tanga	3,191,057,783.69	14,392,250,172	11,201,192,388
	Jumla	**10,173,815,707**	**21,792,360,418**	**14,081,674,412**

Chanzo: *Taarifa ya ukaguzi kwa menejimenti 2021/22*

Masuala haya yalitokana na kutopata msaada wa kiufundi wakutosha kwa watumiaji wa mifumo kutoka Wizara ya Afya, ambayo ilichangia kupatikana kwa taarifa zisizoaminika, na inaweza kusababisha upotoshaji katika taarifa za kifedha. Hali hiyo pia inasababisha Wizara ya Afya kutopata taarifa sahihi za wagonjwa wa wanaotibiwa na hospitali za rufaa na hospitali maalumu

Kwa mujibu wa uchambuzi wangu, kiasi cha makusanyo yasiyofanyiwa usuluhishi kimeongezeka kwa Sh. bilioni 4.7 ambayo ni sawa na asilimia 50 ikilinganishwa na mwaka wa fedha uliopita wa 2020/21. Hii inaonyesha kuwa mapendekezo niliyokuwa nimeyatoa hapo awali hayakutekelezwa kwa ufanisi.

Ili kutatua masuala haya, nashauri Hospitali zishirikiane na Wizara ya Afya kutumia mfumo kwa ufanisi, kushughulikia mapungufu niliyoyataja, na kuanzisha mfumo wa kawaida ambao hospitali za rufaa, kanda na maalumu zitatumia kurekodi taarifa za wagonjwa. Hii itasaidia kuchochea uwajibikaji na uwazi katika mfumo wa ukusanyaji wa mapato.



SURA YA KUMI NA TATU

UKAGUZI WA OFISI ZA BALOZI ZA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

13.1 Utangulizi

Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ina jukumu la kuratibu mahusiano kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na nchi nyingine kupitia Balozi zake, ambapo mwakilishi wa Tanzania anaidhinishwa. Balozi hizi zina jukumu muhimu katika kukuza maslahi ya Tanzania nje ya nchi, kuwezesha biashara na uwekezaji, na kudumisha uhusiano wa kidiplomasia.

Sura hii inabainisha maeneo kadhaa ambayo yanahitaji ufuatiliaji wa Serikali ili kuongeza uwezo wa ofisi za Balozi katika kukuza mahusiano yenye maslahi ya nchi nje ya nchi. Maeneo hayo ni pamoja na usimamizi wa mapato na bajeti, usimamizi wa matumizi, usimamizi wa mali, masuala ya utawala, na masuala ya diplomasia ya kiuchumi:

13.2 Muhtasari wa Fedha na Utekelezaji wa Bajeti

Balozi za Tanzania nje ya nchi huendeshwa kwa kiasi na fedha za matumizi ya kawaida na maendeleo kutoka Hazina ya serikali, pamoja na vyanzo vingine. Mapitio ya taarifa za fedha za ofisi za balozi kwa mwaka wa fedha 2021/22 zinaonesha kuwa serikali iliidhinisha bajeti ya kiasi cha Sh. bilioni 144.51 kwa Balozi arobaini na tatu (43). Kiasi hiki ni jumla tu ya fedha zitakazotolewa na serikali kutoka mfuko mkuu wa Hazina kwenda katika ofisi za Balozi.

Hata hivyo, baada ya mapitio ya kina katika utekelezaji wa bajeti na taarifa za fedha za Balozi hizo, nilibaini kuwa ni Sh. bilioni 128.61 pekee sawa na 89% ya bajeti iliyoidhinishwa, ndiyo iliyotolewa. Hii inaonyesha kuwa

kulikuwa na upungufu wa kiasi cha Sh. bilioni 15.9 ambacho ni sawa na 11% ya bajeti yote iliyoidhinishwa.

Kutolewa kidogo kwa fedha kunaweza kuwa na athari katika uendeshaji wa shughuli za Balozi, kwani kunaweza kusababisha kutokuwepo kwa fedha za kutekeleza shughuli za ofisi za Balozi kwa ufanisi. Kwa kuzingatia kuwa ofisi za Balozi zinategemea kwa kiasi kikubwa fedha kutoka serikalini, hii inaweza kuathiri utendaji na kuathiri juhudi za Balozi katika kukuza maslahi ya nchi yenye thamani nje ya nchi.

Ninapendekeza Serikali iongeze juhudi zake katika kutekeleza kwa ufanisi bajeti zilizoidhinishwa ili kuhakikisha kunakuwa na mgao wa kutosha wa fedha kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa shughuli zilizopangwa.

13.3 Masuala ya Diplomasia ya Uchumi

13.3.1 Mgogoro wa Muda Mrefu Kuhusu Deni Lisilolipwa la Kampuni ya M/S Laemthong Rice Company Ltd Lenye thamani ya dola za Marekani 12,935,685

Baada ya kufanya mapitio ya nyaraka na ripoti za robo mwaka katika Ubalozi wa Tanzania Kuala Lumpur, Malaysia, nilibaini kuwa mwaka 1985, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilisaini mikataba na Kampuni ya M/s Laemthong Rice Company Ltd ya Thailand kununua tani 63,400 za mchele wenye thamani ya Dola za Marekani 12,935,685. Hata hivyo, hadi kufikia Mei 1997, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilikuwa imelipa jumla ya Dola za Marekani 5,700,000.

Kampuni ya M/s Laemthong Rice Company Ltd ilifungua kesi ya madai dhidi ya Serikali katika Mahakama Kuu ya Zanzibar. Mnamo tarehe 16 Mei 1997, Mahakama Kuu ya Zanzibar iliamuru serikali kulipa jumla ya Dola za Marekani 69,044,651, ambazo zinajumuisha deni kuu na riba ya 25% kwa mwaka. Serikali ilipinga uamuzi huo, na kufanya kati ya Mei 1997 na 26 Agosti 1998 Mahakama Kuu ya Zanzibar kuendelea kutoa maamuzi yenye kugusa pande zote mbili. Hata hivyo, Serikali ililipa Dola za Marekani 1,500,470, na kufanya hadi kufikia Machi 1998 malipo yote kuwa Dola za Marekani 7,200,470, huku ikibakiza deni la Dola za Marekani 5,735,215 (bila riba).

Kampuni ya M/s Laemthong Rice Company Ltd haikuridhika na maamuzi yaliyotolewa na kukata rufaa katika Mahakama ya Rufaa ya Tanzania. Tarehe 18 Desemba 2000, Mahakama ya Rufaa ya Tanzania ilibatilisha hukumu ya 26 Agosti 1998, ambayo iliamuru serikali ya Zanzibar kumlipa mdai Dola za Marekani 15,500,000 badala ya deni kuu na riba ya 25% ambayo ilikuwa sawa na Dola za Marekani 69,044,651 kama ilivyoamuliwa katika hukumu ya awali ya 16 Mei 1997. Mahakama ya Rufaa ilielekeza utekelezaji wa hukumu ya 16 Mei 1997.

Taarifa zinaonesha kwamba mwaka 2001, kupitia mpango wa Benki ya Dunia wa kununua madeni, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilipanga kulipa Dola za Marekani 22,612,252.10, ambayo ni 12% ya deni lililokuwapo kwa wakati huo la Dola za Marekani 188,435,434.96. Hata hivyo, M/s Laemthong Rice Company Ltd ilikataa ofa hiyo na kuendelea kutoza riba ya 25%.

Taarifa zinaonesha kuwa hadi tarehe 27 Aprili 2022, deni lilikuwa Dola za Marekani 41,522,475,277.12 ambapo kampuni ya M/s Laemthong Rice Company Ltd imetishia kukamata mali za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iwapo deni hilo halitalipwa. Kampuni hiyo pia ilifanya jaribio ambalo halikufanikiwa la kukamata meli mpya ya Zanzibar wakati ikiwa safarini. Zaidi ya hayo, kampuni hiyo imetishia kupeleka suala hilo kwa Umoja wa Mataifa kupitia Shirika la Biashara Duniani (WTO), jambo ambalo linaweza kuwa na athari kwa serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Napendekeza Serikali ya Tanzania na Zanzibar ifanye mapitio na tathmini ya kina juu ya madai yaliyotolewa na M/s Laemthong Rice Company Ltd kuhusu deni ambalo bado halijalipwa. Iwapo kutatokea kutokuelewana, pande zote zinapaswa kufuata taratibu za kisheria na kutafuta njia mbadala ya kusuluhisha kupitia mazungumzo.

13.3.2 Ushirikiano Usioridhisha kutoka kwa Wizara na Watendaji wengine wa Serikali katika Kutekeleza Fursa Zinazopatikana katika Balozi za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Aya ya 26 ya Sera Mpya ya Mambo ya Nje ya mwaka 2001, inalenga kukuza na kulinda maslahi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia diplomasia ya uchumi na kuoanisha uhusiano na mataifa mengine na vyombo vya kimataifa na maslahi ya kiuchumi. Aya ya 45 inaitaka Wizara ya Mambo ya

Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kushirikiana na Wizara na taasisi nyingine katika kutekeleza kanuni na malengo ya sera hiyo.

Wakati wa ukaguzi, nilitathmini jinsi Balozi za Tanzania zinavyotekeleza mipango yao ili kufikia malengo ya sera ya mambo ya nje ya nchi. Nilibaini kuwa, Balozi hazipewi ushirikiano wakutosha kutoka kwa Wizara na watendaji wengine wa Serikali kuhusu fursa zinazopatikana kutokana na juhudi zao katika nchi zinazosimamia. Licha ya Balozi hizo kufanya ufuatiliaji kadhaa juu ya utekelezaji wa fursa hizo, Balozi zimekuwa zikipokea ushirikiano hafifu kutoka kwa watendaji wa serikali.

Nimetoa muhtasari mfupi wa baadhi ya maeneo yenye fursa hizo hapa chini, na taarifa kwa kina zinapatikana katika **Kiambatisho Na. XXXIII.**

a) Nimepokea taarifa kutoka ubalozi wa Tanzania huko New Delhi, India ambayo inaonesha kuwa Tanzania ilipendekezwa kuwa sehemu ya kuanzisha Chuo cha Taasisi ya Teknolojia ya India. Hata hivyo, hakuna majibu yaliyopatikana kutoka Wizara ya Mambo ya Nje kuhusu ushirikiano kati ya Wizara ya Mambo ya Nje na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuhusu utekelezaji wa fursa hiyo.

b) Pia nilibaini kutoka kwenye Ubalozi wa Tanzania Jijini New Delhi kuwa mapendekezo ya makubaliano ya ushirikiano kati ya Hospitali ya Apollo, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa ajili ya ujenzi wa hospitali maalumu Jijini Dar es Salaam hayajafanikiwa hadi sasa.

c) Kutoka katika ubalozi wa Tanzania Jijini Beijing, China, nilibaini ukosefu wa ushirikiano kutoka kwa watendaji wa Serikali kuhusu uwezekano wa fursa za biashara na kampuni ya Guangzhou Light Holding Limited, ambayo ilikuwa inatafuta kufanya biashara na Tanzania katika bidhaa za maharage ya soya, kahawa mbichi, na korosho ghafi.

d) Taarifa zilizotolewa na Ubalozi wa Tanzania nchini Malaysia zilionesha fursa za ufadhili wa masomo kutoka Chuo Kikuu cha Selangor nchini humo, hata hivyo hakukuwa na majibu mazuri kutoka kwa wahusika wa sekta hiyo.

e) Ubalozi wa Tanzania uliopo mjini Seoul, Korea Kusini uliripoti fursa mbalimbali za biashara, uwekezaji, sayansi na teknolojia, usafirishaji, na ushirikiano na kampuni ya Korea Kusini, ambayo inajishughulisha na uzalishaji wa mafuta ya kupikia, pamoja na kampuni ya Dongil Shipyard Co. Ltd ya Korea Kusini, ambayo inajihusisha na ujenzi, ukarabati na uvuvi wa bahari kuu, lakini, hakukuwa na majibu yoyote kutoka kwa walengwa.

f) Pia, Balozi za Tanzania nchini Malawi, Rwanda, na Brazil pia zilieleza fursa za biashara, uwekezaji, sayansi na teknolojia, pamoja na usafirishaji.

Kwa mtazamo wangu, sababu ya hali hii inatokana na kutokuwa na nia ya dhati miongoni mwa watendaji wa Serikali katika kufuatilia fursa zinazotolewa na Balozi za Tanzania. Hivyo kukatisha tamaa juhudi zinazofanywa na Balozi hizo.

Ninapendekeza Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki iweke utaratibu wa kuimarisha ushirikiano wa karibu na watendaji wengine wa Serikali ili kuhakikisha kwamba fursa zinazotolewa zinachambuliwa na kutumiwa kwa wakati na ufanisi. Hii itahakikisha kwamba Balozi zinapata ushirikiano wa kutosha kuweza kutumia fursa hizi kikamilifu.

13.3.3 Changamoto Zinazokabili Ofisi za Balozi za Tanzania katika Utekelezaji wa Majukumu yake

Aya ya 45 ya Sera Mpya ya Mambo ya Nje ya 2001, inaiagiza Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kuwa mratibu wa sera, kuhakikisha kanuni na malengo ya sera hiyo yanatekelezwa na kufanya kazi. Ili kufikia malengo ya sera, ofisi za Balozi lazima zitengewe rasilimali za kutosha na mazingira mazuri ya kufanyia kazi. Kwa kufanya hivyo, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki inaweza kuboresha ufanisi wa Balozi hizo katika kutoa huduma za kibalozi, kukuza biashara, uwekezaji na maslahi ya kibiashara.

Katika ukaguzi wangu, nilitathmini namna Balozi za Tanzania zinavyosimamia vizuri fedha za umma na rasilimali nyingine katika kukuza diplomasia ya uchumi. Hata hivyo, nimebaini changamoto kadhaa

zinazoathiri utekelezaji wa shughuli za diplomasia ya uchumi katika Balozi. Changamoto hizi zimeorodheshwa hapa chini na maelezo zaidi yanaweza kupatikana katika **Kiambatisho Na. XXXIV.**

a) Nilibaini kuwa Balozi za Tanzania zilizopo nchini Kenya, Nigeria, Zimbabwe, Namibia na Cuba zilikabiliwa na ufinyu wa fedha ulioathiri uwezo wao wa kufanya shughuli mbalimbali zilizopangwa. Hasa, nilibaini kuwa kulikuwa na ucheleweshaji wa fedha, ambao umeelezwa kwa kina katika katika kipengele cha utekelezaji wa bajeti katika sura hii.

b) Kuna uhaba wa wawakilishi wa heshima katika Balozi zinazosimamia nchi zaidi ya moja ambao unaathiri uwezo wa Balozi katika kutoa huduma za kibalozi. Balozi za Tanzania ziliyopo Abuja, Nigeria na Urusi, kila mmoja unasimamia nchi 15 zilizoidhinishwa, wakati Ubalozi wa Tanzania uliopo Canada, unasimamia nchi nne huku Ubalozi wa Tanzania huko Roma, Italia ukisimamia nchi kumi. Ubalozi wa Tanzania uliopo Kuala Lumpur unahitaji mabalozi wa heshima watano kushughulikia maeneo hayo, lakini bado kwa ujumla kuna uhaba wa mabalozi wa heshima.

c) Aidha, kuna ukosefu wa utaratibu mzuri wa kuratibu na kufuatilia mapendekezo ya uwekezaji na biashara yanayobainishwa na Balozi, na kusababisha kuchelewa kwa utekelezaji wake. Kukosekana kwa mpango mkakati unaounganisha malengo ya Balozi na malengo ya Serikali kutoka kwenye mpango mkakati wa Serikali, pia unaathiri ufanisi wa Balozi katika kukuza na kuimarisha diplomasia ya kiuchumi.

Kwa maoni yangu, kwa changamoto hizo ofisi za Balozi zinaweza kuona ugumu katika kukuza diplomasia ya uchumi kwa ufanisi na hivyo, kusababisha ukosefu wa fursa katika jukwaa la kimataifa.

Ninapendekeza Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kuweka mazingira mazuri ya utendaji kazi wa ofisi za Balozi na kushirikiana na watendaji wengine wa Serikali, ili kuhakikisha kuwa rasilimali zinatengwa ipasavyo na kwa wakati ili kuwezesha utekelezaji wa shughuli zao.

13.4 Usimamizi wa Mapato

Nilifanya tathmini ya usimamizi wa mapato katika Balozi za Tanzania, ambao unajumuisha fedha kutoka Serikalini na makusanyo kutoka vyanzo vingine, nilibaini yafuatayo:

13.4.1 Kutokuwasilisha Makusanyo ya Kodi za Pango na Matumizi ya Sh. Milioni 880.76 kutoka katika Akaunti ya Amana katika Ubalozi wa Tanzania New York

Kanuni ya 132 na 133 ya Kanuni za Fedha za Umma za mwaka 2001, zinataka Afisa anayehusika na kuidhinisha marejesho ya amana kuhakikisha kwamba lengo la kuweka amana limefikiwa na mlipwaji ana haki ya kulipwa kutoka kwenye akaunti ya amana au ni mwekaji wa awali. Pia, fedha zilizobaki katika akaunti ya amana kwa zaidi ya miaka mitano bila kudaiwa lazima zirudishwe katika mfuko mkuu.

Ukaguzi wa akaunti ya amana ya ubalozi wa New York katika Benki ya Amerika ulibaini kuwa hadi tarehe 1 Julai 2021, akaunti hiyo ilikuwa na salio la Dola za Marekani 1,038,681 sawa na Sh. bilioni 2.40 ambazo ni makusanyo yatokanayo na kodi zilizopokelewa kutoka kwa wapangaji wa kampuni inayomilikiwa na Serikali iliyopo Jijini New York. Hadi tarehe 30 Juni 2022, akaunti hiyo ilikuwa na salio la dola za Marekani 660,823, sawa na Sh. bilioni 1.52 baada ya ubalozi kuhamisha kiasi cha Dola za Marekani 377,857.64 sawa na Sh. milioni 880.76 kwa ajili ya kutatua changamoto ya fedha katika ofisi hiyo iliyotokana na kuchelewa kupokea fedha kutoka serikalini. Ubalozi ulihamisha fedha hizo ili kufidia upungufu wa fedha ikiwa na lengo la kurejesha fedha hizo pindi watakapopokea fedha kutoka serikalini. Hata hivyo, hawakufanya hivyo kwa wakati kutokana na kuchelewa kwa fedha kutoka Wizarani.

Kwa maoni yangu, hii ni kinyume na kanuni za fedha na inaongeza vihatarishi vya kutumia fedha ambazo hazijapangwa kwenye bajeti, pamoja na kutoa fursa ya matumizi mabaya ya fedha hizo.

Napendekeza menejimenti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango kuhakikisha fedha zinatolewa kwa wakati, na fedha zozote ambazo

hazitumiki zilizopo kwenye akaunti ya amana zinahamishiwa Mfuko Mkuu wa Serikali.

13.4.2 Ucheleweshaji wa Uwasilishaji wa Fedha ambazo Hazikutumika mpaka mwisho wa mwaka kwenda Mfuko Mkuu Sh. Milioni 951.75

Kifungu cha 28 cha Sheria ya Fedha za Umma [Sura. 348 Toleo la mwaka 2020] inasema kwamba, matumizi yoyote ya fedha za umma yanayoidhinishwa na Bunge kwa mwaka wa fedha, pamoja na waranti au idhini nyingine yoyote iliyotolewa chini ya sheria hii kwa mwaka huo wa fedha, yatakwisha mwishoni mwa mwaka huo. Salio lolote lisilotumika la fedha zilizotolewa kutoka kwenye Mfuko mkuu zitarejeshwa kwenye mfuko huo.

Hata hivyo, wakati wa ukaguzi wangu, nilibaini kuwa kiasi cha fedha cha Sh. milioni 951.75 ambacho hakikutumiwa na balozi tatu mpaka mwisho wa mwaka wa fedha hakikurudishwa katika mfuko mkuu kulingana na matakwa ya kifungu cha 28 cha Sheria ya Fedha za Umma. **Jedwali Na. 92** linaonesha orodha ya balozi zinazohusika.

Jedwali Na. 92: Fedha ambazo Hazikurejeshwa kwenye Mfuko Mkuu

Na.	Ubalozi	Kiasi (Sh.)
1.	Ubalozi wa Tanzania Moscow, Urusi	308,506,202
2.	Ubalozi wa Tanzania Beijing, China	638,604,320
3.	Ubalozi wa Tanzania Roma, Italia	4,638,087
Jumla		**951,748,609**

Chanzo: *Ripoti za Ukaguzi*

Nilibaini kwamba kutorejeshwa kwa fedha hizo, kunamaanisha kuwa shughuli zilizopangwa hazikutekelezwa na pia serikali haiwezi kuzitumia fedha hizo kugharamia miradi mingine.

Kutokana na hili, ninapendekeza kwamba kwa siku zijazo, Balozi zihakikishe kuwa fedha zote ambazo hazijatumika zinahamishwa kwa wakati kwenda katika mfuko mkuu kwa ajili ya kupangiwa na kutekeleza shughuli nyingine zilizopangwa na Serikali.

13.5 Usimamizi wa Matumizi

Katika usimamizi wa matumizi ya fedha za umma, nilibaini masuala yafuatayo:

13.5.1 Kupoteza kinga ya Kidiplomasia kwa Jengo lililotelekezwa Kumesababisha Ubalozi wa Tanzania Washington, DC, kulipa Kodi ya Jengo ya Sh. Milioni 283.39

Tarehe 17 Februari 2021, Ubalozi wa Tanzania Jijini Washington, DC ulipoteza hadhi yake ya kidiplomasia kwenye umiliki wa moja ya majengo yake kutokana na kutelekezwa na Serikali kushindwa kulikarabati. Hali hiyo ilisababisha jengo hilo kupoteza kinga yake ya kidiplomasia na Ubalozi kuwajibika kulipa kodi ya majengo kuanzia siku hiyo na kuendelea. Kodi ya majengo ya Dola za Marekani 62,518.67 kwa mwaka ilipaswa kulipwa. Hata hivyo, tarehe 26 Oktoba 2022, Serikali kupitia ubalozi huo ililipa Dola za Marekani 122,885, ambayo ni sawa na Sh. milioni 283.39 ikiwa ni kodi ya jengo hilo pamoja na riba. Ni maoni yangu kuwa, sio tu kwamba kupoteza kinga ya kidiplomasia kwenye umiliki wa jengo kunaharibu sifa ya nchi, lakini pia kunaisababishia Serikali kuingia gharama za ziada ambazo zingeweza kuepukika.

Ninapendekeza kuwa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kuharakisha ukarabati wa majengo ya ubalozi ili kuepuka matukio kama hayo siku za baadaye na kuokoa fedha za umma.

13.5.2 Kodi ya Ongezeko la Thamani iliyolipwa bila Kurejeshwa Sh. Milioni 406.06 katika Ubalozi wa Tanzania Moscow na Stockholm

Kifungu cha 23 na Kifungu cha 28 cha Mkataba wa Vienna wa Mahusiano ya Kidiplomasia wa mwaka 1961 vinahitaji nchi yenye Ubalozi na mkuu wa Ubalozi kusamehewa kodi yoyote inayohusiana na majengo ya Ubalozi, iwe yanamilikiwa au yamekodishwa, na ada na tozo zinazotozwa na Ubalozi wakati wa utekelezaji wa majukumu yake hazitatozwa kodi yoyote.

Kwa kawaida, maafisa ofisi za kibalozi zina kinga ya kodi kulingana na Mkataba wa Vienna. Hata hivyo, nimebaini kuwa kodi ya ongezeko la thamani kiasi cha Sh. milioni 406.06 ililipwa na balozi mbili bila kurudishwa. Malipo hayo yalifanyika kama ifuatavyo:

- Ubalozi wa Tanzania Jijini Moscow ulilipa kodi ya pango ya kuanzia tarehe 7 Octoba 2021 mpaka tarehe 29 Aprili 2022. Kodi hiyo ya pango iliyolipwa ilijumuisha kodi ya ongezeko la thamani ya Sh. milioni 252.82, kunyume na Mkataba wa Vienna.

- Aidha, nilibaini kuwa ubalozi wa Tanzania Stockholm, Sweden, ulilipa kodi ya ongezeko la thamani ya Sh. milioni 153.25 mnamo tarehe 28 Juni 2022 katika malipo ya mkataba wa ukarabati wa jengo. Kwa bahati mbaya, mamlaka ya kodi ya Sweden imezuia kurejeshwa pesa hizo kutokana na kupoteza kinga ya kidiplomasia ya jengo hilo ambalo halikuwa limekarabatiwa kwa muda mrefu.

Ninapendekeza ubalozi wa Tanzania Stockholm, Sweden ushughulikie mchakato wa kurejesha kinga ya kidiplomasia kwenye mali zake ili kuwezesha madai ya kurejeshewa kodi hiyo ya ongezeko la thamani. Zaidi, balozi zote mbili zinapaswa kuweka kipaumbele katika mawasiliano na ushirikiano na mamlaka husika katika nchi mwenyeji ili kuzuia masuala kama haya kutokea tena katika siku zijazo.

13.5.3 Matumizi yaliyofanyika nje ya Bajeti bila Idhini Sh. Milioni 161.94

Kifungu cha 27 (4) cha Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015 kinataka fedha zilizoidhinishwa na kupitishwa kwa ajili ya Serikali na taasisi za umma kutumika kwa kuzingatia malengo yaliyoelezwa na ndani ya makadirio yaliyowekwa.

Katika ukaguzi wangu, nilibaini kwamba kiasi cha Sh. 161.94 zilitumiwa na balozi mbili kwa shughuli ambazo hazikuwa zimeidhinishwa katika bajeti, bila kupata idhini kutoka kwa mamlaka husika kuhusu kubadilisha matumizi ya fedha hizo. Kiasi hiki ni pamoja na Sh. milioni 141.45 katika Ubalozi wa Tanzania Beijing, China na Sh. milioni 20.49 kwa Ubalozi wa Tanzania Addis Ababa, Ethiopia. Hali hii inachangiwa na mapungufu katika hatua ya awali ya maandalizi ya bajeti.

Ni maoni yangu kwamba, kutumia fedha kwa shughuli ambazo hazijaidhinishwa kunaweza kuathiri utekelezaji wa shughuli zilizopangwa na pia kutoa fursa kwa matumizi mabaya ya fedha za Serikali.

Kwa hivyo, ninapendekeza Mabalozi kusimamia kwa karibu utekelezaji wa bajeti ili kuzuia gharama yoyote ambayo haijaidhinishwa. Aidha, kwa siku zijazo, wanapaswa kuhakikisha kuwa kuna mipango madhubuti na kupata idhini ya kubadilisha matumizi ya fedha kabla ya kufanya matumizi.

13.5.4 Shughuli ambazo hazikutekelezwa kama zilivyopangwa zenye thamani ya Sh. Bilioni 1.53

Baada ya kufanya ukaguzi wa utekelezaji wa bajeti katika Balozi za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mwaka wa fedha 2021/22, nilibaini kwamba Balozi sita, kama ilivyobainishwa kwenye ripoti, kutokana na changamoto za kifedha na sababu zisizo za kifedha, kama vile vizuizi vya ugonjwa wa UVIKO-19, zilishindwa kutekeleza ipasavyo shughuli zilizopangwa kwenye bajeti zenye thamani ya Sh. bilioni 1.53. **Jedwali Na. 93** hapo chini linaonesha muhtasari wa bajeti iliyotengwa kwa shughuli husika na taarifa zaidi inapatikana katika **Kiambatisho Na. XXXV**.

Jedwali Na. 93: Bajeti pamoja na Balozi zenye Shughuli ambazo hazijatekelezwa

Na.	Ubalozi	Kiasi (Sh.)
1.	Ubalozi wa Tanzania Abuja, Nigeria	67,303,667
2.	Ubalozi wa Tanzania Harare, Zimbabwe	50,183,294
3.	Ubalozi wa Tanzania Jijini Nairobi, Kenya	243,957,203
4.	Ubalozi wa Tanzania mjini Havana -Cuba	71,802,438
5.	Ubalozi wa Tanzania Jijini Moscow, Urusi	21,185,630
6.	Ubalozi wa Tanzania Jijini Windhoek, Namibia	1,076,742,939
Jumla		**1,531,175,171**

Chanzo: *Ripoti za Ukaguzi*

Kwa maoni yangu, mapungufu haya yana athari kwenye uwezo wa Balozi kutimiza majukumu yao na kufikia malengo yaliyowekwa.

Ninapendekeza Menejimenti ya Balozi husika kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, kupanga upya bajeti ya shughuli ambazo hazijatekelezwa na kuhakikisha kwamba fedha za kutosha zinatengwa kwa wakati ili kufanikisha utekelezaji wake.

13.6 Usimamizi wa Mali

Wakati nikifanya ukaguzi katika usimamizi wa mali za umma, nilibaini kasoro mbalimbali, ambazo zimeelezwa kwa kina hapa chini;

13.6.1 Mapungufu katika utekelezaji wa Mpango wa Ununuzi, Ukarabati, na Ujenzi wa Majengo ya Balozi za Tanzania Nje ya Nchi

Mnamo Novemba 2020, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki iliandaa mpango wa kununua, kukarabati, na kujenga majengo ya Balozi za Tanzania nje ya nchi. Mpango huo ulikadiriwa kugharimu kiasi cha Sh. bilioni 187.18, ikiwa Sh. bilioni 54.75 zilipangwa kutumika katika ukarabati wa majengo yaliyopo katika balozi kumi na moja, huku Sh. bilioni 132.43 zikitengwa kwa ajili ya ujenzi wa majengo mapya na uzio katika balozi kumi na moja. Mradi huo ulipangwa kugharamiwa kikamilifu na Serikali na ulitarajiwa kufanyika kwa miaka mitano, kuanzia mwaka wa fedha 2020/21 hadi 2024/25.

Hata hivyo, hadi kufikia Desemba 2022 wakati wa ukaguzi wangu, baadhi ya maeneo ambayo yalipangwa kuanza kutekelezwa Novemba 2021 bado hayakuwa yamefanyiwa utekelezaji kutokana na taratibu mbalimbali za manunuzi zinazoendelea, na changamoto za kifedha ambazo Wizara inajaribu kukabiliana nazo. Hali hii imesababisha Serikali kuendelea kukabiliana na changamoto mbalimbali kama ifuatavyo:

13.6.1.1 Kuwepo kwa Mali zinazotumika Chini ya Kiwango katika Maeneo ya Kimkakati Kutokana na kuwa Chakavu

Nilibaini kuwa, Tanzania inamiliki mali zilizoko katika maeneo ya kimkakati katika balozi za Tanzania huko Harare, Lilongwe, Lusaka, na Balozi ya Kudumu katika Umoja wa Mataifa huko Geneva, Uswisi. Lakini hata hivyo, mali nyingi kati ya hizo ziko katika hali mbaya na hazitumiki kikamilifu, licha ya kuwa na uwezo wa kuzalisha mapato.

Jedwali Na. 94: Mali zinazotumika Chini ya Kiwango katika Balozi za Tanzania

Na.	Ubalozi	Maelezo
1.	Ubalozi wa Tanzania, Zimbabwe	**Mali zilizopo maeneo ya kimkakati:** - Mali nane zilizopo katika maeneo mbalimbali ndani ya mji wa Harare. - Jengo la biashara lililoko barabara ya 6 Allan Wilson.
2.	Ubalozi wa Tanzania Lusaka, Zambia	**Mali zilizopo maeneo ya kimkakati:** - Kiwanja namba 10-Farm No.377A kilichopo Chitemwiko, Lusaka - Kiwanja Na.6829 kilichopo kona ya Katima Mulilo, Olympia Park Lusaka - Kiwanja Na. 3821at kilichopo Mandai Hill Road, Olympia Park, Lusaka - Kiwanja Na. 5200 kilichopo UN Avenue na Pandit Nehru Rd. - Kiwanja Na. 340 kilichopo eneo la Poisenttia Chelstone. - Kiwanja Na. 32 na Na.377A kilichopo barabara ya Kudu Kabulonga. - Kiwanja Na. 126 na 127 mtaa Jasmondine. - Kiwanja Na. 130 na 131 mtaa Jasmondine.
3.	Ubalozi wa Tanzania mjini Lilongwe, Malawi	**Nyumba zilizo wazi katika maeneo ya kimkakati;** - Nyumba Na. HOM-TZSLLW/HSE/FA/10/536/01. - Nyumba Na. HOC-TZSLLW/HSE/FA/14/160/02. - Nyumba Na. PS-TZSLLW/HSE/FA/10/245/03. - Nyumba Na. AAO-TZSLLW/HSE/FA/43/2/02/04. - Nyumba Na. FA-TZSLLW/HSE/FA/9/57/05.
4.	Ubalozi wa Tanzania Umoja wa Mataifa, Geneva, Uswisi	**Mali zilizopo maeneo ya kimkakati:** - Ardhi yenye ukubwa wa mita za mraba 3,256 katika eneo la kimkakati.

Chanzo: *Ripoti za Ukaguzi*

13.6.1.2 Gharama kubwa zinatumika kulipia Kodi za Pango katika Balozi za Tanzania nje ya Nchi

Nilibaini pia, kutokuwepo kwa majengo ya Serikali na hali mbaya ya baadhi ya majengo katika balozi 34 kumepelekea serikali kuendelea kutumia kiasi kikubwa cha fedha kulipa kodi za makazi pamoja na ofisi za Balozi. Katika mwaka wa fedha wa 2021/22, Balozi hizo 34 ziliripoti matumizi ya kodi za pango jumla ya Sh. bilioni 15.47. Hali hii inatia shaka, hasa ikizingatiwa kuwa Serikali hutumia hadi Sh. bilioni 1 kila mwaka kulipia kodi ya pango

kwa ubalozi mmoja pekee. Orodha ya balozi hizo pamoja na kodi husika imeorodheshwa kwenye **Jedwali Na. 95** hapo chini:

Jedwali Na. 95: Matumizi ya Kodi kwa Kila Balozi kwa Mwaka wa Fedha 2021/22

Na.	Balozi	Kasima	Matumizi ya Kodi kwa Mwaka (Sh.)
1	Ubalozi wa Tanzania Umoja wa Mataifa – Geneva, Uswisi	2020	1,941,772,315
2	Ubalozi wa Tanzania Moscow, Urusi	2009	1,516,898,038
3	Ubalozi wa Tanzania Abuja, Nigeria	2005	1,361,011,469
4	Ubalozi wa Tanzania Seoul - Korea	2039	962,595,040
5	Ubalozi wa Tanzania Windhoek, Namibia	2043	948,373,804
6	Ubalozi wa Tanzania Nairobi, Kenya	2023	702,413,002
7	Ubalozi wa Tanzania Berlin, Ujerumani	2002	682,288,228
8	Ubalozi wa Tanzania Tel Aviv, Israel	2040	583,488,474
9	Ubalozi wa Tanzania New York	2011	550,712,207
10	Ubalozi wa Tanzania Brasília, Brazil	2031	517,737,163
11	Ubalozi wa Tanzania Roma, Italia	2015	469,490,181
12	Ubalozi wa Tanzania Kuala Lumpur, Malaysia	2032	437,375,843
13	Ubalozi wa Tanzania Havana –Cuba	2042	430,937,789
14	Ubalozi wa Tanzania Doha	2041	423,035,074
15	Ubalozi wa Tanzania Muscat, Oman	2029	362,175,224
16	Ubalozi wa Tanzania Lilongwe, Malawi	2030	345,742,419
17	Ubalozi wa Tanzania Brussels, Ubelgiji	2019	327,318,241
18	Tume Kuu ya Tanzania Kigali, Rwanda	2026	301,993,063
19	Ubalozi wa Tanzania Riyadh, Saudi Arabia	2024	293,784,025
20	Ubalozi wa Tanzania Ankara, Uturuki	2037	285,272,756
21	Ubalozi wa Tanzania Addis Ababa, Ethiopia	2001	256,602,570
22	Ubalozi wa Tanzania Washington, DC, Marekani	2018	212,795,854
23	Ubalozi wa Tanzania Paris, Ufaransa	2013	194,391,265
24	Ubalozi wa Tanzania Kampala, Uganda	2021	174,356,876
25	Ubalozi wa Tanzania Abu Dhabi, Falme za Kiarabu	2027	174,263,684
26	Ubalozi wa Tanzania Pretoria, Afrika Kusini	2025	167,166,440
27	Ubalozi wa Tanzania moroni, Comoro	2034	164,472,450
28	Ubalozi wa Tanzania New Delhi, India	2010	161,722,051
29	Ubalozi wa Tanzania Ottawa, Kanada	2012	144,836,884

Na.	Balozi	Kasima	Matumizi ya Kodi kwa Mwaka (Sh.)
30	Ubalozi wa Tanzania Bujumbura, Burundi	2028	112,674,750
31	Ubalozi wa Tanzania The Hague	2033	108,334,064
32	Ubalozi wa Tanzania nchini Kuwait	2035	58,124,499
33	Ubalozi wa Tanzania Kinshasa, DRC	2004	47,966,678
34	Ubalozi wa Tanzania Beijing, China	2014	44,229,873
Jumla			**15,466,352,294**

Chanzo: *Ripoti za Ukaguzi*

13.6.1.3 Uwepo wa Mali zilizotelekezwa na Kutokuendelezwa katika Balozi za Tanzania nje ya Nchi

Nilibaini kwamba, kucheleweshwa kwa utekelezaji wa mpango wa ukarabati na ujenzi wa Balozi za Tanzania kumesababisha mali nyingi zinazomilikiwa na Serikali katika balozi hizo kutokuendelezwa kwa muda mrefu. **Jedwali Na. 96** linaelezea orodha ya Balozi hizo pamoja na mali zinazohusiana na kila moja ya Balozi hizo.

Jedwali Na. 96: Mali zilizotelekezwa na zisizoendelezwa katika Ofisi za Balozi

Na.	Ubalozi	Mali Zilizotelekezwa
1.	Ubalozi wa Tanzania Nairobi, Kenya	- Ardhi iliyotelekezwa tangu 2006.
2.	Ubalozi wa Tanzania Riyadh, Saudi Arabia	- Ardhi kwa matumizi ya makazi na ofisi iliyotelekezwa.
3.	Ubalozi wa Tanzania Umoja wa Mataifa – Geneva, Uswisi	- Kiwanja kilichotelekezwa chenye mita za mraba 3,256.
4.	Ubalozi wa Tanzania Kampala, Uganda	- Nyumba ya makazi iliyopo Kololo ilitelekezwa tangu 2004.
5.	Ubalozi wa Tanzania Kigali, Rwanda	- Kiwanja Namba 428 mtaa wa Paul VI Kyovu kilichotelekezwa. - Kiwanja Na. 1/02/07/01/518KKG.614. - Kiwanja Na. KG. 131 ST. 35 No.2435. - Kiwanja Na. KG. 305 Na. 12886. - Kiwanja Na. KG. 554 ST 4. 1/02/07/01/231. - Kiwanja Na. Plot 2560 Block U.
6.	Ubalozi wa Tanzania Addis Ababa, Ethiopia	- Kiwanja chenye ukubwa wa mita za mraba 2,000, chenye Na. 458/98 kilichopo Bole Sub City neno 17 Kebele 23. - Kiwanja Na. 546/99 kilichopo mji wa Bole Sub.

Na.	Ubalozi	Mali Zilizotelekezwa
7.	Ubalozi wa Tanzania London, Uingereza	- Kiwanja na jengo lililochakaa Na. NGL 706501 vilivyopo Bustani za Colindeep.

Chanzo: *Ripoti za Ukaguzi*

13.6.1.4 Majengo ya Balozi Yanayotumika katika Hali ya Uchakavu

Aidha, nimebaini kwamba majengo ya ofisi na makazi yanayotumiwa hivi sasa na balozi nne yako katika hali mbaya ya uchakavu. Hali hii inasababisha mazingira duni ya kufanyia kazi ambayo si tu yanapunguza morali ya kazi, lakini pia yanaleta hatari kwa usalama wa wafanyakazi wanaotumia majengo hayo. **Jedwali Na. 97** hapo chini linatoa maelezo zaidi:

Jedwali Na. 97: Majengo yaliyochakaa

Na.	Ubalozi	Mapungufu Yaliyobainika
1.	Ubalozi wa Tanzania Umoja wa Mataifa - Geneva, Uswisi	Majengo yenye hali ya uchakavu mkubwa na ardhi isiyotumika.
2.	Ubalozi wa Tanzania Kampala, Uganda	Nyumba ya makazi iliyochakaa na isiyofaa kwa matumizi tangu 2004.
3.	Ubalozi wa Tanzania Lilongwe, Malawi	Majengo yenye hali ya uchakavu mkubwa.
4.	Ubalozi wa Tanzania Kampala, Uganda	Jengo la ofisi pamoja na makazi ya Balozi, yaliyopo Kalolo na Katonga.

Chanzo: *Ripoti za Ukaguzi*

Kwa maoni yangu, ucheleweshaji wa ujenzi na ukarabati umesababisha Serikali kuendelea kutumia fedha nyingi ambazo zingeweza kutumika katika shughuli nyingine za maendeleo. Aidha, suala hili linaweza kuathiri taswira ya nchi na kusababisha maeneo yaliyotengwa kwa shughuli za kidiplomasia kubadilishwa matumizi na nchi husika.

Ninapendekeza Serikali kuharakisha mpango wa ununuzi na ukukarabati wa majengo ya Balozi, ili kupunguza gharama, kuzalisha fursa za kipato, na kulinda taswira ya Tanzania katika jumuiya ya kimataifa.

13.6.2 Mali Zilizochakaa na Hazijauzwa

Katika ukaguzi wangu wa mali za Serikali katika Balozi, nilibaini kuwa kuna mali ambazo hazitaweza kufanyiwa ukarabati tena katika balozi saba, lakini hazijaondolewa na kuuzwa kulingana na mahitaji ya kanuni ya 254(1)

ya Kanuni za Fedha za Umma za mwaka 2001. Orodha kamili ya mali hizo na Balozi husika inapatikana katika **Jedwali Na. 98** hapo chini.

Jedwali Na. 98: Mali zilizochakaa na hazijauzwa

Na.	Ubalozi	Mali zilizochakaa na hazijauzwa
1.	Ubalozi wa Tanzania Berlin, Ujerumani	Gari lililoharibika kwa kiwango kikubwa muda mrefu bila kuuzwa, gari namba 0-131-2 Mercedes Benz 350S.
2.	Ubalozi wa Tanzania Umoja wa Mataifa - Geneva, Uswisi	Samani za ofisi zilizochakaa pamoja na magari.
3.	Ubalozi wa Tanzania Kampala, Uganda	Gari aina ya BMW Jeep GH-FB44 Station Wagon na Nissan Patrol Station Wagon tangu Septemba 2018.
4.	Ubalozi wa Tanzania Lilongwe, Malawi	Vifaa sitini na nne vya ofisini na mali nyingine.
5.	Ubalozi wa Tanzania Roma, Italia	Gari, samani katika makazi ya Balozi na vifaa vingine vya ofisini.
6.	Ubalozi wa Tanzania- The Hague	Vifaa 29 vya ofisini and samani za ofisini.
7.	Ubalozi wa Tanzania Tokyo, Japan	Gari and Komputya nne zilizoaribika.
8.	Ubalozi wa Tanzania Stockholm, Sweden	Gari moja aina ya Volkswagen Multivan (VW) of 2015 Namba. DF003B.

Chanzo: *Ripoti za Ukaguzi*

Ucheleweshaji wa kuondoa mali zilizochakaa husababisha uharibifu zaidi na kupunguza mapato yanayoweza kupatikana kutokana na mauzo yake endapo zingeuzwa mapema.

Ninapendekeza Serikali kupitia wizara husika kutoa vibali vya uuzaji wa mali zilizochakaa kwa wakati, ili kuzuia uharibifu zaidi ambao unaweza kupunguza kiasi cha mapato kinachoweza kupatikana wakati wa uuzaji.

13.7 Usimamizi wa Ununuzi na Mikataba

Kwa mwaka huu, nilifanya ukaguzi wa uzingatiaji wa sheria ya Ununuzi ya Umma katika manunuzi ya kazi za mikataba, bidhaa, na huduma katika ofisi za Balozi za Tanzania nilibaini kasoro zifuatazo:

13.7.1 Mapungufu yaliyobainika kwenye Utekelezaji wa Mkataba Na. ME-13/2017-2018/W/14, wa Ukarabati wa Jengo la Ofisi na Makazi ya Ubalozi wa Tanzania nchini Ubelgiji

Ukaguzi wa mkataba uliotajwa hapo juu uliotolewa na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, ulibaini mapungufu kadhaa yaliyoorodheshwa hapa chini;

i. **Kutofanyika kwa Mapitio ya Mawanda ya Kazi kulipelekea Kazi za ziada zenye thamani ya Euro 328,758.93 sawa na Sh. milioni 800.25**
Mwaka 2017, mwakilishi kutoka Wakala wa Majengo Tanzania alifanya ukaguzi kwenye makazi na majengo ya ofisi ya Balozi ili kubaini mawanda ya kazi na kuandaa nukuu ya bei (BoQ). Hata hivyo, mchakato wa manunuzi haukuanza hadi kufikia Januari 2020, na nukuu ya bei iliyoandaliwa mwaka 2017 ilitumika bila kufanyiwa mapitio. Matokeo yake, wakati wa utekelezaji mkandarasi alitoa nukuu za ziada namba 1 na 2 kwa kazi za ziada zenye thamani ya Euro 328,758.93, ambayo ni sawa na asilimia 48 ya thamani ya awali ya mkataba.

ii. **Kukosekana kwa Mkataba wa Kazi za ziada zenye thamani ya Euro 328,758.93 sawa na Sh. Milioni 800.25**
Wakati wa utekelezaji wa mkataba, ilibainika kuwa kazi za ziada zenye thamani ya Euro 328,758.93, ambayo ni sawa na Sh. milioni 800.25 zilikuwa zikifanyika bila ya kuwa na mkataba wa nyongeza ya kazi unaohusiana na mabadiliko hayo. Hii ni kinyume na Kanuni ya 110(4) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma, 2013 kama ilivyorekebishwa na Kanuni ya 36 (a) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma (Marekebisho) ya mwaka 2016, inayohusu marekebisho ya mkataba baada ya kusainiwa.

iii. **Kutokuwepo ushahidi unaonesha kuwa Mlipaji Mkuu wa Serikali aliidhinisha ongezeko la mawanda ya Kazi kwa Asilimia 48**
Ingawa kibali kilipatikana kutoka kwa Bodi ya Zabuni na Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, kwa

ongezeko la kazi za ziada, sijaweza kuthibitisha kwa ushahidi kuwa idhini ilipatikana kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali au Mamlaka ya Kuidhinisha Bajeti kwa ongezeko hilo linalozidi asilimia 15 ya thamani ya mkataba wa awali, kama inavyotakiwa na Kanuni ya 110(4) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma, 2013 kama ilivyorekebishwa na Kanuni ya 36 (a) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma (Marekebisho) ya mwaka 2016.

Kwa maoni yangu, mapungufu yaliyotajwa hapo juu yanaweza kusababisha kukosekana kwa makubaliano halali yanayotambulika kisheria kwa kazi za ziada, pamoja na ongezeko la gharama ambazo hazikupangwa ambazo pia zinaweza kusababisha changamoto za kibajeti wakati wa malipo ikiwa hayataidhinishwa.

Ninapendekeza uongozi kuzingatia sheria na kanuni za manunuzi na kuhakikisha kwamba mkataba wa nyongeza ya kazi unakuwepo ili kuunda makubaliano ya kisheria kwa mabadiliko yote yaliyofanyika.

13.7.2 Mapungufu Yaliyobainika katika Utekelezaji wa Mkataba Na.ME/013/2011/2012/MZQ/W/03, wa Ukarabati wa Jengo la Ubalozi wa Tanzania Maputo, Msumbiji

Tarehe 17 Januari 2012, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ilitoa kandarasi ya ukarabati wa Jengo la Balozi lililopo Maputo, Msumbiji kwa gharama ya Dola za Marekani 2,107,028.89 (sawa na Sh. bilioni 3.31 kufikia tarehe 17 Januari 2012), ikiwa ni nje na ada ya mshauri elekezi. Mradi huo ulipaswa kukamilika tarehe 19 Februari 2013, lakini baadaye ukaongezewa muda hadi tarehe 30 Januari 2018, kutokana na mabadiliko yaliyofanywa tarehe 7 Machi 2017, ambayo yalipandisha bei ya mkataba hadi Dola za Marekani 3,092,001.80 (sawa na Sh. bilioni 4.86 kufikia tarehe 7 Machi 2017).

Hata hivyo, usimamizi wa mkataba huo ulibainika kuwa na kasoro mbalimbali, ambazo ni:

i. **Kuchelewa kukamilika kwa Mradi na Malipo ya Ziada kwa Mkandarasi Kiasi cha dola za Marekani 482,090.87 sawa na Sh. Bilioni 1.11**

Mpaka kufikia wakati wa ukaguzi huu Novemba 2022, nilibaini kuwa mradi huo ulikuwa bado haujakamilika na mkandarasi alikuwa ametelekeza mradi tangu mwaka 2020. Ukaguzi uliofanywa na timu ya wataalamu kutoka Wizarani tarehe 8 Oktoba 2021, ulibaini kuwa kazi zenye thamani ya Dola za Marekani 2,299,353.91 (sawa na Sh. bilioni 5.28 kufikia 8 Oktoba 2021) zilikuwa ndizo tu zimekamilika, ambayo ni sawa na asilimia 74 ya fedha zote.

Hata hivyo, mkandarasi alikuwa tayari amelipwa Dola za Marekani 2,781,444.78 (sawa na Sh. bilioni 6.38 kufikia 8 Oktoba 2021), na kufanya kuwa na malipo ya zaidi ya kiasi cha Dola za Marekani 482,090.87 (sawa na Sh. bilioni 1.11 kufikia 8 Oktoba 2021) ambazo bado hazijarudishwa. Aidha, mshauri elekezi alikuwa tayari amelipwa Dola za Marekani 256,773.17 (sawa na Sh. milioni 589.19 kufikia 8 Oktoba 2021).

ii. **Malipo Bila Hati ya Kazi Iliyofanyika pamoja na Vipimo vya Kazi Halisi Zilizotekelezwa Zenye Thamani ya dola za Marekani 2,781,444.78 sawa na Sh. Bilioni 6.38**
Kinyume na Kanuni ya 243(2) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma, 2013, ambayo inahitaji malipo kuidhinishwa kulingana na vipimo na hati za uthibitisho kwa kila hatua za kazi zilizokubaliwa katika mkataba, nimebaini kuwa kiasi cha malipo ya Dola za Marekani 2,781,444.7 (Sh. bilioni 6.38 kufikia 8 Oktoba 2021) hayakuwa na nyaraka iliyoonesha kazi zilizopimwa na hati za uthibitisho wa kazi.

iii. **Jenereta Lililotelekezwa Lenye Thamani ya Sh. Milioni 241.68**
Aidha, nilibaini pia kuwa Jenereta lenye thamani ya Sh. milioni 241.68 lilinunuliwa mwaka 2017, hata hivyo hadi wakati wa ukaguzi huu mnamo Novemba 2022, halikuwa limeunganishwa wala kufanyiwa majaribio kwa ajili ya matumizi. Mkandarasi aliwasilisha Hati ya Madai Na. 39 yenye kiasi hicho tarehe 8 Agosti 2017, lakini ilikataliwa kutokana na kutokukamilika kwa kazi ya ufungaji na majaribio ya Jenereta hilo.

Kwa maoni yangu, usimamizi usioridhisha wa mradi huu umesababisha mapungufu ambayo yanaweza kuzuia kufikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa na pia kusababisha matumizi mabaya ya fedha na rasilimali za umma.

Ninapendekeza Wizara ifanye ukaguzi wa mara kwa mara wa miradi inayotekelezwa, ichukue hatua za haraka kushughulikia mapungufu yote yaliyobainika, na kuhakikisha kuwa mradi unakamilika kwa wakati bila kuchelewa zaidi.

13.7.3 Muda Mrefu zaidi ya siku 120 Uliotumika katika Mchakato wa Zabuni Namba ME-013/2020-2021/HQ/W/02 ya Ujenzi wa Ubalozi wa Tanzania Jijini Nairobi, Kenya

Kanuni ya 191 (3) ya Kanuni za manunuzi ya Umma, 2013 inataka taasisi nunuzi kuweka muda wa tathmini ya zabuni, idhini, kibali na ukamilishaji wa mikataba. Hata hivyo, kipindi hiki hakitazidi siku 120 kutoka tarehe ya mwisho iliyowekwa ya uwasilishaji wa zabuni.

Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ilianzisha mchakato wa ununuzi tarehe 15 Februari 2022 kwa ajili ya ujenzi wa ubalozi wa Tanzania Jijini Nairobi, na tarehe ya mwisho ya kuwasilisha ilikuwa tarehe 10 Machi 2022. Hata hivyo, hadi kufikia tarehe 30 Novemba 2022, mchakato huo ulikuwa haujakamilika, licha ya kuchukua zaidi ya siku 120.

Mchakato huu mrefu unaonesha ukosefu wa usimamizi thabiti na ushirikiano wa kutosha, ambavyo vinaweza kusababisha ongezeko la gharama za vifaa na kuzuia kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Ninapendekeza Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ichunguze sababu ya kuchelewa kwa mchakato huu wa manunuzi ambao umekuwa zaidi ya siku 120 na ichukue hatua stahiki kushughulikia changamoto hizo, ili kuzuia ucheleweshaji zaidi.

13.7.4 Kutopeleka Taarifa ya Manunuzi Madogo madogo ya kila Mwezi Kwenye Bodi za Zabuni Sh. Bilioni 1.60

Kanuni ya 166 (7) ya Kanuni ya Ununuzi wa Umma, 2013 inataka kuripotiwa kwa Bodi ya Zabuni kila mwezi kwa manunuzi yote madogo madogo, na kifungu kidogo cha nane kinahitaji kuripotiwa kwa Mamlaka ya Kudhibiti Ununuzi wa Umma kila robo mwaka. Hata hivyo, katika ukaguzi wangu, nimebaini kwamba Balozi tano zilifanya manunuzi madogo madogo yenye

thamani ya Sh. bilioni 1.60 bila kuripotiwa kwa Bodi ya Zabuni kila mwezi. Maelezo ya manunuzi haya yametolewa katika **Jedwali Na. 99**.

Jedwali Na. 99: Manunuzi Madogo madogo ambayo hayajaripotiwa kwenye Bodi ya Zabuni

Na.	Ubalozi	Kiasi cha Sh.
1.	Ubalozi wa Tanzania Ankara, Uturuki	150,124,262
2.	Ubalozi wa Tanzania Berlin, Ujerumani	1,234,922,821
3.	Ubalozi wa Tanzania Kuwait	17,100,741
4.	Ubalozi wa Tanzania Mataifa - Geneva, Uswisi	93,771,865
5.	Ubalozi wa Tanzania London	108,810,066
Jumla		**1,604,729,754**

Chanzo: *Ripoti za Ukaguzi*

Kwa maoni yangu, bodi za zabuni za balozi husika hazipewi fursa ya kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa masharti ya kanuni za manunuzi ya umma.

Ninapendekeza kwamba Mabalozi husika kuhakikisha kwamba manunuzi madogo madogo yanaripotiwa kwenye bodi ya zabuni na mamlaka husika kwa ajili ya ufuatiliaji na udhibiti bora wa manunuzi hayo ili kuzuia matumizi mabaya ya fedha za umma.

13.7.5 Bidhaa na Huduma zilizopokelewa bila Kukaguliwa Sh. Milioni 719.96

Kanuni ya 244(1) na 245 ya Kanuni za manunuzi ya Umma za mwaka 2013, inawataka maafisa masuuli kufanya ukaguzi wa bidhaa na kuhakikisha kuwa zinakidhi vigezo vya mkataba kabla ya kuzikubali. Hata hivyo, wakati wa ukaguzi, nilibaini kuwa Balozi saba zilifanya malipo na kupokea bidhaa na huduma zenye thamani ya Sh. milioni 719.96 kutoka kwa wauzaji, bila kukagua kama ilivyoorodheshwa katika **Jedwali Na. 100** hapo chini:

Jedwali Na. 100: Bidhaa na Huduma Zilizopokelewa na Kukubalika kabla ya Kukaguliwa

Na.	Ubalozi/Ubalozi	Kiasi (Sh.)
1.	Ubalozi wa Tanzania Brussels, Ubelgiji	205,882,485
2.	Ubalozi wa Tanzania Khartoum, Sudan	20,974,299
3.	Ubalozi wa Tanzania Lilongwe, Malawi	22,219,166
4.	Ubalozi wa Tanzania Beijing, China	126,201,037

Na.	Ubalozi/Ubalozi	Kiasi (Sh.)
5.	Ubalozi wa Tanzania Addis Ababa, Ethiopia	49,035,130
6.	Ubalozi wa Tanzania London	88,145,184
7.	Ubalozi wa Tanzania Lusaka, Zambia	207,498,792
Jumla		**719,956,093**

Chanzo: *Ripoti za Ukaguzi*

Kupokea na kukubali bidhaa na huduma ambazo hazijakaguliwa na kamati ya ukaguzi kunaweza kuhatarisha ubora wa bidhaa na huduma husika, na hivyo kusababisha kukubalika kwa bidhaa au huduma ambazo hazijakidhi viwango vya ubora.

Ninapendekeza kwamba, Balozi husika zihakikishe zinazingatia kanuni za manunuzi kwa kuhakikisha kwamba bidhaa na huduma zinakaguliwa ubora na vigezo kabla ya kukubaliwa.

13.7.6 Manunuzi Yaliyofanywa bila Ushindani Sh. Milioni 285.67

Aya ya 32.3 ya Mwongozo wa kutekeleza Kazi kwa kutumia nguvukazi (Force Account), unahitaji angalau nukuu tatu za bei kutolewa na wauzaji walioorodheshwa na kuidhinishwa na taasisi husika, ili kuhakikisha ushindani unazingatiwa katika manunuzi ya bidhaa na huduma.

Nilibaini kwamba, Balozi mbili zilinunua huduma na bidhaa kutoka kwa wauzaji na watoa huduma zenye jumla ya thamani ya Sh. milioni 285.67 bila kutumia njia ya ushindani, kinyume na kanuni iliyotajwa hapo juu. Jumla hiyo ni Sh. milioni 268.45 kwa Ubalozi wa Tanzania Lusaka, Zambia, pamoja na Sh. milioni 17.22 kwa Balozi wa Tanzania Cairo, Misri.

Kwa maoni yangu, kutofuata sheria na kanuni za manunuzi kunaweza kusababisha taasisi kupoteza fursa ya kupata thamani ya pesa na hata kusababisha matumizi mabaya ya fedha za umma.

Ninapendekeza menejimenti ya Balozi husika kuzingatia kanuni zote za manunuzi wakati wa kufanya manunuzi ili kupata thamani ya pesa kwa njia ya ushindani kati ya wauzaji waliothibitishwa kabla ya kufanya malipo.

13.8 Usimamizi wa Rasilimali Watu na Mishahara

13.8.1 Upungufu wa Watumishi muhimu katika Ofisi za Balozi za Tanzania

Kanuni D.7 na D.8 (1) na (4) za Kanuni za Utumishi wa Umma, 2009, zinaeleza jukumu la Sekretarieti ya Ajira katika kujaza nafasi zilizo wazi katika Utumishi wa Umma kwa kuzingatia taratibu zote za ajira.

Hata hivyo, baada ya kupitia taarifa za watumishi, na kwa kuzingatia mapendekezo yangu katika kaguzi zilizopita juu ya idadi ndogo ya wafanyakazi katika balozi za Tanzania, nimebaini kuwa Balozi nane bado zinakabiliwa na changamoto ya kukosa wataalam muhimu ambao wangeweza kusaidia katika kutumia fursa zinazopatikana katika Balozi hizo, kama ilivyoelezwa katika **Jedwali Na. 101** hapo chini:

Jedwali Na. 101: Upungufu wa Watumishi Muhimu katika Balozi za Tanzania

Na.	Ubalozi	Mapungufu Yaliyobainika
1.	Ubalozi wa Tanzania Abu Dhabi, Falme za Kiarabu	Kukosekana kwa mwambata biashara
2.	Ubalozi wa Tanzania Brasillia, Brazil	Kukosekana Mkuu wa utawala ubalozini baada ya aliyekuwepo kumaliza muda wake.
3.	Ubalozi wa kudumu Umoja wa Mataifa - Geneva, Uswisi	Kukosekana kwa mtumishi wa masuala ya afya.
4.	Ubalozi wa Tanzania Moscow, Urusi	Kukosekana kwa Mkuu wa utawala ubalozini (Head of Chancery) pamoja na mwambata utawala.
5.	Ubalozi wa Tanzania Riyadh, Saudi Arabia	Kukosekana kwa mwambata utawala.
6.	Ubalozi wa Tanzania Beijing, China	Kukosekana kwa mwambata utawala.
7.	Ubalozi wa Tanzania Roma, Italia	Kukosekana kwa mwambata utawala.
8.	Ubalozi wa Tanzania Tokyo, Japan	Kukosekana kwa mwambata utawala.

Chanzo: *Ripoti za Ukaguzi*

Ukosefu wa watumishi muhimu katika balozi za Tanzania unaweza kuwa na athari katika kufanikisha utekelezaji wa shughuli za kiuchumi kama vile biashara, uwekezaji, utalii, na elimu. Kukosekana kwa watumishi hawa kunaweza kusababisha taifa kukosa fursa muhimu na zenye faida katika maeneo hayo.

Ninapendekeza kwamba Serikali ifanye tathmini ya mahitaji ya wafanyakazi katika Balozi za Tanzania na kuzingatia tathmini hiyo katika kutenga rasilimali za kutosha ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

13.8.2 Kushindwa kukata na Kuwasilisha Michango ya Wafanyakazi kwa Bodi ya Hifadhi ya Jamii ya Rwanda (Rwanda Social Security Board) katika Ubalozi wa Tanzania Kigali, Rwanda

Kifungu cha 10 cha Sheria Na. 06/2003 inayosimamia hifadhi ya jamii nchini Rwanda kinataka waajiri na wafanyakazi kutoa michango sawa kwa ajili ya mafao ya pensheni, na waajiri wanawajibika kuwasilisha michango hiyo kwenye Bodi ya Hifadhi ya Jamii wa Rwanda, ikiwa ni pamoja na sehemu ya michango iliyokatwa kutoka kwenye mishahara ya wafanyakazi. Hata hivyo, nimebaini kuwa katika mwaka huu, Ubalozi wa Tanzania Kigali, Rwanda umelipa moja kwa moja mishahara ya Sh. milioni 69.27 kwa wafanyakazi tisa wazawa wa Rwanda bila kukata michango ya kisheria inayohitajika.

Hii ni kutokana na kutokuwepo kwa uelewa wa kutosha wa sheria na kanuni zinazotumika. Nilibaini kuwa, kushindwa kukata na kupeleka michango ya wafanyakazi ni kinyume na sheria, na kunaweza kusababisha adhabu za kisheria na kuathiri uwezo wa wafanyakazi kupata mafao yao ya pensheni hapo baadaye.

Ninapendekeza Balozi kuchukuwa hatua za kurekebisha mapungufu hayo na kuhakikisha kuwa michango yote inakatwa na kupelekwa kwenye Bodi kama inavyohitajika.

13.8.3 Kushindwa Kuandaa Mpango wa Bima ya Afya kwa kwa Watumishi wa Ubalozi wa Tanzania mjini Ankara, Uturuki

Kanuni ya 76 (1) ya Kanuni za Utumishi wa Umma (Huduma za Nje ya Nchi), 2016 inaeleza kuwa maafisa wanaohudumu nje ya nchi na familia zao watakuwa na haki ya matibabu, ambapo ofisi ya ubalozi itaandaa na kulipia bima ya matibabu.

Nimebaini kwamba ubalozi wa Tanzania huko Ankara, Uturuki, haujaandaa mpango wa bima ya matibabu kwa maafisa wake na familia zao. Badala

yake, wamekuwa wakilipa moja kwa moja gharama za matibabu zinazotumika. Kwa maoni yangu, kutokuwa na mpango wa bima ya matibabu kunaweza kusababisha ofisi kutumia gharama kubwa za matibabu ambazo zingeweza kulipwa na bima ikiwa tukio kubwa linapotokea.

Ninapendekeza Ubalozi wa Tanzania mjini Ankara, Uturuki uandae mpango wa bima ya matibabu kwa maafisa wake na familia zao ili kuepuka gharama zisizo za kawaida ambazo zinaweza kutokea.

13.9 Udhibiti wa Mifumo ya Ndani na Masuala ya Utawala

13.9.1 Miamala ya Muda Mrefu ambayo haijasuluhishwa katika Taarifa za Usuluhisi wa Kibenki za Sh. Milioni 83.60

Nilibaini miamala ya muda mrefu ambayo haijasuluhishwa katika ripoti za usuluhishi wa kibenki, yenye thamani ya Sh. milioni 83.60 kutoka katika balozi mbili. Miamala hii imebaki bila kusuluhishwa kwa zaidi ya miaka miwili, jambo ambalo limesababishwa na ucheleweshwaji wa kuandaa taarifa za usuluhishi. Jambo hili ni kinyume na Kanuni ya 162 ya Kanuni za Fedha za Umma za mwaka 2001, inayohimiza usuluhishi wa haraka wa taarifa za benki ili kubaini miamala ambayo haijatambuliwa. **Jedwali Na. 102** linatoa maelezo zaidi.

Jedwali Na. 102: Miamala ya Muda Mrefu ambayo Haijasuluhishwa

Na	Jina la utume	Maelezo	Kiasi cha Sh.
1.	Ubalozi wa Tanzania Addis Ababa, Ethiopia	Mapokezi ya fedha tangu 2019/20.	25,946,632
2.	Ubalozi wa Tanzania Paris, Ufaransa	Ada ya visa zilizokusanywa kabla ya mwaka 2019.	57,655,936
Jumla			**83,602,568**

Chanzo: *Ripoti za Ukaguzi*

Kushindwa kufanya usuluhishi kwa wakati kunaficha makosa na kuongeza vihatarishi vya ubadhirifu na matumizi mabaya ya fedha.

Ninapendekeza Mabalozi husika kuchunguza tofauti ambazo hazijasuluhishwa na kuchukua hatua stahiki za kurekebisha ili kushughulikia miamala hiyo ambayo haijasuluhishwa na kufanya marekebisho yatakayo hakikisha kunakuwa na utunzaji sahihi wa kumbukumbu za fedha kwa kuzingatia miongozo.

13.9.2 Kutofungwa kwa Akaunti za Benki ambazo hazitumiki katika Ubalozi wa Tanzania Moscow, Urusi

Wakati wa ukaguzi wangu katika Ubalozi wa Tanzania Moscow, Urusi, nilibaini kuwa licha ya barua rasmi kutoka Wizara ya Fedha na Mipango ya tarehe 9 Machi 2022 iliyoagiza kufungwa mara moja kwa akaunti tano za benki katika benki ya VTB na kufunguliwa kwa akaunti mpya katika benki ya Raiffen, akaunti hizo za zamani bado zilikuwa hazijafungwa hadi kufikia Novemba 2022 . Menejimenti ilieleza ucheleweshaji wa kufunga akaunti hizo ni kutokana na mchakato mrefu unaoendelea katika benki hiyo. Kati ya akaunti hizo tano, tatu hazikuwa na salio, huku akaunti mbili zilizobaki zikiwa na salio la jumla ya Sh. milioni 308.86 hadi kufikia 30 Juni 2022.

Kwa maoni yangu hii inaweza kusababisha upotevu wa fedha au hatari za usalama ikiwa akaunti za benki zitatumiwa na watu wasio waaminifu kwa shughuli zisizoidhinishwa.

Ninapendekeza Ubalozi wa Tanzania Moscow uchukue hatua za haraka kuharakisha mchakato wa kufunga akaunti zote za benki ambazo hazitumiki na kuhamisha fedha zote zilizomo kwenye akaunti hizo kwenda akaunti mpya ilyofunguliwa ambayo inatumika.



SURA YA KUMI NA NNE

VYAMA VYA SIASA

14.1 Utangulizi

Sehemu hii ya ripoti inatoa muhtasari wa masuala muhimu yaliyobainika wakati wa ukaguzi wangu wa Vyama vya Siasa. Ukaguzi huu umefanyika kwa mujibu wa kifungu cha 18A (2) (a) cha Sheria ya Vyama vya Siasa, Sura ya 258 (iliyorejewa 2019). Sheria hii inataka kila chama cha siasa kilichosajiliwa kuandaa na kuwasilisha taarifa za fedha kwa ajili ya ukaguzi.

Kama sehemu ya taratibu zangu za kikaguzi, ninatakiwa kupitia mifumo ya udhibiti wa ndani, bajeti, mali, na usimamizi wa vitega uchumi (uwekezaji) na kutoa uhakikisho unaofaa kwamba taarifa za fedha zilizoandaliwa hazina makosa ya kimahesabu yaliyosababishwa kwa makusudi ama udanganyifu na zimeandaliwa kwa mujibu wa viwango vya kimataifa vya uandaaji hesabu za umma (IPSAS).

Katika ukaguzi nilioufanya nilibaini masuala muhimu ambayo yanahitaji kuangaliwa na kurekebishwa. Masuala haya yamefafanuliwa kwa kina katika sehemu hii, napendekeza Vyama vya Siasa vichukue hatua stahiki kuyashughulikia haraka. Masuala hayo ni kama ifuatavyo:

14.2 Vyama vya Siasa Tisa Havikukusanya Mapato Yaliyobajetiwa ya Sh. Bilioni 25.85

Kama sehemu ya ukaguzi wangu, nilipitia bajeti ya vyama vya siasa mbalimbali, pamoja na taratibu zilizotumika katika kuandaa na kujumuisha bajeti hizo katika kusaidia utekelezaji wa shughuli za kisiasa za vyama. Ukaguzi wangu ulibaini kuwa vyama vya siasa tisa ambavyo ni CCM, CUF, ADC, CHAUMMA, Demokrasia Makini, NCCR-Mageuzi, SAU, TLP na CHADEMA vilikuwa vimejiwekea malengo ya kukusanya mapato ya jumla ya Sh. bilioni

78.75 kwa mwaka wa fedha 2021/22. Hata hivyo, uchambuzi wangu unaonesha kuwa vyama hivyo viliweza kukusanya kiasi cha Sh. bilioni 52.90 tu sawa na asilimia 67 ya mapato yote yaliyobajetiwa, huku vikishindwa kukusanya kiasi cha Sh. bilioni 25.85, sawa na asilimia 33 ya mapato yote ya bajeti. Aidha, nilibaini kuwa vyama vinne vya siasa (ADC, NCCR-Mageuzi, SAU na TLP) vilikusanya chini ya asilimia 10 ya mapato yaliyobajetiwa, hali hii inaonesha tatizo kubwa ambalo linahitaji kushughulikiwa kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 103**.

Jedwali Na. 103: Orodha ya Vyama vya Siasa vilivyoshindwa Kukusanya Mapato yaliyobajetiwa

Na	Jina la Chama cha Siasa	Bajeti (Sh.)	Halisi (Sh.)	Upungufu (Sh.)
1	Chama cha Mapinduzi (CCM)	76,763,471,620	52,387,806,794	24,375,664,826
2	Civic United Font (CUF)	160,926,481	112,035,941	48,890,540
3	Alliance for Democratic Change (ADC)	1,078,506,000	13,850,000	1,064,656,000
4	Chama cha Ukombozi wa Umma (CHAUMMA)	5,300,000	1,010,500	4,289,500
5	Demokrasia Makini	6,000,000	2,230,000	3,770,000
6	NCCR - MAGEUZI)	295,403,200	6,014,751	289,388,449
7	Chama cha Sauti ya Umma (SAU)	40,000,000	1,790,400	38,209,600
8	Chama cha Tanzania Labour Party (TLP)	8,500,000	600,000	7,900,000
9	Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA)	390,000,000	371,616,072	18,383,928
	Jumla	**78,748,107,302**	**52,896,954,458**	**25,851,152,844**

Chanzo: *Taarifa za Fedha za mwaka 2021/22*

Kulingana na tathmini yangu, vyama kushindwa kukusanya mapato yaliyobajetiwa kulisababishwa zaidi na wanachama wa vyama vya siasa

kushindwa kulipa ada zao za uanachama za kila mwezi (monthly subscription fee) kutokana na rejista za uanachama kutokuwa na taarifa sahihi za wanachama. Aidha, tathmini yangu ilibaini kuwa hakuna chama chochote kati ya vyama vilivyohojiwa vilikuwa na utaratibu wowote wa ufuatiliaji ili kuhakikisha kuwa wanachama wanaostahili wanalipa ada zao, jambo lililosababisha vyama hivi kushindwa kukusanya mapato yaliyobajetiwa.

Maoni yangu kuhusiana na suala hili ni kuwa kushindwa kukusanya mapato yaliyobajetiwa kuna athari kubwa kwa vyama, kwani kunazuia vyama vingi vya siasa kutotekeleza shughuli zao zilizopangwa na kufikia malengo yao ya kisiasa. Hii ilikuwa changamoto hasa kwa vyama vinne vya siasa ambavyo vilikusanya chini ya asilimia 10 ya mapato yaliyobajetiwa.

Napendekeza Makatibu Wakuu wa Vyama vya Siasa kuhuisha kanzidata zao za wanachama na kuandaa mfumo wa kielektroniki wa kufuatilia ada ambazo hazijalipwa. Hii itawezesha ufuatiliaji madhubuti wa ada ambazo hazijalipwa na kuboresha ukusanyaji wa mapato, hivyo kuongeza utekelezaji wa shughuli na mipango mbalimbali ya vyama.

14.3 Mapato Yaliyokusanywa na Kutumika Kabla ya Kuwasilishwa Benki Sh. Milioni 40.42

Kwa mujibu wa kifungu cha 15(1) cha Sheria ya Vyama vya Siasa Sura ya 258 (iliyorekebishwa 2019), kila chama cha siasa ambacho kimesajiliwa kisheria kinapaswa kufungua akaunti ya benki ya chama ambayo mapato yote yanayopatikana kutokana na ada za uanachama, michango ya hiari, misaada, ruzuku, au mapato ya uwekezaji yanapaswa kuwekwa. Ukaguzi wangu wa mwaka wa fedha 2021/22 ulibaini kuwa vyama vya siasa saba, ambavyo ni AAFP, ADA-TADEA, SAU, TLP, UDP, UMD, na UPDP, vilikusanya mapato ya jumla ya kiasi cha Sh. milioni 40.42. Hata hivyo, vyama hivyo vilishindwa kuweka mapato haya kwenye akaunti za benki za vyama, hivyo kukiuka Sheria ya Vyama vya Siasa kama ilivyooneshwa katika **Jedwali Na. 104**.

Jedwali Na. 104: Orodha ya Vyama vya Siasa vilivyotumia mapato yaliyokusanywa kabla ya kuwekwa benki

Na	Jina la Chama cha Siasa	Kiasi (Sh.)
1	Chama cha Alliance for Africa Farmers Party (AAFP)	1,588,500
2	Chama cha African Democratic Alliance (ADA-TADEA)	20,223,000

Na	Jina la Chama cha Siasa	Kiasi (Sh.)
3	Chama cha Sauti ya Umma (SAU)	1,790,400
4	Chama cha Tanzania Labour Party (TLP)	600,000
5	Chama cha United Democratic Party (UDP)	8,596,000
6	Chama cha Union for Multiparty Democracy (UMD)	5,560,000
7	Chama cha United Peoples' Democratic Party (UPDP)	2,060,200
	Jumla	**40,418,100**

Chanzo: *Ripoti ya Mapungufu kwa Menejimenti*

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa mapato yote yaliyokusanywa yalitumika kulipia matumizi ya mbalimbali ya vyama. Hata hivyo, hakukuwa na nyaraka zinazotosheleza kuthibitisha matumizi hayo yaliyoripotiwa. Aidha, menejimenti ya chama cha UDP ilieleza kuwa kushindwa kuweka mapato benki kulitokana na akaunti ya benki ya chama hicho kuwa mfu (dormant) kwa muda mrefu, ambayo sasa imefufuliwa na kuwa hai. Menejimenti ya chama cha UDP imetuhakikishia kuwa mapato yote yatakayokusanywa yatawekwa benki ipasavyo. Hata hivyo, hakukuwa na majibu yoyote kutoka katika vyama vingine vilivyohojiwa kuhusiana na suala hili.

Ikilinganishwa na ripoti yangu ya mwaka uliopita mapato yaliyokusanywa lakini hayakuwekwa benki yamepungua kutoka Sh. milioni 571.41 hadi kufikia Sh. milioni 40.42 mwaka huu, na idadi ya vyama vya siasa vyenye upungufu huu imepungua kutoka vyama vya siasa kumi hadi saba. Vyama vitano vya siasa (AAFP, ADA-TADEA, UDP, UMD, na UPDP) vimeripotiwa kuwa na upungufu huu katika miaka yote miwili mfululizo. Hii inaonesha kuwa vyama hivi havikutekeleza ushauri wangu licha ya mapato ambayo hayakuwekwa benki kupungua kutoka Sh. milioni 331.53 mwaka uliopita hadi kufikia Sh. milioni 38.03 mwaka huu. Matumizi ya mapato kabla ya kuwekwa benki hudhoofisha uwajibikaji na kuongeza hatari ya matumizi mabaya na ubadhirifu wa fedha za vyama.

Nashauri Makatibu wa Vyama vya Siasa wachukue hatua stahiki kuhakikisha kuwa mapato yote yanayokusanywa hayatumiki kabla ya kuwekwa benki. Hii itasaidia kuleta uwazi na uwajibikaji madhubuti wa mapato yanayokusanywa.

14.4 Chama cha Mapinduzi (CCM) kilinunua Vitu ambavyo Havitumiki na Vimepitwa na Wakati vya Jumla ya Sh. Milioni 58.60

Katika ukaguzi wa vitabu vya ghala la Chama cha Mapinduzi (CCM), ilibainika kuwa kati ya mwaka wa fedha 2019/20 na 2021/22, chama hicho kilinunua vitu mbalimbali vyenye gharama ya jumla ya Sh. milioni 58.60. Hata hivyo, kutokana na mabadiliko ya haraka ya kiteknolojia, vitu hivyo havitumiki kutokana na kupitwa na muda (outdated).

Menejimenti ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ilieleza kuwa vitu hivyo ni nyeti, na kwa hivyo inasubiri kibali kutoka katika Bodi ya Wadhamini ya Chama ili kuviharibu, badala ya kuviuza. Hii inalenga kuhakikisha kwamba vitu hivyo visije kutumiwa vibaya na watu wasiofaa na kusababisha madhara kwa chama.

Chama kununua vitu ambavyo vimepitwa na muda ni ishara ya menejimenti ya chama kutokuwa makini katika kubainisha mahitaji halisi ya chama kabla ya manunuzi.

Ili kushughulikia suala hili, napendekeza Bodi ya Wadhamini ya Chama cha Mapinduzi (CCM) iharakishe mchakato wa kutoa kibali cha kuharibu vitu vyote vilivyopitwa na wakati. Kufanya hivyo si tu kutapunguza gharama za kuhifadhi vitu visivyo na tija, lakini pia kutapunguza hatari ya kupotea, ama kutumika vibaya kwa vitu hivyo.

14.5 Mapungufu katika Usimamizi wa Mali na Mapato na Kutofuata Kanuni za Fedha Katika Chama cha Wananchi (CUF)

Katika kupitia Kanuni za Fedha za Chama cha Wananchi (CUF) za mwaka 2014, nilibaini kuwa menejimenti ya Chama cha Wananchi (CUF) inatakiwa kutunza kumbukumbu za mali zao na kuweka namba za utambulisho wa mali. Aidha, kulingana na Kanuni za Fedha za Chama cha Wananchi (CUF), mali yoyote ambayo thamani yake ni sifuri(zero net book value) lazima iuzwe kwa kufuata taratibu zilizoainishwa na Bodi ya Wadhamini ya Chama.

Wakati wa ukaguzi, nilibaini kuwa Chama cha Wananchi (CUF) kina magari kumi na kangavuke(jenereta) mbili ambazo zilinunuliwa kati ya mwaka 2008 na 2015, na ziligharimu jumla ya Sh. milioni 302.93. Hata hivyo, mali hizi kwa sasa hazina thamani katika vitabu vya hesabu vya Chama na

hazijafanyiwa matengenezo au kuuzwa. Hii ni kinyume na Kanuni za Fedha za Chama za mwaka 2014. Kulingana na upungufu huu, ni wazi kwamba menejimenti ya Chama cha Wananchi (CUF) haikutekeleza wajibu wake katika kusimamia mali za chama.

Pia, ilibainika kuwa Chama cha Wananchi (CUF) kilikuwa na mali kadhaa zenye thamani ya Sh. milioni 6.04, ikiwa ni pamoja na matenki ya maji, kompyuta, viti vya ofisi, na mashine ya kuchapisha, ambazo hazikuwa na nambari za utambulisho wa mali . Hii inaongeza hatari ya mali hizi kutumiwa vibaya, kuibwa, au kutumiwa kwa njia isiyo sahihi. Aidha, rejista ya mali ilionesha kuwa Chama cha Wananchi (CUF) kilikuwa na mali kadhaa kama viwanja, nyumba, pikipiki, magari, mashine za kuchapisha, kompyuta, kangavuke(jenereta), na mashine ya faksi, lakini gharama na tarehe za ununuzi hazikuwa zimeandikwa katika rejista ya mali. Hivyo, ukaguzi haukuweza kujua gharama halisi na tarehe za ununuzi wa mali hizo. Zaidi ya hayo, ilibainika kuwa Chama cha Wananchi (CUF) kilikuwa na vitabu 23 vya ukusanyaji wa mapato, lakini hakukuwa na taarifa zozote za kimaandishi kuhusiana na vitabu hivyo . Hali hii inaonesha hatari ya kupotea kwa mapato ya chama na kusababisha matumizi mabaya ya fedha za chama.

Uongozi wa Chama cha Wananchi (CUF) ulinieleza kuwa wana mpango wa kuwasilisha suala la mali chakavu kwa Bodi ya Wadhamini kwa ajili ya majadiliano na idhini. Pia, wamekiri umuhimu wa kuboresha rejista ya mali, ambayo itajumuisha thamani ya mali zote zilizonunuliwa na kuhakikisha kumbukumbu zote za vitabu vya ukusanyaji wa mapato zinaandikwa kwa siku zijazo.

Hata hivyo, ukaguzi una maoni kuwa kushindwa kuondoa mali zilizochakaa, kutokutambua vizuri mali kwenye rejista ya mali, na kutoweka kumbukumbu za mali zisizo na thamani kwenye rejista ya mali kunaweza kusababisha hatari ya matumizi mabaya ya mali na ubadhirifu. Hivyo kusababisha kuwepo kwa usimamizi hafifu wa mali za chama.

Kwa kuzingatia mapungufu yaliyobainishwa na ukaguzi, ninapendekeza uongozi wa Chama cha Wananchi (CUF) uchukue hatua za haraka kuimarisha usimamizi wa mali kwa kuhuisha rejista ya mali zake na kutoa namba maalumu za utambulisho wa mali ili kuzuia matumizi mabaya ya mali za Chama. Aidha, Bodi ya Wadhamini ya Chama cha Wananchi (CUF)

inapaswa kukutana ili kujadili na kuidhinisha matengenezo, uondoshaji, na kufanya mapitio ya umri wa mali zilizochakaa ili kupunguza hatari ya upotevu, kutumika vibaya au udanganyifu.

14.6 Bodi za Wadhamini za Chama cha CHADEMA, CUF na DP hazikuwa na Ufanisi katika Kusimamia Utendaji Kazi wa Vyama vyao

Kwa mujibu wa kifungu cha 21(1) cha Sheria ya Vyama vya Siasa Sura ya 258 (iliyorejewa 2019), vyama vya siasa vilivyosajiliwa vinatakiwa kuwa na bodi ya wadhamini iliyosajiliwa yenye jukumu la kusimamia mali za chama, uwekezaji na biashara nyingine yoyote. Aidha, Sheria ya Usajili Udhamini Sura ya 318 (iliyorejewa 2002) inampa mamlaka Kabidhi Wasii Mkuu wa Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA) kusajili Bodi za Wadhamini.

Kama ilivyotajwa katika Kanuni za Fedha za Chama cha Wananchi (CUF) za mwaka 2014, Bodi ya Wadhamini ya Chama cha Wananchi (CUF) inatakiwa kuandaa na kuwasilisha ripoti za mali za Chama kwa Baraza Kuu la Uongozi. Hata hivyo, nilibaini kuwa Baraza la Wadhamini halikuzingatia kanuni hii na hivyo haikuwasilisha ripoti ya mali kwa Baraza Kuu la Uongozi. Hali hii inapunguza uwezo wa Baraza la Uongozi kutambua mali za Chama zilizopo na hali yake.

Aidha, nilibaini kuwa Katiba ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) inaitaka Bodi ya Wadhamini ya Chama kufanya mikutano isiyopungua mitatu kila mwaka. Hata hivyo, nilibaini kuwa Bodi ya Wadhamini ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) haikufanya mikutano yoyote katika mwaka huu wa fedha. Menejimenti ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) ilihusisha suala hili na ukosefu wa fedha,jambo ambalo lilisababisha CHADEMA kushindwa kuitisha vikao vya bodi. Kushindwa kufanya vikao kunatia shaka zaidi kuhusu uwezo wa bodi kukagua mali na uwekezaji wa chama. Pia, uwezo wake katika kubaini matumizi mabaya ya fedha ambayo yanaweza kuhatarisha upotevu wa rasilimali za chama.

Aidha, nilibaini kuwa Katiba ya Chama cha Demokrasia (DP) kinataka chama hicho kuwa na wajumbe watano kwenye Bodi yake ya Wadhamini. Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kuwa chama hicho kwa sasa kina wajumbe watatu tu, kwani wajumbe wawili walikuwa wamejiuzulu tangu mwezi Juni 2021, na hakuna mbadala wao aliyeteuliwa. Kutokana na kutokuwapo kwa

wajumbe hao wawili, Bodi ya Wadhamini haikuitisha vikao vyake katika kipindi cha kuanzia mwezi Juni 2021 hadi Juni 2022, na kusababisha kutokuwepo kwa usimamizi kuhusu utendaji wa kifedha wa chama, mali, uwekezaji na biashara. Ukosefu huu wa usimamizi unaweza kusababisha matumizi mabaya ya rasilimali za chama.

Napendekeza Bodi za Wadhamini za CHADEMA, CUF, na DP zihakikishe zinafanya vikao vyote vilivyotajwa katika Katiba zao ili kusimamia kwa ufanisi masuala ya kifedha ya vyama vyao. Hii itasaidia kupunguza hatari ya matumizi mabaya ya mali, uwekezaji katika miradi isiyo na faida, na makosa mengine ya kifedha.

14.7 Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Chama cha Wananchi (CUF) vilikuwa na Udhahifu katika Kusimamia Miradi yao ya Uwekezaji

Wakati wa ukaguzi wa daftari la uwekezaji la Chama cha Wananchi (CUF), nilibaini kuwa Chama cha Wananchi (CUF) kinamiliki Redio Mwambao, maeneo ya uchimbaji madini mkoani Tanga, na mashamba ya chumvi mkoani Lindi. Hata hivyo, pamoja na taarifa hizo, menejimenti ya Chama cha Wananchi (CUF) haikutoa taarifa zozote za uwekezaji wala za mradi wakati wa ukaguzi. Ukosefu huu wa taarifa ulifanya iwe vigumu kubaini gharama, mapato na faida inayotokana na uwekezaji huo na kushindwa kutambua sehemu ya mapato ambayo Chama cha Wananchi (CUF) kinapaswa kupata ili kusaidia katika uendeshaji wa chama. Kwa maoni yangu, kukosekana kwa taarifa za uwekezaji kumeonesha kuwa Bodi ya Wadhamini ya Chama cha Wananchi (CUF) kimeshindwa kufuatilia utekelezaji wa miradi hii ya uwekezaji, na hivyo kuwa na hatari ya upotevu wa mapato.

Pia, wakati wa ukaguzi wangu, nilibaini kuwa mnamo mwezi Januari 2022, Chama cha Mapinduzi (CCM) na Mwekezaji walitia saini mkataba wa ubia ili kukuza na kuendesha Soko la Kibiashara la Darajani Corridor lilipo Zanzibar kwa kipindi cha miaka 25 kuanzia Januari 2022 hadi Januari 2047. Gharama za mradi zilikadiriwa kuwa Sh. bilioni 7, na mgawanyo wa faida kati ya Chama cha Mapinduzi (CCM) na mwekezaji ulikuwa asilimia 70 kwa 30 kwa miaka 15 ya kwanza na asilimia 60 kwa 40 kwa miaka kumi iliyobaki, mtawalia. Hata hivyo, sikuweza kukokotoa msingi wa kuamua mgao wa faida kwa kuwa hapakuwa na taarifa za kifedha za kuthibitisha mgao huo. Aidha, mkataba wa ubia haukuwa na kifungu cha ukaguzi wa gharama za mradi

baada ya mradi kukamilika, jambo ambalo linaweza kuathiri usahihi wa gharama zilizokadiriwa.

Uongozi wa Chama cha Mapinduzi (CCM) ulieleza kuwa mgao wa faida utazingatia faida halisi itakayopatikana. Hata hivyo, mkataba wa ubia hauhitaji Mwekezaji kuandaa na kuwasilisha taarifa za kifedha. Kutokuwepo kwa taarifa za kifedha kutafanya iwe vigumu kujua faida halisi itakayopatikana, na kutia shaka ya usawa na usahihi wa mgao wa faida. Aidha, nilibaini kuwa Kanuni za Fedha za Chama cha Mapinduzi (CCM) zinahitaji uteuzi wa Msimamizi wa Mradi kwa mradi wowote unaotekelezwa na Chama cha Mapinduzi (CCM). Msimamizi wa Mradi anawajibika kufuatilia na kuripoti maendeleo ya mradi kwa Bodi ya Wadhamini ya Chama. Hata hivyo, wakati wa ukaguzi, hakukuwa na Msimamizi wa Mradi aliyeteuliwa ili kusimamia utekelezaji wa mradi huu. Hii inamaanisha kuwa Bodi ya Wadhamini ya Chama haikuwa na taarifa za kutosha kuhusu maendeleo ya mradi. Kukosekana kwa taarifa za utekelezaji wa mradi kunaweza kusababisha matumizi mabaya ya rasilimali za chama na kushindwa kugundua vitendo vya udanganyifu kwa wakati.

Kwa kuzingatia matokeo ya ukaguzi wangu, nina maoni kuwa uwekezaji uliofanywa na Chama cha Wananchi (CUF) na Chama cha Mapinduzi (CCM) una mapungufu kutokana na kutokuwapo kwa taarifa za kifedha na kutokuwapo kwa usimamizi. Mapungufu haya yanadhoofisha uwazi na uwajibikaji katika utekelezaji wa miradi ya chama. Kwa matokeo hayo, ni vigumu kuthibitisha kama uwekezaji huu ni wenye manufaa kwa vyama vyote na kunatia shaka katika utendaji.

Napendekeza Bodi za Wadhamini za CUF na CCM zikutane mara kwa mara na menejimenti ili kujadili maendeleo ya miradi ya uwekezaji na kuhakikisha mapato yanayotokana na uwekezaji yanasaidia katika uendeshaji wa shughuli za vyama ili kufikia bajeti.

14.8 Vyama vya Siasa Vitano Havikuwasilisha Tamko la Kila Mwaka la Mali Kwa Msajili wa Vyama vya Siasa

Nilibaini kuwa vyama vitano vya siasa (CHADEMA, DP, NRA, UMD, na UPDP) havikuwasilisha tamko la mali za chama la kila mwaka kwa Msajili wa Vyama vya Siasa kama inavyotakiwa na Kifungu cha 14 (1) (b) (ii) cha Sheria ya Vyama vya Siasa Sura ya 258 (iliyorejewa 2019). Kutofuatwa kwa matakwa

ya kisheria na vyama hivi kunaibua mashaka juu ya uwazi, umiliki na usimamizi wa mali.

Aidha, nilibaini kuwa vyama vya DP na UPDP havina daftari la mali, jambo lililosababisha kushindwa kuandaa na kutoa orodha kamili ya mali kwa Msajili wa Vyama vya Siasa. Ingawa vyama vya CHADEMA, UMD na NRA vilikuwa na daftari la mali, bado vilishindwa kuwasilisha orodha ya mali zinazomilikiwa kwa Msajili wa Vyama vya Siasa kama inavyotakiwa na kifungu cha 14 (1) (b) (ii) cha Sheria ya Vyama vya Siasa Sura ya 258 (iliyorejewa 2019).

Idadi ya Vyama vya Siasa vilivyoshindwa kuwasilisha orodha ya mali kwa Msajili wa Vyama vya Siasa imeongeza kutoka chama kimoja hadi vyama vitano ikilinganishwa na ripoti yangu ya mwaka uliopita. Ongezeko hili la vyama kushindwa kuwasilisha orodha ya mali zao inaonesha kuwa Msajili wa Vyama vya Siasa hatekelezi majukumu yake ipasavyo.

Kutokuwepo kwa ufuatiliaji wa mara kwa mara na Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa kunafanya iwe vigumu katika kufuatilia mali zinazomilikiwa na vyama vya siasa na kuongeza hatari ya mali za vyama kutumiwa vibaya, kutaifishwa, au kuporwa na viongozi au wanachama.

Napendekeza Msajili wa Vyama vya Siasa ahakikishe kila chama cha siasa kinazingatia Sheria ya Vyama vya Siasa kwa kuwasilisha orodha ya mali zinazomilikiwa. Aidha, kutengeneza kanzidata ya kielektroniki ya kufuatilia mali zote za vyama vya siasa kutamwezesha Msajili kufanya uhakiki na utambuzi kwa ufanisi zaidi. Hivyo kupunguza hatari ya mali za vyama kuibwa, kuporwa au kutumika vibaya na watu wasio waaminifu.

14.9 Vyama Vitatu vya Siasa Vilishindwa Kuzingatia Matakwa ya Uwasilishaji wa taarifa za Wajumbe wa Bodi ya Wadhamini kwa Wakala wa Usajili, Ufilisi, na Udhamini (RITA)

Sheria ya Usajili wa Wadhamini, Sura ya 318 (iliyorejewa 2019), inaipa RITA mamlaka ya kusimamia usajili wa Bodi za Wadhamini za vyama vya siasa. Kifungu cha 16(3) cha Sheria hiyo kinahitaji kila Bodi ya Wadhamini iliyosajiliwa kuwasilisha taarifa za wajumbe kila mwaka kwa Kabidhi Wasii Mkuu wa RITA ndani ya mwezi mmoja baada ya tarehe ya maadhimisho,

ambayo itaonesha jina, anwani ya makazi, na anwani ya posta ya kila mdhamini.

Wakati wa ukaguzi, ilibainika kuwa katika mwaka wa fedha 2021/22,Vyama vitatu vya Siasa (AAFP, TLP, na NRA) havikuwasilisha taarifa zao kila mwaka za wajumbe wa Bodi ya Wadhamini kwa RITA. Aidha, Chama cha TLP kimeendelea kushindwa kuwasilisha taarifa zao za kila mwaka kwa RITA kwa kipindi cha miaka miwili mfululizo (mwaka wa fedha 2020/21 na 2021/22).

Hata hivyo, ripoti yangu inaonesha kuongezeka kwa idadi ya vyama vya siasa ambavyo havikuwasilisha taarifa za kila mwaka za wajumbe wa Bodi ya Wadhamini, kutoka chama kimoja hadi vyama vitatu, ikilinganishwa na ripoti yangu ya mwaka uliopita. Hii inaonesha kwamba RITA haivifuatilii vyama vya siasa ili kuhakikisha vinafuata na kutekeleza matakwa ya Sheria ya Usajili wa Bodi za Udhamini.

Kushindwa kwa vyama vya siasa kuwasilisha taarifa za kila mwaka za wajumbe wa Bodi ya Wadhamini kunapunguzia uwezo wa RITA katika kupata taarifa sahihi za wadhamini wa vyama. Kukosekana kwa taarifa hizi kunaweza kusababisha kufanyika kwa shughuli za udanganyifu unaoweza kufanywa na wajumbe waliondolewa ikiwemo kubadilisha taarifa za kibenki au kumbukumbu za umiliki wa mali za vyama, uwekezaji, au biashara. Vitendo hivi vinaweza kusababisha upotevu wa mali na fedha za chama.

Ili kupunguza hatari hizo, napendekeza Vyama vya Siasa kuzingatia Katiba za vyama vyao katika uteuzi wa wajumbe wa Bodi za Wadhamini na kuifahamisha RITA kuhusu mabadiliko yoyote kwa wakati. Aidha, RITA inapaswa kuunda Kanzidata ya kielektroniki ili kutunza taarifa za wajumbe wa Bodi za Wadhamini wa Vyama vya Siasa.

14.10 Kushindwa Kuhuisha Rejista za Wanachama na Viongozi

Kwa mujibu wa kifungu cha 8C (1) cha Sheria ya Vyama vya Siasa, Sura ya 258 (iliyorejewa 2019), vyama vyote vya siasa vilivyosajiliwa vinatakiwa kutunza daftari (rejista) ya viongozi na wanachama wake katika kila ngazi ya utawala. Pamoja na matakwa hayo, mapitio yangu ya uzingatiaji wa Sheria hii nilibaini kuwa vyama vya siasa vitano (ADA-TADEA, DP, NRA, UMD, na UPDP) vilishindwa kuhuisha rejista za viongozi na wanachama wao.

Aidha, tathmini yangu ilibaini kuwa vyama vya UMD na UPDP vilishindwa kuhuisha rejista zao kwa kipindi cha miaka miwili mfululizo (mwaka wa fedha 2020/21 na 2021/22), na kusababisha ongezeko la idadi ya vyama vya siasa visivyofuata sheria kutoka vyama vinne hadi vyama vitano ikilinganishwa na ripoti yangu ya mwaka jana. Matokeo haya yanaonesha haja ya vyama vya siasa kuweka kipaumbele katika uzingatiaji wa Sheria ambayo ni muhimu katika kuleta utendaji kazi mwenye uwazi na uwajibikaji.

Aidha, ukaguzi umebaini kuwa Msajili wa Vyama vya Siasa hajawahi kuviwajibisha vyama vya siasa ambavyo havijawasilisha rejista zao au taarifa zozote zinazohusiana na wanachama kulingana na matakwa ya Kifungu cha 8C (2) cha Sheria ya Vyama vya Siasa, Sura 258 (iliyorejewa 2019). Kutokuwepo kwa uwajibishaji huu, pamoja na baadhi ya vyama vya siasa kushindwa kuhuisha rejista zao,kumesababisha kuwepo kwa taarifa zisizo sahihi kuhusu idadi ya wanachama. Kwa upande mwingine, inafanya kuwa vigumu kusimamia ukusanyaji wa ada kutoka kwa wanachama, ambazo ni muhimu Katika kuboresha uwezo wa kifedha wa vyama.

Ili kuboresha usahihi na upatikanaji wa taarifa za wanachama na viongozi wa vyama vya siasa, napendekeza vyama vyote vya siasa vihuishe rejista zao kwa kuandaa kanzidata ya kielektroniki. Hii itawezesha upatikanaji wa taarifa sahihi, hivyo kupunguza hatari ya makosa au usahulifu. Aidha, natoa wito kwa Msajili wa Vyama vya Siasa kusimamia uwasilishaji wa rejista hizi kama inavyotakiwa na Sheria.

14.11 Kuchelewa Kuwasilisha Taarifa za Fedha kwa ajili ya Ukaguzi

Kwa mujibu wa kifungu cha 18A (2) (a) cha Sheria ya Vyama vya Siasa Sura ya 258 (iliyorejewa 2019), vyama vyote vya siasa vilivyosajiliwa vinatakiwa kuwasilisha taarifa zao za fedha kwa ajili ya ukaguzi ifikapo tarehe 30 Septemba ya kila mwaka. Katika mwaka wa fedha uliofanyiwa ukaguzi, nilipokea taarifa za fedha kwa ajili ya ukaguzi kutoka vyama vya siasa 19. Hata hivyo, nilibaini kuwa vyama vya siasa tisa vilishindwa kuwasilisha taarifa zao za fedha hadi kufikia tarehe ya mwisho ya uwasilishaji (30 Septemba 2022). Hali hii inaonesha kuwepo kwa kiwango kikubwa cha kutozingatia matakwa ya kisheria na inahatarisha uwazi na uwajibikaji wa shughuli za kifedha za vyama vya siasa. Orodha ya Vyama vya Siasa imeoneshwa katika **Jedwali Na. 105**:

Jedwali Na. 105: Orodha ya Vyama vya Siasa ambavyo havikuwasilisha taarifa za fedha kwa ajili ya ukaguzi ifikapo tarehe 30 Septemba, 2022

Na	Jina la Chama cha Siasa	Tarehe inayotakiwa	Tarehe ya uwasilishaji	Ucheleweshaji (Siku)
1	Chama cha Alliance for Democratic Change (ADC)	30 Septemba 2022	1 Desemba 2022	62
2	Chama Cha Kijamii (CCK)	30 Septemba 2022	2 Januari 2023	94
3	Chama cha Ukombozi wa Umma (CHAUMMA)	30 Septemba 2022	27 Desemba 2022	88
4	Demokrasia Makini	30 Septemba 2022	7 Novemba 2022	38
5	Chama cha National League for Democracy (NLD)	30 Septemba 2022	18 Novemba 2022	49
6	Chama cha National Reconstruction Alliance (NRA)	30 Septemba 2022	15 Novemba 2022	46
7	Chama cha United Democratic Party (UDP)	30 Septemba 2022	24 Novemba 2022	55
8	Chama cha Union for Multiparty Democracy (UMD)	30 Septemba 2022	27 Oktoba 22	27
9	Chama cha United Peoples' Democratic Party (UPDP)	30 Septemba 2022	7-Novemba-2022	38

Chanzo: *Taarifa za Fedha za Vyama*

Kuchelewa kuwasilisha taarifa za fedha, kwa kipindi cha siku 27 hadi 94, baada ya tarehe ya mwisho ya uwasilishaji kulisababisha kuchelewa kwa mchakato wa ukaguzi. Hata hivyo, nimebaini kuwa vyama vya siasa vilivyoshindwa kufikia tarehe ya mwisho ya kuwasilisha taarifa zao za kifedha havina ruzuku kutoka Serikalini kwa sababu havina uwakilishi wa mjumbe aliyechaguliwa katika bunge au mamlaka ya serikali za mitaa. Kwa hiyo, vyama hivi vimeona jambo la kuandaa taarifa za fedha ni kama la hiari. Ikumbukwe kuwa Sheria ya Vyama vya Siasa haina kifungu cha hatua stahiki zinazopaswa kuchukuliwa na Msajili wa Vyama vya Siasa endapo taarifa za fedha hazitawasilishwa au zitacheleweshwa.

Ili kutatua pungufu hili, napendekeza Serikali ifanye marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa ili kuweka hatua zinazoweza kuchukuliwa na Msajili wa Vyama vya Siasa endapo vyama vya siasa vitashindwa kuandaa

ama kuwasilisha taarifa za fedha kwa wakati. Hatua zinazopendekezwa zinapaswa kujumuisha adhabu, faini, au kufutwa kwa usajili kwa vyama ambavyo vitaendelea kutozingatia matakwa ya kisheria. Hatua hizi zitaongeza uwazi, uwajibikaji, na kuimarisha uadilifu katika vyama vya siasa.



SURA YA KUMI NA TANO

KAGUZI MAALUMU NA ZA KIUCHUNGUZI

15.1 Utangulizi

Sura hii inatoa muhtasari wa masuala yaliyobainika katika kaguzi Maalumu na za Kiuchunguzi zilizofanywa na Ofisi yangu kwa mujibu wa kifungu cha 27 na 29 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Sura ya 418 (iliyorejewa mwaka 2021). Katika mwaka huu, nilifanya kaguzi maalumu tatu. Mojawapo ya ukaguzi ulilenga kuchunguza usimamizi wa Mfuko wa Tuzo na Tozo na Mfuko wa Kufa na Kuzikana katika Jeshi la Polisi Tanzania. Kaguzi zingine mbili zilifanyika katika Ofisi ya Taifa ya Mashtaka (NPS), na zililenga kupitia taratibu za makubaliano ya kukiri kosa na kupunguziwa adhabu na taratibu za utaifishaji mali, pamoja na usimamizi wake.

Ukaguzi huu ulibaini mapungufu kadhaa katika usimamizi wa fedha hizo, ambayo yameelezwa hapa chini.

15.2 Ukaguzi Maalumu wa Mfuko wa Tuzo na Tozo na Mfuko wa Kufa na Kuzikana katika Jeshi la Polisi Tanzania

Kwa mujibu wa Amri za Jumla za Polisi (PGO), Jeshi la Polisi Tanzania linatakiwa kuanzisha Mfuko wa Tuzo na Tozo, ambao unaendeshwa kupitia utoaji wa huduma za ulinzi kwa taasisi mbalimbali, kama vile taasisi za Serikali, benki za biashara, maeneo ya uchimbaji madini, na kampuni binafsi. Fedha zinazopatikana kutokana na utoaji wa huduma hizo zimelengwa kwa madhumuni kadhaa, ikiwa ni pamoja na kusaidia familia za maafisa wa polisi ambao wamefariki, kutoa zawadi kwa maafisa wa polisi waliopona kutokana na mashambulizi ya silaha, na kugharamia matumizi mengineyo yenye manufaa katika Jeshi la Polisi. Hata hivyo, malipo kutoka katika mfuko huu yanaweza tu kufanywa kwa idhini ya Mlipaji Mkuu wa Serikali, ambaye ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango.

Aidha, Jeshi la Polisi linasimamia Mfuko wa Kufa na Kuzikana, ambao unaendeshwa kupitia makato ya mishahara kutoka kwa askari polisi na wasio polisi (raia). Lengo kuu la mfuko huu ni kutoa rambirambi kwa wanafamilia wa afisa wa polisi au raia aliyefariki, pamoja na kutoa rambirambi kwa afisa wa polisi au raia baada ya kifo cha mke, mtoto, au mtegemezi wake. Kama ilivyo katika Mfuko wa Tuzo na Tozo, utoaji wa fedha kutoka mfuko huu katika Makao Makuu ya Jeshi ya Polisi unaweza kufanyika tu baada ya kupata kibali kutoka kwa Meneja wa Mfuko, wakati kwa kamandi zingine za polisi maofisa nidhamu (staff officers) wanawajibika kutoa vibali.

Kufuatia ombi la Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Ofisi yangu ilifanya ukaguzi maalumu wa Mfuko wa Tuzo na Tozo na Mfuko wa Kufa na Kuzikana uliohusu kipindi cha kuanzia Julai 2018 hadi Novemba 2021. Ukaguzi huu ulilenga kuchunguza uwezekano wowote wa matumizi mabaya ya fedha katika mifuko hii, kubaini kiwango cha hasara, na kubaini wahusika ambao wanaweza kuwa wamehusika katika matumizi mabaya ya fedha za mifuko hii. Wakati wa ukaguzi, timu yangu ilibaini masuala kadhaa ambayo yamefafanuliwa hapa chini.

15.2.1 Kutofatiliwa kwa Mikataba ya Ulinzi na Usimamizi Usioridhisha wa Mapato Kulisababisha Sh. Bilioni 3.88 za Mfuko wa Tuzo na Tozo kutokukusanywa na Jeshi la Polisi

Katika uchunguzi wangu, niligundua kuwa Jeshi la Polisi Tanzania (TPF) lina akaunti ya benki katika Benki Kuu ya Tanzania (BOT) mahsusi kwa ajili ya kukusanya fedha zinazohusiana na Tuzo na Tozo zinazotokana na huduma za ulinzi. Kati ya Julai 2018 na Novemba 2021, akaunti hii ilipokea jumla ya Sh. bilioni 38.23 kutoka taasisi 60, zikiwemo taasisi 10 za serikali, benki 30, maeneo 13 ya uchimbaji madini na mashirika binafsi saba, ambazo zote zilikuwa zimepata huduma za kiulinzi kutoka Jeshi la Polisi.

Uchunguzi wangu ulibaini kuwa taasisi 31 zilikuwa zimepokea huduma za ulinzi kutoka Jeshi la Polisi, lakini mikataba yao ilikuwa imemalizika bila malipo ya Sh. bilioni 2.26. Pia, nilibaini kuwa Jeshi la Polisi lilishindwa kukusanya madeni ya huduma za ulinzi yenye jumla ya Sh. bilioni 1.62 kutoka taasisi 28 ambazo zilikuwa na mikataba halali. Aidha, nilibaini kuwa Jeshi la Polisi lilikuwa limetoa huduma za ulinzi kwa mojawapo ya benki ya

kibiashara bila ya kuwa na mkataba. Uchunguzi zaidi ulibaini kuwa ukusanyaji wa fedha za Mfuko wa Tuzo na Tozo ulikuwa ukifanyika kupitia Mfumo wa Mapato ya Ulinzi ambao haukuunganishwa na Mfumo wa Ukusanyaji Mapato Serikalini (GePG). Hii ilisababisha ankara kutengenezwa bila ya kuwapo kwa nambari za malipo (control number), hivyo kuongeza hatari ya ankara kughushiwa.

Aidha, niligundua kuwa kompyuta iliyokuwa na Mfumo wa Mapato ya Ulinzi haikuwa na nywila, hivyo ilitoa mianya ya kutumiwa kwa mtu yeyote na kuongeza hatari ya udanganyifu wa ankara. Pia, Mfumo wa Mapato ya Ulinzi ulikuwa ukijitegemea, na Mhasibu mmoja alikuwa na uwezo wa kuufikia na kuudhibiti kikamilifu (full control), ikiwa ni pamoja na kutengeneza ankara, kupitisha ankara,kuchapisha ankara na kuhifadhi taarifa za makusanyo (backup). Hali hii ilileta hatari kubwa ya udanganyifu wa makusanyo ya fedha za mfuko.

Maoni yangu ni kuwa Jeshi la Polisi lilikosa mifumo madhubuti ya ufuatiliaji na kushindwa kukusanya mapato ya ulinzi ya jumla ya Sh. bilioni 3.88 kutoka kwa wateja wenye mikataba iliyoisha muda wake na wateja waliokuwa na mikataba halali. Hali hii inaweza kusababisha upotevu wa mapato ikiwa fedha hizi hazitakusanywa.

Kulingana na matokeo ya uchunguzi, napendekeza Jeshi la Polisi Tanzania kukusanya madeni yote, kuhuisha mikataba iliyoisha muda wake, na kuunganisha Mfumo wa Mapato ya Ulinzi na Mfumo wa Ukusanyaji Mapato Serikalini (GePG). Hii itawezesha ufuatiliaji na usimamizi mzuri wa fedha za Mfuko wa Tuzo na Tozo. Aidha, Jeshi la Polisi linapaswa kuanzisha mifumo ya udhibiti kama vile nywila na vikwazo vya upatikanaji wa mfumo (restricted access controls) ili kupunguza hatari za udanganyifu na kughushi, na hivyo kuimarisha uwazi na uwajibikaji.

15.2.2 Usimamizi Usioridhisha na Matumizi Mabaya ya Fedha za Mfuko wa Tuzo na Tozo katika Jeshi la Polisi Tanzania Jumla ya Sh. Bilioni 1.04

Kwa mujibu wa Kanuni ya 4(1) ya Kanuni za Fidia za Jeshi la Polisi na Magereza za mwaka 2010, afisa polisi ambaye atapata majeraha mabaya au kifo wakati akitekeleza wajibu wake atastahili fidia kulingana na kiwango cha jeraha au kifo. Jeshi la Polisi Tanzania liliweka kiwango cha malipo ya fidia ya Sh. milioni 15 kwa afisa polisi atakayefariki kutokana na majeraha atakayopata wakati wa kutekeleza majukumu yake. Malipo haya hutolewa kwa ndugu wa karibu au mrithi wa afisa atakayefariki.

Kati ya Julai 2018 na Novemba 2021, Jeshi la Polisi lilitoa kiasi cha Sh. bilioni 26.52 kutoka katika Mfuko wa Tuzo na Tozo kwa ajili ya matumizi mbalimbali ya Jeshi la Polisi yaliyoainishwa na Sheria ya Uanzishwaji wa Mfuko, pamoja na kutoa mafao kwa askari polisi waliopata majeraha wakati wa kutekeleza majukumu yao. Ukaguzi ulibaini kuwa kati ya fedha zilizotolewa kwenye Mfuko, kiasi cha Sh. bilioni 1 kililipwa kwa walengwa 223 waliopata majeraha wakati wakitekeleza majukumu yao. Viwango vya malipo ya fidia vilitofautiana kutoka Sh. milioni 1.05 hadi kiwango cha juu cha Sh. milioni 15, badala ya kiasi halisi (fixed) cha Sh. milioni 15 ambacho kilikuwa kimeanishwa katika miongozo ya ulipaji fidia. Hata hivyo, baada ya uchunguzi zaidi, iligundulika kuwa hakukuwa na afisa yeyote wa Jeshi la Polisi aliyepata majeraha kwa kiwango ambacho alistahili malipo ya fidia. Hii inathibitisha uwapo na ubadhirifu wa fedha katika Mfuko wa Tuzo na Tozo.

Tukio jingine la matumizi mabaya linahusisha kuidhinishwa na Mlipaji Mkuu wa Serikali utaoji wa kiasi cha Sh. milioni 446.03 mnamo mwezi Machi 2021 ili kulipa mafao ya maafisa wa polisi wanaostahili. Hata hivyo, iligundulika kuwa mnamo mwezi Juni 2021, Mhasibu Mkuu wa Jeshi la Polisi alitumia hati za malipo saba na kuchepusha kiasi cha Sh. milioni 34.90 katika kiasi kilichoidhinishwa na kufanya matumizi yasiyoendana na malengo yaliyokusudiwa ya mfuko.

Kulingana na matokeo ya uchunguzi, ukaguzi ulithibitisha kuwa Jeshi la Polisi Tanzania lilitumia vibaya kiasi cha Sh. bilioni 1.04 kutoka kwenye Mfuko wa Tuzo na Tozo kutokana na uchepushaji na matumizi yasiyohusiana

na dhumuni la Mfuko. Hii ilichangiwa zaidi na Jeshi la Polisi kushindwa kutekeleza maelekezo ya vibali vilivyotolewa na Mlipaji Mkuu wa Serikali. Ni maoni ya ukaguzi kuwa matumizi mabaya na ubadhirifu katika Mfuko wa Tuzo na Tozo yalitokea kutokana na kutokuwepo kwa miongozo ya matumizi sahihi ya fedha za mfuko na kuhakikisha kunakuwepo na uwajibikaji wa matumizi ya fedha kutoka katika Komandi zote za Jeshi la Polisi.

Aidha, Mhasibu Mkuu wa Jeshi la Polisi alichangia kwa kiasi kikubwa katika usimamizi mbovu wa fedha za Mfuko kwa kugeuza matumizi ya fedha za Mfuko bila ya kuzingatia maelekezo ama vibali vilivyotolewa na Mlipaji Mkuu wa Serikali. Uchunguzi umebainisha masuala yanayohitaji hatua za haraka kuchukuliwa ili kuboresha usimamizi bora wa mfuko,na kuhakikisha kuwa fedha za mfuko zinatumika katika malengo yaliyokusudiwa.

Napendekeza hatua za haraka za kinidhamu na kisheria zichukuliwe dhidi ya wote waliohusika na usimamizi mbovu wa matumizi ya fedha za Mfuko wa Tuzo na Tozo katika Jeshi la Polisi.

15.2.3 Mapungufu yaliyobainika katika Usimamizi wa Fedha za Mfuko wa Kufa na Kuzikana Katika Jeshi la Polisi Tanzania

Uchunguzi uliofanyika ulibaini kuwa Jeshi la Polisi Tanzania lilikuwa likipokea makato ya fedha kutoka katika mishahara ya askari polisi na wasio polisi (raia) ili kuchangia katika Mfuko wa Kufa na Kuzikana. Fedha hizi zilikuwa zikiwekwa kwenye akaunti mojawapo ya benki ya kibiashara na zilikuwa zikisimamiwa na Makao Makuu ya Jeshi la Polisi.Aidha, ilibainika kuwa Jeshi la Polisi lilikuwa likihamisha fedha hizo kwenda katika akaunti 62 tofauti za benki zilizotengwa kwa ajili ya kulipa mafao ya Kufa na Kuzikana. Akaunti hizi zilikuwa katika Komandi zote za Jeshi la Polisi zilizopo Tanzania Bara na Zanzibar.

Aidha, Jeshi la Polisi liliandaa miongozo mahsusi ya kusimamia matumizi ya fedha za Mfuko wa Kufa na Kuzikana, ambapo ilihitajika kuanzishwa kwa sekretarieti na uteuzi wa watia saini wa benki. Uongozi wa mfuko huo ulikuwa chini ya Mwenyekiti na Meneja wa mfuko, huku Inspekta Jenerali wa Polisi (IGP) akiteuliwa kuwa mwangalizi wa mfuko, mwenye jukumu la kuhakikisha miongozo iliyowekwa inafuatwa na kuzingatiwa.

Kwa mujibu wa miongozo hiyo, Meneja wa Mfuko wa Kufa na Kuzikana alikuwa na jukumu la kupanga vikao vya Sekretarieti, huku Mwenyekiti alipewa jukumu la kuitisha Mikutano Mikuu ya mwaka ya wanachama. Hata hivyo, baada ya uchunguzi, ilibainika kuwa mfuko haukuwa na Sekretarieti na hivyo kushindwa kufanya vikao vya sekretarieti kati ya mwaka 2018 na 2022. Aidha, Inspekta Jenerali wa Polisi (IGP), akiwa kama mwangalizi wa mfuko, hakumwelekeza Mwenyekiti wa mfuko kuandaa mikutano mikuu ya mwaka ya wanachama. Uchunguzi zaidi ulibaini kuwa mfuko haukuwa na mhasibu, na majukumu ya uhasibu yalikabidhiwa kwa meneja wa mfuko. Matokeo yake, taarifa za fedha hazikuandaliwa wala kukaguliwa, na daftari la wanachama halikutunzwa na kusababisha kushindwa kujua idadi ya wanachama na wanufaika wao.

Ni maoni yangu kuwa usimamizi na udhibiti wa matumizi ya fedha za Mfuko wa Kufa na Kuzikana ulikosekana kwa kuwa hakukuwa na Sekretarieti. Hivyo kushindwa kufanyika kwa vikao vya Sekretarieti na mikutano mikuu ya mwaka. Aidha, kukokesekana kwa Mhasibu kulisababisha taarifa za fedha kushindwa kuandaliwa na ukaguzi kufanyika. Mapungufu haya makubwa yalisababisha matumizi mabaya na ubadhirifu wa fedha za Mfuko na yakiendelea yatahatarisha ustawi na usalama wa fedha za Mfuko.

Ili kukabiliana na mapungufu yaliyobainika, napendekeza Jeshi la Polisi Tanzania lichukue hatua za haraka za kuanzisha Sekretarieti, kuteua Mhasibu mwenye uzoefu, na kufanya ukaguzi wa mara kwa mara ili kuhakikisha kunakuwepo na utawala bora na usimamizi madhubuti wa fedha za Mfuko. Hii ni muhimu kufanyika ili kulinda ustawi na usalama wa fedha za wanachama wa mfuko.

15.2.4 Ubadhirifu wa Fedha za Mfuko wa Kufa na Kuzikana uliofanyika Katika Jeshi la Polisi Tanzania Bara, jumla ya Sh. Bilioni 2.44

Kwa mujibu wa uchunguzi , hadi kufikia Juni 2018, akaunti ya benki ya Mfuko wa Kufa na Kuzikana, iliyokuwa ikisimamiwa na Makao Makuu ya Jeshi la Polisi katika benki ya biashara, ilikuwa na bakaa ya Sh. bilioni 2.98. Kati ya Julai 2018 na Novemba 2021, mfuko ulikusanya jumla ya Sh. bilioni 19.27 na kufanya jumla yote ya fedha za Mfuko kuwa Sh. bilioni 22.25. Iligundulika wakati wa uchunguzi kuwa Sh. bilioni 22.25 zilitolewa katika akaunti ya benki ya Mfuko wa Kufa na Kuzikana na kuhamishiwa kwenye akaunti 62

tofauti za benki zilizopo Tanzania Bara na Zanzibar kwa ajili ya kufanya malipo ya mafao ya mazishi na rambirambi.

Katika kuchunguza matumizi ya fedha zilizotolewa katika Mfuko ya Kufa na Kuzikana, ukaguzi ulibaini matukio kadhaa ya matumizi mabaya na ubadhirifu. Mojawapo ya tukio lililoibuliwa lilikuwa la watia saini wanne, wakiwamo watatu waliotoroka katika Jeshi la Polisi ili kuepuka kuwajibishwa kwa vitendo vyao, na mmoja aliyestaafu, waliotoa kiasi cha Sh. milioni 754.65 kutoka katika akaunti ya mfuko bila ya kuwapo kwa taarifa zozote za walengwa. Aidha, ukaguzi ulibaini kuwa Meneja wa mfuko alijihamishia kwa njia za udanganyifu kiasi cha Sh. milioni 5 kwenye akaunti yake binafsi ya benki kwa kudanganya kuwa alikuwa miongoni mwa wafiwa. Hata hivyo, Meneja huyo wa mfuko alikuwa miongoni mwa waliotoroka katika Jeshi la Polisi na hakuweza kupatikana, hivyo kuwa na ugumu wa kumwajibisha kwa vitendo vyake.

Uchunguzi zaidi ulibainisha ushahidi wa Meneja wa mfuko kuwashawishi makarani watatu wa mkoa wa Morogoro kwa nyakati tofauti, na kusababisha kuhamishwa kwa kiasi cha jumla ya Sh. milioni 23.50 katika nyakati tofauti kwenda kwenye akaunti ya benki ya mmojawapo wa ndugu zake. Akaunti hiyo ya benki ilidaiwa kutumika kukusanya fedha za udanganyifu. Makarani hawa husika walieleza kuwa uhamishaji wa fedha hizo ulikuwa muhimu ili kujenga uhusiano kati ya Ofisi ya Morogoro na Makao Makuu ya Jeshi la Polisi. Vitendo hivi vinaashiria kukosekana kwa uadilifu kwa upande wa Meneja wa mfuko na kuibua mashaka kuwa huenda matumizi mabaya ya fedha za mfuko yalikuwa tu sio kwa makarani bali yalijumuisha viongozi wa ngazi za juu ndani ya Jeshi la Polisi.

Baada ya uchunguzi zaidi wa fedha zilizotolewa kutoka katika Mfuko wa Kufa na Kuzikana, ilibainika kuwa katika Ofisi ya Mkoa wa Kinondoni, askari polisi sita walipokea malipo ya jumla ya Sh. milioni 28.20 kwa kisingizio kuwa yalikuwa marejesho ya mkopo waliokopesha Mfuko. Hata hivyo, hakukuwa na ushahidi ulionesha kuwa polisi hao walikopesha Mfuko na hivyo ukaguzi kuthibitisha kuwa malipo hayo yalikuwa ya udanganyifu.

Kadhalika, uchunguzi ulibaini kuwa watia saini nane kutoka Ofisi za Polisi za Mikoa ambazo ni Ilala, Kinondoni, Temeke na Ofisi ya Polisi Kanda Maalumu ya Dar es Salaam walifanya malipo ya hundi 256 kwa mnufaika mwenye jina

moja na kujipatia kwa udanganyifu kiasi cha Sh. milioni 179.67 kutoka kwenye mfuko. Aidha, uchunguzi zaidi ulibaini kuwa Jeshi la Polisi Tanzania lilikopa jumla ya Sh. milioni 991.45 kutoka katika Mfuko wa Kufa na Kuzikana kati ya miaka ya fedha 2018/19 na 2020/19. Hata hivyo, Jeshi la Polisi lilifanikiwa kurejesha kiasi cha Sh. milioni 232.26 pekee, kati ya fedha zote zilizokopwa, na kiasi cha Sh. milioni 759.19 kikiwa bado hakijarejeshwa hadi kufikia kipindi cha ukaguzi mnamo mwezi Machi 2022. Pia, ukaguzi ulibainisha kuwa kiasi cha Sh. milioni 855.84 kati ya fedha zote zilizokopwa kilitumiwa vibaya na Jeshi la Polisi, kwa kuwa hakukuwa na ushahidi wowote wa nyaraka za matumizi zilizowasilishwa.

Aidha, baada ya kufanya uchunguzi wa kina, ilibainika kuwa Mfuko wa Kufa na Kuzikana ulitoa mafao kwa jumla ya wanufaika 2,195 katika Ofisi ya Kanda Maalumu Dar es Salaam,na Ofisi za mikoa ya kipolisi Ilala, Temeke na Kinondoni. Kati ya wanufaika hao, wanufaika 1,442 walihojiwa na timu ya ukaguzi, huku wanufaika 753 hawakuhojiwa kutokana na sababu mbalimbali kama vile kifo, kustaafu au uhamisho. Hata hivyo, wakati wa mahojiano, wanufaika wote 1,442 walikana kupokea malipo yoyote kutoka kwenye mfuko, na maelezo yao yalithibitishwa zaidi na taratibu za ukaguzi zilizofanyika. Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kuwa watia saini 11 kutoka Ofisi hizo zilizotajwa hapo juu walihusika katika kuchukua Kiasi cha Sh. milioni 687.15 zilizokusudiwa kuwalipa wanufaika 1,442 kwa njia za udanganyifu na kusababisha wanufaika hao kutopata malipo yao.

Kulingana na uchunguzi uliofanyika, imebainika kuwa Mfuko wa Kufa na Kuzikana wa Tanzania Bara ulisimamiwa vibaya na Meneja wa mfuko, Mwenyekiti na Mlezi, ambao walishindwa kuweka nidhamu na udhibiti katika ya matumizi sahihi ya fedha za Mfuko. Usimamizi huu mbovu ulisababisha ubadhirifu wa kiasi cha Sh. bilioni 2.44 kutoka kwenye Mfuko.

Napendekeza hatua za kinidhamu na kisheria zichukuliwe dhidi ya watu wote waliohusika na ubadhirifu huo wakiwemo wale waliotoroka katika Jeshi la Polisi. Vyombo vya usalama vya ndani vinapaswa kuhakikisha kuwa watu wote waliotoroka wanapatikana na kuwajibishwa kwa ubadhirifu walioufanya.

15.2.5 Ubadhirifu wa Fedha za Mfuko wa Kufa na Kuzikana uliofanyika katika Jeshi la Polisi Zanzibar Jumla ya Sh. Bilioni 2.40

Uchunguzi zaidi ulibaini kuwa Jeshi la Polisi Zanzibar lilikuwa na akaunti tisa za benki zilizotengwa kwa ajili ya kulipa mafao ya mazishi katika Ofisi zote sita za Polisi Mikoa na Makao Makuu ya Polisi Zanzibar. Ukaguzi ulithibitisha kuwa akaunti zote hizo zilipokea fedha kutoka Makao Makuu ya Jeshi la Polisi yaliyopo Tanzania Bara. Baada ya kufanya ukaguzi zaidi, ilibainika kuwa Makao Makuu ya Polisi Bara ilihamisha kiasi cha Sh. bilioni 3.56 kwenda akaunti nane za benki kwa lengo la kulipa mafao ya mazishi kwa walengwa wote waliopo Zanzibar katika kipindi cha mwezi June 2018 hadi Novemba 2021.

Wakati wa uchunguzi, ilibainika kuwa Ofisi ya Polisi ya Mkoa Kusini-Unguja ilikuwa na akaunti mbili za benki, huku moja ikiwa hai (active) na nyingine ikiwa mfu (dormant). Iligundulika kuwa maafisa wawili wa polisi waliokuwa watia saini katika akaunti ya benki iliyokuwa mfu walishirikiana na Meneja wa tawi la benki ya biashara katika Ofisi ya Polisi ya Mkoa Kusini-Unguja na kughushi saini ili kuamsha akaunti hiyo. Matokeo yake, waliweza kuiba Sh. milioni 988.45. Pia, ilibainika kuwa watia saini watatu wa akaunti ya benki iliyokuwa hai (active) walitoa benki kiasi cha Sh. milioni 576.50 kwa nia ya kulipa mafao ya mazishi kwa walengwa. Hata hivyo, ilibainika kuwa watia saini wawili waliiba Sh. milioni 511.50 kabla ya walengwa hao kulipwa.

Katika uchunguzi zaidi, ilibainika kuwa Ofisi ya Polisi ya Mkoa Kaskazini-Unguja ilikuwa imepokea kiasi cha Sh. milioni 631.28 kutoka katika akaunti kuu ya Mfuko wa Kufa na Kuzikana iliyopo Tanzania Bara.Lengo la fedha hizo lilikuwa ni kulipa mafao ya mazishi kwa walengwa. Hata hivyo, ilibainika kuwa watia saini watatu walitoa kiasi cha Sh. milioni 590.39 kutoka katika akaunti ya Ofisi ya Polisi Mkoa Kaskazini-Unguja ili kulipa fedha hizo kwa walengwa. Baada ya uchunguzi zaidi, ilibainika kuwa Sh. milioni 543.89 kati ya fedha zilizotolewa hazikuthibitishwa kama zilipokelewa na walengwa hao. Hivyo uchunguzi kuthibitisha kuwa fedha hizo zilichukuliwa na watia saini hao watatu kwa njia za udanganyifu.

Jeshi la Polisi Zanzibar lilithibitisha kwa timu ya ukaguzi kuwa watia saini hao watatu walikuwa wameachishwa kazi katika Jeshi la Polisi na Jeshi la Polisi Zanzibar halikuweza kuwapata. Hivyo, hawakuweza kuhojiwa kuhusu

kuhusika kwao na ubadhirifu huo. Aidha, timu ya ukaguzi ilielezwa na mmojawapo wa Makarani (clerk) waliohusika na ulipaji wa fedha za Mfuko kwa walengwa kuwa baadhi ya fedha hizo za mfuko zilikuwa zikitolewa kwa viongozi wa juu wa Jeshi la Polisi ingawa sikupata uthibitisho. Hata hivyo, ukaguzi ulibaini akaunti ya benki ya ndugu wa Meneja wa Mfuko ilipokea kiasi cha Sh. milioni 5 kutoka kwa mmojawapo wa Makarani. Matokeo haya yanaonesha kuwa ubadhirifu huo haukuwa tu kwa watia saini watatu na kwamba huenda kulikuwa na njama (collusion).

Aidha, uchunguzi zaidi ulibaini kuwa Makao Makuu ya Jeshi la Polisi Zanzibar ilitoa jumla ya Sh. milioni 400.50 kutoka katika akaunti ya Mfuko wa Kufa na Kuzikana kwa ajili ya kulipa mafao kwa walengwa. Hata hivyo, ni Sh. milioni 94.50 pekee ndizo zilizolipwa kwa walengwa wanaostahili huku kiasi cha Sh. milioni 306 kilichobaki kilitumika kwa njia za udanganyifu. Pia, ukaguzi ulibaini kuwa Ofisi ya Polisi Mkoa wa Kusini Pemba ilipokea Sh. milioni 175 kwa nia ya kulipia mafao kwa walengwa. Hata hivyo, walitumia kiasi cha Sh. milioni 39.95 kwa shughuli zisizohusiana na lengo la Mfuko.

Aidha, nilibaini kuwa Ofisi ya Polisi ya Mkoa wa Kaskazini-Pemba ilipokea Kiasi cha Sh. milioni 154 lakini ilitumia kiasi cha Sh. milioni 2.16 katika kukarabati magari ya Jeshi la Polisi.

Pia,uchunguzi umebaini matukio mbalimbali ya usimamizi mbovu wa fedha za Mfuko wa Kufa na Kuzikana uliofanywa na Jeshi la Polisi Zanzibar. Usimamizi huu mbovu ulitokana na kukosekana kwa mifumo mizuri ya usimamizi na udhibiti wa fedha za Mfuko ambao ulipaswa kutekelezwa na Meneja, Mwenyekiti na Mlezi wa mfuko. Kutokana na usimamizi huo mbovu, kumekuwapo na ubadhirifu wa fedha za Mfuko wa kiasi cha Sh. bilioni 2.40 uliosababishwa kwa kuwapo na ushirikiano baina ya Jeshi la Polisi Zanzibar na Makao Makuu ya Jeshi la Polisi Tanzania Bara.

Kulingana na matokeo ya uchunguzi, napendekeza hatua za kinidhamu na kisheria zichukuliwe dhidi ya watu wote waliohusika katika matumizi mabaya ya fedha za Mfuko wa Kufa na Kuzikana. Hatua hii itatumika kama kizuizi kwa wengine wenye nia kama hiyo na kuhakikisha kuwa wahusika wanawajibika kwa makosa yao.

Aidha, ili kuzuia matukio ya baadaye ya ubadhirifu, ni muhimu udhibiti thabiti wa kifedha, ikiwa ni pamoja na ukaguzi wa mara kwa mara, uanzishwe, na kutekelezwa ili kurejesha imani ya wanachama katika mfumo huo. Udhibiti huu unapaswa kutekelezwa katika ngazi zote za uongozi na usimamizi wa mfuko ili kuhakikisha uwazi na uwajibikaji.

Ili kuhakikisha kuwa fedha za umma zinatumika katika malengo yaliyokusudiwa na kurejesha imani ya wananchi, ni muhimu kuchukua hatua za kinidhamu na kisheria dhidi ya watu wote waliohusika na matumizi mabaya ya fedha za Mfuko za jumla ya Sh. bilioni 4.84 kutoka katika Ofisi ya Polisi Tanzania Bara na Zanzibar. Aidha, utekelezaji wa udhibiti madhubuti wa kifedha ni muhimu katika kufikia malengo haya.

15.3 Ukaguzi Maalumu Kuhusu Usimamizi na Uendeshaji wa Mikataba ya Makubaliano ya Kukiri Kosa iliyosimamiwa na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka.

Nimefanya Ukaguzi Maalumu wa Usimamizi na Uendeshaji wa Makubaliano ya Kukiri Kosa na Kupunguza adhabu uliosimamiwa na Ofisi ya Taifa ya Mashitaka (NPS) na Mkurugenzi wa Mashitaka (DPP). Lengo lilikuwa ni kutathmini hatua mbalimbali za kesi za kukiri makosa na kupunguza adhabu kuanzia tarehe 1 Julai 2019 hadi tarehe 31 Machi 2022. Madhumuni ya Mikataba ya Kukiri Kosa na Kupunguziwa Adhabu kati ya Mwendesha Mashtaka na Mshtakiwa ni kutatua kesi za jinai kwa ufanisi na haraka.

Kwa mujibu wa Kifungu cha 194A cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, DPP ana mamlaka ya kuingia Makubaliano ya Kukiri Kosa na Kupunguza Adhabu ili kuharakisha mchakato wa kesi na kupunguza msongamano wa wafungwa magerezani. Makubaliano haya yanahusisha mshtakiwa na DPP kusaini hati na Mshtakiwa kulipa fidia iliyokubaliwa kwenye akaunti maalumu ya DPP iliyopo Benki Kuu ya Tanzania.

Wakati wa ukaguzi, niligundua kuwa kesi 352 za Kukiri Kosa na Kupunguza Adhabu zilitokea katika Mikoa 26 ya Tanzania Bara. Katika kesi hizi, washitakiwa 893 walitia saini makubaliano 380 na kukubaliana kulipa jumla ya Sh. bilioni 219.13. Kati ya tarehe 1 Julai 2019 na 31 Machi 2022, Sh. bilioni 55.87 zilikusanywa na kuwekwa katika akaunti ya Kukiri Kosa na Kupunguza Adhabu inayosimamiwa na DPP. Kiasi hiki kinajumuisha Sh.

bilioni 45.51 kama fidia kwa makosa ya washitakiwa waliokiri Kosa, Sh. bilioni 2.11 kama faini za Mahakama, na Sh. bilioni 8.26 ni malipo yaliyofanywa bila ya kuwepo na Makubaliano ya Kukiri Kosa.

Pia, niligundua kuwa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka (NPS) ilipokea jumla ya Sh. bilioni 55.87, ambapo Sh. bilioni 42.68 zilihamishwa kutoka katika akaunti ya Kukiri Kosa na Kupunguza Adhabu. Uhamisho huu ulijumuisha Sh. bilioni 38.80 zilizohamishwa kwenda Mfuko Mkuu, Sh. bilioni 3.43 zilizohamishwa kwenda Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), na Sh. milioni 450.56 zilizorejeshwa kwa waathirika. Ukaguzi umebaini mapungufu kama ifuatavyo:

15.3.1 Washitakiwa Kushindwa Kukamilisha Malipo ya Ahadi zao

Kati ya majalada 352 niliyopitia, 297 yalikuwa na ahadi za Sh. bilioni 219.13. Hata hivyo, ni Sh. bilioni 48.52 pekee ndizo zilizolipwa na washtakiwa katika majalada 195 ya kesi, na kuacha majalada 102 yakiwa na ahadi ambazo hazijalipwa zenye thamani ya Sh. bilioni 170.61 bilioni. Ukiukaji huu wa mikataba unampa Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma (DPP) haki ya kufungua upya mashtaka dhidi ya washtakiwa.

Aidha, niligundua kuwa DPP hajachukua hatua stahiki za kuhakikisha makusanyo ya fedha ambazo bado hazijalipwa kutoka kwa washtakiwa au kuwasilisha maombi ya kukamata mali zao kwa ajili ya kulipa fidia, kama inavyotakiwa na Kifungu cha 328 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai Sura ya 20. DPP kushindwa kukusanya ahadi na kuchukua hatua kuna leta sintofahamu na kuwepo kwa nia ya ufuatiliaji wa kina na kuchukua hatua za kisheria ili kuhakikisha kuwa washtakiwa wanatimiza wajibu wao chini ya Makubaliano ya Mikataba ya Kukiri Kosa na hukumu za Mahakama.

Napendekeza Mkurugenzi wa Mashitaka (DPP) kuhakikisha Makusanyo ya Fidia ambazo hazijalipwa kutoka kwa washitakiwa yanafanyika na pia Mahakama iweke utaratibu mzuri wa kupokea na kusikiliza malalamiko kutoka kwa wale watakaopinga fidia zao. Hatua hizi zitasaidia kuimarisha uadilifu katika mfumo wa sheria, kuhakikisha haki inatendeka, na kulinda haki za washtakiwa.

15.3.2 Kutofatwa kwa Masharti ya Mikataba ya Kukiri Kosa na Kupunguza Adhabu

Wakati wa uchunguzi wa akaunti ya Benki ya kupokea fedha za Mikataba ya Kukiri Kosa na Kupunguza Adhabu inayosimamiwa na DPP, iligundulika kuwa washtakiwa watatu walilipa kiasi cha Sh. milioni 328.53 kwenye akaunti hiyo, licha ya kesi zao kutatuliwa kwa utaratibu wa kawaida wa kukiri makosa katika Mahakama, badala ya kupitia katika utaratibu wa Mikataba ya Kukiri Kosa. Pia, DPP alipokea kiasi cha Sh. bilioni 1.62 kutoka kwa mnufaika wa kesi ya uhujumu uchumi, ingawa hakukuwa na kesi iliyokuwa ikiendelea, wala mikataba ya kukiri kosa, ama amri ya Mahakama. Pia, niligundua kuwa Sh. bilioni 6.10 zilikamatwa na kutaifishwa kutoka kwa washitakiwa wanne waliohusika na rushwa, kesi za michezo ya upatu, na kushindwa kuthibitisha vyanzo vya mapato. Kiasi hicho kilichokusanywa kiliwekwa kwenye akaunti ya Benki ya kukiri kosa badala ya akaunti ya kutaifisha mali.

Pia, DPP alikusanya Sh. bilioni 2.11 kama malipo ya ada za Mahakama kutokana na kesi 170 zilizoamuliwa na Mahakama ya Tanzania, lakini badala ya kulipa ada kwenye akaunti za benki za Mahakama kama inavyotakiwa. Ada hizo zililipwa kwenye akaunti ya benki ya kukiri kosa. Hadi kufikia Machi 2022, bakaa ya akaunti ya kukiri kosa ilikuwa ni Sh. bilioni 13.20. Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kuwa jumla ya Sh. bilioni 10.16 zililipwa kwenye akaunti ya kukiri kosa bila kuhusishwa na mchakato wa kukiri kosa. Hali hii inaonesha kuwa mchakato wa Makubaliano ya kukiri kosa haukuwa ukisimamiwa kwa kufuata miongozo na taratibu zilizowekwa.

Napendekeza Mkurugenzi wa Mashitaka (DPP) kuchukua hatua stahiki ili kuhakikisha kuwa mchakato na taratibu za makubaliano ya kukiri kosa zinafatwa kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizowekwa ili kuzuia matukio kama hayo kutokea tena katika siku za usoni.

15.3.3 Kuwepo kwa Uwezekano wa Ukiukwaji wa Maadili Katika Mikataba ya Kukiri Kosa na Kupunguziwa Adhabu

Wakati wa ukaguzi, nilibaini masuala kadhaa muhimu yanayohusiana na usimamizi wa makubaliano na taratibu za kukiri kosa. Kwanza kabisa, ukosefu wa uwazi kutokana na upungufu wa nyaraka katika majalada ya kesi 92 kati ya 352 niliyoyapitia, kulisababisha mashaka juu ya uadilifu katika mchakato. Upungufu huu wa nyaraka umeathiri wigo wa ukaguzi.

Pili, kulibainika kutokuwepo na usawa katika kushughulikia maombi ya kuongezwa muda wa mwisho wa malipo ya fidia, huku baadhi ya maombi yakichukua hadi siku 621 kukamilika badala ya siku 30, kama ilivyoelezwa katika mikataba ya kukiri kosa. Pia, hapakuwa na Miongozo au Masharti yaliyowekwa ya kuahidi dhamana katika mikataba ya kukiri kosa. Hali hii ilisababisha uwepo wa utofauti katika masharti ya mikataba ya kukiri kosa. Pia,uamuzi wa kuhitaji dhamana au kutokuhitajika kwa dhamana kuliachwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka.

Pia, ukaguzi uligundua uwezekano wa ukiukwaji wa maadili na matumizi mabaya ya madaraka, ikiwa ni pamoja na kuchukua kiasi cha Sh. bilioni 1.5 katika malipo ya fidia bila idhini na kufungua mashitaka na kuwashikilia kinyume cha sheria washitakiwa watatu kwa makosa ya kodi nje ya majukumu yao. Aidha, iligundulika uwepo wa nyaraka bandia katika mikataba ya kukiri kosa.

Aidha, nilifanya mahojiano na washitakiwa ambao walikiri kuandika na kusaini barua za kukiri kosa na kupunguziwa adhabu ambazo zilipatikana katika majalada ya kesi zao. Hata hivyo, washitakiwa wao walidai kulazimishwa kusaini makubaliano hayo.

Hali hii inaonesha uwepo wa ukiukwaji wa Kanuni namba 12 na 14 za Kanuni za Mwenendo wa Makosa ya Jinai (Makubaliano ya Kukiri Kosa) za Mwaka 2021, ambao unaleta shaka juu ya uwazi na uadilifu katika mchakato wa makubaliano ya kukiri kosa. Pia, uwepo wa ukiukwaji wa haki za washitakiwa wakati wa kukamatwa, kufunguliwa mashtaka, na usimamizi wa kesi zilizoamuliwa kupitia makubaliano ya kukiri kosa.

Napendekeza Mamlaka za uteuzi za aliyekuwa Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) ziunde Tume huru ya kuchunguza uwezekano wa ukiukwaji wa maadili na matumizi mabaya ya ofisi ya umma katika mchakato wa makubaliano ya kukiri kosa. Tume hiyo inapaswa kuchunguza madai ya kulazimishwa kwa washitakiwa na ukiukwaji wa Kanuni za Mwenendo wa Mashitaka ya Jinai (Makubaliano ya Kukiri Kosa) za Mwaka 2021, na kutoa mapendekezo ya uboreshaji wa mapungufu yote yaliyobainika.

15.4 Ukaguzi Maalumu Kuhusu Taratibu za Utaifishaji Mali pamoja na Taratibu za Makabidhiano, Ugawaji na Usimamizi wa Mali zilizotaifishwa na Ofisi ya Taifa ya Mashitaka

Nimefanya ukaguzi kati ya Julai 2019 na Machi 2022 na lengo la ukaguzi lilikuwa ni kuthibitisha utekelezaji wa sheria na kanuni zinazohusiana na utaifishaji mali kupitia makubaliano ya kukiri kosa au katika kesi ambazo mali zilizotaifishwa zilihusiana na mashtaka ya jinai. Aidha, nililenga kutathmini taratibu zinazohusiana na uhamishaji, uhakiki, usimamizi, na hali ya mali zote zilizotaifishwa, kama ilivyoelezwa katika Kifungu cha 14 hadi 15 cha Sheria ya Mazalia ya Uhalifu Sura ya 256 na Kifungu cha 194B cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20.
Katika kipindi cha ukaguzi, niligundua kuwa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ilichukua na kutaifisha mali kadhaa, ikiwa ni pamoja na kiasi cha Sh. bilioni 16.02 na Dola za Kimarekani milioni 7.75. Fedha hizi ziliwekwa katika akaunti za benki ya urejeshwaji na utaifishaji mali iliopo Benki Kuu ya Tanzania.

Hata hivyo, ukaguzi wangu ulibaini ukiukwaji wa taratibu na mapungufu katika usimamizi wa mali zilizotaifishwa kama ifuatavyo:

15.4.1 Mapungufu Katika Usimamizi wa Mali na Fedha Zilizotaifishwa

DPP alitaifisha mali bila amri au hukumu za Mahakama, mali hizo ni pamoja na magari manne, gramu 864.97 za dhahabu, na karati 71,654.56 za almasi zenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 29.51.

Pia,niligundua kuwa kiasi cha Sh. bilioni 1.3 kilitaifishwa na kukabidhiwa Hazina bila kuzingatia utaratibu uliowekwa wa kuhamishia fedha zilizotaifishwa kwenye akaunti maalumu ya ukusanyaji iliopo Benki Kuu. Vilevile, kiasi cha Sh. milioni 355.48 kilichopatikana kutokana na mali

zilizotaifishwa kiliwekwa kwenye Akaunti ya Mapato, badala ya akaunti maalumu ya utaifishaji mali iliyopo Benki Kuu ya Tanzania, kinyume na matakwa ya kisheria. Aidha, Mkurugenzi wa Mashtaka hakuwa na daftari la kutunza maelezo na kumbukukumbu za fedha na mali zilizotaifishwa, na kasoro kadhaa katika ukamilifu wa taarifa za msingi za mali zilizotaifishwa baada ya maamuzi ya Mahakama kutambulika.

Napendekeza Mkurugenzi wa Mashtaka aweke mifumo na udhibiti imara wa kufuatilia mali na fedha zilizotaifishwa, ikiwa ni pamoja na kutumia taratibu zilizoboreshwa za kurekodi na kuripoti mali zilizotaifishwa ili kuwepo na uwazi na uwajibikaji, kwa mujibu wa sheria.

15.4.2 Mapungufu katika Usimamizi wa Mali Zilizotaifishwa

Niligundua kukosekana kwa mwongozo wa kusimamia mali zilizotaifishwa, jambo lililosababisha mapungufu. Vitu vilivyotaifishwa kama vile madini, magogo na vinginevyo vilisalia bila kusimamiwa kwa miaka mingi bila hatua yoyote sahihi ya usimamizi, hivyo kusababisha hasara kubwa kwa Serikali. Aidha, mali mbalimbali zilizotaifishwa, ikiwa ni pamoja na kemikali, makontena, vinywaji, mafuta, matandiko, na mashine za kamari hazikufuatiliwa kwa usahihi, na hakukuwa na taarifa za mahali zilipo.

Katika ukaguzi wangu, nimegundua kuwa mali kadhaa zilizotaifishwa hazipati matengenezo ya kawaida, na hivyo kuendelea kuharibika. Kwa mfano, nyumba tatu zilizopo Dar es Salaam na nyumba moja iliyopo Kagera hazijapata matengenezo ya kawaida. Aidha, magogo 7,751 yaliyotaifishwa katika mkoa wa Njombe, yenye thamani ya Sh. milioni 38, hayakuhifadhiwa ipasavyo, na magogo 4,751 yalihifadhiwa katika gereji binafsi bila makubaliano rasmi. Magogo 3,000 yalibaki katika mji wa Makambako, ambapo yaliharibiwa na mvua na jua kwa muda mrefu. Matokeo yake, haya magogo kwa sasa hayafai kuuzwa kwa njia ya mnada, na hivyo kusababisha hasara kubwa kwa Serikali.

Pia, nimegundua masuala yanayohusu usahihi na uhalali wa mali zilizotaifishwa, hususan magari. Maelezo ya usajili na umiliki wa baadhi ya magari yaliyotaifishwa, kama magari manne, trekta mbili, na pikipiki tatu, hayakutambuliwa na Mamlaka ya Mapato (TRA), na kutia shaka juu ya usahihi wa taarifa zinazohusiana na mali hizi. Aidha, uhalali wa magari 230

yaliyotaifishwa ulileta maswali, kwani maelezo ya usajili na umiliki hayafanani na taarifa zilizopo TRA.

Aidha, ukaguzi ulibaini kuwa baadhi ya mali zilizotaifishwa hazina ushahidi wa nyaraka za uhamisho, na kuibua mashaka juu ya umiliki na uhalali wa mali hizo. Kwa mfano, kati ya viwanja 17, mashamba manne, na nyumba 36 zilizotaifishwa na Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), kiwanja kimoja, shamba moja, na nyumba saba tu zilikuwa zimekabidhiwa rasmi kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango kwa mujibu wa nyaraka za uhamisho husika.

Pia, ukaguzi ulibaini kutofautiana kwa ulipaji wa kodi za pango katika nyumba nane zilizotaifishwa. Kodi za pango zililipwa kabla ya kutolewa kwa amri ya mahakama, kuanzia siku 120 hadi 669, ikionyesha kukosekana kwa taratibu na udhibiti sahihi.

Nimetoa mapendekezo kwa DPP kuandaa miongozo na taratibu za wazi za ukusanyaji taarifa zinazohusiana na mali na fedha zilizotaifishwa. Aidha, DPP anapaswa kuzingatia amri za mahakama na kuhakikisha kuwa mali zote zilizotaifishwa kwa wamiliki halali zinarejeshwa haraka baada ya kutolewa kwa amri za mahakama.

Kiambatisho Na. I: Mtiririko wa Hati Zilizokaguliwa kwa Miaka Mitatu

Na.	Taasisi	Aina	2021/2022	2020/2021	2019/2020
1	Fungu 3:Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi	Fungu	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
2	Fungu 4:Ofisi ya Rais – Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa	Fungu	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
3	Fungu 5:Tume ya Taifa ya Umwagiliaji	Fungu	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
4	Fungu 7:Msajili wa Hazina	Fungu	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
5	Fungu 10:Tume ya Pamoja ya Fedha (JFC)	Fungu	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
6	Fungu 11:Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara	Fungu	Inayoridhisha	Haikuwepo	Haikuwepo
7	Fungu 12:Tume ya Huduma za Mahakama	Fungu	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
8	Fungu 13:Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu	Fungu	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
9	Fungu 14:Jeshi la Zimamoto na Uokoaji	Fungu	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
10	Fungu 15:Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA)	Fungu	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
11	Fungu 16:Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali	Fungu	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
12	Fungu 18:Tume ya Taifa ya UNESCO	Fungu	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Mbaya
13	Fungu 19:Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali	Fungu	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
14	Fungu 20:Ofisi ya Rais – Ikulu	Fungu	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
15	Fungu 21:Idara ya Hazina	Fungu	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
16	Fungu 22:Idara ya Deni la Taifa na Huduma za Jumla	Fungu	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
17	Fungu 23:Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali	Fungu	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
18	Fungu 24:Tume ya Maendeleo ya Ushirika	Fungu	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
19	Fungu 25:Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu	Fungu	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
20	Fungu 26:Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais	Fungu	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
21	Fungu 27:Msajili wa Vyama vya Siasa	Fungu	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
22	Fungu 28:Jeshi la Polisi la Tanzania	Fungu	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha

Na.	Taasisi	Aina	2021/2022	2020/2021	2019/2020
23	Fungu 29:Jeshi la Magereza	Fungu	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
24	Fungu 30:Ofisi ya Rais – Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri	Fungu	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
25	Fungu 31:Ofisi ya Makamu wa Rais	Fungu	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
26	Fungu 32:Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora	Fungu	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
27	Fungu 33:Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma	Fungu	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
28	Fungu 34:Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki	Fungu	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
29	Fungu 35:Ofisi ya Taifa ya Mashtaka (NPS)	Fungu	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
30	Fungu 37:Ofisi ya Waziri Mkuu	Fungu	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
31	Fungu 38:Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (TPDF)	Fungu	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
32	Fungu 39:Jeshi la Kujenga Taifa (JKT)	Fungu	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
33	Fungu 40:Mahakama ya Tanzania	Fungu	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
34	Fungu 41:Wizara ya Katiba na Sheria	Fungu	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
35	Fungu 42:Bunge la Tanzania	Fungu	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
36	Fungu 43:Wizara ya Kilimo	Fungu	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
37	Fungu 44:Wizara ya Viwanda na Biashara	Fungu	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
38	Fungu 46:Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia	Fungu	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
39	Fungu 48:Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi	Fungu	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
40	Fungu 49:Wizara ya Maji	Fungu	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
41	Fungu 50:Wizara ya Fedha na Mipango	Fungu	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
42	Fungu 51:Wizara ya Mambo ya Ndani	Fungu	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
43	Fungu 52:Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto	Fungu	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
44	Fungu 53:Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu	Fungu	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha

Na.	Taasisi	Aina	2021/2022	2020/2021	2019/2020
45	Fungu 55:Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora	Fungu	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
46	Fungu 57:Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa	Fungu	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
47	Fungu 58:Wizara ya Nishati	Fungu	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
48	Fungu 59:Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania	Fungu	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
49	Fungu 60:Wizara ya Viwanda na Biashara	Fungu	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
50	Fungu 61:Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC)	Fungu	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
51	Fungu 62:Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Uchukuzi)	Fungu	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
52	Fungu 64:Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Sekta ya Uvuvi)	Fungu	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
53	Fungu 65:Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu	Fungu	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
54	Fungu 67:Ofisi ya Rais – Sekretarieti ya Ajira	Fungu	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
55	Vote 68:Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari	Fungu	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
56	Fungu 69:Wizara ya Maliasili na Utalii	Fungu	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
57	Fungu 91:Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Madawa ya Kulevya	Fungu	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
58	Fungu 92:Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS)	Fungu	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
59	Fungu 93:Idara ya Uhamiaji Tanzania	Fungu	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
60	Fungu 94:Ofisi ya Rais- Tume ya Utumishi wa Umma	Fungu	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
61	Fungu 96:Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo	Fungu	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
62	Fungu 98: Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Ujenzi)	Fungu	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
63	Fungu 99:Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Mifugo)	Fungu	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
64	Fungu 100:Wizara ya Madini	Fungu	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
65	Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM)	Wakala	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Isiyoridhisha
66	Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini (GPSA)	Wakala	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Isiyoridhisha
67	Wakala wa Mbegu za Kilimo (ASA)	Wakala	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha

Na.	Taasisi	Aina	2021/2022	2020/2021	2019/2020
68	Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA)	Wakala	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
69	Wakala wa Usajili na Utoaji wa Leseni za Biashara (BRELA)	Wakala	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
70	Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika	Wakala	Yenye Shaka	Inayoridhisha	Inayoridhisha
71	Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA)	Wakala	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
72	Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (FETA)	Wakala	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
73	Wakala wa Utafiti wa Madini Tanzania (GST)	Wakala	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
74	Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali	Wakala	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
75	Wakala wa Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo (LITA)	Wakala	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
76	Chuo cha Taifa cha Utalii	Wakala	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
77	Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA)	Wakala	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
78	Wakala wa Usalama na Afya Mahala pa Kazi (OSHA)	Wakala	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
79	Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA)	Wakala	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
80	Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA)	Wakala	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
81	Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSuBa)	Wakala	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
82	Mfuko wa Kuchochea Kilimo Tanzania	Wakala	Inayoridhisha	Haikuripotiwa	Haikuripotiwa
83	Wakala wa Ndege za Serikali (TGFA)	Wakala	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
84	Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA)	Wakala	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
85	Wakala wa Majengo Tanzania (TBA)	Wakala	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
86	Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFSA)	Wakala	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
87	Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA)	Wakala	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
88	Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA)	Wakala	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
89	Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania (TPSC)	Wakala	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
90	Wakala wa Maabara ya Mifugo Tanzania (TVLA)	Wakala	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
91	Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS)	Wakala	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
92	Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA)	Wakala	Mbaya	Inayoridhisha	Inayoridhisha

Na.	Taasisi	Aina	2021/2022	2020/2021	2019/2020
93	Chuo cha Maji	Wakala	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
94	Wakala wa Vipimo (WMA)	Wakala	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
95	Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo (CDCF)	Mfuko	Taarifa ya Hesabu haikuandaliwa	Taarifa ya Hesabu haikuandaliwa	Taarifa ya Hesabu haikuandaliwa
96	Mfuko Jumuifu	Mfuko	Taarifa ya Hesabu haikuandaliwa	Taarifa ya Hesabu haikuandaliwa	Taarifa ya Hesabu haikuandaliwa
97	Mfuko wa Ukimwi	Mfuko	Inayoridhisha	Haikuwepo	Haikuwepo
98	Mfuko wa Maendeleo ya Umwagiliaji (IDF)	Mfuko	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Haikuwepo
99	Mfuko wa Taifa katika Sekta ya Maji -Wizara	Mfuko	Inayoridhisha	Haikuripotiwa	Haikuripotiwa
100	Mfuko wa Mikopo ya Wafanyakazi Hazina	Mfuko	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
101	Mfuko wa Pembejeo wa Taifa (AGITF)	Mfuko	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
102	Mfuko wa Uwezeshaji Maendeleo ya Madini (EMDF)	Mfuko	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
103	Mfuko wa Ukaguzi na Usimamizi wa Ushirika (ISCF)	Mfuko	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
104	Mfuko wa Maendeleo ya Mifugo(LDF)	Mfuko	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
105	Mfuko wa Taifa wa Usimamizi wa Majanga	Mfuko	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
106	Mfuko wa Taifa wa Mambo ya Kale (NFA)	Mfuko	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
107	Mfuko wa Taifa katika Sekta ya Maji (NWF)	Mfuko	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
108	Mfuko wa Maendeleo ya Hatimiliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea	Mfuko	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
109	Bodi ya Mfuko wa Barabara	Mfuko	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
110	Akaunti ya Mfuko wa Barabara – Wizara ya Ujenzi	Mfuko	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
111	Mfuko wa Misitu Tanzania (TaFF)	Mfuko	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
112	Mfuko wa Uhifadhi Wanyamapori Tanzania(TWPF)	Mfuko	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
113	Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake (WDF)	Mfuko	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha

Na.	Taasisi	Aina	2021/2022	2020/2021	2019/2020
114	Ubalozi wa Tanzania- Windhoek,Namibia	Balozi	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Haikuwepo
115	Ubalozi wa Tanzania- Addis Ababa, Ethiopia	Balozi	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Isiyoridhisha
116	Ubalozi wa Tanzania – Abuja, Nigeria	Balozi	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
117	Ubalozi wa Tanzania – Harare, Zimbabwe	Balozi	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
118	Ubalozi wa Tanzania - Kuala Lumpur, Malaysia	Balozi	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
119	Ubalozi wa Tanzania – London, Uingereza	Balozi	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
120	Ubalozi wa Tanzania – Lusaka, Zambia	Balozi	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
121	Ubalozi wa Tanzania - New Delhi, India	Balozi	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
122	Ubalozi wa Tanzania – Ottawa, Kanada	Balozi	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
123	Ubalozi wa Kudumu wa Umoja Mataifa – Geneva, Uswisi	Balozi	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
124	Ubalozi wa Kudumu wa Umoja wa Mataifa- New York	Balozi	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
125	Ubalozi wa Tanzania- Havana,Cuba	Balozi	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
126	Ubalozi wa Tanzania- Seoul, Korea Kusini	Balozi	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
127	Ubalozi wa Tanzania-The Hague, Uholanzi	Balozi	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
128	Ubalozi wa Tanzania- Abu Dhabi, Umoja wa Falme za Kiarabu	Balozi	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
129	Ubalozi wa Tanzania- Algiers, Algeria	Balozi	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
130	Ubalozi wa Tanzania- Ankara, Uturuki	Balozi	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
131	Ubalozi wa Tanzania- Beijing, China	Balozi	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
132	Ubalozi wa Tanzania- Berlin, Ujerumani	Balozi	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
133	Ubalozi wa Tanzania- Brasillia, Brazil	Balozi	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
134	Ubalozi wa Tanzania- Brussels, Ubelgiji	Balozi	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
135	Ubalozi wa Tanzania- Bujumbura, Burundi	Balozi	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
136	Ubalozi wa Tanzania- Cairo, Misri	Balozi	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
137	Ubalozi wa Tanzania- Doha, Qatar	Balozi	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
138	Ubalozi wa Tanzania- Kampala, Uganda	Balozi	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha

Na.	Taasisi	Aina	2021/2022	2020/2021	2019/2020
139	Ubalozi wa Tanzania- Khartoum, Sudan	Balozi	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
140	Ubalozi wa Tanzania- Kinshasa, Kongo	Balozi	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
141	Ubalozi wa Tanzania- Kuwait	Balozi	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
142	Ubalozi wa Tanzania- Lilongwe, Malawi	Balozi	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
143	Ubalozi wa Tanzania- Maputo, Msumbiji	Balozi	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
144	Ubalozi wa Tanzania- Moroni, Komoro	Balozi	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
145	Ubalozi wa Tanzania- Moscow, Urusi	Balozi	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
146	Ubalozi wa Tanzania- Muscat, Oman	Balozi	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
147	Ubalozi wa Tanzania- Nairobi, Kenya	Balozi	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
148	Ubalozi wa Tanzania- Paris, Ufaransa	Balozi	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
149	Ubalozi wa Tanzania- Pretoria, Afrika Kusini	Balozi	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
150	Ubalozi wa Tanzania- Riyadh, Saudi Arabia	Balozi	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
151	Ubalozi wa Tanzania- Rome, Italia	Balozi	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
152	Ubalozi wa Tanzania- Stockholm, Swiden	Balozi	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
153	Ubalozi wa Tanzania- Tel Aviv,Israel	Balozi	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
154	Ubalozi wa Tanzania- Tokyo, Japan	Balozi	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
155	Ubalozi wa Tanzania- Washington, DC, Marekani	Balozi	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
156	Ubalozi wa Tanzania- Kigali, Rwanda	Balozi	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
157	Chama Cha Ukombozi wa Umma (CHAUMMA)	Chama	Inayoridhisha	Mbaya	Taarifa ya Hesabu haikuandaliwa
158	Democratic Party (DP)	Chama	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Taarifa ya Hesabu haikuandaliwa
159	African Democratic Alliance (ADA-TADEA)	Chama	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Kushindwa kutoa maoni

Na.	Taasisi	Aina	2021/2022	2020/2021	2019/2020
160	Alliance For African Farmers Party (AAFP)	Chama	Kushindwa kutoa maoni	Kushindwa kutoa maoni	Kushindwa kutoa maoni
161	Alliance for Democratic Change (ADC)	Chama	Inayoridhisha	Mbaya	Kushindwa kutoa maoni
162	Chama cha Sauti ya Umma (SAU)	Chama	Mbaya	Inayoridhisha	Kushindwa kutoa maoni
163	Demokrasia Makini(DM)	Chama	Yenye Shaka	Kushindwa kutoa maoni	Kushindwa kutoa maoni
164	National Reconstruction Alliance (NRA)	Chama	Yenye Shaka	Inayoridhisha	Kushindwa kutoa maoni
165	Tanzania Labour Party (TLP)	Chama	Inayoridhisha	Mbaya	Kushindwa kutoa maoni
166	Union for Multi-Party Democracy (UMD)	Chama	Yenye Shaka	Mbaya	Kushindwa kutoa maoni
167	United Peoples' Democratic Party (UPDP)	Chama	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Kushindwa kutoa maoni
168	Chama Cha Kijamii (CCK)	Chama	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
169	Civic United Front (CUF)	Chama	Yenye Shaka	Isiyoridhisha	Inayoridhisha
170	National League for Democracy (NLD)	Chama	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
171	United Democratic Party (UDP)	Chama	Isiyoridhisha	Isiyoridhisha	Inayoridhisha
172	ACT – WAZALENDO	Chama	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
173	Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA)	Chama	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
174	Chama cha Mapinduzi (CCM)	Chama	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
175	National Convention for Construction and Reform (NCCR - MAGEUZI),	Chama	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
176	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa-Morogoro	Hospitali	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Mbaya

Na.	Taasisi	Aina	2021/2022	2020/2021	2019/2020
177	Hospitali ya Kanda-Chato	Hospitali	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Haikuwepo
178	Hospitali ya Kanda-Mtwara	Hospitali	Inayoridhisha	Haikuwepo	Haikuwepo
179	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa-Shinyanga	Hospitali	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Isiyoridhisha
180	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa-Sumbawanga	Hospitali	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Isiyoridhisha
181	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa-Temeke	Hospitali	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Isiyoridhisha
182	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Amana	Hospitali	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
183	Hospitali ya Benjamini Mkapa	Hospitali	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
184	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa-Bombo Tanga	Hospitali	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
185	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Bukoba	Hospitali	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
186	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Dodoma	Hospitali	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
187	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa-Geita	Hospitali	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
188	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa-Iringa	Hospitali	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
189	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa-Katavi	Hospitali	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
190	Hospitali Maalumu ya Magonjwa ya Kuambukiza Kibong'oto	Hospitali	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
191	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa-Ligula	Hospitali	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
192	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa-Manyara	Hospitali	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
193	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa-Maweni	Hospitali	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
194	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa-Mawenzi	Hospitali	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
195	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa-Mbeya	Hospitali	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
196	Hospitali ya Kanda-Mbeya	Hospitali	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
197	Hospitali ya Mirembe	Hospitali	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
198	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa-Mount Meru	Hospitali	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
199	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa-Musoma	Hospitali	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
200	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa-Mwananyamala	Hospitali	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
201	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa-Njombe	Hospitali	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha

Na.	Taasisi	Aina	2021/2022	2020/2021	2019/2020
202	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa-Sekotoure	Hospitali	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
203	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa-Simiyu	Hospitali	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
204	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa-Singida	Hospitali	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
205	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa-Sokoine	Hospitali	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
206	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa-Songea	Hospitali	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
207	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa-Songwe	Hospitali	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
208	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa-Tabora	Hospitali	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
209	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa-Tumbi	Hospitali	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Inayoridhisha
210	Bodi ya Usajili wa Wathamini	TN	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Haikuwepo
211	SUMAJKT-Kampuni ya Vinywaji	TN	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Haikuwepo
212	SUMAJKT- Kampuni ya Ushonaji	TN	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Haikuwepo
213	SUMA JKT Umeme	TN	Inayoridhisha	Haikuwepo	Haikuwepo
214	SUMA JKT- Kampuni ya Huduma za Chakula	TN	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Haikuwepo
215	SUMA JKT-Kampuni ya Minada	TN	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Haikuwepo
216	SUMA JKT- Kampuni ya Utengenezaji Samani Chang'ombe	TN	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Haikuwepo
217	SUMA JKT- Kampuni ya Usafi na Unyunyuziaji Dawa	TN	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Haikuwepo
218	SUMAJKT -Kampuni ya Huduma za Bandarini	TN	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Haikuwepo
219	SUMAJKT -Kampuni ya Ushauri Elekezi	TN	Inayoridhisha	Haikuwepo	Haikuwepo
220	Tume ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano	TN	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Haikuwepo
221	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira-Bunda Daraja C	TN	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Haikuwepo
222	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira-Ifakara Daraja C	TN	Inayoridhisha	Haikuripotiwa	Haikuwepo
223	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira-Igunga Daraja C	TN	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Haikuwepo
224	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira-Kibaigwa Daraja C	TN	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Haikuwepo
225	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira-Mpwapwa Daraja C	TN	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Haikuwepo

Na.	Taasisi	Aina	2021/2022	2020/2021	2019/2020
226	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira-Mugumu daraja C	TN	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Haikuwepo
227	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira-Orkesument Daraja C	TN	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Haikuwepo
228	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira-Ruangwa Daraja C	TN	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Haikuwepo
229	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira-Sengerema Daraja C	TN	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Haikuwepo
230	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira-Tarime Daraja C	TN	Yenye Shaka	Inayoridhisha	Haikuwepo
231	Mamlaka ya Usambazaji Maji Safi na Tunduma Daraja C	TN	Inayoridhisha	-	Haikuwepo
232	Mamlaka ya Usambazaji Maji Safi na Tunduru Daraja C	TN	Inayoridhisha	-	Haikuwepo
233	Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano (NICTBB)-Dar es Salaam	TN	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Haikuwepo
234	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa MazingiraBiharamulo	TN	Inayoridhisha	Haikuripotiwa	Haikuripotiwa
235	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira-Busega Daraja C	TN	Inayoridhisha	Haikuripotiwa	Haikuripotiwa
236	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira-Chato Daraja C	TN	Inayoridhisha	Haikuripotiwa	Haikuripotiwa
237	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira-Chunya Daraja C	TN	Inayoridhisha	Haikuripotiwa	Haikuripotiwa
238	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira-Gairo Daraja C	TN	Inayoridhisha	Haikuripotiwa	Haikuripotiwa
239	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira-Itumba-Isongole Daraja C	TN	Inayoridhisha	Haikuripotiwa	Haikuripotiwa
240	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira-Kasulu Daraja C	TN	Inayoridhisha	Haikuripotiwa	Haikuripotiwa
241	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira-Kibaya Daraja C	TN	Inayoridhisha	Haikuripotiwa	Haikuripotiwa
242	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira-Kibondo Daraja C	TN	Inayoridhisha	Haikuripotiwa	Haikuripotiwa
243	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira-Kilindoni Daraja C	TN	Inayoridhisha	Haikuripotiwa	Haikuripotiwa
244	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira-Kilwa Masoko Daraja C	TN	Inayoridhisha	Haikuripotiwa	Haikuripotiwa
245	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira-Kiomboi Daraja C	TN	Inayoridhisha	Haikuripotiwa	Haikuripotiwa
246	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira-Kishapu Daraja C	TN	Inayoridhisha	Haikuripotiwa	Haikuripotiwa
247	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira-Kondoa Daraja C	TN	Inayoridhisha	Haikuripotiwa	Haikuripotiwa

Na.	Taasisi	Aina	2021/2022	2020/2021	2019/2020
248	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira-Liwale Daraja C	TN	Inayoridhisha	Haikuripotiwa	Haikuripotiwa
249	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira-Loliondo Daraja C	TN	Inayoridhisha	Haikuripotiwa	Haikuripotiwa
250	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira-Ludewa Daraja C	TN	Inayoridhisha	Haikuripotiwa	Haikuripotiwa
251	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira-Lushoto Daraja C	TN	Inayoridhisha	Haikuripotiwa	Haikuripotiwa
252	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira-Maganzo Daraja C	TN	Inayoridhisha	Haikuripotiwa	Haikuripotiwa
253	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira-Mahenge Daraja C	TN	Inayoridhisha	Haikuripotiwa	Haikuripotiwa
254	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira-Manyoni-Itigi Daraja C	TN	Inayoridhisha	Haikuripotiwa	Haikuripotiwa
255	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira-Mbinga Daraja C	TN	Inayoridhisha	Haikuripotiwa	Haikuripotiwa
256	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira-Mbulu Town Daraja C	TN	Inayoridhisha	Haikuripotiwa	Haikuripotiwa
257	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira-Mombo Daraja C	TN	Inayoridhisha	Haikuripotiwa	Haikuripotiwa
258	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira-Mugango/Kiabakari daraja C	TN	Inayoridhisha	Inayoridhisha	Haikuripotiwa
259	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira-Mwanhuzi Daraja C	TN	Inayoridhisha	Haikuripotiwa	Haikuripotiwa
260	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira-Namanyere Daraja C	TN	Inayoridhisha	Haikuripotiwa	Haikuripotiwa
